**2 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 2 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini sasa aulize swali lake.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba swali langu lijibiwe na Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa, namba ya swali, Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, swali namba 196.

Na. 196

### Tatizo la Ajira kwa Vijana

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la ajira kwa vijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Patrobass Katambi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ili kutatua tatizo la ajira kwa vijana. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(a) Kubuni na kutekeleza programu maalum zinazowawezesha vijana kujifunza kwa vitendo kupitia sekta zinazozalisha ajira kwa wingi;

(b) Kufanya maboresho ya sera mbalimbali ikiwemo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007, Toleo la mwaka 2024 na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la mwaka 2023;

(c) Kuwezesha vijana kupitia ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati inayochochea uchumi;

(d) Kubuni na kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi;

(e) Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na

(f) Kuboresha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Ninashukuru Serikali kwa majibu, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; katika halmashauri zetu kuna Mfuko wa kukopesha vijana ile asilimia nne katika mapato ya ndani ya halmashauri. Serikali ina mpango gani kuongeza Mfuko huu uwe mkubwa kuongeza mafungu pale ili vijana wapate mikopo mingi zaidi na vijana wengi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika ajira chache zilizopo za Serikali labda unakuta *TRA* au jeshini au wapi wanaajiriwa vijana nafasi 200, nafasi mia ngapi lakini zinalalamikiwa kwamba zinaenda sehemu moja ya nchi au sehemu chache za nchi. Unakuta mkoa katika nafasi 200 unaambulia nafasi moja au mbili; hili likoje na Serikali inalishughulikia vipi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la kwanza, halafu la pili Mheshimiwa Mbunge atanisaidia kwa sababu sikupata usikivu mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza kuhusiana na kuongeza kiwango cha mikopo ya asilimia nne ya pato ghafi la halmashauri linalotolewa kwa vijana. Suala hili tunalifanya kulingana na hali ya kiuchumi, lakini hata hivyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliona umuhimu huo na kuamua kuanza kupeleka mikopo kwenye sekta mbalimbali ambapo vijana wapo pia. Kwa mfano kwenye programu ya uchimbaji wa madini wana programu ambayo Mheshimiwa Waziri Mavunde anaisimamia ya *Minning for Brighter Tomorrow* ambayo huko vijana wanapewa mafunzo, wanapea vitalu bure, lakini pia na kupewa mikopo kama *startup capital* kwenye mashine.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine upo kwenye Wizara ya Elimu ambapo zaidi ya shilingi bilioni tano zilitolewa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kukopesha walio kwenye sanaa na masuala ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwenye Wizara ya Kilimo kuna ule mpango wa *Building Better Tomorrow* ambapo vijana napo pia wanapewa. Wizara ya Mifugo na Uvuvi napo kuna vijana wanapewa, zaidi ya shilingi bilioni 10.3 zilitolewa na walipewa boti zaidi ya 100 na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuwasaidia wale walio kwenye sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, umekuwa pia ni mpango endelevu kwenye sekta nyingine. Hata walio kwenye biashara na masuala ya uchumi na uwekezaji kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi, zaidi ya shilingi trilioni 2.7 na sasa zimefikia trilioni tatu ambazo zilitolewa kwa vijana pamoja na makundi mbalimbali zaidi ya wananchi milioni 24 walinufaika na mpango huo na hivyo kufikia hata ajira zilizoongezeka kufikia 8,084,000 kwa kipindi cha miaka minne ambayo ni mapinduzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ameyafanya katika kupambania ajira za vijana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza swali la pili sikulipata vizuri kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Kwa majibu ulivyotoa kwa kirefu kwa sehemu ya kwanza kuna swali tena? Mheshimiwa naona umesimama.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ninataka nifafanue swali la pili hakulisikia vizuri kwamba humu ndani ya Bunge tumelalamika sana kwamba hata hizi za Serikali zinazotolewa ajira chache zilizopo kwenye Wizara mbalimbali na idara mbalimbali mgawanyo haupo sawa. Nimetoa mfano kwamba kuna ajira 200 Wizara fulani, unakuta mkoa mmoja unaambulia nafasi moja au mbili, lakini mkoa mwingine nafasi 50 au zaidi. Hivi usawa ukoje na Serikali ina mpango gani kusimamia usawa katika suala hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwanza msingi wa ajira umekuwa *well founded* au umejikita

vizuri zaidi katika msingi wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 ambayo inaitaka Serikali au Mamlaka zozote za Serikali zilizopo na zilizoanzishwa kwa mujibu wa Katiba kutoa nafasi zozote za utumishi wa nchi bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo hata Sheria ya Utumishi wa Umma na michakato yote ya kiajira ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Utumishi wa Umma zinakataza zote ubaguzi. Kwa hiyo, msingi wa ajira uliopo unatokana na ushindani na ajira zinapotolewa zinatolewa kulingana na kuangalia hali ya Uchumi, lakini pia uhitaji wa ikama kwenye taasisi mbalimbali na zinatangazwa *publicly* (kwa watu wote, kwa umma kuomba).

Mheshimiwa Spika, inapotokea pengine mkoa mmoja umepata nafasi mbili au tatu siyo tatizo la kwamba wamepangiwa hivyo isipokuwa inaweza ikawa ni ule ushindani watu wamejitokeza, inawezekana mkoa fulani walikuwa wameamka kielimu wakajikuta wamekamata nafasi nyingi zaidi lakini hakuna msingi wowote wa upendeleo katika utoaji wa ajira za sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kutambua kwamba Serikali siyo mwajiri mkuu leo duniani imebadilika hivyo kwenye maeneo mengi, ndiyo maana tumeenda na mipango mingine ya kubadilisha Sera ya Maendeleo ya Vijana, tumebadilisha Sera ya Elimu, lakini pia tumefanya mpango wa kubadilisha Sera pia ya Uwekezaji nchini pamoja na uratibu wa ajira za wageni ili kutanua *private sector* iweze kuajiri vijana walio wengi zaidi kwa sababu tunafahamu changamoto hiyo ni kubwa na kila mwaka zaidi ya *demographic population* na wale ambao wanamaliza vyuo vikuu ni zaidi ya laki moja...

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere nimekuona lakini umesimama baadaye kwa hivyo keti, watauliza wawili tu. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali kwa kifupi.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. sasa hivi kila halmashauri kuna miradi mingi na kazi nyingi zinaendelea huko. Je, Wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanapata *database* ya vijana waliomaliza vyuo vikuu katika kila halmashauri ili wapewe hizo kazi zinazofanyika katika halmashauri zetu hata kama ni za muda mfupi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, tayari jambo hilo alilolieleza Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara limezingatiwa na Serikali. Tunayo kanzidata, lakini hatua hiyo tulibadilisha Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sheria Namba 410 ili kuweza kuhakikisha tunawaakisi vijana walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, agizo lililopo la mwongozo ni kwamba katika *tender* zote zinazotolewa na halmashauri nchini, 30% wanapewa vijana na tayari kampuni zaidi ya 1,148 zimepata nafasi hiyo na zimenufaisha vijana zaidi ya 164,443. Kwa hiyo, ni hatua endelevu ambayo tutaendelea kuifanyia kazi kama alivyoeleza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa sera iliyoanzisha mikopo ya 10% kwa vijana, akinamama na watu wenye ulemavu manispaa ilikuwa ni sera ya kuwasaidia wananchi kiuchumi na kwa kuwa kuna wanaume ambao wanahitaji na hawana namna nyingine ya kupata hiyo mikopo; nini mpango wa Serikali kusaidia wanaume wanaohitaji mikopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo swali la msingi kabisa, lakini hilo swali ninadhani ni la TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nitalijibu.

**SPIKA:** Unaweza kulijibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Ndiyo.

**SPIKA:** Kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, katika mgawanyo wa 10% ile ya kusema sera ya wanawake na hawa wanaume na vijana bado inaingia kwenye *premises* zile zile kwa sababu hawa wanaosema wanaume japo Mheshimiwa hajafafanua umri kwa sababu wanaume pia wapo vijana ni wanaume, ni kwamba mipango ya kimikopo ipo kulingana na kisekta. Wapo ambao wanapata kupitia 4:4:2, 10% ya pato ghafi la halmashauri. Wapo ambao wanapewa kutokana na maeneo ya kisekta kwa mfano kwenye mifugo, kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile wapo ambao wanapata kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo wanaume wengi ambao anawasema kwa muktadha huo kwa sababu hajataja umri ni pamoja na wale walio kwenye bodaboda, walio kwenye sekta za uchimbaji na uzalishaji wamekuwa wakipewa kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na ndiyo ndani ya idadi ile ya wananchi milioni 24 waliopata kunufaika na shilingi trilioni 2.7...

**SPIKA:** Huo Mfuko nao upo kwa halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naam?

**SPIKA:** Huo Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi upo nao kwa halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na unaratibiwa kupitia halmashauri (Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi).

**SPIKA:** Kwa hiyo wanaume wakaombe kule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, wanaweza kupata kwenye hiyo kwani zaidi ya shilingi trilioni tatu zimetolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, umesikia?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nimesikia.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 197

**Kujenga Mitaro katika Kata za Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga mitaro katika kata za Msalala?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imejenga mitaro yenye urefu wa mita 1,400 yenye thamani ya shilingi milioni 161.8 katika Kata ya Ntobo kupitia fedha za Mfuko wa Barabara. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilijenga mitaro yenye urefu wa mita 4,600 yenye thamani ya shilingi milioni 410 katika Kata ya Bulyanhulu kupitia fedha za *CSR*. Pia mitaro yenye urefu wa mita 300 na kalavati tatu zenye thamani ya shilingi milioni 97 katika Kata ya Bulyanhulu kupitia fedha za mfuko wa barabara ilijengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itajenga mitaro yenye urefu wa mita 1,300 yenye thamani ya shilingi milioni 246.4 katika Kata ya Bugarama kupitia fedha za *CSR*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itajenga mitaro yenye urefu wa mita 200 yenye thamani ya shilingi milioni 31.2 katika Kata ya Mwalugulu. Pia, mitaro yenye urefu wa mita 300 kwa shilingi milioni 43.2 katika Kata ya Bugarama itajengwa na *TARURA* kupitia fedha za mfuko wa barabara.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imeweka katika mipango ujenzi wa mitaro mita 2,600 yenye thamani ya shilingi milioni 309.9 kupitia fedha za *CSR* katika Kata ya Bulyanhulu. Serikali itaendelea kuhudumia mtandao wa barabara na madaraja katika Jimbo la Msalala kwa kujenga, kukarabati na kutengeneza kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya kujenga mitaro kupitia fedha za *CSR* na tunafahamu kwamba bajeti ya *CSR* na Serikali ni tofauti kwani bajeti ya CSR inaanza mwezi wa kwanza. Ni lini sasa Mkurugenzi atawaelekeza watu wa mgodi waanze mara moja ujenzi wa mitaro hii kwenye Kata ya Bulyanhulu kwa sababu fedha ya *CSR* zipo zimeshaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 tuliahidiwa kujengewa kilometa tano za lami inayotoka Kata ya Bulyanhulu kwenda kata ya jirani ya Nyakagwe na tayari hatua za manunuzi zimeshafanyika na ukaguzi umeshafanyika; sasa ni lini Serikali itaanza mara moja ujenzi wa barabara hii inayotoka Bulyanhulu kwenda Nyakagwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kuweza kusimamia kuhakikisha kwamba kwa mujibu wa taratibu fedha hizi za *CSR* zinaweza kutumika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinaenda kutekeleza mradi wa ujenzi wa mtaro.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ninaomba nimhakikishie kwamba dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA* na ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, shilingi bilioni 8.03 zimetumika katika upande wa barabara hizi za wilaya.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2024/2025, shilingi bilioni 1.9 zimetengwa kibajeti kwa ajili ya kuhakikisha zinaendelea kuboresha miundombinu ya barabara hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii aliyoitaja katika Jimbo lake itajengwa na nichukue nafasi hii kumkumbusha na kuendelea kumsisitiza Meneja wa *TARURA* ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya kusimamia kuhakikisha kwamba utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii unaanza kwa wakati na unaweza kukamilika kwa wakati na kwa viwango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Tandale-Ilundo pale Kiwira, barabara hiyo ni muhimu sana kwa sababu wanawake wanasumbuka kuvusha mizigo yao wanapokwenda kuuza pale Tandale? Wanawake wa Kiwira ni mabingwa sana wa biashara. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza maradufu bajeti ya *TARURA* kwa maana ya kufahamu umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za wilaya ambazo zinawasaidia wananchi kiuchumi na zinawawezesha kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii kama alivyosema Mheshimiwa Suma Fyandomo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwamba barabara hii katika eneo hili la Tandale itajengwa na Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali itafika na kuhakikisha kwamba barabara hii imejengwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita utaona bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 kwa mwaka, lakini muda huu tunavyozungumza tunatarajia katika mwaka wa fedha 2025/2026, bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18. Kwa hiyo, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuimarisha na kuboresha miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa ambazo zinasimamiwa na *TARURA*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara sasa aulize swali lake.

Na. 198

**Kutatua Upungufu wa Madawati**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa madawati katika Shule za Msingi na Sekondari – Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya madawati (dawati moja wanafunzi watatu) katika Jimbo la Mwibara ni 13,989 yaliyopo ni 9,102 na upungufu ni 4,887, ambapo uwiano ni dawati moja kwa wanafunzi watano (1:5). Upande wa sekondari meza na viti mahitaji ni 17,346 zilizopo ni 16,714 na upungufu ni 632 sawa na asilimia 3.64

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa kukabiliana na upungufu wa madawati, meza na viti ni pamoja na kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri. Mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imetenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 150.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuhakikisha kuwa kila darasa jipya linalojengwa linawekewa madawati 15 (dawati moja wanafunzi watatu) kwa shule za msingi na seti ya viti na meza 40 kwa shule za sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri kwamba kuna upungufu wa madawati na kwamba Halmashauri katika kutumia vyanzo vyake vya mapato haina uwezo.

Je, Serikali ina mkakati gani mbadala wa kutatua tatizo hilo la madawati katika Jimbo la Mwibara? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sekta ya elimu na hususan elimu hii msingi kwa maana kuanzia madarasa ya awali, shule ya msingi na sekondari inaweza kuimarika, ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita utaona kwamba uwekezaji wa shilingi trilioni 5.1 umefanyika katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaelewa kuna umuhimu mkubwa sana wa upatikanaji wa madawati ikiwemo viti na meza kwa ajili ya wanafunzi wetu. Kupitia fedha kutoka Serikali Kuu na kupitia fedha kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri, pia kutumia wadau mbalimbali wa maendeleo Serikali inakusudia kuendelea kuhakikisha kwamba inaleta viti, meza na madawati katika shule zetu ili wanafunzi waweze kupata sehemu nzuri ya kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imepanga kutumia zaidi ya shilingi bilioni 613 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu mbalimbali katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu. Tunatarajia kwamba katika kipindi cha mwaka huo wa fedha viti 47,979 vitatengenezwa kwa ajili ya kusambazwa katika shule zetu, pia tunatarajia madawati 71,482 yatatengenezwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shule zetu zinapata mazingira mazuri ya wanafunzi kusomea lakini na mazingira mazuri ya walimu wetu kufundishia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafika Mwibara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha na kuimarisha sekta ya elimu kwa kupeleka madawati, lakini viti na meza kwa ajili ya wanafunzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali kwa kifupi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya TAMISEMI ipo tayari kutoa mwongozo mahsusi kwa Halmashauri zote zenye uwezo mkubwa wa mapato ili mwaka wa fedha ujao kila Halmashauri hizo ziweke mpango wa namna ya kumalizia shida ya viti, meza na madawati ili watoto wetu wa shule za msingi na sekondari wasiweze kukaa chini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na hasa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri inatarajia kutumia shilingi bilioni 613 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinachangia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo shughuli ya kuhakikisha kwamba madawati yanapatikana katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwita Waitara kwamba Serikali itaendelea kusimamia Halmashauri zetu hizi ili ziweze kutimiza majukumu yake ya msingi ya kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuendelea kuimarisha sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuendelea kutoa msisitizo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote 184 waweze kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa msingi wa kutenga fedha kutoka kwenye mapato ya ndani na kuweza kuziweka katika mipango na bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 199

**Mwongozo wa Ajira kwa Wanaojitolea**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mwongozo wa kutoa kipaumbele cha ajira zinazotangazwa kwa wanaojitolea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Kujitolea katika Utumishi wa Umma *(Volunteering Guidelines in Public Service)*. Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia maoni ya wadau muhimu wakiwemo waajiri wote ndani ya utumishi wa umma na utaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe Mosi Julai, 2025.

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu unabainisha mambo muhimu ya kuzingatiwa na vijana wa kujitolea, pamoja na taasisi za umma ikiwa ni pamoja na kutoa fursa kwa vijana wa kujitolea kuweza kujipatia faida ya ziada pamoja na kuwapa uzoefu na uwezo wa kushindana pindi ajira zitakapotangazwa ili kukidhi matakwa ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo Na. 2 la Mwaka 2008.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwepo na fikra kwa vijana wetu walio wengi wa kitanzania wanapoomba ajira kwamba ili uweze kupata ajira Serikalini lazima uwe na *Godfather* kwa maana ya *connection* kwenye Serikali ili uweze kupata ajira. Je, nini kauli ya Serikali kuwaondoa vijana katika hali ya fikra hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa ruhusa yako kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jambo kubwa ambalo alilifanya jana lililoleta matumaini makubwa kwa watumishi wa umma, kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 370,000 mpaka kufikia shilingi 500,000. Hili ni jambo kubwa limeleta matumaini makubwa kwa watumishi wa umma na hii ni jitihada kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuifanya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma na kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo kubwa kwa kweli ambalo tunamshukuru Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Noah kwamba katika utumishi wa umma kumekuwa na dhana kwamba ili upate ajira lazima uwe na *Godfather*. Ninaomba nimwondoe shaka Mheshimiwa Noah, kwa utaratibu ajira zote zinapatikana kwa njia ya ushindani na kupitia Sera yetu ya Ajira ya Utumishi wa Umma, Toleo Na. 2 la mwaka 2008 limetamka wazi kwamba ajira zote zitapatikana kwa njia ya ushindani, ndiyo maana unaona ajira nyingi ambazo Mheshimiwa Rais ametoa, takribani ajira za hivi juzi 15,000 zilizotolewa zote zimefanyika kwa njia ya ushindani. Kwa hiyo, nisisitize nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata fursa na haki inatendeka kwa ajira zinazopatikana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali kwa kifupi.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na vijana wanaojitolea zaidi ya miaka mitatu kada ya elimu na kada ya afya na hapa Mheshimiwa Spika ulitoa tangazo kwamba ni vema tukawajali hao wanaojitolea.

Je, Serikali imechukua hatua gani na kusikiliza ombi aliloomba Mheshimiwa Spika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaendelea kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Sophia kwa namna anavyofuatilia vijana wanaojitolea, amekuwa *champion* mzuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba tayari tumeandaa mwongozo ambao utaanza kutumika tarehe Mosi Julai mwaka huu. Mwongozo huo umezingatia mambo matatu, kwanza ni utaratibu bora wa kuwapata vijana wanaojitolea kwa sababu mwanzo utaratibu haukuwa mzuri, namna ya kumpata wa kujitolea ilikuwa haijakaa vizuri, kwa hiyo, mwongozo huu utatupa utaratibu wa kuwapata wanaojitolea.

Mheshimiwa Spika, pili, wengi walikuwa wanajitolea bila kulipwa chochote, lakini tumeona sasa tuanze kuwapa fedha walau ya kujikimu ili mtu anapojitolea apate moyo wa kufanya kazi. Tatu, tutawaweka kwenye kanzidata na tutatumia kigezo cha kujitolea ikiwa sifa ya ziada kulingana na utendaji kazi na nidhamu na namna alivyofanya kazi ya kujitolea ili kumpa sifa ya ziada wakati tunapotangaza ajira. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 200

**Fedha za Kudhibiti Mito Iliyopanuka – Kawe**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza:-

Je, lini ahadi ya kupeleka fedha za ujenzi wa Mito iliyopanuka katika Jimbo la Kawe itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya kupanuka kwa mito iliyopo katika Jimbo la Kawe ikiwemo mito Nyakasangwe, Tegeta, Mbezi, Mlalakuwa, Mpiji na Ndubwi inayotiriririsha maji yake katika Bahari ya Hindi. Kupanuka kwa mito hiyo ni kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kufanyika kwa shughuli zisizoendelevu za kibinadamu ndani ya mita 60 kinyume na Kifungu Na. 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali itaendelea kutenga fedha pamoja na kutafuta fedha kupitia mifuko ya hifadhi ya usimamizi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo *GEF, GCF* na *AF* kwa ajili ya ujenzi wa mito hiyo. Kwa muktadha huo, ujenzi wa mito iliyopanuka katika Jimbo la Kawe utatekelezwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kutoa wito kwa Serikali za Mitaa kote nchini kuendelea kusimamia kikamilifu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ili kuzuia shughuli za kibinadamu kama vile uchimbaji wa mchanga na kuelimisha jamii juu ya utunzaji wa mazingira ili kudhibiti upanukaji wa mito na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa hali ya mito katika Jimbo la Kawe ikiwemo Mto Nyakasangwe ni mbaya, imefikia hatua sasa inakwenda kwenye makazi ya wananchi, nyumba zinadondoka. Je. Serikali ina

mpango gani basi wa dharura kusaidia maeneo hayo ili kunusuru hizo nyumba za wananchi zinazoanguka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; changamoto ya kutiririka kwa maji pia inayakumba maeneo ya Temeke katika Kata ya Kilakala, eneo la Bongotonyo, maji yanajaa na wananchi wanakuwa hawana cha kufanya hadi waletewe *pump,* hali hiyo imeendelea kwa muda wa miaka zaidi ya kumi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kufuatana na mimi akaone hali halisi ya Bongotonyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii niwape pole wananchi wa maeneo hayo ya jimbo hilo kwa mvua ambazo zinaendelea na kwa athari ambazo zinaendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali inatambua changamoto hiyo ya kupanuka kwa mito na changamoto hii inasababishwa na shughuli za wenyewe binadamu, ipo mipango ya dharura ambayo tayari imeshafanywa na Serikali. Tunashukuru wenzetu wa *TARURA* tayari kuna baadhi ya vivuko vimeshaanza kujengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaondoa hii changamoto, lakini tayari tumeshaongea na wenzetu wa *NEMC* kwa kushirikiana na TAMISEMI na *TARURA* ili kuona namna ambavyo tunaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusiana na athari ya kufanya shughuli zikiwemo za uchimbaji wa mchanga na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi tumepita tukiwaelimisha wananchi kuwaeleza waache kujenga katika maeneo ambayo maji yanatuama au karibu na vyanzo vya maji, lakini kubwa zaidi tumeendelea kuwaelimisha wazingatie zaidi hii sheria ya mita 60. Hizo ni baadhi tu ya hatua za dharura ambazo tumezichukua.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba nipo tayari kuambatana na yeye ama kuambata na

Mheshimiwa Gwajima kwenda Jimboni kwake ili kuweza hiyo hali na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 201

**Kutokomeza Wizi katika Malipo ya Wakulima wa Korosho**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza wizi kwa baadhi ya Makatibu wa *AMCOS* katika malipo ya wakulima wa korosho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, imeanzisha mfumo wa malipo kupitia Vyama vya Ushirika, ambapo kwa sasa mkulima analipwa na Chama Kikuu moja kwa moja badala ya kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi *(AMCOS)*. Malipo hayo hufanyika baada ya kupokea taarifa zilizohakikiwa na kuthibitishwa na timu maalum ya Maafisa wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; ni kweli malipo yote yanapitia kwenye vyama vya ushirika, lakini waandaaji wa taarifa ni Makatibu ambao wapo kwenye *AMCOS* ndipo ambapo

changamoto hizo zilijitokeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wale ambao wameathirika na malipo hawajapata wanalipwa malipo yao kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wapo Makatibu ambao wanategemea hizo *AMCOS* ili wapate chochote, inakuwa chanzo cha kufanya huo udanganyifu ili wapate chochote. Je, ni lini Serikali itawaajiri sasa Makatibu wa *AMCOS* ili kuwaondolea tamaa ya kuwaibia wakulima ambao wanashindwa kupata fedha zao kwa wakati? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa wale wote ambao wameathirika na bado hawajalipwa sisi tutahitaji taarifa zao ili tufanye uhakiki na walipwe kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuajiri Makatibu katika *AMCOS,* kwa kuwa vyama hivi vya ushirika vinaanzishwa na wanajumuiya bado jambo hili tunajaribu kuliangalia na kuona namna bora ya kulitekeleza. Kwa hiyo, tunafanya tathmini ya kuona namna bora ambayo inaweza kuondoa hizi athari zinazosababishwa na Makatibu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 202

**Kukamilisha Barabara ya Handeni – Mafuleta – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, kuna mpango mkakati upi wa kumsimamia Mkandarasi anayejenga barabara ya Handeni kwenda Mafuleta kilomita 20 kukamilisha kwa muda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Handeni – Mafuleta kilometa 20 umefikia 46% na kazi za ujenzi zinaendelea. Ujenzi wa barabara hii umekuwa ukisuasua kutokana na migogoro iliyojitokeza katika maeneo ya uchimbaji wa kifusi na kokoto, mvua za *El-Nino* na Mkandarasi kutokuwa na mtiririko mzuri wa fedha. Ili kuhakikisha kuwa kazi ya ujenzi wa barabara inakamilika kwa wakati, Serikali imemlipa Mkandarasi madai yake yote na kumwelekeza Mhandisi Mshauri kumsimamia Mkandarasi ili kuhakikisha anafanya kazi usiku na mchana. Aidha, Mkandarasi ameshapeleka wataalam wapya *site* na kuongeza mitambo ili waongeze nguvu na kasi ya ujenzi wa barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kiuhalisia mkandarasi hayuko *site,* je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufanya ziara ya kukagua barabara hii yenye kilometa 20, ambayo ina takribani miaka mitatu sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipofanya ziara kwenye Mkoa wa Tanga. Siku anamalizia ziara kwenye Bandari ya Tanga alielekeza barabara hii, kwa umuhimu wake na kwa gharama kubwa ambayo Serikali imetumia kwenye Bandari ya Tanga, ijengwe kwa utaratibu wa *PPP*. Je, Serikali imefikia wapi hatua hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kufanya ziara kwenye barabara hii kwa sababu, mkandarasi tayari tumeshamlipa kwa hiyo. Wakati wowote tunaweza tukaongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kutembelea hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli katika ziara, wakati Mheshimiwa Rais yuko Tanga, alitoa maelekezo barabara hii ijengwe kwa mpango ama mfumo wa *PPP*. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wabunge, Watanzania wa Tanga wa Jimbo la Kilindi na Watanzania kwa jumla kwamba, tayari Serikali ilishaunda timu ambayo inahusisha Wataalam kutoka *TANROADS* na bandari, kwa sababu, pia, wanufaika wakubwa watakuwa ni Bandari yetu ya Tanga kupitisha mizigo ili tuone namna bora tutakavyopata wawekezaji ama mwekezaji, kwa ajili ya kujenga hiyo barabara kwa ubia kwa mpango wa *PPP*. Kwa hiyo, tayari kazi imeshaanza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona, maswali kwa kifupi, moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa, Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Tarafa ya Kibosho wanaishukuru sana Serikali kwa kutoa pesa ya kukamilisha Barabara ya *International School* – Kibosho – *KNCU* hadi kwa Raphael. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha barabara hii inakamilika, kama ilivyo kwenye mkataba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mkandarasi ameshapatikana na tayari ameshaanza kufanya *mobilization*, ili kukamilisha hizo kilomita sita ambazo Mheshimiwa Mbunge anaziulizia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mtiririko wa pesa usioridhisha umesababisha Barabara ya Itoni – Msitu, kilometa 50 nayo kujengwa kwa wakati. Kwa nini Serikali isifikirie kubadilisha utaratibu kwa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ya kawaida badala ya zege, ambayo ni gharama sana na inasababisha barabara hii ichelewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tu nimkumbushe ama nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari mkandarasi tumeshamlipa, tunavyoongea sasa hivi, shilingi bilioni 4.7, ili aweze kuendelea na kazi. Kuhusu kubadilisha usanifu ni kwamba, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, najua anataka tu tubadilishe kwa sababu, anataka barabara ijengwe haraka.

Mheshimiwa Spika, vilevile hii barabara imesanifiwa kwa utaratibu huo tukitambua kwamba, ni barabara ambayo itahudumia na kusafirisha makaa ya mawe na chuma kwa sababu, ndiyo itakayoyatoa kwenye machimbo na kuyaleta kwenye *stockpile* zake ambazo zitakuwa huku Njombe, kwa maana ya Itoni, lakini pia, ni eneo ambalo lina milima na miinuko na *terrain* yake haitaruhusu tujenge kwa barabara hiyo, vinginevyo itakuwa kila wakati inatengenezwa. Kwa hiyo, cha muhimu ni kumsimamia mkandarasi ili akamilishe kwa usanifu wa kiwango cha zege. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kibaoni – Stalike imekuwa ujenzi wake unasuasua na imeharibika sana, wananchi walikuwa wakitumia saa moja kwa sasa wanatumia zaidi ya saa nne mpaka tano. Je, ipi Kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, barabara hii tuna mkandarasi yuko *site* na muda wowote atalipwa, lakini nimwelekeze tu Meneja wa Mkoa wa Katavi kuhakikisha kwa kuwa, mkandarasi yuko *site* ahakikishe kwamba, anatengeneza barabara hiyo, ili iweze kupitika kwa sababu, mkataba unamtaka afanye hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi na nimwandalie mkutano mkubwa jimboni, ili aweze kuwaeleza wananchi wangu ni lini upembuzi yakinifu ama mshauri mwelekezi ataanza kazi, kwa ajili ya Barabara ya Kalumwa – Busisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Niko tayari kwa sababu, kama alivyosema, amekuwa akiulizwa na nadhani tuko mahali pazuri. Kwa hiyo, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenye huo mkutano atakaokuwa ameandaa ilimradi tu muda utaruhusu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Cheleni – Kahe – Mabogini – *TPC* ni ya muhimu sana na kuna mafuriko makubwa kwenye maeneo ya Kahe na Mabogini. Je, ni lini Serikali itamwezesha mkandarasi aliyepo kukamilisha hiyo barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, sijasikia changamoto ya hiyo barabara vizuri.

**SPIKA:** Ni lini itajengwa kwa lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara zote tunatamani tuzijenge kwa kiwango cha lami, ikiweko na hiyo Barabara ya kwenda Kahe. Kama usanifu utakuwa umekamilika maana yake ni maandalizi sasa ya kutafuta fedha, ili tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami hiyo barabara ya Mheshimiwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA SIMON MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ujenzi wa Daraja la Mto Itembe umesimama sasa kwa muda wa miezi sita. Mkandarasi hayuko site kwa sababu, hajalipwa pesa zake. Je, ni lini Serikali itamlipa pesa mkandarasi huyu ili arudi kuendelea na ujenzi wa hilo Daraja la Itembe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Daraja hilo la Itembe ambalo liko karibu zaidi ya 80% kwa ujenzi tumeshapokea haki za madai na tunaandaa hayo madai ya mkandarasi huyo, *TRONIC* ili tuweze kumlipa na aweze kukamilisha hiyo kazi ya Barabara, ambayo inaunganisha Maswa na Singida. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Handeni – Kibirashi, ambayo inapita Kiteto – Chemba mpaka Singida, awali tulikuwa tunajenga kwa *EPC+F* baadaye wakatuondoa, lakini Waziri alikuja na majibu hapa akatuambia kwamba, tuko kwenye mchakato, tuko kwenye makubaliano; leo tena anatuambia kuna timu. Tunataka kujua, timu hiyo ni lini itamaliza kazi, ili barabara hiyo ianze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais utaratibu tuliokuwa nao tumeubadilisha na sasa tunajenga kwa Mfumo wa *PPP*. Kwa hiyo, timu ya wataalam ipo inalifanyia kazi. Ni barabara ndefu, ambayo itakuja na mpango mzuri, kama ni mbia mmoja, wawili au watatu kulingana na itakavyokuwa. Kwa hiyo, tunategemea wataalam watakaokuwa wamefanya hiyo kazi, basi tutawajulisha kwamba, lini itakamilika, lakini hatuwezi kusema ni kesho kwa sababu, ni kazi ambayo hatujawa na utaratibu wa muda mrefu; hatujafanya hizo kazi kwa hiyo, ndiyo kwanza tunaanza kutumia utaratibu huu wa *PPP,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, ni lini mkandarasi wa barabara ya lami kutoka Mlandizi kwenda *Station* ya *SGR,* Ruvu, aliyepatikana atasainishwa mkataba na kukabidhiwa *site* aanze kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara zote zinazokwenda kwenye vituo vya *SGR* ziko kwenye mpango wa kujengwa, ikiwepo hiyo barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, muda si mrefu kwa sababu, alikuwa ameshaomba fedha za awali, kwa maana ya *advance* na muda si mrefu tutamkabidhi, ili aanze hiyo kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 203

**Ujenzi wa Barabara ya *Manyoni East* – Heka – Sanza – Chali Igongo – Bihawana – Dodoma**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kujenga Barabara ya *Manyoni East* – Heka – Sanza – Chali Igongo – Bihawana – Dodoma Mjini kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya *Manyoni East* – Heka – Sanza – Chali – Igongo *(Singida/Dodoma Boarder)* – Kipanga – Kidiho – *Bihawana Junction* yenye urefu wa kilometa 192 yameanza, ambapo taratibu za manunuzi za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinatarajiwa kukamilika

mwezi Julai, 2026. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ujenzi wa hii barabara, katika swali la msingi, unategemea ukamilishwaji wa ujenzi wa Daraja la Sanza. Je, ni lini sasa ujenzi wa Daraja la Sanza utaanza ambapo mkandarasi ameshapatikana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kikao cha Mkoa cha Ushauri *(RCC)* kilipitisha azma ya kuhamisha Barabara ya Kintinku – Makanda – Chemba kwenda Kondoa kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* kwa kupitia barua ya tarehe 25 Februari. Je, ni lini sasa *TANROADS* wataanza kuihudumia hii barabara? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Daraja la Sanza tumeshakamilisha usanifu, ikiwa ni pamoja na *approach roads* zenye kilometa 14 ambazo zote tumeshapata mkandarasi na tunachosubiri sasa hivi ni kusaini, ili mkandarasi aanze hiyo kazi ya kujenga hilo daraja na kuhusu barabara ya kuipandisha hadhi inayotoka Kitiku kwenda Chemba, kama alivyofanya mkutano mwezi Februari, sisi kazi yetu Wizara, ni kupokea na kutuma wataalam kwenda kufanya tathmini kuona kama vigezo vinakidhi, basi hiyo barabara itapandishwa hadhi na kuanza kuhudumiwa na *TANROADS,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Katika nyakati tofauti tofauti Mheshimiwa Waziri amekuwa akilieleza Bunge hapa kwamba, hatua zote za ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba umekamilika, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea kule *site*.

Je, ni ipi kauli, tena yako Mheshimiwa Waziri, lini ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuko kwenye hatua za mwisho kabisa za manunuzi kwa maana tuko kwenye majadiliano na mkandarasi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha kazi hiyo itakuwa imeanza kuanza kilomita tano upande wa Mheshimiwa Condester, Momba na upande wa Mlowo, ambapo kila upande wakandarasi wataanza kazi, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawaona, lakini mnauliza maswali marefu sana, mpaka uanze na historia, Serikali inakuwa inayajua hayo yote. Nenda moja kwa moja kwenye swali, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, ni lini tutakamilisha ujenzi wa Barabara ya Muleba – Nshamba – Kishanda – Buganguzi kipande cha kilomita saba kilichobaki? Ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, huu ni mwezi Mei, kwa hiyo, tunaendelea na kukamilisha hicho kipande na bado hata katika bajeti inayofuata tumeshaipangia iendelee kukamilika, ili kilomita hizo saba ziweze kukamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kujua Wananchi wa Korogwe na Lushoto, Bumbuli, watarajie ni lini ujenzi wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindila – Korogwe utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ilishapata kibali cha kujengwa na tuko kwenye hatua za manunuzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, kwa nyakati tofauti Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba, taratibu za manunuzi za Barabara ya kuanzia Mtakuja kwenda Kakola zimekwishakamilika. Ni lini barabara hiyo inaanza kujengwa? Ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli taratibu zimeshakamilika na hatua ambayo tunaisubiri sasa hivi ni kusaini mkataba na mkandarasi, ambaye tumeshampata. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 204

**Kuvilinda Vyanzo Vinavyotiririsha Maji Bwawa la Julius Nyerere**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha vyanzo vinavyotiririsha maji Bwawa la Nyerere vinahifadhiwa na kuwa endelevu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji, inaendelea na Programu Maalum ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji likiwemo

Bwawa la Julius Nyerere iliyoanza mwaka 2021 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2035. Kupitia Programu hiyo kazi mbalimbali za uhifadhi wa vyanzo vya maji zinatekelezwa, ikiwemo kutambua vyanzo vya maji, kuweka mipaka na kuvitangaza vyanzo hivyo kwenye Gazeti la Serikali. Kupanda miti rafiki ya maji kwenye vyanzo vya maji na kufanya kilimo na ufugaji rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uhifadhi na uendelevu wa vyanzo vinavyotiririsha maji kwenda bwawa la kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Rufiji, jumla ya vyanzo 70 vimetambuliwa na kuwekwa alama za kudumu za mipaka *(Beacons)* katika Bonde la Mto Rufiji. Aidha, Serikali imepanda miti rafiki ya maji 400,000 kandokando ya vyanzo vikuu vya Mto Rufiji, ikiwemo Mito ya Ruaha Mkuu, Ruhudji, Kilombero, Luwegu, Kizigo na Ndembera. Serikali itaendelea kutunza na kulinda Bwawa la Nyerere kwa kushirikiana na wananchi katika maeneo ya hifadhi za vyanzo vya maji, sanjari na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji wa bwawa hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, mifugo ndiyo inachangia zaidi uharibifu wa vyanzo vya maji katika maeneo, ambayo yanazunguka Bwawa la Mwalimu Nyerere. Je, Serikali ina mkakati gani kuweza kudhibiti shughuli hizi, ili Bwawa la Mwalimu Nyerere na vyanzo vyake viendelee kubaki salama na endelevu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kupandisha hadhi maeneo yale ya kimkakati yanayochangia maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere ili maeneo haya yawe ni hifadhi ya Taifa, ili kupunguza zile harakati za kinadamu ambazo zinachangia kuharibu bwawa hili? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru, lakini kubwa, Wizara ya Maji moja ya kipaumbele chake ni suala zima la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji na suala la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji hatuwezi tukasema tutafanya Wizara ya Maji peke yetu. Kwa hiyo, mkakati wa Wizara ni kufanya kazi kwa pamoja na Wizara nyingine mtambuka, ikiwemo Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, mkakati wetu wa pamoja ni kuhakikisha tunatambua vyanzo vya maji, kuweka mipaka ya kuvitangaza vyanzo hivyo katika gazeti la Serikali, kupanda miti rafiki kwenye vyanzo vya maji na kufanya kilimo na ufugaji rafiki wa mazingira. Eneo la pili, tumepokea ushauri, kwa ajili ya utekelezaji katika kuhakikisha kwamba, tunafanya mustakabali wa ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Mpemba na Kata ya Katete zina ongezeko kubwa la watu. Nilitamani kujua ni upi mkakati wa dharura kuhakikisha kata hizi zinapatiwa maji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, japokuwa haliendani na swali la msingi, lakini maadamu wewe ni Waziri wa Maji, basi mjibu Mheshimiwa Mbunge.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu kuu la Serikali ama Wizara ya Maji ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa, tunayo magari ya uchimbaji wa visima, ni jambo yawezekana la dharura, tupo tayari kuhakikisha kwamba, tunasaidia, ili kuhakikisha wananchi hawa wanaweza kupata huduma ya maji safi na salama. Nipo tayari kukutana naye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kwa mvua zinazonyesha Bwawa la Mkomalilo limebomoka lote na jana

Meneja wa *RUWASA* aliendа kuangalia hilo bwawa. Ni lini Serikali itapeleka magari ya kusaidia wananchi kuziba hilo bwawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hili jambo ni la dharura basi nilielekeze kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, timu ya Wizara ifike kwa haraka na kuweza kuchukua hatua ya haraka, ili wananchi hawa waweze kupata huduma hii muhimu ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini kazi ya kusambaza maji yanayotokana na Mradi mkubwa wa Maji Mkoani Arusha wa shilingi bilioni 520 utakamilika, hususani kwenye maeneo mradi unapopita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa Jiji la Arusha tuna mradi mkubwa ambao tumeujenga kwa zaidi ya shilingi bilioni 520 na una uzalishaji mkubwa wa maji, zaidi ya lita milioni 200. Kwa hiyo, mkakati wetu ni kuhakikisha maji yale yanafika katika maeneo mbalimbali, moja ya wilaya ni Wilaya ya Monduli. Ninataka nimhakikishie, wakandarasi wapo *site,* jukumu letu, kama Wizara, ni kuhakikisha kwamba, tunawasimamia, tunawafuatilia, kazi hizi zikamilike kwa wakati, ili wananchi hawa waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Wilaya ya Bukombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge. Ukiangalia kuna baadhi ya maeneo wamekuwa na changamoto kubwa sana hasa maji yaliyokuwa

chini ya ardhi, mojawapo ni Wilaya hii ya Bukombe. Nimefika na mkakati wa Wizara na hata katika Bajeti yetu tutaipa kipaumbele kuhakikisha maji yale yanatoka Ziwa Victoria, yanafika Bukombe mpaka Wilaya ya Mbogwe ili kuhakikisha kuwa wanatumia maji ya Ziwa Victoria na kwamba wawe na chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge Ulyankulu swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

Na. 205

**Wananchi wa Kata ya Ulyankulu Kuanza Kutumia Sheria Na. 7**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA K.n.y. MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, lini wananchi wa Kata za Milambo, Kanindo na Igombemkulu wataanza kutumia Sheria Na. 7 ya TAMISEMI badala ya Sheria Na. 9 ya Wakimbizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Milambo, Kanindo na Igombemkulu kuna makundi matatu ya wakazi yenye hadhi tofauti ambayo ni raia wazawa, raia tajnisi na wakimbizi kutoka nchi ya Burundi. Ikumbukwe kuwa, eneo la Ulyankulu lilitengwa na kuanzishwa mahususi kwa ajili ya shughuli za kuhifadhi wakimbizi, na sehemu kubwa ya watu wanaoishi humo kwa sasa ni raia tajnisi ambao wanatokana na kundi la wakimbizi wanaotoka nchi ya Burundi walioingia Tanzania tangu mwaka 1972 na baadaye kupewa uraia wa Tanzania kama suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kutafuta suluhisho la kudumu kwa wakimbizi wanaoishi katika eneo hilo pamoja na hatma ya eneo hilo la Ulyankulu kwa ujumla. Tunawaomba wakazi wa eneo hilo kuendelea kuwa na subira na uvumilivu wakati Serikali ikiwa inaendelea kukamilisha mchakato wa kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi waliosalia pamoja na hatima ya kudumu la eneo hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, kwa majibu haya mazuri, kwanza ninaipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyochukulia mambo yale ya wakimbizi. Kwa majibu mazuri haya ya Serikali sina swali la nyongeza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Sylivia Sigula.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Lucy Sabu…

**SPIKA:** Hebu ngoja, Mheshimiwa Sylivia naona kuna Mheshimiwa Esther Midimu alisimama hapa nani kati yenu ana majibu ya hilo swali?

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, mimi hapa.

**SPIKA:** Wewe ndiye una majibu?

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa swali Namba 206 la Mheshimiwa Lucy Sabu lipatiwe majibu.

Na. 206

**Mikopo Nafuu na Mafunzo kwa Vijana Wafugaji na Wavuvi**

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. LUCY J. SABU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa mikopo nafuu na mafunzo ya kisasa kwa vijana wanaojihusisha na ufugaji na uvuvi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Mnyeti majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imetoa mafunzo kwa vijana 2,078 wanaojishughulisha na unenepeshaji wa ng'ombe, uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imetoa mafunzo kwa wafugaji 47,183 wakiwemo vijana 34,215.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imewezesha jumla ya vijana 106 kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* yenye jumla ya shilingi milioni 934,231,000. Aidha, vijana hao wamepatiwa jumla ya ekari 1,060 kwa ajili ya unenepeshaji wa ng'ombe katika Ranchi ya Kagoma iliyopo Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi 7,000,000,000 kimepangwa kwa ajili ya kuwezesha vijana 200 kupata mikopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylivia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali, lakini bado wavuvi wa Mkoa wa Rukwa wameachwa nyuma sana, hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wavuvi wa Wilaya ya Kalambo Kasanga walipatiwa mikopo ambayo haina tija. Wao walihitaji vifaa vya kuvulia lakini mikopo waliyopewa ni vifaa vya kutafutia

Samaki. Je, Serikali iko tayari kupitia upya ili kuona mikopo ile inaleta tija?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa akituambia hapa Bungeni, kwamba vijana na wavuvi waombe vizimba kwa sababu vipo, lakini Mkoa wa Rukwa una vizimba visivyopungua vinne tu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kufanya ziara kwenye Mkoa wa Rukwa ili kwenda kuwaeleza wavuvi kuhusu upatikanaji wa vizimba hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nianze na hili la kwanza la aina ya mkopo tunaotoa Wizarani. Ukweli ni kwamba, mikopo hii haina riba na mikopo hii ni makubaliano kati ya Benki ya *TADB* na mvuvi mwenyewe. Sasa mvuvi anasema shida yake ni nini. Kama shida yake ni boti tunampa boti, kama shida yake ni nyavu tunampa nyavu, kama shida yake ni *fish finder* tunampa *fish finder.* Sasa kama anataka vyote pia tunampa vyote. Yawezekana hawa wavuvi walitaka *fish finder* tukawapa *fish finder;* wakitaka nyavu tunawapa vyavu, inategemea na mvuvi ana shida gani kulingana na mahitaji yake katika eneo hilo analotaka kuvua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuko tayari kufanya mazungumzo na hao wavuvi watuambie wanataka nini zaidi ya kile tulichowapa na Serikali iko tayari kuwapatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwa kweli nimelipokea kwa mikono miwili, niko tayari kuongozana tukazunguke kwenye mkoa wake, tukafanye kazi ya wananchi. Mimi ni nani nikatae kuongozana na Mheshimiwa Mbunge Sylivia kwa kweli niko tayari kufanya kazi hiyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake.

Na. 207

**Uvamizi wa Tembo Vijiji Vinavyopakana na Pori la Swagaswaga – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya uvamizi wa tembo mashamba ya vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Swagaswaga Wilaya ya Chemba – Magungu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dustan Kitandula majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kufanya doria za mwitikio wa haraka. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya matukio 15 yaliripotiwa, ambapo doria zenye siku 123 zimefanyika katika maeneo yanayopakana na pori hilo ikiwemo Kijiji cha Magungu Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali imekamilisha kuchimba bwawa lenye ujazo wa lita za maji 20,750,000 katika Pori la Akiba Swagaswaga ili kuwezesha wanyamapori kupata maji ndani ya hifadhi na kupunguza uwezekano wa wanyamapori kwenda kutafuta maji katika maeneo ya wananchi. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ikiwemo ndege nyuki *(drone)* na mabomu baridi katika kukabiliana na changamoto ya tembo kwenye eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza;

usiku wa leo tembo wameharibu hekari 22 kwenye Kijiji cha Magu lakini juzi wameharibu hekari 84 kwenye Kijiji cha Itwalo. Ni wazi mkakati wa Serikali wa doria umefeli. Ninaomba kujua ni mkakati upi sasa ambao unaweza kuwasaidia wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali imekuwa ikitoa kifuta jasho kwa ajili ya wananchi ambao mazao yao yanaharibiwa. Ni ukweli kifuta jasho ni hisani. Je, ni lini itaanza kulipa fidia kwa wale watu ambao wameharibiwa mazao yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna changamoto ya Tembo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na changamoto hii ni kubwa. Tunakabiliwa na changamoto hii kwa sababu; moja, tembo wanatoka katika hifadhi na kuja kwenye maeneo ya watu kwa sababu ya shughuli za kibanadamu katika maeneo ya hifadhi; pili wananchi wamesogea karibu sana na hifadhi kwenye maeneo wanayoishi; na tatu, tumefanya kazi kubwa ya kudhibiti majangili kwa hiyo Tembo wameongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali inafanya mikakati, kwanza tunafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa tunawatoa watu ambao wameingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi. Pili, tunafanya kazi kubwa ya kuchimba mabwawa ndani ya hifadhi ili tembo wale wasitoke kwenye hifadhi na kuja kwenye maeneo ya wananchi. Hivi karibuni tumekamilisha uchimbaji wa bwawa ndani ya Hifadhi ya Swagaswaga kule, jambo ambalo nina uhakika litasaidia sana kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kwamba, maafisa wanyapori wa halmashauri zetu walioko kule kwenye maeneo yale wawe wanatoa taarifa kwa haraka kwa Wizara ili tuweze kuchukua tahadhari na hatua za haraka za kuwadhibiti wanyamapori hawa. Tuna ndege nyuki sasa ambazo tunazitumia kwenda

kufukuza tembo hao. Tunapopata taarifa kwa haraka njia hii imeonekana inasaidia sana kufukuza tembo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hili la pili la kifuta jasho. Wizara ya Maliasili na Utalii imejitahidi sana kulipa kifuta jasho na kifuta machozi. Kwa Wilaya hii ya Chemba tayari tumekamilisha kazi ya uhakiki wa madai tunayodaiwa kwenye wilaya hii. Tayari tunajua kwamba tunadaiwa takriban milioni 14 ambazo ndani ya kipindi kifupi kijacho wananchi wale watalipwa. Ninaomba wananchi wawe na subira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 208

**Kuimarisha Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji Hifadhini**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa watalii kwenye maeneo ya hifadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji wa watalii inaboreshwa ipasavyo kwenye maeneo ya hifadhi za Taifa hapa nchini, Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* imeandaa mikakati ya muda mfupi na ya muda mrefu ili kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inapitika wakati wote wa mwaka. Miundombinu hii ni pamoja na barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Mathalani, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara kupitia TANAPA inakusudia shilingi bilioni 23.18 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 2,381.7 na vivuko 69 katika hifadhi mbalimbali za Taifa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na kutengwa kiasi cha bilioni 23.18 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Je, ni hifadhi gani mahususi ambazo fedha hizo zitaenda kuifanya kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mvua kubwa imekuwa ikiathiri sana miundombinu ya Barabara. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapitika kwa mwaka na pia kutafuta teknolojia mbadala ya kutengeneza barabara hizi za hifadhini ili zisiathiri ekolojia pia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba tunakusudia kutumia bilioni 23 na fedha hizi zinakwenda kwenye takriban hifadhi zetu zote. Kwa uchache niseme, hifadhi za Serengeti, Kilimanjaro, Tarangire, Manyara, Arusha na kwingineko zitafaidika na matengenezo hayo tunayoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala lake la pili la kuharibika kwa miundombinu, na kwamba ipo haja ya kuzitengeneza kwa teknolojia ambayo ni rafiki; tayari Serikali iliweka kwenye mpango kwa kutengeneza barabara hizi. Kwa kuanzia tunaanza na Barabara ile ya kutoka Ngorongoro mpaka Golini ambayo ni kilometa 88. Tumekusudia kujenga kilometa 29 kwa gharama ya bilioni 67, lakini kwa kuanzia tunaanza na kilometa 29 kutoka Luduale mpaka Seneto. Tunalishukuru Bunge mwaka huu wa fedha walitutengea bilioni nane. Tunaamini kwamba kazi hii ndani ya kipindi kifupii kijacho itaanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunakusudia kwenye upande wa Serengeti tunagawa barabara zile katika mafungu manne ambako na kwenyewe tunaanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili barabara zile nazo ziweze kujengwa kwa kiwango cha baka gumu. Tayari takriban *Euro 500* zimetengwa kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na Subira, jambo hili linaenda kutekelezeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 209

**Kuimarisha Sekta ya Sanaa, Michezo na Burudani**

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha sekta ya sanaa, michezo na burudani kuwa chanzo cha ajira kwa vijana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwinjuma majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa sekta ya sanaa, michezo na burudani katika utoaji wa ajira kwa vijana hapa nchini. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewekeza katika miundombinu, matukio ya kitaifa na kimataifa na programu mbalimbali za kukuza vipaji, jambo lililochangia kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hatua tulizochukua ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja mbalimbali vya michezo hapa nchini, uratibu na utekelezaji wa matukio mbalimbali kama vile sanaa mtaa kwa mtaa, tuzo za muziki, tuzo za filamu, tuzo za wacheshi, tamasha la muziki wa dansi na *Samia Serengeti Music Festival.* Vile vile Serikali kwa kushirikiana na

wadau huendesha mafunzo, warsha na makongamano ili kuongeza ubora na ushindani katika sekta hizi. Hatua hizi zinachochea ukuaji wa ajira za muda mfupi na mrefu kwa vijana. Kwa njia hizi sekta hizi zinaendelea kuwa chanzo thabiti cha ajira na maendeleo kwa vijana nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira Khatib, swali la nyongeza.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sera yetu haijashirikisha sekta binafsi kwa eneo kubwa. Je, Serikali ipo tayari kurekebisha Sera ya Michezo hususan kupitia wawekezaji kwa eneo la michezo, sanaa na burudani ili vijana wengi waweze kupata ajira?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 imetaja mambo ya michezo kama masuala mtambuka na imebainisha ushiriki wa sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali ili kujaribu kuleta maendeleo ya michezo nchini. Hata hivyo, sera hiyo sasa hivi iko katika marekebisho makubwa na miongoni mwa mambo ambayo tunakwenda kuyarekebisha ni kuongeza ushiriki na kutambulika kwa sekta binafsi na wawekezaji wake katika kuleta maendeleo ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, unaweza kuona ushahidi kwa jinsi ambavyo sekta binafsi imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa wenye mafanikio katika miaka ya hivi karibuni kwenye masuala ya michezo; na huo ushahidi unaonekana kwenye uwekezaji uliofanywa na makampuni kama *Azam, GSM, EMTL, Sport Pesa, M-BET* na kadhalika. Hata hivyo, kama ambavyo nimetangulia kusema, marekebisho ambayo yanafanyika sasa hivi kwenye sera ya maendeleo ya michezo ya mwaka 1995 yataongeza wigo wa kutambulika kwa sekta binafsi kwenye kuwekeza kwenye masuala ya michezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Suala la dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Tangazo la Wageni walioko hapa Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni 28 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini; wapo Mhandisi Yahya Samamba ambaye ni Katibu Mkuu; Ndugu Msafiri Mbibo, Naibu Katibu Mkuu; *IGP* Mstafu Balozi Simon Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo pia ndugu Yokbeth Myumbilwa, Mwenyekiti wa Bodi, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania; Mhandisi Theonestina Mwasha, Kamishna wa Tume ya Madini; Dkt. Abdulrahaman Mwanga, Kamishna wa Madini; Mhandisi Ramadhani Lwamo, Katibu Mtendaji Tume ya Madini; Dkt. Venance Mwasse, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)*. *(Makofi)*

Wengine ni ndugu Mariam Mgaya, Katibu Mtendaji Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; Dkt. Mussa Budeba, Mtendaji Mkuu Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania; Mhandisi Ally Maganga, Mratibu Kituo cha Jiolojia Tanzania; ndugu John Bina, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania. *(Makofi)*

Wapo ndugu Zaituni Mtawa, mdau wa Sekta ya Madini; Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Mheshimiwa Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma; Dkt. Fredrick Sagamiko, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma; Profesa Davis Mwamfupe, Meya wa Jiji la Dodoma; Alhaj Dkt. Mustafa Shabani, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; *Father* Raphael Maligite,

Mwakilishi Baraza la Maaskofu Tanzania, Jimbo Mkuu Katoliki la Dodoma; na Alhaj Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anatropia na mwenzako hebu tulieni kidogo, nimesimama.

Wapo vilevile, ndugu Charles Mamba, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma; ndugu Neema Majule, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma; ndugu Jafar Mwanyemba, Mjumbe wa Baraza Kuu la Wazazi CCM Taifa; na ndugu Abdulhabib Mwanyemba. Ahaa! Haya majina yapo sawa? Haya, Mwenyekiti UVCCM Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, hebu nirekebishie haya majina kama yako sawa, ama yako sawasawa? ahaa! Haya Ndugu Pili Mbanga, Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma; ndugu Sofia Kibaba, Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma; na ndugu Aman Mulagizi, Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mavunde, wanafunzi 116 na walimu 10 wa Shule ya Msingi ya Feza kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 125 wa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, hawa ni wapigakura wake kutoka Isimani, Mkoani Iringa.

Waheshimiwa Wabunge, hapo kuna Wenezi wa Matawi wa Chama Cha Mapinduzi Isimani; kuna Makatibu Wenezi wa Matawi; na kaka yake huyu anaitwa *Mr. Chota* kutoka Idodi. Pia wapo wasaidizi wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Isimani, karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Wafanyabiashara kutoka Karagwe Mkoani Kagera wakiongozwa na Johnbosco Selestine, ambaye baba mdogo wa Mheshimiwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hawa ni familia ya *Together Forever* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Kata ya Isangala Mkoani Mbeya, huyu ni ndugu Gabriel Kilembe. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli ambaye ni Ndugu Adelina Ikonje, huyu ni Mkurugenzi Shirika lisilo la Kiserikali la *Soul and Mind Youth Counseling*. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ambaye ni Ndugu Jackson Ashery, mpigakura wake kutoka Muhambwe. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jonas Mbunda, Menejimenti ya Kiwanda cha Kukoboa Kahawa kutoka Mbinga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni Makada watiifu wa CCM kutoka Moshi Mjini. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, wapigakura wake kutoka Mwanga Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda kutoka kwenye Asasi isiyo ya Kiserikali ya Rungwe Yetu ya Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Sasa nina wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; yupo ndugu Jeremia Andrea ambaye ni Mwananchi kutoka Mkoani Dodoma; Ndugu Godfrey Zakaria Mwananchi kutoka Mkoani Dodoma; na wafanyakazi watatu wa *Ijenga Petrol Station* ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice.

**JAMBO LA DHARURA**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninasimama kwa Kanuni ya Na. 54, jana ilikuwa Siku ya Wafanyakazi Duniani ambayo kwa Tanzania, Kitaifa imefanyika Mkoa wa Singida na mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kama kuna kilio kikubwa kwa Watanzania hasa watumishi kwa zaidi ya miaka tisa ilikuwa ni suala zima la kupanda mishahara kulingana na maisha yanavyopanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengi ambayo anayo Mheshimiwa Rais anatekeleza miradi mbalimbali, ametoa bilioni kwenye mikoa na halmashauri zetu, lakini kumbuka huu ni mwaka wa uchaguzi una mambo mengi angeweza kutoa *excuse*. Kwa miaka tisa mishahara haijapanda, lakini jana Rais msikivu na mthubutu anayetambua michango ya wafanyakazi ambayo huwa *income tax* inaenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Taifa, amethubutu kupandisha mishahara kima cha chini kutoka 370,000 mpaka 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wabunge wenzangu ambao wamekuwa wachangiaji wakubwa kwenye suala hili. Waniunge mkono kwenye pongezi hii ni dharura ya kipongezi, Bunge limpongeze Mheshimiwa Rais. Uamue mwenyewe utatuongozaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana tuketi. Waheshimiwa Wabunge, tuketi ahsante sana.

Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa Kanuni ya 76 mapema leo asubuhi wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, Patrobass Katambi akijibu swali Na. 196 alieleza kwamba ile mikoa ambayo watu wengi zaidi wanapata ajira za Serikali, ni kwa sababu mikoa ile ina mwamko mkubwa zaidi wa elimu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kutambua kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya katika uwekezaji wa sekta ya elimu hakuna mkoa ambao umeachwa nyuma katika maendeleo ya elimu. Kwa hivyo, ningependa kufahamu je, kauli ile ni sawa kwamba mikoa ambayo haipati watu wengi kwenye ajira za Serikali kwamba ni kwa sababu mikoa hiyo ina mwamko wa chini wa elimu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage amesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 54 akieleza jambo la dharura na amesema hiyo ni dharura, lakini ni dharura ya kipongezi. Kwa hivyo, kwa sababu kanuni zetu zinatoa fursa ya Bunge kutoa pongezi na linatoa fursa kwa Spika kuzungumza kwa niaba ya Bunge kwa upande huo wa pongezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kwa sababu sisi ndio wawakilishi wao, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua aliyoichukua siku ya jana (Siku ya Mei Mosi). Kuhakikisha kwamba anawapandishia mishahara Watumishi wa Serikali ambao wanapata kima cha chini na alitoa ahadi kwa ajili ya watu ambao hawapati mshahara wa kima cha chini kwamba na wao watapata asilimia zao kwa kadiri muda unavyokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, sote kwa pamoja kama Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Taifa hili. Tunaamini kwamba na waajiri binafsi sasa na wao wataendelea kuangalia mwongozo huu uliotolewa na Mheshimiwa Rais kuona namna ambavyo wanaweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika maeneo yao pia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo pongezi zimetolewa kwa niaba ya yenu wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia amesimama Mheshimiwa Neema Lugangira. Akiomba Mwongozo kwa mujibu wa kanuni yetu ya 76 akitaka kujua kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi, kutokana na majibu ambayo alikuwa ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi kwa swali alilokuwa ameliuliza Mheshimiwa Dkt. Rweikiza kwamba mikoa mingine inakuwa haipati mgao sawa kwenye ajira zinapotolewa na Serikali.

Sasa Mheshimiwa Neema anaona kwamba hapo kidogo kauli ile ya kusema mikoa mingine pengine mwamko uko chini ya elimu haoni kama hilo jibu liko sawasawa. Sasa kwa sababu sikumbuki vizuri namna alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu jibu hili inabidi nikapitie Taarifa Rasmi za Bunge kisha nitatoa mwongozo Mheshimiwa Neema Lugangira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, aje awasilishe hotuba ya bajeti ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Madini, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba hotuba yangu yenye kurasa 131 ingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa kwenye Ofisi za Bunge. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii adhimu kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, wenye weledi, maono mapana na dhamira thabiti ya kuwaletea Watanzania maendeleo jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwapongeza dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za urais kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kua Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu, pamoja na Watanzania wote kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali juu katika sekta ya madini. Katika kipindi hicho tumeshuhudia kuendelea kuimarika kwa mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa na kukua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021, asilimia 9.1 mwaka 2023 na kufikia 10.1% mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa shughuli za uchimbaji madini imeongezeka kutoka 10.8% mwaka 2022 hadi 11.3% mwaka 2023. Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali uliongezeka kutoka shilingi bilioni 623.2 mwaka 2021/2022 na shilingi bilioni 678 kwa mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 753.2 kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, vituo vya ununuzi wa madini vimeongezeka kutoka 102 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia 109 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ununuzi wa mitambo 10 ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuanza kwa Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Chumvi katika Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na hatua za uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati ambapo Serikali imetoa leseni ya uchimbaji mkubwa wa Madini ya Kinywe kwa Kampuni *ya Duma Tanza Graphite Limited* katika Wilaya ya Mahenge, Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kutoka na maelekezo na miongozo yenye tija kutoka kwa Mheshimiwa Rais katika kusimamia sekta na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM. Sekta ya madini imefanikiwa kuvuka lengo la kuchangia 10.1% kwenye pato la Taifa mwaka mmoja kwa ya muda ulioainishwa kwenye Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na kufikia mchango wa 10.1% kwa mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Spika, Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake mbalimbali anayoitoa yenye lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa na mchango endelevu katika kuwanuifaisha Watanzania na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao madhubuti na maelekezo wanayoyatoa mara kwa mara ili kufanikisha utendaji kazi Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa dhati wewe mwenyewe kwa uongozi wako mahiri ambao umeendelea kulifanya Bunge hili kuwa chombo madhubuti umeendelea kuonesha ustadi, hekima, busara, ubunifu na uwajibikaji katika kuliongoza Bunge hili kwa weledi na uaminifu mkubwa. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika; na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaaomba niwapongeze sana Mwenyekiti, Dkt. David Mathayo David, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuendelea kuiongoza Kamati kwa umahiri mkubwa. Aidha, ninawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kwa ufanisi na kutoa maelekezo yenye tija kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri wote kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Muungano wa Tanzania katika kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa heshima kubwa nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa imani yao na ushirikiano wanaouonesha kwangu kama Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Mhandisi Yahya Ismail Samamba, Katibu Mkuu, kwa kusimamia utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nampongeza Bwana Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Abdulrahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini kwa kazi zao na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji mzuri wa kazi, katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishukuru kwa dhati familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Kigamboni kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile. Mwenyezi Mungu amrehemu na awape faraja familia na wananchi aliokuwa akiwaongoza.

Mheshimiwa Spika, aidha, kufuatia majanga mbalimbali zikiwemo mvua zilizosababisha madhara katika baadhi ya maeneo ya nchi na ajali za barabarani. Ninaomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote kwa ujumla kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, ninaomba nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba yangu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, bei ya Madini ya Dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 2,655 ikilinganishwa na bei ya wastani wa dola za Marekani 2,078 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo hapa duniani kama njia ya kuhifadhi thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, mwenendo wa biashara ya Madini ya Almasi duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto zinazosababishwa na mdororo wa uchumi wa dunia; uwepo wa almasi zinazotengenezwa kwenye maabara *(Lab-Grown Diamonds)* na kupungua kwa uhitaji katika masoko makubwa yakiwemo ya China na Marekani.

Mheshimiwa Spika, aidha, bei ya madini hayo imeshuka kutoka wastani wa Dola za Marekani 206 kwa karati Mwaka wa Fedha2023/2024 hadi kufikia Dola za Marekani 168 kwa karati katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 sawa na upungufu wa 18%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; mapato. Mwaka wa fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 231.98 kwa Wizara ya Madini. Kati ya bajeti hiyo, shilingi bilioni 91.32 ni bajeti ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 66.45 za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 24.87 mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, shilingi bilioni 140 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya marejeo ya bajeti yaliyofanyika, fedha za maendeleo ziliongezwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 299 na kufanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni 531. Aidha, kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, katika mwaka 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.16. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni moja zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi

bilioni164 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 62 sawa na 68% kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 47.82 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 14 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 329 zilipokelewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele:

(a) Mheshimiwa Spika, Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilikusanya na kuwasilisha Hazina maduhuli ya shilingi bilioni 783 sawa na 78% ya lengo la makusanyo kwa mwaka. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara kukusanya na kutumia shilingi bilioni 66 kwa kipindi rejea.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali ya thamani ya shilingi bilioni 17.756. Aidha, madini yaliyokamatwa yalitaifishwa na wahusika 75 walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, Kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati. Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika madini muhimu na mkakati ambapo katika kipindi husika leseni ya uchimbaji wa Madini ya Kinywe imetolewa kwa Kampuni ya *Duma Tanz Graphite Limited* katika eneo la Epanko, Wilaya ya Ulanga. Aidha, leseni nyingine zilizotolewa ni pamoja na leseni 58 za utafiti, leseni 278 za uchimbaji mdogo, leseni tatu za uchimbaji wa kati na leseni tatu za uchenjuaji.

(c) Mheshimiwa Spika, Kuhamasisha Uwekezaji, Uanzishwaji wa Minada, Maonesho ya Madini ya Vito na uongezaji thamani Madini; Wizara ya Madini ilifanya mnada wa kwanza wa madini ya vito ndani ya nchi tarehe 14 Desemba, 2024 na mnada wa pili tarehe 8 Aprili, 2025 katika Mkoa wa Kimadini wa Mirerani.

Mheshimiwa Spika, katika minada hiyo, jumla ya wanunuzi 47 walipatikana kama washindi wa mnada na kufanikiwa kununua madini yenye thamani ya shilingi bilioni 1.14 na kuwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi milioni 80 ikijumuisha mrabaha, ada ya ukaguzi na ada ya usimamizi wa mnada.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kupitia Tume ya Madini inategemea kufanya minada na maonesho ya kitaifa katika Mikoa ya Kimadini ya Arusha, Mirerani, Mahenge, Ruvuma na Tanga. Vilevile, maonesho ya kimataifa yanatarajiwa kufanyika Zanzibar na katika Miji ya Dar es Salaam na Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa Umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi, kwenye vyombo vya habari na kwenye mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa; ikiwemo Mikutano ya Kimataifa ya Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika *JNICC* Dar es Salaam ambao uliandaliwa kwa mafanikio makubwa kwa kushirikiana na *Tanzania Chamber of Mines,* ambao wamekuwa ni wadau wakubwa muhimu katika kuendeleza Sekta ya Madini Nchini.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) za Mwaka 2020 zimeendelea kusimamiwa ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni ya kusafisha madini ya dhahabu kwa kampuni ya *Giant Machine and Equipment Limited.*

(d) Mheshimiwa Spika, Kuendelea Kufanya Utafiti wa kina wa Jiofizikia kwa Njia ya Kurusha Ndege *(High-resolution Airborne Geophysical Survey)*. Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa kurusha ndege za utafiti wa madini

kwa njia ya *high-resolution airborne geophysical survey* kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hili, Wizara imefanya majaribio kwa kurusha ndege nyuki katika maeneo ya Mkoa wa Dodoma, Shinyanga, Geita, Lindi na Mkoa wa Kimadini Mererani. Hatua hii ililenga kuthibitisha ufanisi wa matumizi ya ndege nyuki katika utafutaji wa kina wa madini.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo umebainisha uwezekano wa kutumia ndege nyuki kwenye utafutaji wa madini kwa maeneo ya wachimbaji wadogo. Hatua hii itawasaidia wachimbaji wadogo kutumia gharama ndogo kuwezesha kufanya utafiti na kuepusha kufanya uchimbaji wa kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *GST* inaendelea na hatua mbalimbali kwa kushirikiana na Wakala wa Ndege za Serikali, ili kuwezesha ununuzi na upatikanaji wa Helikopta ambayo itatumika katika mradi mkubwa wa utafiti wa madini nchini, kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa utafiti wa kina wa Jiofizikia. Hatua hii itasaidia sana kukusanya taarifa nyingi za kina kwa wakati na kuwezesha taarifa hizo kukuza uwekezaji katika Sekta ya Madini; kama vile, kurahisisha utafutaji kama vile uchorongaji mahali sahihi na hatimaye kupelekea uanzishwaji wa migodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa hizi zitatumika kuwapanga wachimbaji kulingana na aina ya madini katika maeneo yenye rasilimali madini, ili kupunguza upotevu wa mitaji yao.

(e) Mheshimiwa Spika, Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na kuwasogezea Huduma za Ugani. Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* limetoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 471 kupitia vituo vya mfano vya Katente, Lwamgasa na Itumbi ambapo mpaka sasa wachimbaji wa madini 12 wameanzisha vituo vyao baada ya kujifunza kupitia vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia vituo vya mfano, huduma ya uchenjuaji mbale za dhahabu kwa wateja 41 ilitolewa

ambapo dhahabu ya uzito wa kilogramu 119.57 yenye thamani ya shilingi bilioni 23 ilichenjuliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuanzisha vikundi katika shughuli za madini na kutunza kumbukumbu za uzalishaji biashara za madini ikiwa ni miongoni mwa vigezo vya kuwawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya shilingi bilioni 51.42 zilikopeshwa kwa wachimbaji wadogo 127. Natumia fursa hii kuzishukuru Benki za *NMB, NBC, CRDB,* Azania na *KCB* kwa kukubali kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo, niwaombe waendelee kupanua wigo wa ukopeshaji. Nitoe rai kwa taasisi za fedha nyingine, zione umuhimu wa kuwakopesha wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa tija.

(f) Mheshimiwa Spika, Kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini, ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi; Wizara imewezesha Tume ya Madini magari 34 kwa ajili ya ukusanyaji wa maduhuli na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ambao umefikia 92%. *STAMICO* imewezeshwa kununua mitambo miwili ya uzalishaji wa nishati mbadala *(Rafiki Briquettes)* ambayo imesimikwa Kisarawe - Pwani na Kiwira - Songwe pamoja na mitambo 10 ya uchorongaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo; *GST* imewezeshwa na Kituo cha *TGC* kimewezeshwa kuboresha miundombinu ya kufundishia, kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maeneo mengine kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025:

(a) Mheshimiwa Spika, *Mining Vision 2030:* Madini ni Maisha na Utajiri; Wizara ya Madini inaendelea na utekelezaji wa *Mining Vision 2030:* Madini ni Maisha na Utajiri inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti

wa rasilimali madini, ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa;

Mheshimiwa Spika, kuboresha maisha ya Watanzania; na kutoa fursa kwa Mtanzania yeyote wakiwemo akinamama, vijana na wenye mahitaji maalum kujiongezea kipato na hatimaye kutajirika kupitia shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hili, mambo yafuatayo yamezingatiwa ikiwa ni maeneo makuu yanayounda misingi ya maono hayo ni: upatikanaji wa taarifa za jiosayansi hususan taarifa za kina za jiofizikia *(High Resolution Geophysical Survey)* kutoka 16% ya sasa hadi kufikia angalau 50% ifikapo mwaka 2030; kuboresha mfumo wa kisheria na kitaasisi ili kuwa na usimamizi makini na ulio wazi wa Sekta ya Madini; na kuiwezesha Sekta ya Madini kufungamana na sekta nyingine za kiuchumi hususan Sekta za Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Fedha na nyingine zinazotoa huduma kwenye Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayozingatiwa katika *Mining Vision* 2030 ni pamoja na kuboresha shughuli za wachimbaji wadogo hususan urasimishaji wa shughuli zao, kuwezesha upatikanaji wa teknolojia za kisasa na rahisi, masoko ya madini na upatikanaji wa mitaji; na usimamizi thabiti wa shughuli za utunzaji mazingira kwa kushirikiana na Taasisi nyingine, ili shughuli za madini zisiwe na athari hasi kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha *Mining Vision* 2030 inafikiwa, Wizara kupitia *STAMICO* imeendelea kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo kwa kununua mitambo 10 ya uchorongaji. Mitambo hiyo itachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa za kina za jiosayansi hususan kuthibitisha uwepo wa madini mbalimbali katika maeneo yanayomilikiwa na wachimbaji wadogo.

(b) Mheshimiwa Spika, Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow – MBT;* Wizara ya Madini imekamilisha maandalizi ya Programu ya *MBT* ambayo itatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Mwaka 2025 hadi 2030.

Mheshimiwa Spika, programu hii ni ya kimageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kushughulikia changamoto na kuboresha fursa kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum ili kuongeza ushiriki wa makundi hayo katika mnyororo wa thamani wa madini.

(c) Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania; Wizara ya Madini ipo katika hatua za mwisho kukamilisha uandishi wa Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la mkakati huu ni kuwa na maendeleo endelevu ya rasilimali madini muhimu na madini mkakati, ili madini hayo yaweze kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa, pia kuboresha maisha ya Watanzania na kuchangia katika Agenda ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu Uchumi wa Kijani na kidijiti.

(d) Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Sheria; Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini, Sura 123 na kuhakikisha taratibu zote zinazingatiwa kwa ustawi wa Sekta ya Madini nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kufanya marekebisho ya mifumo ya kisheria ya usimamizi wa Sekta ya Madini pale inapoonekana kuna umuhimu ili kurahisisha usimamizi wa Sheria ya Madini na kuendelea kuweka mazingira wezeshi na bora ya uwekezaji katika sekta.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeleta utulivu mkubwa kwenye sekta na kuwezesha Wizara na Serikali kufikia malengo ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2025 Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwenye Kifungu cha 88 kwa kuongeza kifungu kipya cha 88A, ili kuweka jukumu kwa taasisi za umma zenye kandarasi za ujenzi kuzuia au kukata malipo ya mrabaha na ada za ukaguzi kutoka kwenye fedha zinazolipwa kwa kampuni za ujenzi zinazotumia madini ujenzi na kuziwasilisha

Tume ya Madini ndani ya siku saba tangu siku ya kukusanya mrabaha husika na ada ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na matumizi ya madini katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya marekebisho kwenye Kanuni za Masoko ya Madini ya mwaka 2019, ili kurejesha minada na maonesho ya kimataifa ya madini nchini. Kanuni tajwa zimefanyiwa marekebisho katika Jedwali la Kanuni hii kuruhusu madini ya vito yanayouzwa katika minada au maonesho ya madini kusafirishwa nje ya nchi kwa kulipa kiwango kikubwa cha mrabaha wa 15%.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuvutia wanunuzi wa madini kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye minada, ili kununua madini kwa bei shindani na kuwezesha bei ya madini hususan *Tanzanite* kuendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha utungwaji wa Kanuni Mpya za Madini (Msaada wa Kiufundi kwa Wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini) za mwaka 2025. Kanuni hizi mpya zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na. 260 la tarehe 25 Aprili, 2025 zinatoa fursa kwa mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini kuingia mkataba wa msaada wa kiufundi na mwezeshaji kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 8(3) cha Sheria ya Madini, Sura 123.

Mheshimiwa Spika, kanuni hizi zinaweka misingi, utaratibu na mazingira wezeshi ya wamiliki wa *PML* kuingia mikataba yenye tija. Kwa lengo la kuhakikisha kuwa wamiliki wa leseni hizo wanapata teknolojia ya kisasa ya uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji madini.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itarahisisha shughuli za uchimbaji madini hapa nchini. Kupitia mikataba hiyo, itawawezesha wachimbaji wengi kukua kiuchumi na hatimaye

kuendesha migodi yao kwa uchimbaji bora unaotunza mazingira na kukuza matumizi ya teknolojia na utaalamu bora.

Mheshimiwa Spika, kwa wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini *(PML)* ambao watataka kunufaika na msaada wa kiufundi kutoka kwa wawezeshaji, wanashauriwa wachimbe wenyewe badala ya kuingiza wachimbaji wadogo ndani ya maeneo ya leseni. Ili wakipata msaada wa kiufundi iwe rahisi kwao kufanya makubaliano na wawezeshaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna mchimbaji mdogo anayepoteza haki yake kwa kuingia makubaliano yasiyokuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia Tangazo la Serikali Na.253 la tarehe 25 mwaka 2025, imekamilisha marekebisho ya Kanuni za Haki Madini za 2018 ili kusimamia ipasavyo shughuli za uchimbaji madini zinazofanywa katika vitalu maalum vya uchimbaji (maduara) na watu wengine isipokuwa mmiliki wa leseni, wafanyakazi wake, au mawakala wake, ndani ya eneo la leseni ndogo ya uchimbaji madini iliyotolewa chini ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, kanuni hizo zinaweka masharti kama ifuatavyo: Ikiwa mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini anaruhusu watu ambao siyo wafanyakazi wake au mawakala wake kufanya shughuli za uchimbaji madini katika kitalu cha uchimbaji mdogo ndani ya eneo la leseni, anapaswa kusajili mkataba Tume ya Madini ambao unabainisha haki na wajibu wa watu hao; na mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini atatakiwa kuandaa na kutunza rejista ya watu wote wanaofanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya uchimbaji mdogo kwa kuzingatia maelekezo ambayo Tume ya Madini itaamua.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini atahakikisha kwamba mmiliki wa kitalu cha uchimbaji mdogo (maduara) anazingatia masuala ya kisheria na ya kiuthibiti ambayo yanahusu mazoea mazuri ya uchimbaji bora, afya, usalama na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mmiliki wa kitalu cha uchimbaji mdogo anashindwa kuzingatia sharti lolote la leseni au

sharti lolote la kisheria linalotumika kwenye leseni hiyo, mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji atakuwa amekiuka sheria na atachukuliwa hatua kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Madini, Sura 123.

Mheshimiwa Spika, mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini anayekusudia kuhamisha umiliki wake wa haki madini au sehemu ya umiliki huo kwenda kwa mtu mwingine, atalazimika kupata ridhaa kutoka kwa Tume ya Madini. Pia, pale ambapo uhamisho wa umiliki wa haki madini unahusisha leseni ndogo ya uchimbaji madini ambayo ina ombi la msaada wa kiufundi chini ya kifungu cha 8(3) cha sheria, Tume ya Madini itazingatia haki na wajibu wa mmiliki wa leseni pamoja na watu wengine wanaofanya kazi katika vitalu vya uchimbaji mdogo kwa mujibu wa makubaliano yaliyosajiliwa na Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe msisitizo kuwa, leseni zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya vikundi vya wachimbaji wadogo, limewekwa sharti la lazima la kukitaka kikundi chenye lengo la kupata msaada wa kiufundi au kuuza leseni yake kwa mwekezaji, kupata kwanza kibali cha Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini baada ya kujiridhisha juu ya msaada wa kiufundi unaotaka kutolewa na pia kujiridhisha namna ambavyo pande zote zitanufaika ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurekebisha sheria na kanuni. Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwenye vifungu vifuatavyo: kifungu cha 88 kwa kuongeza kifungu cha 88 (A) kuhusu utaratibu wa malipo ya mrabaha na ada za ukaguzi; kifungu cha tano kwa kuongeza kifungu cha 5B ili kutambua madini muhimu na madini mkakati; kifungu cha 27F kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) na (6) ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki madini ambao wanatoa taarifa za kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini; kifungu cha 8 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (c) ili kuweka ukomo wa muda wa maombi ya kupewa haki madini; na kanuni za haki madini za mwaka 2018 katika kanuni ya 5 kwa kuongeza kanuni ya 5A ambayo inamtaka mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini iwapo ataruhusu watu ambao sio wafanyakazi wake au mawakala kufanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya

uchimbaji mdogo ndani ya eneo la leseni kuingia mkataba na wahusika hao na kuwasilisha mkataba huo Tume ya Madini kwa ajili ya ridhaa na kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Katika kipindi cha Julai mwaka 2024 hadi Machi, 2025 Wizara ya Madini na taasisi zake imejaza nafasi 55 kwa utaratibu wa uhamisho. Aidha, kupitia uhamisho huo, Wizara imepata watumishi 14, *STAMICO* watumishi tisa, Tume ya Madini 15, *TEITI* saba na *GST* 10. Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati. Vilevile, watumishi 544 wamewezeshwa kupata mafunzo ambapo 487 walipata mafunzo ya muda mfupi na 57 ya muda mrefu katika masuala mbalimbali yahusuyo Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha watumishi wake wanapatiwa vitendea kazi. Aidha, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara umefikia 92.8% na jengo la Makao Makuu ya Tume umefikia 92%. Kukamilika kwa majengo hayo kutawezesha watumishi kuwa na mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara imeendelea kuiwezesha Tume ya Madini katika maandalizi ya awali ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa mitatu ya kimadini ya Songwe, Rukwa na Mahenge. Sambamba na hili, taratibu za ununuzi wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Maafisa Madini Wakaazi katika Mikoa mitano ya Kimadini ya Mbogwe, Dar es Salaam, Iringa, Mwanza na Manyara zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara. Tume ya Madini, imetekeleza shuguli zifuatazo; utoaji na usimamizi wa leseni za madini, usimamizi na ukaguzi wa biashara ya madini, utambuzi na uthaminishaji wa madini, ukaguzi wa hesabu za fedha na kodi, ukaguzi wa migodi, mazingira na usimamizi wa baruti na kufuatilia utekelezaji wa matakwa ya kanuni za ushikirishwaji Watanzania migodini *(local content)* na wajibu wa kampuni kwa jamii *(CSR)*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* limetekeleza miradi mitano ya maendeleo ikiwemo Mradi Wa Makaa ya Mawe wa Kabulo – Kiwira; Mradi wa Nishati Mbadala, Mradi wa Uchorongaji, Mradi wa Kuchimba Kokoto na Mradi Wa Usimamizi wa Vituo vya Mfano vya Wachimbaji Wadogo wa Madini. Aidha, kwa upande wa Mradi wa Ubia, kampuni tanzu *STAMICO* imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ubia ambayo ni kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza, mgodi wa dhahabu wa *BUCKREEF* na kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* - Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Jiolojia na utafiti wa madini Tanzania *(GST)* imetekeleza shughuli zifuatazo: Kufanya tafiti za *geoscience* na kuboresha kanzidata ya rasilimali madini ya Taifa, uboreshaji wa huduma za maabara na ufuatiliaji wa majanga ya asili ya Jiolojia na kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jemolojia Tanzania *(TGC)* kimeendelea na utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali ikiwemo ujenzi wa jengo la kituo cha *TGC*, udahili wa wanafunzi na utoaji wa mafunzo, uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa wadau wa madini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na gesi asilia *(TEITI)* imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo maandalizi ya ripoti ya 15 ya *TEITI* ya mwaka wa fedha 2022/2023, kushiriki katika mikutano ya kimataifa ya uwazi na uwajibikaji, uzinduzi wa ripoti ya 14 ya *TEITI* kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kuweka wazi mikataba ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa kwenye ripoti za *TEITI*, kuimarisha mahusiano ya uwanachama na asasi za kimataifa *(EITI)* na kuratibu Mkutano wa 62 wa Bodi ya Kimataifa ya *EITI* uliofanyika tarehe 13 hadi 14 Machi, 2025 Jijini Arusha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika kuandaa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa

Maandalizi ya Mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 mpaka 2025/2026, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Mpango Mkakati wa Wizara, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Sheria ya Bajeti, Sura 433 kifungu cha 21, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yalitolewa kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2025/2026; kwanza, ni kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli wa Serikali, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ya kuimarisha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji kwa usawa. Kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ya ujenzi, soko la *Tanzanite* na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti na kuzuia utoroshaji wa madini ya *Tanzanite* katika mwaka ujao wa fedha, Wizara kupitia Tume ya Madini inakusudia kuja na mfumo wa utaratibu thabiti ambao utawataka wakaguzi na wathamini wa madini kuvaa kofia ngumu zenye *camera* wakitekeleza majukumu yao ili kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa mwenendo kwenye eneo tengefu la Mererani na masoko kunakofanyika biashara ya madini hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio yatakayopatikana, utaratibu huu utatumika kwenye madini mengine ya vito. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na

usimamizi wa Sekta ya Madini, Wizara inatarajia kununua magari 26 kwa ajili ya kuimarisha shughuli zinazotekelezwa na Tume ya Madini. Hatua hii itachangia katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli, udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya madini pamoja na kufuatilia shughuli mbalimbali za madini.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa. Katika kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: Kuhamasisha uanzishwaji wa migodi mipya, kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji, kusimamia utekelezaji wa sheria inayotaka migodi yote mikubwa kuajiri na kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuwasilisha mpango wa ushirikishwaji wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini na wajibu wa wamiliki wa leseni kwa jamii *(CSR)* na kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa wawekezaji wote waliopewa leseni za uchimbaji wa madini wanaanza uzalishaji mara baada ya kukamilisha taratibu za matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati. Madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na *Lithium, Graphite, Helium, Nickel, Cobalt, Titanium, Copper*, *Aluminium* na *Niobium* na *Rare Earth Elements* ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya kisayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na mkakati kwa uchumi wa Taifa, Wizara imepanga kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini hayo kwa kufanya yafuatayo: Kufanya utafiti kwa lengo la la kubaini maeneo yenye madini muhimu na madini mkakati kwa ajili ya kufanya uwekezaji; kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani; kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini mkakati; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini mkakati na kukamilisha maandalizi ya mpango mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini mkakati nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ni msimamo wa Serikali kwamba hatutatoa leseni za uchimbaji wa kati na uchimbaji mkubwa wa madini muhimu na ya mkakati kwa mwekezaji yeyote kama hatakuwa na mpango mzuri wa kuongeza thamani ya madini hayo hapa nchini. Lengo ni kuifanya nchi yetu ya Tanzania kunufaika na rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini. Ili kuhamasisha uwekezaji, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezwaji wa bidhaa za madini, kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya *LDMA,* kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ikiwemo ujenzi wa viwanda vya kuyeyushia *(smelters)*, viwanda vya kusafisha *(refineries)* na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kituo cha Jemologia ili kiweze kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ni kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito. Katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: Kuendeleza minada na maonesho ya madini ya vito katika maeneo yenye uzalishaji mwingi wa madini ya vito na kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita ni kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini. Katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya yafuatayo: Kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia, *(High Resolution Airborne of Geophysical Survey)* kwa kuzingatia matokeo ya tafiti za majaribio ili kuainisha uwepo na upatikanaji wa madini mbalimbali yakiwemo madini mkakati na kujenga mfumo wa kutunza na kusambaza taarifa za *Geoscience*. Aidha, Wizara itashirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kusaidia kufanya utafiti wa madini katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa utafiti wa kina wa madini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la saba ni kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Wizara itaendelea na juhudi za kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayohamasisha kufanya uwekezaji, kuendelea kuhamasisha taasisi za kifedha kutoa mikopo ya fedha na vifaa kwa wachimbaji wadogo, kuboresha utendaji wa vituo vya mfano ili kuimarisha utoaji wa huduma na mafunzo kwa wachimbaji wadogo na kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wao.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za jiolojia, kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki mikutano, maonesho, makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujifunza na kutangaza shughuli zao na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye minada na maonesho ya madini ya vito nchini ili kupanua wigo wa biashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kunufaika na rasilimalimadini, Serikali imeunda timu ya wataalamu sita wenye uzoefu na masuala ya fedha, madini na sheria kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji. Hatua hii itawawezesha wachimbaji hao kufanya uchimbaji wenye tija na kunufaika zaidi kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia *STAMICO* itaendelea kuwalea na kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwajengea vituo vya mfano vya kuchenjua dhahabu kwa kusimika mitambo mingine ya *CIP* katika maeneo yenye uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hatua hizo, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inakusudia kuanzisha vituo vya kuuza na kukodisha vifaa na mashine mbalimbali za kufanyia shughuli za madini. Vituo ambavyo vitawekwa katika maeneo ambako uchimbaji unafanyika ili kurahisisha upatikanaji wa vifaa na mashine hizo kwa wachimbaji wadogo kwa uharaka, uhakika na wepesi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza uzalishaji mkubwa wa madini kupitia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nane ni kuzijengea uwezo taasisi zilizochini ya Wizara ya Madini. Ili kuzijengea uwezo taasisi, Wizara itafanya mambo yafuatayo: Kwanza, kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimalifedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kuendelea kuiimarisha *STAMICO* ili ishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini ikiwemo kuwawezesha wachimbaji wadogo kwenye masuala ya mafunzo, mikopo na vifaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuiimarisha *GST* ili iweze kufanya utafiti mkubwa wa madini kuweza kubaini maeneo mapya yenye mashapu ya madini, kukiimarisha kituo cha *TGC* ili kiweze kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini na kuiwezesha *TEITI* kupata rasilimali mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yatakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2025/2026. Eneo la kwanza ni *Mining Vision 2030*, Madini ni Maisha na utajiri. Wizara ya Madini itaendelea na utekelezaji wa *Mining Vision 2030*, Madini ni Maisha na Utajiri inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti wa rasilimalimadini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa, kuboresha maisha ya Watanzania na kutoa fursa kwa Mtanzania yeyote wakiwemo akinamama, vijana na watu wenye mahitaji maalum kujiongezea kipato na hatimaye kutajirika kupitia shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayozingatiwa katika *Mining Vision 2030* ni pamoja na kuboresha shughuli za wachimbaji wadogo hususan katika urasimishaji wa shughuli zao, upatikanaji wa teknolojia za kisasa na rahisi, masoko ya madini, upatikanaji wa mitaji na usimamizi thabiti wa shughuli za utunzaji wa mazingira kwa kushirikiana na taasisi zingine ili shughuli za madini zisiwe na athari hasi kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, dhana ya madini ni maisha na utajiri inamaanisha huwezi kutenganisha maisha ya Mtanzania na Sekta ya Madini. Kwa

kuwa kufanikiwa kwa tafiti za kina na kupatikana kwa taarifa sahihi kutochochea sekta nyingine kukua ikiwemo sekta ya maji, kilimo, utalii, ujenzi na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu ya *Mining for Brighter Tomorrow (MBT)*. Wizara ya madini itaendelea kutekeleza programu ya *MBT* kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2030. Programu hii ni ya kimageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kushughulikia changamoto na kuboresha fursa kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum ili kuongeza ushiriki wa makundi hayo katika mnyororo wa thamani wa madini.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kusomesha wataalam kwenye maeneo muhimu katika sekta ya madini. Ili kukidhi mahitaji ya wataalam, Wizara itawajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Madini kwa kuwasomesha ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo ukadiriaji wa mashapo *(resource modelling) model* za kifedha, ukaguzi na usimamizi wa rasilimali madini, uthaminishaji wa madini, ukataji wa madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara na uongezaji thamani madini. Mafunzo haya yatajikita zaidi kwenye teknolojia ambazo zinapatikana nje ya nchi mathalani teknolojia za *gemstone*, *heat treatment*, *enhancement* and *jewelry manufacturing* ambapo shughuli hizo zitafanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kuboresha usimamizi wa shughuli za madini ya kidijiti. Wizara inakusudia kujenga mfumo wa kidijiti kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa shughuli za madini kwa kuweka wazi shughuli mbalimbali za madini, hususan biashara ya madini, ukusanyaji wa maduhuli, usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini. Mfumo huu utaweza kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za Serikali zinazohusiana na shughuli za madini ili mifumo iweze kusomana na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa Wizara na taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile mfumo utarahisisha uratibu, ufuatiliaji wa karibu (mubashara) na uendeshaji mfumo wa shughuli za madini kisasa.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni mkakati wa madini muhimu na madini mkakati. Wizara ya Madini itakamilisha na kuanza kutekeleza mikakati mbalimbali iliyoainishwa kwenye mkakati wa madini muhimu na madini mkakati. Lengo kuu la mkakati huu ni kuwezesha Serikali kusimamia madini hayo na kupata manufaa zaidi kwa kuboresha maisha ya Watanzania na kuleta maendeleo endelevu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekelezwa na taasisi chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Tume ya Madini, kuimarisha utendajikazi wa masoko na vituo vya ununuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha biashara ya madini inaimarika, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na biashara ya madini katika masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini. Uimarishaji wa masoko hayo utalenga kununua vifaa vya uthaminishaji wa madini zikiwemo mashine za XRF, mizani, mashine za uthaminishaji wa madini ya vito sambamba na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa soko la uthaminishaji madini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuimarisha usimamizi wa udhibiti wa Sekta ya Madini katika uzalishaji na biashara ya madini. Katika kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kukokana na shughuli za madini nchini, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha mkakati wa uthibiti wa sekta hii katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwa masuala yatakayozingatiwa ni pamoja na:

Kuimarisha utendaji kazi wa ofisi za Maafisa Madini wa kazi na Maafisa Migodi wa kazi kwa kuziongezea vitendeakazi na kukiongezea kikosi kazi cha kuzuia utoroshaji madini vitendea kazi, yakiwemo magari na vifaa vya kupimia madini.

Kuimarisha madawati ya ukaguzi wa madini katika maeneo muhimu kama mipakani, viwanja vya ndege na bandarini; na kuimarisha utoaji wa vibali vya biashara ya madini ili vitolewe katika mfumo wa kidijitali na kuendeleza minada ya ndani ya madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na ufuatiliaji wa leseni za madini. Ili kuhakikisha uwekezaji unakuwa na tija kwa nchi. Tume ya Madini itafanya ufuatiliaji na tathmini ya leseni zilizotolewa ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Aidha, katika kuvutia uwekezaji na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha mfumo wa uandaaji na utoaji wa leseni za madini nchini.

Mheshimiwa Spika, kufanya ukaguzi wa masuala ya afya na mazingira. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na shughuli za uchimbaji salama wa madini, endelevu na zenye tija, Tume ya Madini itaendelea kufanya shughuli katika masuala ya usalama, afya na mazingira katika migodi midogo au ya kati na migodi mikubwa, sambamba na ukaguzi wa mabwawa ya kuhifadhia topetaka *(TSF), Waste Rock Dam (WRD),* pamoja na maghala ya kuhifadhia baruti. Pia Tume itafanya ufuatiliaji wa uwasilishaji mpango wa ufungaji mgodi, kuidhinisha na kuweka hati fungani.

Mheshimiwa Spika, kuboresha mazingira ya utendajikazi na kuwajengea uwezo watumishi. Tume ya Madini itaendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa watumishi kwa kuongezea ujuzi, weledi na ubobezi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa huduma zitakazokidhi viwango kwa wateja na wadau wa sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora ya utendaji kazi, Tume ya Madini itaendelea na ujenzi wa ofisi za Maafisa Madini wa Kazi katika Mikoa ya kimadini ya Songwe, Rukwa, Mahenge sambamba na ununuzi wa samani na vitendeakazi yakiwemo magari na pikipiki.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini. Katika kusimamia masuala ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini, Tume ya Madini itaendelea kutekeleza na kuhakikisha kampuni zinazowekeza zinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini na zinatoa kipaumbele kwa ajira na mafunzo kwa Watanzania pamoja na kutumia huduma mbalimbali zinazotolewa na Watanzania au kampuni za kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026, *GST* inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

Kufanya tafiti za jiosayansi na kuboresha kanzidata ya Taifa ya taarifa za miamba na madini. Ili kuboresha kanzidata ya rasilimali madini ya Taifa, *GST* itafanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege ili kuongeza eneo lenye taarifa za kina za jiofizikia kutoka 16% za sasa hadi kufikia 34% ifikapo mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, aidha, *GST* itafanya tafiti maalumu kwa ajili ya kutambua maeneo yenye madini muhimu na madini mkakati *(critical and strategic minerals)* pamoja na kufanya ugani wa jiosayansi na utafiti wa madini katika maeneo hayo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, *GST* itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mfumo wa kanzidata wa taarifa za jiosayansi, utafiti wa jiolojia na jiokemia pamoja na utafiti wa kimkakati katika *QDS* mbili na kuchora ramani zake katika skeli ya 1:100,000; tafiti maalum za jiosayansi, utafiti wa kina kwenye madini ya kimkakati, viwandani na metali. Vilevile kufanya utafiti kwa lengo la kuongeza uelewa wa wadau kuhusu masuala ya jiosayansi na kuchapisha kwenye jarida linalotambulika na kutoa ushauri elekezi kwa wadau kwenye nyanja za jiolojia, jiokemia, jiofizikia na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, *GST* itachora ramani 24, kudurufu ramani 30 na kuchakata picha za *satellite*, kuingiza taarifa na machapisho 500 katika mfumo wa dijitali, kukusanya, kuhakiki na kuthamini uhalisia wa taarifa na takwimu za kisayansi kutoka leseni 47 za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini na kuhuwisha kanzidata ya rasilimali madini ya taifa pamoja na kitabu cha madini yapatikanayo Tanzania na kukusanya miamba choronge mita 1,000 na kuchakata taarifa zake.

Mheshimiwa Spika, kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Katika kuendeleza wachimbaji wadogo, *GST* inalenga kufanya utafiti wa jiosayansi na kutoa mafunzo kwa lengo la kutambua

ulalo, mwelekeo na tabia za mbale na namna ya kuchenjua katika mikoa minne ya shughuli hai za uchimbaji mdogo wa madini nchini na kufanya utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo wa madini katika eneo moja lililotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuboresha huduma za maabara; katika kuboresha huduma za maabara, *GST* zitaendelea kufanya uchunguzi kwa kuzingatia vigezo vya ithibati *(accreditation)*. Aidha, *GST* itajenga maabara mpya ya kisasa *(State of the Art Geoscientific Laboratory)* katika eneo la Kizota, Dodoma, maabara hiyo itafanya uchunguzi wa madini ikiwemo yale yanayohitajika kwenye nishati safi kama vile *nickel*, *cobalt* na *lithium*.

Mheshimiwa Spika, vilevile *GST* itaendelea na ujenzi wa maabara nyingine katika maeneo ya Chunya - Mbeya na Geita kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini. *GST* inaendelea kutengeneza *crucibles* 200,000 na *cupels* 50,000 kwa ajili ya kuyeyusha sampuli za dhahabu, uchunguzi wa sampuli 25,000 za udongo, miamba au madini na uandaaji wa sampuli rejea *(certified reference sample materials)* za dhahabu, shaba, fedha, zinki, chuma na *cobalt*.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia na kuelimisha umma namna bora ya kupunguza athari za majanga. Katika kutekeleza jukumu hilo, *GST* itakusanya takwimu kutoka vituo vitano vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyomo katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya na kuchakata taarifa za kutoka katika vituo hivyo na kuhuwisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini, kufanya matengenezo ya vifaa vya kunakili mitetemo, kuendelea kuunganisha vituo viwili vya kupima mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha katika mfumo mbashara *(real time)* ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea pamoja na kusimika mtambo mpya mmoja kwa ajili ya ukanda wa Bonde la Ufa mkondo wa magharibi Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, *GST* itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga asili ya jiolojia, elimu itatolewa kwa njia ya machapisho, semina na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha uwezo wa taasisi katika kutekeleza majukumu yake. Ili kuimarisha uwezo wa taasisi katika kutekeleza majukumu yake, *GST* itaboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi, usambaza wa taarifa na takwimu za jiosayansi, taarifa za uwepo wa madini pamoja na kuwajengea uwezo watumishi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali ikiwemo masuala ya maabara kwa mujibu wa *program* ya mafunzo ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, *GST* imepanga kununua vitendea kazi ikiwemo helkopta ya utafiti, vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa sampuli za madini mbalimbali yakiwemo ya kimkakati, kukarabati majengo, kujenga maabara ya kisasa, kuboresha maslahi ya watumishi, kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la *STAMICO* katika kutekeleza mwaka wa fedha 2025/2026 *STAMICO* inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

Kwanza, kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ili kuhakikisha mapato ya shirika yanakuwa na yanaimarika Serikali imepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo:

(i) Uzalishaji wa makaa ya mawe na nishati mbadala, shirika litaendelea na uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo Kiwira ambao katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya tani 732,770 zimepangwa kuchimbwa ili kuimarisha na kuongeza uzalishaji huo.

(ii) Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa mbalimbali zikiwemo *dump trucks (3)*, *bulldozer D8 (1)*, *longwall coal shearer (2), Hydraulic Prop (1),* kifaa

maalum cha mawasiliano mgodini (1) na *excavator (1)* yenye uwezo wa tani 50.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa kuzalisha nishati mbadala, shirika litaendelea na uzalishaji wa nishati safi ya kupikia. Aidha, shirika litakamilisha usimikaji wa mitambo miwili katika Mkoa wa Dodoma na Tabora. Vilevile shirika litanunua mtambo mwingine mmoja utakaosimikwa katika Mkoa wa Geita ili kuongeza uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mitambo hiyo kutaliwezesha shirika kuzalisha nishati safi *(Rafiki briquettes)* kwa kiwango cha tani 32,761 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za uchorongaji. Shirika linatarajiwa kuimarisha shughuli za uchorongaji wa kutangaza na kutafuta kandarasi katika migodi mikubwa na ya kati. Aidha, shirika limepanga kununua mitambo na vifaa kwa ajili ya uchorongaji ambavyo ni *deep hole drilling rig (1), underground rig (1), light vehicles (5), compressor (1)* na *booster (1)* ili kukidhi ongezeko la uhitaji wa huduma za uchorongaji.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa kokoto Chigongwe, katika mwaka wa fedha 2025/2026 shirika limepanga kuzalisha mita za ujazo 89,604 za kokoto. Aidha, ili kuendelea kuwa na soko la kutosha la kokoto shirika litaendelea kufanya mazungumzo na kampuni mbalimbali kubwa za ujenzi katika miradi ya Serikali ikiwemo ya ujenzi wa majengo, barabara, reli, viwanja vya mpira na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha shughuli za uchimbaji mdogo na kuimarisha vituo vya mfano. *STAMICO* itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa Vituo vya mfano vya Itumbi, Rwamgasa na Katente;

(ii) Kuendelea na uzalishaji katika Mgodi wa mfano wa Rwamgasa;

(iii) Kufanya upanuzi wa Kituo cha mfano cha Katente kwa kusimika mtambo wa *CIP* na *elution*;

(iv) Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Usafishaji Chumvi kilichopo Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi na ujenzi wa *CIP* mpya katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza leseni za shirika. Shirika limepanga kufanya utafiti kwenye leseni zake tatu za madini ya dhahabu zilizopo katika Mikoa ya Geita na Mara. Aidha, kutokana na uhitaji mkubwa wa madini mkakati, shirika limepanga kufanya utafiti wa madini Kinywe katika leseni zake zilizopo katika Mikoa ya Kimadini ya Manyara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, vilevile shirika linatarajiwa kuwa na migodi yake ya uchimbaji wa madini itakayoimiliki kwa 100% katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya ubia na kampuni tanzu. Shirika litaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya ubia ambayo ni mgodi wa *Buckreef,* kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza, kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuiwezesha *STAMIGOLD* kufanya utafiti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, mgodi huo wamepanga kufanya utafiti ambao utajumuisha uchorongaji wa mita 6,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha Jemolojia Tanzania (*TGC*); katika mwaka wa fedha 2025/2026 kituo cha *TGC* kinatarajiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kituo cha *TGC* kimepanga kuimarisha miundombinu ya kutolea mafunzo kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nane, ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchakataji na upimaji madini kwa lengo la kuhakikisha kuwa wadau wanapatiwa huduma bora.

(ii) Ufunguzi wa kituo cha mauzo kwa ajili ya kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini na;

(iii) Kuuza bidhaa za madini katika eneo la *AICC;*

(iv) Kuimarisha maabara ya madini ya vito kwa kufanya ununuzi wa mashine za kisasa.

Mheshimiwa Spika, (b) Kuhusu utoaji wa mafunzo na huduma nyinginezo. Kituo cha *TGC* kinafanya udahili wanafunzi 50 wa Astashahada, 65 ufundi sanifu na Stashahada katika fani ya teknolojia ya vito na usonara. Aidha, kituo cha *TGC* kitafanya udahili wa wanafunzi 40 wa kozi za muda mfupi. Kozi hizo zitahusisha fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito (lapidary), utengenezaji wa madini na bidhaa za *usonara (jewellery design and manufacturing),* na utambuzi wa madini ya vito *(gemology)* na uchongaji wa vinyago na madini ya vito na miamba.

Mheshimiwa Spika, kituo kitatoa huduma za utambuzi wa kimaabara kwa madini ya vito kwa sampuli 520, kufanya ukataji wa vipande 243 ya madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara 240 kutoka kwa wadau, kutoa ushauri kwa wadau wa madini, kufanya tafiti za kuongezea thamani madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji madini nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa bidhaa. Kituo kinatarajiwa kuzalisha bidhaa za madini ya vito ikiwemo vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyingine za urembo na mapambo. Aidha, bidhaa za usonara 3,120 zinatarajiwa kutengenezwa kwa kutumia metali za fedha, dhahabu na shaba. Vilevile, vipande vya vito 2,880 vitakatwa sambamba na kuzalisha vinyago 7,500 vya miamba ya madini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhamasishaji, Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(TEITI)*. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 *TEIT* inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kuweka wazi ripoti ya 16 ya *TEITI* inayoonesha ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

(ii) Kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia;

(iii) Kukamilisha rejista ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia;

(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu na ripoti ya *TEITI* ili kutambua mchango wa sekta ya uziduaji katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, *TEITI* itaendelea na ukamilishaji wa mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na kampuni za uziduaji pamoja na taasisi za Serikali katika kuripoti malipo yanayofanywa na kampuni hizo kwa Serikali na kufanya tafiti mbalimbali za namna wananchi watakavyonufaika na wanavyoweza kunufaika zaidi na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, shukrani, ninatambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika, kasi na juhudi na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi unaendelea na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kichocheo kwa kuwa na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo anayotupatia katika sekta ya madini ambayo wanaifanya sekta hii kuendelea kukua na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa. Nichukue nafasi hii tena kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo ambayo amekuwa akiitoa kwa sekta ya madini ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa shughuli mbalimbali za madini kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni utekelezaji wa programu mbalimbali za kitaifa, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 pamoja na msisitizo alioutoa kwenye maeneo mahsusi ikiwemo masuala ya kuzingatia katika ukamilishaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, hakika hotuba hiyo imetoa mwelekeo utakaokuwa na tija katika kupanga, kusimamia, kuratibu shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye ameisaidia sekta ya madini kupitia ushauri, maelekezo na miongozo ili kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa na mchango endelevu kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,405,537,268,755, ninaomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupisha makadirio ya shilingi 224,984,150,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa mchanganuo ufuatao:

Mheshimiwa Spika, shilingi 124,604,784,000 sawa na asilimia 55 ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Shilingi 100,379,362,000 sawa na asilimia 44.62 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 24,268,585,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 76,110,777,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* ya Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *www.madini.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, muweza wa yote kwa neema na fadhila zake zisizo na kikomo ambazo zimeijalia nchi yetu amani, utulivu na afya njema kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamuomba aendelee kutujalia rehema, hekima, busara na umoja katika kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa nia ya kuendeleza Taifa letu [illegible] kuboresha ustawi na maendeleo ya watanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii adhimu kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, weledi, maono mapana na dhamira thabiti ya kuwaletea watanzania maendeleo jumuishi. Aidha, Mheshimiwa Rais ameendelea kudhihirisha dhamira

yake ya dhati ya kuimarisha mazingira bora ya uwekezaji, usimamizi wa rasilimali zetu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Pia, Mheshimiwa Rais wakati wote ameendelea kuhimiza uwajibikaji, utawala bora na mshikamano wa kitaifa.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussen Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Sekta ya Madini. ***Ni ahadi yangu kwake, na kwa Bunge lako Tukufu pamoja na watanzania kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote ili kuendeleza sekta hii muhimu***.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika Sekta ya Madini. Mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kukua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021, asilimia 9.1 mwaka 2023 na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024.

***Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kutokana na maelekezo na miongozo yenye tija kutoka kwa Mheshimiwa Rais katika kusimamia sekta na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Sekta ya Madini imefanikiwa kuvuka lengo la kuchangia asilimia 10 kwenye Pato la Taifa mwaka mmoja kabla ya muda***

***ulioainishwa katika Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na kufikia mchango wa asilimia 10.1 mwaka 2024.***

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada za kuimarisha usimamizi wa rasilimali zetu zimewezesha kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za uchimbaji madini kutoka asilimia 10.8 mwaka 2022 hadi asilimia 11.3 mwaka 2023. Aidha, ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali uliongezeka kutoka shilingi 623,237,296,973.40 mwaka 2021/2022, shilingi 678,042,598,813.92 mwaka 2022/2023 hadi shilingi 753,175,680,203.96 mwaka 2023/2024. Mafanikio haya ni matokeo ya mikakati madhubuti ya Serikali ikiwemo kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini, kudhibiti utoroshwaji wa madini, kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za madini na kuanzisha minada ya madini ya vito.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa vituo vya ununuzi wa madini kutoka 102 mwaka 2023/2024 hadi kufikia 109 mwaka 2024/2025. Kupitia masoko 43 na vituo vya ununuzi 109 kulifanyika biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 1,930,698,791,589.30 kwa mwaka 2023/2024 na shilingi 2,819,220,651,824.38 kwa mwaka 2024/2025 mtawalia. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imeyatambua na kuyapa hadhi ya vituo vya ununuzi jumla ya maeneo 142 yanayotumika kufanyia biashara ya madini kwa wingi (bulk minerals) kupitia Gazeti la Serikali Na. 906 ya tarehe 15 Novemba, 2024.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo, Serikali imenunua mitambo 10 ya uchorongaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuchakata chumvi katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendeleza madini muhimu na madini mkakati, tarehe 03 Machi, 2025 Serikali ilitoa

leseni ya uchimbaji mkubwa (SML) wa madini ya Kinywe kwa mradi wa Epanko Graphite (Kampuni ya Duma Tanzgraphite Limited) uliopo Wilaya ya Mahenge, Mkoa wa Morogoro. Kutekelezwa kwa mradi huo kutaongeza ajira na mapato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake mbalimbali anayoitoa yenye lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa na mchango endelevu katika kuwanufaisha watanzania na Taifa kwa ujumla.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao madhubuti na maelekezo wanayoyatoa mara kwa mara ili kufanikisha utendaji kazi Serikalini. Viongozi hawa wamekuwa tayari kushirikiana nasi muda wote, kutusikiliza na kutupa maelekezo na miongozo ambayo imetusaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake iliyojaa maono mazuri aliyoiwasilisha hapa bungeni ambayo inatoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo kwa kiasi kikubwa imeonesha mafanikio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa dhati wewe mwenyewe kwa uongozi wako mahiri ambao umeendelea kulifanya Bunge kuwa

chombo madhubuti. Umeendelea kuonesha ustadi, hekima, busara, ubunifu na uwajibikaji katika kuliongoza Bunge hili kwa weledi na uaminifu mkubwa. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kushirikiana nawe katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa weledi mkubwa. Ni dhahiri kuwa mmeonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa wakati wote wa kuendesha vikao vya Bunge. Tunaamini kuwa chini ya uongozi wako na wasaidizi wako Bunge litaendelea kufanya maamuzi sahihi yenye manufaa kwa maendeleo ya Taifa letu na kufanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya nchi yetu.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuendelea kuiongoza Kamati hii kwa umahiri mkubwa. Aidha, nawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kwa ufanisi na kutoa maelekezo yenye tija wakati wote. Wizara inaishukuru Kamati kwa ushauri wake makini ambao imekuwa ikiutoa mara kwa mara katika kuhakikisha kuwa sekta hii inakuwa na tija kwa Taifa na kuwanufaisha watanzania. Vilevile, ninaishukuru Kamati kwa kujadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kuyapitisha kwa kauli moja.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi kubwa na yenye tija ya kuisimamia na kuishauri Serikali, hususan katika masuala yanayohusu Sekta ya Madini. Kupitia kwako, naliomba Bunge liendelee kushirikiana nasi ili kuimarisha mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania katika kuongoza Wizara mbalimbali. Ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo na ustawi wa watanzania.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima kubwa, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa imani yao na ushirikiano wanaouonesha kwangu kama Mbunge wao. Uvumilivu na mshikamano wao umekuwa chachu ya kuniongezea ari ya kutekeleza majukumu yangu sio tu kama mwakilishi wao bali pia kama Waziri wa Madini katika kulitumikia Taifa letu. ***Naahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujituma ili kuwaletea maendeleo na kuboresha ustawi wa jamii ya wana Dodoma na Taifa kwa ujumla.***

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini, kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Eng. Yahya Ismail Samamba, Katibu Mkuu kwa kusimamia utendaji wa Wizara. Vilevile, nampongeza Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini kwa kazi zao na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, nichukue fursa hii kuishukuru Menejimenti ya Wizara pamoja na Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuishuru kwa dhati familia yangu, mke wangu mpendwa Jacquelyne Moses Lupasa na watoto wangu Atarah na Allan kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya familia.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na watanzania wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Kigamboni kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wao Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile. Mwenyezi Mungu amrehemu marehemu na awape faraja familia na wananchi aliokuwa akiwaongoza.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia majanga mbalimbali zikiwemo mvua zilizosababisha madhara katika baadhi ya maeneo ya nchi na ajali za barabarani naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kwa ujumla kutokana na vifo, majeraha, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa salamu za shukrani, pongezi na pole, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa biashara ya madini duniani umeendelea kubadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na mahitaji ya soko. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 2,655.80 ikilinganishwa na bei ya wastani wa dola za Marekani 2,078.09 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo duniani kama njia ya kuhifadhi thamani ya fedha.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, mwenendo wa biashara ya madini ya almasi duniani umeendelea kukabiliwa na changamoto

zinazosababishwa na mdororo wa uchumi wa dunia; uwepo wa almasi zinazotengenezwa kwenye maabara (Lab-Grown Diamonds) na kupungua kwa uhitaji katika masoko makubwa yakiwemo ya China na Marekani. Aidha, bei ya madini hayo imeshuka kutoka wastani wa dola za Marekani 206.61 kwa karati mwaka 2023/2024 na kufikia dola za Marekani 168.95 kwa karati katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 sawa na upungufu wa asilimia 18.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha wastani wa mauzo ulikuwa karati 281,021.99 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 47.48 ikilinganishwa na karati 164,837.94 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 34.06 katika kipindi kama hicho cha mwaka uliopita.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hii, wazalishaji wakubwa wa almasi duniani wamepunguza uzalishaji ili kuimarisha bei. Aidha, kwa upande wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha biashara ya almasi kwa kuanzisha minada, maonesho, masoko na kuhamasisha uwekezaji katika uchakataji wa madini ya almasi ndani ya nchi.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa kuwa na madini mkakati na madini muhimu (strategic and critical minerals) ambayo yanazidi kuhitajika duniani kwa ajili ya matumizi katika teknolojia za kisasa na nishati mbadala. Mahitaji ya madini haya, yakiwemo *lithium, cobalt, nickel, copper, aluminium, zinc, graphite,* na *rare earth elements* (REE), yameendelea kuongezeka kutokana na jitihada za kimataifa za kupunguza hewa ya ukaa ifikapo mwaka 2050 (Net Zero Emission). Kuongezeka kwa mahitaji haya kunatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa magari ya umeme, betri za kuhifadhi nishati, na vifaa vya teknolojia ya kisasa vikiwemo simu janja, darubini na kompyuta.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali hii inatoa fursa kubwa kwa Tanzania kuhakikisha madini haya yanaongezwa thamani ndani ya nchi ili kuongeza mapato, ajira, na mchango wake katika uchumi wa Taifa. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kimkakati ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje katika Sekta ya Madini, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata madini haya ili kuyauza yakiwa yameongezwa thamani.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na madini mkakati, Serikali imeendelea kuhimiza ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kisasa cha usafishaji madini mbalimbali (Multi Metals Processing Facility) katika eneo maalumu la ukanda wa kiuchumi la Buzwagi *(*Buzwagi Special Economic Zone) lililopo Wilaya ya Kahama.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### a.Mapato

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 231,983,614,000.00 kwa Wizara ya Madini. Kati ya bajeti hiyo, shilingi 91,322,414,000.00 ni bajeti ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi 66,449,539,000.00 za matumizi mengineyo na shilingi 24,872,875,000.00 mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, shilingi 140,661,200,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya marejeo ya bajeti yaliyofanyika, fedha za maendeleo ziliongezwa kwa kiasi cha shilingi 299,285,830,006.46 na kufanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi 531,269,444,006.46.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, katika mwaka 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,164,850,027,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi

1,000,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi 164,850,027,000.00 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imepokea jumla ya shilingi 62,778,516,974.99 sawa na asilimia 68.74 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 47,819,516,169.98 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 14,959,000,805.01 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi 329,589,099,832.01 zilipokelewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Vilevile, shilingi 4,053,782,322.88 zimepokelewa kupitia akaunti ya amana kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Wizara ya Madini Makao Makuu, Mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma.

### b.Miradi ya Maendeleo

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara ilipokea na kutumia fedha za maendeleo shilingi 329,589,099,832.01 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali ambazo ni: ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume ya Madini Makao Makuu; ujenzi wa jengo la Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) jijini Arusha; ununuzi wa mitambo ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo; Timu ya Serikali ya Majadiliano (Government Negotiation Team - GNT) na Timu ya Serikali ya wataalamu (Government Technical Team - GTT) kwa ajili ya kupitia mikataba ya uwekezaji kwenye Sekta ya Madini; na kugharamia malipo ya mihadi ya kisheria (deed of settlement) kati ya Serikali na Kampuni za Uwekezaji.

### c.Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Sekta ya Madini inaendelea kukua na kuwanufaisha watanzania ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa mchango wake kwenye Pato la Taifa, Mwaka wa Fedha 2024/2025

Wizara ilijielekeza katika kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji, uanzishwaji wa minada ya madini, maonesho ya madini ya vito na uongezaji thamani madini; kuendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege (High-resolution Airborne Geophysical Survey); kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani; na kuzijengea uwezo Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi.

**(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilipangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 1,164,850,027,000.00 kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,000,000,000,000.00 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina ambapo hadi Machi 2025 shilingi 783,875,962,446.79 zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 78.39 ya lengo la makusanyo kwa mwaka.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangiwa kukusanya na kutumia shilingi 164,850,027,000.00. Hadi kufikia Machi 2025 shilingi 66,812,328,104.74 zilikusanywa sawa na asilimia 40.53 ya lengo la makusanyo kwa kipindi rejewa. Aidha, lengo hilo halikufikiwa kutokana na STAMICO: kuchelewa kukamilisha zoezi la usimikaji wa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala (coal briquettes) iliyosababishwa urefu wa taratibu za ununuzi nje ya nchi; baadhi ya mikataba ya uchorongaji kutotekelezwa kwa mujibu wa makubaliano; na kupungua kwa mauzo ya makaa ya mawe kuliko sababishwa na mnunuzi mkubwa kusitisha ununuzi kutokana na kufunga shughuli za kiwanda chake.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini nchini unaofanywa na baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi 17,757,009,262.37 katika Mikoa ya kimadini ya Geita, Ruvuma, Kahama, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Dar es salaam, Mirerani, Simiyu, Singida, Chunya, Arusha, na Lindi. Aidha, madini hayo yaliyokamatwa yalitaifishwa na watuhumiwa 75 walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

***Ni rai yangu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kujiepusha na utoroshaji wa madini ili kuepuka hasara kwenye biashara zao na Taifa kwa ujumla.***

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na jitihada zilizofanyika kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya shilingi 783,875,962,446.79 zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikilinganishwa na shilingi 548,297,119,748.13 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 42.97. Aidha, ili kuongeza maduhuli ya Serikali, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya ununuzi wa madini na mipaka ya nchi.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Madini na mchango wake kwenye Pato la Taifa imeendelea kuimarika. Mathalani, mwaka 2023 Sekta ya Madini ilikua kwa kasi ya asilimia 11.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.9 mwaka 2022. Aidha, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 9.1 mwaka 2023 na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Madini imefanikiwa kuvuka lengo la kuchangia asilimia 10 kwenye Pato la Taifa mwaka mmoja kabla ya muda ulioainishwa katika Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mapato ya fedha za kigeni kupitia Sekta ya Madini, ukusanyaji wa mapato hayo umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2024 thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa dola za Marekani milioni 4,119.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,551.4 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 16.0. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu ambapo thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 11.8 na kufikia dola za Marekani milioni 3,419.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,058.9 mwaka 2023. Aidha, mauzo ya madini yalichangia asilimia 60.0 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024, jumla ya vibali 9,540 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 8,809 vilivyotolewa Mwaka 2023. Ongezeko la vibali hivyo kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa uhitaji wa madini ya vito, makaa ya mawe, dhahabu na kinywe nje ya nchi. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vibali 116 vyenye thamani ya dola za Marekani 14,813,664.38 vya uingizaji madini nchini vilitolewa ikiwa ni hatua mojawapo ya kusimamia na kudhibiti biashara ya madini nchini.

### (b) Kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha madini muhimu na mkakati yananufaisha Taifa. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya tafiti, kuhamasisha uwekezaji, kutoa leseni za

utafutaji, uchimbaji, uchakataji, uongezaji thamani na biashara ya madini ya kimkakati na madini muhimu na kutangaza fursa za uwepo wa madini nchini kupitia ***Mining Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri***.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** suala la madini muhimu na madini mkakati ni miongoni mwa maboresho yaliyofanyika katika Sheria ya Madini, Sura 123 kupitia muswada wa marekebisho ya Sheria mbalimbali namba 12 wa Mwaka 2024 ambao ulisomwa na kupitishwa na mkutano wa 14 wa Bunge. Marekebisho hayo yalifanyika katika Kifungu cha 5 kwa kuongeza Kifungu cha 5B ili kutambua madini muhimu na madini mkakati. Lengo la maboresho hayo ni kuweka usimamizi thabiti wa madini mkakati na madini muhimu ili kupata manufaa mapana kupitia mnyororo wa thamani wa madini hayo.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni za madini muhimu na mkakati kama ifuatavyo: leseni 1 ya uchimbaji mkubwa; leseni 58 za utafiti; leseni 275 za uchimbaji mdogo; leseni 3 za uchimbaji wa kati; na leseni 3 za uchenjuaji. Leseni hizo zinajumuisha utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini aina ya *graphite, nickel, cobalt, lithium, heavy mineral sand* na *rare earth elements*.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika madini muhimu na mkakati ili madini hayo yaweze kunufaisha Taifa kutokana na uhitaji wake kwa ajili ya teknolojia mbalimbali pamoja na kupunguza hewa ya ukaa duniani. Kutokana na uhamasishaji huo Wizara imetoa leseni ya uchimbaji wa madini ya kinywe kwa Kampuni ya Duma Tanzgraphite Limited (DTL) katika eneo la Epanko, Wilaya ya Ulanga.

***Wakati dunia ikijielekeza katika matumizi ya nishati safi, ni wakati sahihi kwa nchi kusisitiza wadau wa madini kutumia fursa hii kuwekeza nchini kwenye utafutaji,***

***uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani kwenye madini muhimu na mkakati.***

**(c) Kuhamasisha Uwekezaji, Uanzishwaji wa Minada, Maonesho ya Madini ya Vito na Uongezaji Thamani Madini**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini ilifanya mnada wa kwanza wa madini ya vito ndani ya nchi tarehe 14 Desemba, 2024 na mnada wa pili tarehe 8 Aprili, 2025 katika Mkoa wa kimadini wa Mirerani. Katika minada hiyo, jumla ya wanunuzi 60 walipatikana kama washindi wa mnada na kufanikiwa kununua madini yenye thamani ya shilingi 2,509,245,216.00 na kuwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi 163,084,534.84 ikijumuisha mrabaha wa shilingi 149,218,787.80, ada ya ukaguzi ya shilingi 11,390,747.16, ada ya usimamizi wa mnada ya shilingi 2,509,245.22 na ada ya ushiriki wa mnada shilingi 6,850,852.50. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Madini inategemea kufanya minada na maonesho ya kitaifa katika mikoa ya kimadini ya Arusha, Mirerani, Mahenge, Ruvuma na Tanga. Vilevile, maonesho ya kimataifa yanatarajiwa kufanyika Zanzibar na katika Miji ya Dar es Salaam na Arusha.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha uwekezaji nchini, Wizara ilitangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa Umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi, kwenye vyombo vya habari na kwenye mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Wizara ilishiriki kwenye mikutano, makongamano na maonesho ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kuvutia wawekezaji. Fursa hizo zilitangazwa kupitia Mkutano wa Future Minerals Forum – Saudi Arabia, Mining Indaba–Afrika Kusini, Prospectors and Developers Association of Canada (PDAC) – Canada, Africa Down Under – Australia, African Diamond Producers Association (ADPA) – Zimbabwe na kwenye Maonesho ya 68 ya Vito na Usonara yaliyofanyika jijini Bangkok nchini Thailand.



**Picha Na. 1**: *Mheshimiwa Dkt. Doto M. Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati (katikati) akisikiliza maelezo kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini kutoka kwa Kamishna wa Madini Dkt. Abdulrahman Mwanga (aliyeshika kipaza sauti) alipotembelea Banda la Wizara ya Madini katika Maonesho ya Saba ya Teknolojia na Uwekezaji kwenye Sekta ya Madini yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Bombambili mkoani Geita.*

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kushiriki mikutano na maonesho ya ndani ikiwemo Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika JNICC, Dar es Salaam ambao uliandaliwa kwa mafanikio makubwa kwa kushirikiana na Tanzania Chamber of Mines (TCM) ambao wamekuwa wadau muhimu katika kuendeleza Sekta ya Madini nchini, Maonesho ya NaneNane Mkoani Dodoma, Maonesho ya Saba ya Teknolojia na Uwekezaji katika Sekta ya Madini yaliyofanyika mjini Geita.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maonesho mengine yalifanyika katika Mkutano wa Chama cha Wajiolojia Tanzania (TGS) -Tanga, Mkutano wa Shirikisho la Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania (FEMATA) uliofanyika Dodoma na Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya

Sabasaba yaliyofanyika Dar es Salaam. Washiriki waliotembelea mabanda ya Wizara na taasisi zake ambapo walipata elimu kuhusu majukumu, sera, sheria na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini pamoja na kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo.




**Picha Na. 2:** *Washiriki wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini uliofanyika Novemba 2024 Jijini Dar es Salaam***.**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mikutano hiyo kampuni mbalimbali zilionesha nia ya kuwekeza nchini na washiriki walipata nafasi ya kujifunza na kuongeza ujuzi kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli za madini, kujenga na kukuza diplomasia ya uchumi ambayo ni msingi wa ustawi wa biashara na uwekezaji baina ya nchi yetu na nchi nyingine.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** watanzania na wadau wameendelea kuelimishwa na kufahamishwa kuhusu uwepo wa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini ikiwemo sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta. Aidha, elimu imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwa ni pamoja na Jarida la Madini na programu maalumu za urushwaji wa vipindi mubashara vilivyoelezea masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini. Vyombo hivyo ni pamoja na *TBC, Clouds Media, Crown Media, ITV, Kiss FM, Azam Media, Wasafi Media, VOA, BBC, DW, TRT, Radio France, ZBC na Morning Star.*

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kusimamia Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini) za Mwaka 2020 ambazo zinasimamia na kuratibu shughuli za uongezaji thamani madini kwa kila aina ya madini yapatikanayo hapa nchini. Aidha,



katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni ya kusafisha madini ya dhahabu kwa kampuni ya Giant Machine and Equipment Limited-Chunya.

**Picha Na. 3:** *Mheshimiwa Athony P. Mavunde Akikagua Ujenzi wa Kiwanda cha Uongezaji Thamani Madini ya Shaba cha Kampuni ya Mineral Access System Tanzania (MAST).*

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya majadiliano na wachimbaji wakubwa wa madini ya dhahabu nchini kwa ajili ya kutenga asilimia 20 ya sehemu ya uzalishaji wao ili isafishwe katika viwanda vilivyopo na kuuzwa nchini. Kupitia utaratibu huu, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kununua na kuhifadhi dhahabu ambapo hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha tani 3.16

zimenunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo na wa kati. Aidha, Wizara kupitia Kituo cha TGC kilichopo Jijini Arusha imeendelea kusimamia na kuboresha utolewaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito na baadhi ya madini ya metali.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuvutia na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini kwa kupunguza mrabaha kutoka asilimia 6 hadi asilimia 4, kuondoa ada ya ukaguzi ya asilimia 1 na kuondoa asilimia 18 ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kuwa asilimia sifuri kwa madini ya dhahabu yanayosafishwa kwenye viwanda vya usafishaji dhahabu vilivyopo nchini. Kupitia mkakati huu, katika kipindi husika, kiasi cha dhahabu kilichopokelewa na kusafishwa katika viwanda vya ndani kilikuwa ni tani 4.55 ambapo dhahabu iliyonunuliwa na BoT ni tani 2.97.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi sasa Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni nane (8) za viwanda vya kusafisha madini nchini. Kati ya hizo, leseni saba (7) ni za viwanda vya kusafisha dhahabu na leseni moja (1) ni kiwanda cha kusafisha madini ya shaba, nikeli na kobati. Aidha, leseni hizo zimetolewa kwa kampuni za Geita Gold Refinery (GGR), Mwanza Precious Metal Refinery Company Limited, Banjul Limited, Sab Gold Limited, Eyes of Africa Limited, Africa Eyes Limited, Giant Machine and Equipment Limited na Tembo Nickle Refining Company Limited. Vilevile, kiwanda cha kusafisha dhahabu GGR kimepata cheti cha utambuzi kinachojulikana kama Responsible Minerals Initiative (RMI) ikiwa ni hatua mojawapo kuelekea kupata Ithibati ya *London Bullion Market Association* (LBMA).

***Nitoe rai kwa kampuni zote za uchimbaji na wafanyabiashara wa madini ya dhahabu kusafisha madini kupitia viwanda vilivyopo nchini kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123.***

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito nchini, Wizara kupitia

Kituo cha TGC imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8) litakalokuwa na madarasa, hosteli ya wanafunzi, karakana ya uongezaji thamani madini, maabara za madini ya vito, bidhaa za usonara na ofisi za watumishi.

**(d) Kuendelea Kufanya Utafiti wa Kina wa Jiofizikia kwa Njia ya Kurusha Ndege (High-resolution Airborne Geophysical Survey)**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa kurusha ndege za utafiti wa madini kwa njia ya *high-resolution airborne geophysical survey* kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo. Katika kutekeleza hili, Wizara imefanya majaribio kwa kurusha ndege nyuki katika maeneo ya Mkoa wa Dodoma, Shinyanga, Geita, Lindi na Mkoa wa kimadini Mirerani. Hatua hii ililenga kuthibitisha ufanisi wa matumizi ya ndege nyuki katika utafutaji wa kina wa madini. Matokeo ya utafiti huo umebainisha uwezekano wa kutumia ndege nyuki kwenye utafutaji wa madini kwa maeneo ya wachimbaji wadogo. Hatua hii itawasaidia wachimbaji wadogo kutumia gharama ndogo kuwezesha kufanya utafiti na kuepusha kufanya uchimbaji wa kubahatisha.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia GST inaendelea na hatua mbalimbali kwa kushirikiana na Wakala wa Ndege za Serikali (Tanzania Government Flight Agency - TGFA) ili kuwezesha ununuzi na upatikanaji wa Helikopta ambayo itatumika katika mradi mkubwa wa utafiti wa madini nchini kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa utafiti wa kina wa Jiofizikia. Hatua hii itasaidia sana kukusanya taarifa nyingi za kina kwa wakati na kuwezesha taarifa hizo kukuza uwekezaji katika sekta ya madini kama vile kurahisisha utafutaji kama vile uchorongaji mahali sahihi na hatimae kupelekea uanzishwaji wa migodi. Aidha, taarifa hizi zitatumika kuwapanga wachimbaji kulingana na aina

ya madini katika maeneo yenye rasilimali Madini ili kupunguza upotevu wa mitaji yao.

**(e) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kuwasogezea Huduma za Ugani**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) imeendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo kwa kutoa huduma za kitaalamu kwa wachimbaji wadogo katika nyanja za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji madini pamoja na utunzaji wa mazingira. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wachimbaji wadogo 471 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano vya Katente, Lwamgasa na Itumbi ambapo mpaka sasa wachimbaji 12 wa madini wameanzisha vituo vyao baada ya kujifunza kupitia vituo hivyo. Aidha, kupitia vituo vya mfano, huduma ya uchenjuaji mbale za dhahabu kwa wateja 41 ilitolewa ambapo dhahabu ya uzito wa kilogramu 119.57 yenye thamani ya shilingi 23,318,849,170.45 ilichenjuliwa.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata taarifa za jiolojia, huduma za uchorongaji kwa gharama nafuu zilitolewa kwa wachimbaji wadogo 14 katika maeneo ya Tambi–Mpwapwa, Nyawa–Bariadi, Matondo, Makongolosi na Matundasi–Chunya, Lwamgasa, Nyaruyeye, Nyakagwe na Nyamalimbe–Geita, Endabash-Karatu pamoja na Mavota–Biharamulo. Jumla ya mita 3,306.47 zimechorongwa katika maeneo hayo.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuwahamasisha wachimbaji wadogo kuanzisha vikundi katika shughuli za madini na kutunza kumbukumbu za uzalishaji na biashara za madini ikiwa ni miongoni mwa vigezo vya kuwawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya shilingi 51,422,401,572.00 zilikopeshwa kwa wachimbaji wadogo 127.

***Nitumie fursa hii kuzishukuru benki za NMB, NBC, CRDB, AZANIA* na *KCB kwa kukubali kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo, pia niwaombe waendelee kupanua wigo wa ukopeshaji. Nitoe wito kwa taasisi nyingine za fedha zione umuhimu wa kuwakopesha wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa tija.***

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada hizo za Serikali, tarehe 27 Machi 2025 Wizara ilikutana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini wakiwemo FEMATA na kujadiliana namna bora ya kuwasaidia wachimbaji wadogo waweze kunufaika zaidi na rasilimali za madini. Katika majadiliano hayo, vyama vya wachimbaji vilitoa maoni yao kuhusu namna Wizara inavyoweza kusaidia wachimbaji wadogo ili waweze kuzalisha madini mengi kwa ubora unaotakiwa. Aidha, kupitia majadiliano hayo, masuala mbalimbali yaliafikiwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya wachimbaji wadogo na Wizara inayafanyia kazi.

**(f) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini ili Ziweze Kutekeleza Majukumu Yake kwa Ufanisi na Tija Zaidi**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizo chini yake zinatekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuzipatia vitendea kazi na rasilimaliwatu. Tume ya Madini imewezeshwa kupata magari 34 kwa ajili ya ukusanyaji wa maduhuli na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ambao umefikia asilimia 92.8; STAMICO imewezeshwa kununua mitambo 2 ya uzalishaji wa mkaa mbadala (coal briquette) ambayo imesimikwa Kisarawe-Pwani na Kiwira-Songwe pamoja na mitambo 10 ya uchorongaji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo; GST imewezeshwa kununua vitendea kazi (generators, GDD IP receivers with IP Generator, Abem Terramiter LS2, electrical equipment, IT, geological equipment, advance grinding and polishing machine, UVVIS machine, projector, data communication equipment, television, aluminium reels

and copper wire, mounting pressing machine, Seismic Survey Equipment, Proton Magnetometer, GPS na External Battery, Forklift na Sectioning Machine) kwa ajili ya shughuli za utafiti wa madini; na Kituo cha TGC kimewezeshwa kuboresha miundombinu ya kufundishia kwa lengo la kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini.



**Picha Na. 4:** *Mheshimiwa Athony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini Akizindua Magari 34 ya Tume ya Madini kwa ajili ya kuimarisha shughuli za Tume ya Madini.*

**d.Utekelezaji wa Maeneo Mengine kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imetekeleza majukumu yake mengine kama ifuatavyo:

**(i) *Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini inaendelea na utekelezaji wa ***Mining Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri*** inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti wa rasilimali madini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa; kuboresha maisha ya watanzania; na kutoa fursa kwa mtanzania yeyote wakiwemo wakina mama, vijana na wenye mahitaji maalum kujiongezea kipato na hatimaye kutajirika kupitia shughuli za madini.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha hili, mambo yafuatayo yamezingatiwa ikiwa ni maeneo makuu

yanayounda misingi ya maono hayo: Upatikanaji wa taarifa za jiosayansi hususan taarifa za kina za jiofizikia *(High Resolution Geophysical Survey)* kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia angalau asilimia 50 ifikapo mwaka 2030; kuboresha mfumo wa kisheria na kitaasisi ili kuwa na usimamizi makini na uliowazi wa Sekta ya Madini; na kuiwezesha Sekta ya Madini kufungamana na sekta nyingine za kiuchumi hususan Sekta za Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Fedha na nyingine zinazotoa huduma kwenye Sekta ya Madini.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine yanayozingatiwa katika *Mining Vision 2030* ni pamoja na kuboresha shughuli za wachimbaji wadogo hususan urasimishaji wa shughuli zao, kuwezesha upatikanaji wa teknolojia za kisasa na rahisi, masoko ya madini, na upatikanaji wa mitaji; na usimamizi thabiti wa shughuli za utunzaji mazingira kwa kushirikiana na Taasisi nyingine ili shughuli za madini zisiwe na athari hasi kwenye mazingira.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ***Mining Vision 2030*** inafikiwa, Wizara kupitia STAMICO imeendelea kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo kwa kununua mitambo 10 ya uchorongaji. Mitambo hiyo itachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa za kina za jiosayansi hususan kuthibitisha uwepo wa madini mbalimbali katika maeneo yanayomilikiwa na wachimbaji wadogo.

**(ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini imekamilisha maandalizi ya Programu ya MBT ambayo itatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2030. Programu hii ni ya kimageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kushughulikia changamoto na kuboresha fursa kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum ili kuongeza ushiriki wa makundi hayo katika mnyororo wa thamani wa madini.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu hii inatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo: kuongeza kipato na kuboresha maisha ya wanawake, vijana na wenye mahitaji maalum; kuwaongezea fursa za ajira; na kuongezeka kwa kiwango cha uwekezaji kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika Sekta ya Madini. Aidha, Programu hii itasaidia kuboresha viwango vya afya, usalama na utunzaji wa mazingira katika maeneo yenye shughuli za madini.

**(iii) Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania (Tanzania Critical and Strategic Minerals Strategy)**

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini ipo katika hatua za kukamilisha uandishi wa Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati Tanzania. Lengo kuu la mkakati huu ni kuwa na maendeleo endelevu ya rasilimali madini muhimu na madini mkakati ili madini hayo yaweze kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa, kuboresha maisha ya watanzania, na kuchangia katika agenda ya kitaifa na kimataifa kuhusu uchumi wa kijani na kidijitali (green and digital economy).

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za kuandaa mkakati wa madini muhimu, GST imeainisha orodha ya madini muhimu na madini mkakati ambapo aina ya madini muhimu (critical minerals) ni 25 na madini mkakati (strategic minerals) ni 18. Hivyo, Wizara inaendelea na taratibu za kuwashirikisha wadau kabla orodha hiyo kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**(iv) Usimamizi wa Sheria**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini Sura 123 na kuhakikisha taratibu zote zinazingatiwa kwa ustawi wa Sekta ya Madini nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau

imeendelea kufanya marekebisho ya mifumo ya kisheria ya usimamizi wa Sekta ya Madini pale inapoonekana kuna umuhimu ili kurahisisha usimamizi wa Sheria ya Madini na kuendelea kuweka mazingira wezeshi na bora ya uwekezaji katika sekta. Hatua hii imeleta utulivu mkubwa katika sekta na kuwezesha Wizara na Serikali kufikia malengo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025 Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwenye Kifungu cha 88 kwa kuongeza kifungu kipya cha 88A ili kuweka jukumu kwa taasisi za umma zenye kandarasi za ujenzi kuzuia au kukata malipo ya mrabaha (royalty) na ada za ukaguzi kutoka kwenye fedha zinazolipwa kwa Kampuni za ujenzi zinazotumia madini ujenzi na kuziwasilisha Tume ya Madini ndani ya siku 7 tangu siku ya kukusanya mrabaha husika na ada ya ukaguzi. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na matumizi ya madini katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali nchini.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho kwenye Kanuni za Masoko ya Madini ya Mwaka 2019 ili kurejesha minada na maonesho ya kimataifa ya madini nchini. Kanuni tajwa zimefanyiwa marekebisho katika Jedwali la Kanuni hii kuruhusu madini ya vito yanayouzwa katika minada au maonesho ya madini kusafirishwa nje ya nchi kwa kulipa kiwango kikubwa zaidi cha mrabaha wa asilimia 15. Lengo la marekebisho hayo ni kuvutia wanunuzi wa madini kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye minada ili kununua madini kwa bei shindani na kuwezesha bei ya madini hususan *tanzanite* kuendelea kuimarika.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha utungwaji wa Kanuni Mpya za Madini (Msaada wa Kiufundi kwa Wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini) za Mwaka 2025. Kanuni hizi mpya zilizotangazwa katika

Gazeti la Serikali kupitia Tangazo Na.260 la tarehe 25 Aprili, 2025 zinatoa fursa kwa mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini (PML) kuingia mkataba wa msaada wa kiufundi na Mwezeshaji kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 8(3) cha Sheria ya Madini, Sura 123. Kanuni hizi zinaweka misingi, utaratibu na mazingira wezeshi ya wamiliki wa PML kuingia mikataba yenye tija kwa lengo la kuhakikisha kuwa wamiliki wa leseni hizo wanapata teknolojia ya kisasa ya uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji na usafishaji madini. Hatua hii itarahisisha shughuli za uchimbaji madini hapa nchini. Kupitia mikataba hiyo, itawawezesha wachimbaji wengi kukua kiuchumi na hatimaye kuendesha migodi yao kwa uchimbaji bora unaotunza mazingira na kukuza matumizi ya teknolojia na utaalamu bora.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini (PML) ambao watataka kunufaika na msaada wa kiufundi kutoka kwa wawezeshaji, wanashauriwa wachimbe wenyewe badala ya kuingiza wachimbaji wadogo ndani ya maeneo ya leseni ili wakipata msaada wa kiufundi iwe rahisi kwao kufanya makubaliano na Wawezeshaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna mchimbaji mdogo anayepoteza haki yake kwa kuingia makubaliano yasiyokuwa na tija.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia Tangazo katika Gazeti la Serikali Na.253 la tarehe 25 Aprili 2025, imekamilisha marekebisho ya Kanuni za Haki Madini, 2018 ili kusimamia ipasavyo shughuli za uchimbaji madini zinazofanywa katika vitalu maalum vya uchimbaji (maduara), na watu wengine isipokuwa mmiliki wa leseni, wafanyakazi wake, au mawakala wake, ndani ya eneo la leseni ndogo ya uchimbaji madini iliyotolewa chini ya Sheria. Aidha, Kanuni hizo zinaweka masharti kama ifuatavyo: Ikiwa mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini anaruhusu watu ambao si wafanyakazi wake au mawakala wake kufanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya uchimbaji mdogo ndani ya eneo la leseni, anapaswa kusajili mkataba

Tume ya Madini ambao unabainisha haki na wajibu wa watu hao; na Mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini atatakiwa kuandaa na kutunza rejista ya watu wote wanaofanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya uchimbaji mdogo, kwa kuzingatia maelekezo ambayo Tume ya Madini itaamua.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini atahakikisha kwamba mmiliki wa kitalu cha uchimbaji mdogo anazingatia masuala ya kisheria na ya kiudhibiti yanayohusu mazoea mazuri ya uchimbaji bora, afya, usalama, na utunzaji wa mazingira; na Pale ambapo mmiliki wa kitalu cha uchimbaji mdogo anashindwa kuzingatia sharti lolote la leseni au sharti lolote la kisheria linalotumika kwenye leseni hiyo, mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji atakuwa amekiuka sheria na atachukuliwa hatua kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Madini, Sura 123.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini anayekusudia kuhamisha umiliki wote wa haki madini au sehemu ya umiliki huo kwenda kwa mtu mwingine, atalazimika kupata ridhaa kutoka kwa Tume ya Madini; na Pale ambapo uhamisho wa umiliki wa haki madini unahusisha leseni ndogo ya uchimbaji madini ambayo ina ombi la msaada wa kiufundi chini ya Kifungu cha 8 (3) cha Sheria, Tume ya Madini itazingatia haki na wajibu wa mmiliki wa leseni pamoja na watu wengine wanaofanya kazi katika vitalu vya uchimbaji mdogo kwa mujibu wa makubaliano yaliyosajiliwa na Tume ya Madini.

***Naomba nitoe msisitizo kuwa Leseni zote zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya vikundi vya wachimbaji wadogo, limewekwa sharti la lazima la kukitaka kikundi chenye lengo la kutaka kupata msaada wa kiufundi au kuuza leseni yake kwa Mwekezaji kupata kwanza kibali cha Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini baada ya kujiridhisha juu ya msaada wa kiufundi unaotaka***

***kutolewa na pia kujiridhisha namna ambavyo pande zote zitanufaika ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.***

**(v) Marekebisho ya Sheria na Kanuni**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 kwenye Kifungu cha 88 kwa kuongeza kifungu cha 88A. Kifungu hiki kinalenga kutoa jukumu kwa taasisi za umma kuzuia malipo ya mrabaha (royalty) na ada za ukaguzi kutoka kwenye fedha zinazolipwa kwa kampuni za ujenzi na kuziwasilisha Tume ya Madini ndani ya siku 7 tangu siku ya kukusanya. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa kodi, kudhibiti ukwepaji wa kodi na kuongeza mapato yatokanayo na mrabaha na ada za ukaguzi yanayolipwa na wakandarasi katika Sekta ya Ujenzi.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Madini katika kifungu cha 5 kwa kuongeza Kifungu cha 5B ili kutambua madini muhimu na madini mkakati. Kupitia marekebisho hayo, Waziri wa Madini ataweza kutangaza madini muhimu na madini mkakati baada ya kupokea mapendekezo ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na kupata idhini ya Baraza la Mawaziri. Lengo ni kuweka usimamizi thabiti ili kupata manufaa mapana kupitia mnyororo wa thamani wa madini hayo.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Madini katika kifungu cha 27F kwa kuongeza Kifungu kidogo cha 5 na 6 ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki madini ambao wanatoa taarifa za uongo au zenye kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini. Aidha, kifungu kidogo cha (6) kilichopo kimefanyiwa marekebisho kwa kuongeza takwa la kuhakiki taarifa za sampuli za madini ambazo zinasafirishwa nje ya nchi na wamiliki wa haki madini na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST). Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha wamiliki wa haki madini wanawasilisha taarifa sahihi za madini GST

kama inavyotakiwa chini ya Sheria; na kufahamu ubora na aina za madini zilizopo katika sampuli za madini zinazosafirishwa nje ya nchi.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Madini katika kifungu cha 8 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (c) ili kuweka ukomo wa muda wa maombi ya kupewa haki madini na pale ambapo muombaji ameshindwa kulipa ada ya maombi ya eneo husika ndani ya siku ishirini na nane (28) ombi hilo litaondolewa na eneo litakuwa wazi kwa waombaji wengine. Lengo la marekebisho ni kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati. Kupitia marekebisho haya waombaji wa leseni za madini watalazimika kulipa ada kwa wakati ili kuanza shughuli za madini katika maeneo yao jambo ambalo litachochea ukuaji wa Sekta ya Madini.

**(vi) Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Rasilimaliwatu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha utendaji kazi unaimarika na malengo ya Wizara yanafikiwa. Hivyo, Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kusimamia utendaji kazi na maslahi ya watumishi wake pamoja na kujaza nafasi zilizo wazi. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara na Taasisi zake imejaza nafasi 55 kwa utaratibu wa uhamisho. Aidha, kupitia uhamisho huo, Wizara imepata watumishi (14), STAMICO (9), Tume ya Madini (15), TEITI (7) na GST (10). Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana kwa wakati.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa masuala ya mafunzo kwa watumishi, Wizara na Taasisi zake zimewawezesha watumishi 544 kupata mafunzo. Aidha, kati yao watumishi 487 walipata mafunzo ya muda

mfupi na 57 ya muda mrefu katika masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuwa na Rasilimaliwatu, suala la mazingira bora ya kufanyia kazi ni muhimu. Hivyo, Wizara imeendelea kuhakikisha watumishi wake wanapatiwa vitendea kazi. Aidha, ujenzi wa jengo la makao makuu ya Wizara umefikia asilimia 92.8 na jengo la makao makuu ya Tume ya Madini umefikia asilimia 92. Kukamilika kwa majengo hayo kutawezesha watumishi kuwa na mazingira bora ya kufanyia kazi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuiwezesha Tume ya Madini katika maandalizi ya awali ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mikoa mitatu (3) ya kimadini ya Songwe, Rukwa na Mahenge. Sambamba na hili, taratibu za ununuzi wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Maafisa Madini Wakazi katika mikoa mitano (5) ya Kimadini ya Mbogwe, Dar es Salaam, Iringa, Mwanza na Manyara zinaendelea.

### (vii) Masuala Mtambuka

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** suala la afya ya watumishi ni jambo muhimu ili kuwezesha watumishi kutoa huduma nzuri na inayofaa. Hivyo, Wizara imeendelea kutoa mafunzo yanayohusu udhibiti wa Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY). Aidha, Wizara imeendelea kuziwezesha timu za michezo kushiriki mashindano ya SHIMIWI, SHIMUTA na MEIMOSI. Vilevile, watumishi wa Wizara na Taasisi zake wamehamasishwa kushiriki mazoezi na bonanza yanayoandaliwa kwa ajili ya kuimarisha afya na mahusiano. Pia, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU waliojitokeza kwa hiari yao. Huduma hizo ni pamoja na kuwapatia fedha kwa ajili ya huduma ya lishe bora. Wizara imeendelea kushawishi watumishi kupima afya

kwa hiari na kuwapatia vifaa kinga ili kupambana na maambukizi ya VVU.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na suala la afya, maadili ya watumishi ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu yao. Hivyo, Wizara na Taasisi zake imeendelea kutoa mafunzo kuhusu maadili katika utumishi wa Umma, masuala ya kupambana na rushwa, kuunda Kamati za Kusimamia Maadili ya Watumishi katika maeneo ya kazi, kuweka Mkataba wa Huduma kwa Wateja pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaokiuka maadili ya utumishi.

### e. Utekelezaji wa Shughuli za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuzisimamia na kuziwezesha taasisi zake tano (5) ili ziendelee kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuzingatia Sera, Sheria na Miongozo inayosimamia Sekta ya Madini. Taasisi hizo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC); na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI). Taarifa ya utekelezaji wa taasisi ni kama ifuatavyo:

### a. *TUME YA MADINI*

#### (i) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Tume ya Madini ilitoa leseni 8,501 ikilinganishwa na lengo la kutoa leseni 10,294. Leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Leseni ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini (SMLs)–1; Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs) - 25; Leseni za Utafutaji wa Madini (PLs) - 396; Leseni za Uchimbaji Mdogo (PMLs) – 6,227; Leseni Kubwa za Biashara (DLs) – 548; Leseni Ndogo za

Biashara (BLs) – 1,290; Leseni za Uyeyushaji (RFLs) – 1; na Leseni za Uchenjuaji wa Madini (PCLs) – 13.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, leseni 118 za utafutaji wa madini na leseni 41 za uchimbaji wa kati wa madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutozingatia masharti ya leseni ikiwa ni pamoja na kutolipa ada za mwaka na kutoendeleza maeneo ya leseni. Aidha, leseni 5 za utafutaji madini na leseni 9 za uchimbaji wa kati zilifutwa baada ya wamiliki wake kushindwa kurekebisha makosa hayo.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Madini imeendelea kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambapo hadi kufikia Machi 2025 maeneo 65 yametengwa katika Mikoa ya kimadini ikiwemo Geita, Mara, Mbogwe, Kahama, Chunya na Songwe.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** sampuli 972 za makinikia ya Shaba zilipokelewa na kufanyiwa uchunguzi kutoka katika migodi ya Bulyanhulu Gold Mine, Katavi Mining Company Limited, Jiuxing (TZ) Mining Limited pamoja na ZEM (T) Company Limited. Vilevile, sampuli 4,011 za wateja binafsi zilipokelewa na kufanyiwa uchunguzi. Lengo ni kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi katika uchimbaji na biashara ya Madini. Kutokana na uchunguzi huo, shilingi 296,732,000.00 zilikusanywa kama tozo stahiki za Serikali.

**(ii) Usimamizi, Ukaguzi na Biashara ya Madini**

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 madini yenye thamani ya shilingi 11,376,270,882,758.50 yalizalishwa na kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi 726,219,317,398.14 ambapo shilingi 612,593,046,886.50 ni malipo ya mrabaha na shilingi 113,626,270,511.64 ni malipo ya ada ya Ukaguzi.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, vituo saba (7) vipya vya ununuzi wa madini vilianzishwa ambavyo ni Nhungwiza - Geita, Nachingwea, Liwale na Likofia - Lindi, Mugumu na Serengeti - Mara, na Ikinabusu - Simiyu. Hii inafanya idadi ya vituo vya ununuzi wa madini kufikia 109. Aidha, katika kipindi husika, Wizara imeyatambua na kuyapa hadhi ya vituo vya ununuzi jumla ya maeneo 142 yanayotumika kufanyia biashara ya madini kwa wingi (bulk minerals) kupitia Gazeti la Serikali Na. 906 ya tarehe 15 Novemba, 2024.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali ziliendelea kusimamia uendeshaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini. Kupitia usimamizi huo, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mauzo ya shilingi 2,819,220,651,824.38 yalifanyika katika masoko ikilinganishwa na mauzo shilingi 1,930,698,791,589.30 yaliyofanyika katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Kutokana na mauzo hayo, Serikali imekusanya kiasi cha shilingi 182,043,495,150.21 ikiwa ni tozo ya mrabaha na ada ya ukaguzi ikilinganishwa na shilingi 136,731,358,413.41 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2023/2024.

### (iii) Utambuzi na Uthaminishaji wa Madini

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini iliendelea kusimamia shughuli za uchambuzi na uthaminishaji wa madini yote yaliyozalishwa na kutoa vyeti vya uthaminishaji wa madini pamoja na vibali vya usafirishaji (export permits na kimberley process certificates) na uingizaji madini (import permits). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vibali 9,540 vya usafirishaji madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 8,809 vilivyotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Thamani ya madini kwa vibali hivyo ni shilingi 9,252,791,412,068.11. Aidha, jumla ya vibali 116 vya uingizaji madini nchini (Import permits)

vilitolewa ambapo madini yenye thamani ya dola za Marekani 14,813,664.38 yaliruhusiwa kuingia nchini.

**(iv) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Tume ya Madini imefanya ukaguzi kwa kampuni 21 za uchimbaji, miradi ya barabara na biashara ya madini. Kati ya kampuni hizo, sita (6) ni za uchimbaji madini ya dhahabu, 11 miradi ya barabara ambayo inatumia madini ujenzi, moja (1) ni ya uchimbaji madini ujenzi, moja (1) ni ya uchimbaji wa madini ya Almasi, moja (1) ni ya umwagiliaji ambayo inatumia madini ujenzi na moja (1) ni kiwanda cha kusafisha dhahabu.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** kaguzi hizo zimewezesha kuibua hoja mbalimbali zinazohusiana na kutolipwa kwa malipo ya Serikali shilingi 1,255,950,666.52. Kati ya fedha hizo, shilingi 576,917,781.17 zimelipwa baada ya ukaguzi. Kampuni tano (5) zinazodaiwa shilingi 676,032,885.35 zimeahidi kuendelea kulipa deni kwa awamu. Sambamba na hilo, Tume ya Madini imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha deni lote linalipwa kupitia vikao vya maridhiano na pale inapobidi kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123.

**(v) Shughuli za Ukaguzi wa Migodi, Mazingira na Usimamizi wa Baruti**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, shughuli za ukaguzi wa migodi na mazingira zilihusisha masuala ya usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti katika shughuli za madini kama ifuatavyo**:**

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji Wakubwa**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, migodi mikubwa saba (7) ilikaguliwa. Migodi hiyo ni Dangote Cement Co. Ltd, Williamson Diamond Ltd, El-Hillal Minerals, North Mara Gold Mine, Geita Gold Mine, STAMIGOLD na Bulyanhulu Gold Mine.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ukaguzi huo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo kutokuwepo kwa Mipango ya Ufungaji Mgodi (Mine Closure Plans), Mipango ya uchimbaji Madini (Mine Plans), kutokuwepo kwa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhia miambataka (waste rock dumps), uwepo wa visima vya ufuatiliaji wa ubora wa maji (monitoring boreholes) vilivyoharibiwa kutokana na uvamizi pamoja na upanuaji wa mabwawa la topetaka. Migodi ilielekezwa kurekebisha mapungufu hayo na tayari



wamerekebisha.

**Picha Na. 5:** *Baadhi ya Wataalamu wakiwaongoza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutembelea Eneo la Uchimbaji wa chini ya ardhi katika Mgodi wa Bulyanhulu uliopo Msalala, Wilaya ya Kahama.*

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji wa Kati**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya migodi 53 ya uchimbaji wa kati ilikaguliwa katika sehemu mbalimbali nchini. Katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo kukosekana kwa taarifa za usanifu wa maeneo ya kuhifadhi miambataka pamoja na mabwawa ya topetaka. Aidha, wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwa kuzingatia Sheria ya Madini, Sura 123 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambapo migodi husika imerekebisha mapungufu yaliyobainika.

- **Ukaguzi katika Migodi ya Wachimbaji Wadogo**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, ukaguzi ulifanyika kwenye migodi ya wachimbaji wadogo 14,847 katika mikoa 30 ya kimadini nchini. Katika kaguzi hizo baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni pamoja na kutofukiwa kwa mashimo ya uchimbaji yasiyotumika (abandoned pits), kutotumika kwa vifaa kinga, matumizi hafifu ya vifaa kinga na uhifadhi usio salama wa baruti na kukosekana kwa Mipango ya utunzaji wa mazingira (Environmental Protection Plan - EPP). Wahusika walielekezwa kufanyia kazi mapungufu yaliyobainika ili kuwa na uchimbaji salama, endelevu na wenye tija.

- **Ukaguzi wa Maghala, Stoo na Masanduku ya Kuhifadhia Baruti**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya maghala 164, Stoo 268 na masanduku 207 yalikaguliwa katika mikoa yote ya kimadini. Kaguzi hizo zilibaini uwepo wa mpangilio hatarishi wa vilipuzi, ukosefu wa leseni za uendeshaji wa maghala na kutokulipwa kwa ada za mwaka za leseni za maghala. Aidha, wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** mahitaji na matumizi ya baruti kwa sasa yameongezeka kutokana na kuimarika kwa shughuli za uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, vibali 267 vya kuingiza, kupitisha, kutengeneza na kuuza baruti nchini pamoja na vibali vya kusafirisha baruti nje ya nchi vimetolewa. Fedha zilizopatikana kupitia utolewaji wa vibali hivyo ni jumla ya dola za Marekani 133,438.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini ilifanya ukaguzi kwenye maeneo yaliyoombewa kujengwa maghala ya kuhifadhi baruti. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni Indo African Explosives Limited (Dar es salaam); Lindi Jumbo Limited (Lindi); AECI Mining Tanzania Ltd kwa mgodi wa Shanta Singida Gold Mine, Williamson Diamond Limited Shinyanga, Shanta New Luika Gold Mine Songwe; Ruvuma Coal Limited (Ruvuma); na East Africa Harmony Mining Co. Ltd (Tanga). Ukaguzi huo ulibaini kuwa maeneo hayo yalikidhi matakwa ya Sheria ya Baruti, Sura 45 na hivyo kupewa vibali vya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi baruti.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini imetoa vibali kwa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia baruti ambapo maghala nane (8) mapya ya kuhifadhi baruti yamejengwa na kampuni za Heshem Tanzania Co. Ltd (Chunya), China Civil Engineering Construction Corporation (Nzega), Ideal Detonators Tanzania Limited (Pwani), Canuck Company Limited (Kahama), Sekenke One Mining Cooperative Society Limited (Singida), Esap

Mining Services Limited (Songwe) na Tianpin (T) Investment Management Limited (Kahama). Aidha, maghala hayo yatasaidia katika utoaji wa huduma za uchimbaji katika maeneo husika.

- **Ukaguzi wa Mitambo ya Kuchenjua Dhahabu (Vat Leaching, CIP and Elution Plants)**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Tume ya Madini ilifanya ukaguzi wa mitambo ya *Vat leaching* 1,243 kati ya 1,949 iliyopo nchini, CIP 48 kati ya 52 zilizopo nchini na *elution plants* zote 204 zilizopo nchini. Mitambo hiyo ilikaguliwa katika mikoa 25 ya kimadini. Kaguzi hizo zilibaini mapungufu kwenye baadhi ya mitambo ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa mifereji kwenye maeneo yenye udongo wa mabaki ya dhahabu (tailings) na baadhi ya *elution plants* kutokuwa na mfumo wa kuchuja hewa wakati wa uchomaji. Wahusika walirekebisha mapungufu hayo kama walivyoelekezwa.

- **Ukaguzi wa Mabwawa ya Kuhifadhia Topetaka (TSF)**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya mabwawa 36 ya kuhifadhia topetaka yalikaguliwa kwa lengo la kutoa vibali vya ujenzi au kuruhusu matumizi ya mabwawa hayo. Katika ukaguzi huo miradi miwili (2) kati ya 36 ya uchimbaji madini ilikidhi vigezo na kupewa vibali vya ujenzi wa TSF.

- **Ukaguzi wa Mifumo ya Kupandisha na Kushusha Watu na Mizigo Migodini (Hoisting Systems)**

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Jumla ya migodi 20 ya uchimbaji madini iliwasilisha maombi ya uidhinishaji wa mifumo ya kupandisha na kushusha watu na mizigo mgodini ambapo mifumo katika migodi tisa (9) ilikaguliwa.

Ukaguzi ulilenga kuhakikisha kama mifumo hiyo imekidhi vigezo stahiki ili iweze kupata idhini ya matumizi kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Migodi. Hata hivyo ukaguzi huo ulibaini kuwa migodi miwili (2) haikukidhi vigezo kwa kuwa ilikutwa na mapungufu mbalimbali ya kiufundi.

- **Kupitia Taarifa za Mipango ya Ufungaji Migodi (MCP) na Uchimbaji Madini (Mine Plan)**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mipango ya Ufungaji Migodi 26 ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi (National Mine Closure Committee – NMCC). Kati ya Mipango hiyo, Mipango ya migodi 11 ilikidhi vigezo na kuidhinishwa na mipango 15 haikuidhinishwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kukosekana kwa miradi ya kiuchumi (social closure projects) kwa jamii baada ya maisha ya mgodi, kukosekana kwa bajeti ya mwaka ya urejeshwaji wa mazingira na kukosekana kwa mpango wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, NMCC ilifanya ukaguzi katika Mgodi wa Buzwagi kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa ufungaji mgodi na kubaini kuwa Mgodi uko katika hatua za mwisho za kukamilisha ufungaji. Vilevile, NMCC ilitembelea mgodi wa dhahabu wa North Mara kwa lengo la kukagua maendeleo ya ujenzi wa kuinua tuta (Lift 9) katika bwawa la topetaka ikiwa ni hatua ya ufungaji wa bwawa hilo.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa taarifa za mipango ya uchimbaji madini, Tume ya Madini ilipokea na kuchambua mipango ya uchimbaji (Mine Plans) kutoka katika migodi mikubwa na migodi ya kati. Hadi sasa jumla ya mipango 26 imejadiliwa ambapo mipango 11 ilikidhi vigezo na kuidhinishwa, mipango miwili (2) ilikataliwa na migodi husika ilielekezwa kuandaa mipango mipya na mipango 13 haikuidhinishwa

kutokana na kutokidhi vigezo na kuelekezwa kufanya maboresho yanayotakiwa.

**(vi) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Matakwa ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania Migodini**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Tume ya Madini ilifanya jumla ya kaguzi 10 za utekelezaji wa ushirikishwaji wa watanzania. Taarifa za kaguzi katika kampuni za Williamson Diamonds Limited - Kishapu Shinyanga, Capital Quarry – Dodoma, Cata Mining Co. Ltd - Musoma Mara, Zem Development Tanzania limited - Shinyanga na Mwanza Precious Metals Refinery zimekamilika na matokeo kubainisha kuwa baadhi ya vifungu vya Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania havikuzingatiwa na kupelekea kuzipatia adhabu na elimu kuhusu Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za mwaka 2018 na marekebisho yake. Ukaguzi wa kampuni za ubia za METC - Paulsam Company Limited na Sphinx Limited ambayo yanatoa huduma migodini ili kubaini iwapo uwepo wa ubia huo una manufaa ya uhawilishaji wa teknolojia kwa kampuni za kitanzania. Matokeo ya ukaguzi yalibaini kampuni za kitanzania zinanufaika kwa kupata maarifa stahiki. Hata hivyo, bado upo umuhimu wa kampuni hizo kuwa na Viashiria muhimu vya Utendaji Kazi ili kuweza kufuatilia maeneo ambayo kampuni za kitanzania zinanufaika na kwa kiwango kipi.

- **Ushirikishwaji wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content) na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Tume ya Madini ilipokea na kuidhinisha jumla ya mipango 1,444 ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini. Mipango hiyo ilitoka katika kampuni saba (7) zinazomiliki Leseni ya Uchimbaji Mkubwa (SML), kampuni 16 zinazomiliki Leseni za Uchimbaji wa Kati (ML), Kampuni 17 zinazomiliki Leseni za Utafiti (PL), kampuni 15 zinazomiliki Leseni za

Uchimbaji Mdogo (PML) na kampuni 1,389 za watoa huduma mbalimbali (Contractors and Sub-contractors) kwa wamiliki wa leseni za madini.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa maombi ya idhini ya ununuzi kutoka kwa Wamiliki wa Leseni na Wakandarasi mbalimbali, jumla ya maombi 787 yalipokelewa na kuchambuliwa. Kampuni zilizowasilisha maombi hayo ni pamoja na Bulyanhulu Gold Mining Limited (133), Geita Gold Mining Limited (263), North Mara Gold Mine Limited (104), Mantra Tanzania Ltd (20), Sotta Mining Corporation (89), Buckreef Gold Company Ltd (36), Mamba Minerals Corporation Limited (4), Africa Underground Mining Services Geofields Tanzania (57), Ruvuma Coal Limited (11), Orica Tanzania Ltd (6), Faru Graphite Corporation Limited (4), Tancoal Limited (12), Shanta Mining Company Tanzania Limited (29), Lindi Jumbo Limited (7), Knauf Gypsum Tanzania Limited (6) na CMS Tanzania Limited (6). Maombi 764 yaliidhinishwa na maombi 23 hayakuidhinishwa kwa kuwa hayakukidhi kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za mwaka 2018 na marekebisho yake.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanyika migodini yalifikia dola za Marekani 2,037,145,620. Kati ya mauzo hayo, kampuni za kitanzania zilichangia dola za Marekani 1,797,989,648 sawa na asilimia 88 ya manunuzi yote ikilinganishwa na mwaka 2023 ambapo kampuni za kitanzania ziliuza bidhaa na huduma zenye thamani ya dola za Marekani 1,478,676,709 sawa na asilimia 90 ya manunuzi yote.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** hii inaonesha kuwa, licha ya kushuka kwa asilimia ya ushiriki wa kampuni za kitanzania kutoka asilimia 90 hadi 88, thamani ya mauzo yao imeongezeka kwa zaidi ya dola za Marekani 319,312,940 ikidhihirisha ukuaji wa ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa watanzania wanapewa kipaumbele kwenye ajira zinazozalishwa katika migodi mikubwa na ya kati ya uchimbaji madini hapa nchini. Hadi kufikia Machi 2025 kulikuwa na jumla ya ajira 19,874 ambapo ajira 19,371 sawa na asilimia 97.5 zilitolewa kwa watanzania na ajira 503 sawa na asilimia 2.5 zilikuwa za wageni. Ajira kwa watanzania kwenye migodi zitaendelea kuongezeka ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Madini, Sura 123 na Kanuni za Madini (Ushirikishwaji wa Watanzania) za mwaka 2018.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kwamba wawekezaji kwenye Sekta ya Madini wanawajibika kwa jamii kupitia utekelezaji wa Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za Mwaka 2023. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kiasi cha shilingi 20,145,106,956.29 kimetumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya CSR kwa Halmashauri na miji inayozunguka migodi inayomilikiwa na kampuni mbalimbali ikiwemo Geita Gold Mining Limited, Bulyanhulu Gold Mine Limited, North Mara Gold Mine Limited, Williamson Diamond Limited, Shanta Mining Company Limited, Dangote Cement Limited, Sotta Minerals Corporation Limited, Duma Tanzgraphite na Zem Development Limited.

***Nitoe rai kwa wamiliki wa leseni za Madini na Halmashauri husika kufuata Sheria ya Madini na Kanuni zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za CSR.***

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na usimamizi wa utekelezaji wa CSR, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara na Taasisi zake imetoa mafunzo kuhusu Kanuni za CSR kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini. Wadau hao ni pamoja na kampuni za Buckreef Gold Limited na Sotta Mining Corporation Limited, wachimbaji wa kati na wadogo katika mikoa ya kimadini ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mirerani na Mahenge. Mafunzo

hayo yalisaidia kuongeza uelewa wa kanuni za CSR na wajibu wa kila mdau katika utekelezaji wake.

**b. *SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)***

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imepewa dhamana ya kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwenye mnyororo wa thamani wa madini kwa niaba ya Serikali na kuwezesha, kuhamasisha na kusaidia shughuli za wachimbaji wadogo ili ziwe na tija na zinazozingatia utunzaji wa mazingira. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 STAMICO imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Inayomilikiwa na Kusimamiwa na STAMICO**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO inamiliki na kusimamia miradi mitano (5) ambayo ni: mradi wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira; mradi wa nishati mbadala (Rafiki Briquettes); mradi wa uchorongaji; mradi wa kuchimba kokoto; na mradi wa usimamizi wa vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo wa madini.

- **Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo – Kiwira**

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea na shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya tani 208,866.05 za makaa ya mawe zimezalishwa. Kati ya tani hizo, tani 192,141 ziliuzwa na kuliingizia Shirika fedha kiasi cha shilingi 7,842,310,279.00 na shilingi 1,464,973,702.00 zimelipwa Serikalini ikiwa ni mrabaha na tozo mbalimbali. Kati ya fedha zilizolipwa serikalini, shilingi 448,537,443.00 ni mrabaha, shilingi 163,187,047.00 ni ada ya ukaguzi, shilingi 19,627,762.00 ushuru wa huduma na shilingi 833,621,450.00 ni tozo nyingine.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, mradi huu umetekeleza mpango wa CSR

na kutumia shilingi 50,000,000.00 kwenye ujenzi wa shule ya msingi Kapeta. Aidha, mgodi unatoa huduma ya maji kwa kijiji cha Lema pamoja na huduma ya Zahanati kwa kata zinazozunguka eneo la mgodi za Busale, Ikinga na Ilima.

- **Mradi wa Uchorongaji**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya mita 63,373.80 zilichorongwa kupitia kandarasi za Shirika kwenye mgodi wa GGM, Buckreef, Shanta - Singida na Shanta - Chunya. Kutokana na uchorongaji huo, shilingi 26,244,533,793.38 zimepatikana. Aidha, STAMICO ilipata kandarasi mbili (2) mpya za uchorongaji katika Mgodi wa Shanta Gold Mine – Chunya yenye thamani ya shilingi 3,847,500,000.00 kwa njia ya *reverse circulation* (RC) na Geita Greenfield – Chemba Dodoma yenye thamani ya shilingi 567,200,000.00 kwa njia ya *rotary air blast* (RAB).

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imefanikiwa kununua mitambo miwili (2) ya kisasa kwa ajili ya shughuli za uchorongaji kwa njia ya DD na RC. Mitambo hiyo ina uwezo wa kuchoronga mita 3,000 na mita 400 chini ya ardhi, mtawalia.

- **Mradi wa Nishati Mbadala (Rafiki Briquettes)**

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imeendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa nishati safi itokanayo na makaa ya mawe inayotambulika kama *Rafiki Briquettes*. Katika kipindi rejewa, Shirika limekamilisha usimikaji na kuanza uzalishaji kwa wingi kwa kutumia mitambo miwili (2) katika maeneo ya Kisarawe – Pwani na Kiwira – Songwe.



**Picha Na. 6:** *Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipokea zawadi ya mkaa utokanao na makaa ya mawe wa Rafiki Briquettes unaozalishwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo Dkt. Venance Mwasse, Jijini Mbeya.*

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na usimikaji wa mitambo mingine miwili (2) katika maeneo ya Dodoma na Tabora ambapo ujenzi wa majengo itakaposimikwa mitambo hiyo ipo katika hatua za ukamilishwaji. Hadi sasa Shirika limezalisha tani 1,500.2 za *Rafiki Briquettes* ambazo zimeuzwa kwa taasisi mbalimbali na mawakala. Lengo la Shirika ni kuendana na agenda ya nishati safi ya kupikia ili ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi.



**Picha Na. 7:** *Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Wakikagua Nishati Mbadala (Rafiki Briquettes) katika Mtambo uliopo Kiwira, Songwe.*

- **Mradi wa Kokoto - Chigongwe**

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, STAMICO imekamilisha usimikaji wa mtambo wa kuzalisha kokoto katika eneo la Chigongwe, Dodoma. Mtambo huo una uwezo wa kuzalisha tani 150 hadi 200 kwa saa ambapo hadi kufikia Machi 2025 tani 28,750 zimezalishwa. Kati ya hizo, tani 5,179.95 ziliuzwa na kuliingizia Shirika mapato ya shilingi 278,774,682.00. Aidha, STAMICO imekamilisha usimikaji wa mizani kwa ajili ya kupima uzito wa magari yanayobeba kokoto hizo. Katika kuimarisha shughuli za uzalishaji, Shirika limenunua vitendea kazi ikiwemo *dump trucks* mbili (2), *wheel-loader* moja (1) na *excavator* moja (1).

- **Mradi wa Vituo vya Mfano na Uratibu wa Uchimbaji Mdogo**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya majukumu ya STAMICO ni kuwezesha, kuhamasisha na kusaidia uendelezaji wa shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kutoa huduma za kitaalamu kwa wachimbaji wadogo katika nyanja za utafiti, uchimbaji, uchenjuaji madini pamoja na utunzaji wa mazingira. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wachimbaji wadogo 471 wamepatiwa mafunzo kupitia vituo vya mfano na wiki ya madini iliyofanyika Jijini Dodoma. Aidha, Shirika limetoa huduma za uchenjuaji mbale ya dhahabu katika vituo vya mfano kwa wateja 41 ambapo kilogramu 119.57 za dhahabu zenye thamani ya shilingi 23,318,849,170.45 zilichenjuliwa na kuipatia Serikali mapato ya shilingi 1,739,168,144.04.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika pia limeendelea kutoa huduma ya uchorongaji kwa bei nafuu kwa wachimbaji wadogo. Aidha, katika kipindi husika wachimbaji wadogo 16 wamepata huduma hiyo katika maeneo ya Tambi – Mpwapwa, Nyawa – Bariadi, Matondo, Makongolosi na Matundasi – Chunya, Lwamgasa,

Nyaruyeye, Nyamalimbe na Nyakagwe – Geita, Mavota – Biharamulo, Endabash – Karatu, Mwakitolyo – Shinyanga na Mbangala - Songwe. Katika utekelezaji huo jumla ya mita 3,450.37 zimechorongwa katika maeneo hayo. Ili kuongeza wigo wa huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo, Shirika limeongeza mitambo mingine 10.



**Picha Na. 8:** *Mitambo 10 ya Uchorongaji iliyonunuliwa kwa ajili ya kutoa huduma ya uchorongaji kwa wachimbaji wadogo.*

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto za wazalishaji wa chumvi hapa nchini ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa masoko, Shirika limefanikiwa kuagiza mtambo wa kuchakata na kusafisha chumvi ambapo awamu ya kwanza ya sehemu ya vifaa vya mtambo huo vimewasili. Ujenzi wa kiwanda hicho katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi ulianza Machi 2025 na unatarajiwa kukamilika Agosti 2025.

**(ii) Utekelezaji wa Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, STAMICO imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya ubia ambayo ni Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza na Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef pamoja na kampuni tanzu ya STAMIGOLD Biharamulo.

- **Mradi wa STAMIGOLD – Biharamulo**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMIGOLD ni mgodi unaomilikiwa na Serikali kupitia STAMICO inayomiliki hisa asilimia 99 na Ofisi ya Msajili wa Hazina inayomiliki hisa asilimia 1. Katika kipindi husika mgodi umezalisha dhahabu wakia 3,116.62 na wakia 411.07 za madini ya fedha na kupata shilingi 21,966,481,716.37. Aidha, kutokana na mauzo hayo, mgodi umelipa shilingi 878,659,268.65 Serikalini kama mrabaha na shilingi 65,899,445.15 kama ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo - Kagera. Vilevile, mgodi umeendelea kufanya tafiti katika leseni zake ili kuongeza mashapo na uhai wa mgodi kutoka miaka minne ya sasa hadi miaka nane. Pia, mgodi umenunua vifaa vya uchimbaji ambavyo ni *excavators* mbili (2), *bulldozzer* moja (1), *wheel loader* moja (1), *tipper trucks* sita (6) na *water bowser* moja (1) ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** STAMIGOLD imetekeleza shughuli za CSR ambapo katika kipindi husika imechangia shilingi 16,075,200.00 katika kuboresha miundombinu ya shule ya msingi ya Mafukwe na Nyabusozi katika Wilaya ya Biharamulo.

- **Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza**

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza kinamilikiwa na STAMICO kwa asilimia 25 na Mbia asilimia 75. Kina uwezo wa kusafisha kilo 480 kwa siku za dhahabu kwa kiwango cha kimataifa cha asilimia 99.99. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kiwanda kimenunua dhahabu ghafi tani 1.218 yenye thamani ya dola za Marekani 97,176,222.02 na kulipa Serikalini jumla ya shilingi 10,880,598,074.26 ikiwa ni mrabaha na ushuru wa huduma. Aidha, kiwanda kimetoa huduma za usafishaji dhahabu jumla ya tani 2.304 kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pamoja na wateja wengine (dealers) kwa gharama ya shilingi 1,039,647,854.96. Kiwanda kimeendelea kupokea dhahabu inayonunuliwa na BoT kutoka kwa wachimbaji pamoja na wafanyabiashara, kwa kuifanyia uhakiki wa

ubora kabla ya malipo na kuisafisha kwa ubora wa asilimia 99.99.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa dhahabu kwa ajili ya kusafishwa kiwandani, STAMICO imeendelea kuweka mkakati wa kuwahamasisha wachimbaji wa madini ya dhahabu nchini kupeleka madini hayo katika kiwanda cha usafishaji. Lengo ni kuwezesha kiwanda kupata dhahabu na wachimbaji wadogo kunufaika na fursa ya punguzo la mrabaha katika viwanda vya kusafisha dhahabu.

- **Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef***

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa dhahabu wa Buckreef uliopo mkoani Geita unamilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO yenye hisa asilimia 45 na kampuni ya TANZAM2000 yenye hisa asilimia 55. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2025, mgodi umezalisha wakia za dhahabu 12,971.72. Aidha, ikijumuisha uzalishaji wa nyuma, mgodi umeuza wakia 13,976.99 zenye thamani ya shilingi 94,766,119,964.21. Kutokana na mauzo hayo, mgodi umelipa Serikalini kiasi cha shilingi 6,850,262,275.37 kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** mgodi unaendelea kufanya uchorongaji na utafiti ili kuongeza mashapo ya mgodi ambapo kwa kipindi husika imegundulika uwepo wa mashapo nje ya shimo la uchimbaji. Utafiti unaendelea ili kubaini kiasi cha mashapo yaliyopo kwenye eneo hilo.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mgodi umetumia fedha kiasi cha shilingi 360,913,998.78 kwa ajili ya shughuli za CSR katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Fedha hizo zimetumika kujenga jengo la watumishi katika hospitali ya Busanda, Kituo cha afya Lwamgasa na ujenzi wa madarasa manne (4) na vyoo vinne (4) katika shule za Msingi Shikizi, Katangalo na Kaesa. Miradi hii ni kwa kata

tatu (3) zinazozunguka mgodi kwa mujibu wa bajeti ya mgodi ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, hadi kufikia Machi, 2025 baadhi ya miradi imekamilika na mingine ipo katika hatua za ukamilishaji.

### c. *TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST)*

**147.** ***Mheshimiwa* Spika**, jukumu la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni kufanya tafiti za jiosayansi na ugani wa jiolojia kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini huandaliwa ili kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji wa madini wa kina (detailed exploration) kwa lengo la kuanzisha migodi mipya.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa hizo za jiosayansi zinazozalishwa hutumika katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji, ujenzi na mipango miji. Pia, GST ina jukumu la ufuatiliaji wa majanga ya asili ya jiolojia ikiwemo matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano na maporomoko ya ardhi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, GST imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

#### (i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu ya utafiti, GST imekamilisha mapitio ya taarifa za jiosayansi na kuchapisha toleo jipya la Kitabu cha Madini ya Viwandani. Aidha, GST imetoa ushauri elekezi wa jiolojia, jiokemia na jiofizikia kwa wadau mbalimbali ikiwemo wachimbaji wadogo na wa kati 17 na taasisi tatu (3) za Serikali.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza mashirikiano, GST kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar ilifanya utafiti maalum katika

visiwa vya Unguja na Pemba. Matokeo ya utafiti huo yalibaini uwepo wa madini mbalimbali ikiwemo *heavy mineral sands* (ilmenite na zircon), *strontium* na chokaa. Kufuatia matokeo hayo, GST iliandaa ramani na ripoti ya utafiti na iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 12 Septemba, 2024. Vilevile, ramani hiyo imeainisha maeneo ya vivutio vya utalii wa jiolojia pamoja na maeneo hatarishi yanayoweza kukumbwa na majanga ya asili ya jiolojia.




**Picha Na. 9:** *Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Akikabidhiwa Ripoti ya Utafiti Maalum wa Jiosayansi uliofanyika katika katika visiwa vya Unguja na Pemba.*

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST ilipokea ripoti 455 kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafiti na uchimbaji madini kutoka kampuni 25. Kati ya ripoti zilizopokelewa, ripoti 305 zimehakikiwa na kuhifadhiwa kwenye Kanzidata ya Taifa ya Madini.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, GST imekamilisha uchoraji wa ramani 12 katika QDS 218, 219, 221, 222, 223, 236, 237, 243, 252, 269, 270 na 271 sawa na kilomita za mraba takribani 35,643. QDS hizo zinagusa maeneo ya mikoa ya Pwani, Morogoro, Lindi na Songwe. Aidha, jumla ya

ramani 7 zinaendelea kuhaririwa ambapo hadi sasa kazi hii imefikia asilimia 98.



**Picha Na. 10:** *Baadhi ya Wataalamu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) wakiwa kwenye shughuli za utafiti katika Mkoa wa Lindi.*

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST inaendelea na kazi ya kuhamisha nakala ngumu za taarifa na kumbukumbu mbalimbali za kijiolojia jumla ya taarifa za nakala ngumu 140 zilizopo katika maktaba ya jiolojia (archive*)* zimechakatwa na kuwa nakala laini na kuwekwa

kwenye mfumo wa kidijitali (KOHA). Aidha, jumla ya vitabu 347 vimeingizwa kwenye mfumo.

154. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha kanzidata ya taifa ya uhifadhi wa taarifa za jiosayansi, GST imekamilisha hatua za awali za ujenzi wa mfumo huo.

**(ii) Uboreshaji wa Huduma za Maabara**

155. ***Mheshimiwa Spika,*** GST imeendelea kudumisha Ithibati yake (maintained accreditation status) ambayo itadumu kwa kipindi cha miaka mitano (5) hadi kufikia mwaka 2029. Ithibati hiyo imetolewa na Shirika la udhibiti ubora wa huduma za maabara katika nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika (SADCAS). Hatua hii imefikiwa baada ya Serikali kufanya maboresho katika maabara ya GST hususan kwenye ununuzi wa vifaa vya kisasa, mafunzo kwa wataalamu na kufanya ukaguzi wa ndani kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025.

***Napenda kutoa wito kwa wadau wa Sekta ya Madini kuendelea kuitumia maabara ya GST kwa kuwa ina ithibati na inakidhi viwango vilivyothibitishwa kimataifa.***

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, sampuli 18,448 za miamba na udongo zimefanyiwa uchunguzi wa maabara. Ili kupunguza gharama za uagizaji vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu kutoka nje ya nchi, GST imetengeneza vyungu 15,703 ambavyo vimetumika katika maabara ya GST na maabara nyingine hapa nchini. Hatua hii imesaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza vyungu hivyo kutoka nje ya nchi.

**(iii) Ufuatiliaji wa Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kutoa Elimu kwa Wananchi**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, GST imechakata taarifa za mitetemo kutoka katika vituo vinne (4) vilivyopo Dodoma, Mbeya,

Geita na Arusha. Aidha, GST imefanya uchunguzi wa athari za milipuko kwenye maeneo yanayozunguka mgodi wa Bulyanhulu ili kubaini athari za milipuko iliyotolewa taarifa na wananchi. Pia, GST ilifanya uchunguzi wa bubujiko la tope kutoka ardhini katika maeneo ya Kwamtoro-Chemba Dodoma. Vilevile, elimu kuhusu namna ya kujikinga na kuchukua tahadhari wakati wa majanga ya asili ya jiolojia yanapotokea imeendelea kutolewa kwa wananchi.

### d. *KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)*

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ngazi ya astashahada na stashahada katika fani za utambuzi wa madini ya vito; uchongaji wa vinyago vya miamba na madini; ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, TGC inatoa huduma za utambuzi wa madini ya vito kupitia maabara yake. Pia, TGC inatengeneza bidhaa zinazotokana na madini ya vito na miamba. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 TGC imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

#### (i) Ujenzi wa Jengo la Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8) umeanza Agosti, 2024. Jengo hili litakuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, maabara za madini ya vito na bidhaa za usonara, *mineral gallery*, ofisi, hosteli kwa ajili ya wanafunzi, kantini na maduka. Aidha, hadi kufikia Machi 2025 Mkandarasi amelipwa malipo ya awali shilingi 3,342,936,526.00 kwa ajili ya ujenzi huo.

#### (ii) Utoaji wa Mafunzo na Huduma Nyingine

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha TGC kilidahili wanafunzi 34 katika ngazi ya *Basic Technician*. Aidha, Kituo kimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 71 kwa

ngazi za *Technician* na *Ordinary Diploma* katika fani ya Teknolojia ya Vito na Usonara. Vilevile, Kituo kilidahili wanafunzi 27 katika kozi za muda mfupi za miezi mitatu na sita katika fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito (lapidary), sayansi ya madini ya vito (gemology) na usonara (jewellery).



***Picha Na. 11:*** *Wanafunzi wakipata mafunzo ya uongezaji thamani madini katika Kituo cha TGC, Arusha.*

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kinaendelea na utoaji wa huduma mbalimbali kwa wadau ikiwemo utambuzi wa madini ya vito, ukataji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Kituo kilitoa huduma ya upimaji wa sampuli 423 za madini ya vito kutoka kwa wadau mbalimbali na kutoa taarifa za utambuzi wa kimaabara. Vilevile, Kituo kilitoa huduma za ukataji na ung'arishaji kwa vipande 243 vya madini ya vito. Pia, Kituo kimeendelea kutoa huduma za usonara kwa wadau mbalimbali.

**(iii) Uzalishaji wa Bidhaa**

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Kituo kimeendelea kufanya shughuli za uzalishaji wa bidhaa za madini ya vito ikiwa ni pamoja na kutengeneza bidhaa za usonara na uchongaji wa miamba ambapo bidhaa 987 zilizalishwa. Aidha, bidhaa za usonara 543 zilizalishwa na vinyago 1,266 vitokanavyo na miamba vilichongwa. Kutokana na uzalishaji huo, shilingi 60,055,742.00 zilipatikana.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Kituo kimepata eneo lililopo katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa-Arusha (AICC) kwa ajili ya kuonesha shughuli na bidhaa za madini zilizoongezwa thamani. Aidha, kwa sasa Kituo kinaendelea na utaratibu wa kukarabati eneo hilo.

**e. *TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI)***

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI ina jukumu la kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ili kuongeza mapato na manufaa yatokanayo na Sekta ya Uziduaji hapa nchini.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, TEITI imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Uandaaji wa Ripoti ya 15 ya TEITI kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI imekamilisha ripoti ya awali ya upembuzi (scoping report) ambayo imeainisha Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ambazo zitaingia katika zoezi la ulinganishi katika ripoti ya 15 ya TEITI. Hatua hii ni maandalizi ya kupata Kampuni zitakazoingia katika zoezi la ulinganishi kwa kuzingatia mwongozo wa Kamati ya TEITI. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kampuni zilizolipa Serikalini kiasi cha kuanzia shilingi bilioni 2 zitahusishwa katika ulinganishi. Kwa kuzingatia kigezo hicho, kampuni 58 za madini, mafuta na gesi asilia pamoja na watoa huduma katika Sekta ya Uziduaji zimechaguliwa kwa ajili ya zoezi la ulinganishi. Ripoti hiyo ya upembuzi iliwasilishwa katika Kamati ya TEITI ambayo iliridhia kuendelea kwa hatua ya uandaaji wa ripoti ya 15 ambayo inatarajiwa kuwekwa wazi kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

**(ii) Uzinduzi wa Ripoti ya 14 ya TEITI kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo Juni, 2024 TEITI iliweka wazi kwa Umma ripoti ya 14 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 ili kukidhi matakwa ya kimataifa ya uwazi na uwajibikaji ambapo kila nchi wanachama wa EITI inatakiwa kuweka wazi kwa Umma ripoti ya ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kila mwaka. Aidha, ripoti hiyo ilizinduliwa Septemba, 2024 ambapo viongozi mbalimbali wa Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Asasi za Kiraia, Wajumbe wa Kamati ya TEITI na Waandishi wa Habari walihudhuria.

**(iii) Kuweka Wazi Mikataba ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia**

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuweka wazi mikataba ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, TEITI imechambua taarifa za mikataba ya msingi (framework agreements) sita (6) ya Sekta ya Madini. Kati ya Kampuni hizo, Kampuni nne (4) zimeridhia mikataba yao kuwekwa wazi. Aidha, TEITI inaendelea kufanya majadiliano na Kampuni nyingine ili waweze kuridhia kuwekwa wazi mikataba yao kwa mujibu wa Kifungu cha 16(1) (a) cha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Sura 447.

**(iv) Utoaji wa Elimu kwa Umma kuhusu Matumizi ya Takwimu Zinazotolewa kwenye Ripoti za TEITI**

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, TEITI imeendelea kuelimisha Umma kuhusu matumizi ya ripoti zake kupitia runinga (TBC, AZAM na Channel Ten), redio, tovuti, mitandao ya kijamii, warsha kwa wanachama wasioona na kwenye maonesho mbalimbali. Aidha, TEITI ilishiriki katika Jukwaa la uziduaji lililoandaliwa na kuratibiwa chini ya mwamvuli wa Asasi za Kiraia zinazojihusisha na shughuli za uziduaji. TEITI ilitumia jukwaa hilo kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya takwimu zilizopo kwenye ripoti zake.

**(v) Kuimarisha Mahusiano ya Uanachama na Asasi ya Kimataifa ya EITI**

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilikuwa mwenyeji na mratibu wa mkutano wa 62 wa Bodi ya Kimataifa ya EITI uliofanyika tarehe 13 hadi 14 Machi 2025 jijini Arusha. Katika mkutano huo zaidi ya washiriki 100 walihudhuria wakiwemo wajumbe kutoka Mataifa mbalimbali duniani, wawakilishi wa kampuni kubwa zinazojihusisha na shughuli za uchimbaji na utafutaji wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Asasi za Kiraia zinazojihusisha na shughuli za uziduaji, Sekretarieti ya EITI na wawakilishi wa nchi wanachama wa EITI.




*Picha Na. 12: Mheshimiwa Anthony P. Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini akiwa na Wajumbe wa Bodi ya EITI walioshiriki katika mkutano wa 62 wa Bodi ya Kimataifa ya EITI uliofanyika tarehe 13 hadi 14 Machi 2025, Arusha.*

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano huo wa Bodi ya EITI ulifunguliwa na Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye alimwakilisha Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Mkutano huo ulitoa fursa ya kuelezea shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo Utalii, Madini, Mafuta, Gesi Asilia pamoja na masuala ya Utawala Bora.

**(vi) Kutengeneza Mfumo wa Kielektroniki kwa ajili ya Uandaaji wa Ripoti za TEITI**

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI inaendelea kutengeneza Mfumo wa Kielektroniki utakaotumika kuandaa ripoti za TEITI za kila mwaka utakaojulikana kama "*Extractive Data Reporting Management Information System (EDR-MIS)*". Mfumo huu utatumiwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanya malipo mbalimbali Serikalini, Taasisi za Serikali zinazopokea malipo hayo, Sekretarieti ya TEITI inayoandaa ripoti na wadau wengine wanaohusika na ripoti hiyo.

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2025 mfumo huu umefikia hatua za ukamilishaji kwa asilimia 75. Hatua inayofuata ni kufanya majaribio (System Testing) ambayo itahusisha wadau wote wanaohusika katika uandaaji wa ripoti. Mfumo huu unatarajiwa kukamilika Juni 2025.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2025/2026; Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Mpango Mkakati wa Wizara; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Sheria ya Bajeti, Sura 439, Kifungu cha 21; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na Maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

### I. Vipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Madini itatekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini za kina; kurasimisha na kuendeleza wachimbaji wadogo wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye

ulemavu; na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara ya madini.

**(i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli**

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ya kuimarisha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji kwa usawa; kuimarisha na kusimamia masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini; na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ya ujenzi, soko la tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

**177.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha udhibiti na kuzuia utoroshaji wa madini ya tanzanite, katika mwaka ujao wa fedha Wizara kupitia Tume ya Madini inakusudia kuja na mfumo na utaratibu thabiti ambao utawataka wakaguzi na wathamini wa madini hayo kuvaa kofia ngumu zenye kamera wakati wakitekeleza majukumu yao ili kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa mwenendo kwenye Eneo Tengefu la Mirerani na masoko kunakofanyika biashara ya madini hayo. Kutokana na mafanikio yatakayopatikana, utaratibu huu utatumika kwenye madini mengine ya vito.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na usimamizi wa Sekta ya Madini, Wizara inatarajia kununua magari 26 kwa ajili ya kuimarisha shughuli zitakazotekelezwa na Tume ya Madini. Hatua hii itachangia katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli, udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya madini pamoja na kufuatilia shughuli mbalimbali za madini.

**(ii) Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini Kwenye Pato la Taifa**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mchango wa wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo: kuhamasisha uanzishaji wa migodi mipya, kuimarisha usimamizi wa migodi ya uchimbaji; kusimamia utekelezaji wa Sheria inayoitaka migodi yote mikubwa kuajiri, kununua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini na kuwasilisha mpango wa ushirikishwaji wa Watanzania katika mnyororo wa uchumi wa Madini (Local Content) na Wajibu wa Wamiliki wa Leseni kwa Jamii (CSR); na kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa wawekezaji wote waliopewa leseni za uchimbaji wa madini wanaanza uzalishaji mara baada ya kukamilisha taratibu za matakwa ya kisheria.

**(iii) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani Katika Madini Muhimu na Madini Mkakati**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** madini muhimu na madini mkakati ni madini ambayo yana mahitaji makubwa kwenye maendeleo ya uchumi na ulinzi wa Taifa. Madini hayo ni pamoja na *lithium*, *graphite*, *helium, nickel, cobalt, titanium*, *copper, aluminium, niobium* na *rare earth elements* ambayo yanatumika kutengeneza vifaa vya kisayansi na kiteknolojia.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini muhimu na mkakati kwa Uchumi wa Taifa, Wizara imepanga kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini hayo kwa kufanya yafuatayo: kufanya tafiti kwa lengo la kubaini maeneo yenye madini muhimu na madini mkakati kwa ajili ya kufanya uwekezaji; kufanya utafiti wa mahitaji ya madini mkakati ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani; kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini mkakati; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini mkakati; na kukamilisha maandalizi ya

mpango mkakati wa uendelezaji na uvunaji wa madini mkakati nchini.

***Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ni msimamo wa Serikali kwamba hatutatoa Leseni za uchimbaji wa Kati (ML) na Mkubwa (SML) wa madini muhimu na ya mkakati kwa mwekezaji yeyote kama hatokuwa na mpango mzuri wa kuongeza thamani ya madini hayo hapa nchini, lengo ni kuifanya nchi yetu ya Tanzania kunufaika na rasilimali madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.***

**(iv) Kuhamasisha Uwekezaji na Uongezaji Thamani Madini**

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha ***uwekezaji***, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; kuendelea kutoa ushirikiano kwa wamiliki wa viwanda vya usafishaji wa madini ya dhahabu nchini ili kupata ithibati ya LBMA; kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini ikiwemo ujenzi wa viwanda vya kuyeyushia (smelters) na kusafisha (refineries); na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Jemolojia ili kiweze kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini kwa ufanisi.

**(v) Kuimarisha Uendeshaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito**

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kuendeleza minada na maonesho ya madini ya vito katika maeneo yenye uzalishaji mwingi wa madini ya vito; na kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mnyororo wa thamani wa madini nchini kupitia makongamano, maonesho, tovuti na vyombo vya habari.

### (vi) Kuongeza Uwekezaji kwenye Tafiti za Kina za Madini

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa shughuli hii, Wizara itafanya yafuatayo: kufanya tafiti za kina za jiofizikia (High-resolution Airborne Geophysical Survey) kwa kuzingatia matokeo ya tafiti za majaribio ili kuanisha uwepo na upatikanaji wa madini mbalimbali yakiwemo madini mkakati; na kujenga mfumo wa kutunza na kusambaza taarifa za jiosayansi. Aidha, Wizara itashirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kusaidia kufanya utafiti wa madini katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa utafiti wa kina wa madini nchini.

### (vii) Kuwarasimisha na Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na juhudi za kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuweka mazingira wezeshi yatakayowahamasisha kufanya uwekezaji; kuendelea kuhamasisha taasisi za kifedha kutoa mikopo ya fedha na vifaa kwa wachimbaji wadogo; kuboresha utendaji wa vituo vya mfano ili kuimarisha utoaji wa huduma na mafunzo kwa wachimbaji wadogo; na kuimarisha huduma za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo na kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana taarifa za jiolojia; kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki mikutano, maonesho na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujifunza na kutangaza shughuli zao; na kuhamasisha wachimbaji wadogo kushiriki kwenye minada na maonesho ya madini ya vito nchini ili kupanua wigo wa biashara.

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kunufaika na rasilimali madini, Serikali

imeunda Timu ya Wataalamu sita (6) wenye uzoefu na masuala ya fedha, madini na sheria kwa ajili kutoa mapendekezo ya namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji. Hatua hii itawawezesha wachimbaji hao kufanya uchimbaji wenye tija na kunufaika zaidi kiuchumi. Aidha, Wizara kupitia STAMICO itaendelea kuwalea na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwajengea vituo vya mfano vya kuchenjua dhahabu kwa kusimika mitambo mingine ya CIP katika maeneo yenye uchimbaji mdogo.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** sanjari na hatua hizo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inakusudia kuanzisha vituo vya kuuza na kukodisha vifaa na mashine mbalimbali za kufanyia shughuli za madini, vituo ambavyo vitawekwa katika maeneo ambapo uchimbaji unafanyika ili kurahisisha upatikanaji wa vifaa na mashine hizo kwa wachimbaji wadogo kwa uharaka, uhakika na wepesi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza uzalishaji mkubwa wa madini kupitia wachimbaji wadogo.

**(viii) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Madini**

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuzijengea uwezo taasisi, Wizara itafanya yafuatayo: kuiwezesha Tume ya Madini kupata rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi; kuendelea kuiimarisha STAMICO ili ishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini ikiwemo kuwawezesha wachimbaji wadogo kwenye masuala ya mafunzo, mikopo na vifaa.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuiimarisha GST ili iweze kufanya utafiti mkubwa wa madini kuweza kubaini maeneo mapya yenye mashapo ya madini; kukiimarisha Kituo cha TGC ili kiweze kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini; na kuiwezesha TEITI kupata rasilimali

mbalimbali ikiwemo vifaa na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**II. Maeneo Mengine Yatakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza maeneo mengine yatakayosaidia kuboresha zaidi ufanisi wa sekta. Utekelezaji huo umejikita zaidi katika kupata taarifa za jiosayansi kwa kufanya tafiti za kina kupitia "***Mining Vision 2030*: Madini ni Maisha na Utajiri**"; kuendelea na utekelezaji wa ***Programu ya Mining for a Brighter Tomorrow - MBT*** kwa ajili ya kuwainua wachimbaji wanawake, vijana na makundi yenye uhitaji maalum; kusomesha vijana kwenye maeneo muhimu katika Sekta ya Madini; kuwezesha biashara ya madini kufanyika kidigitali (Digitalizing Mineral Business); na kutekeleza Mkakati wa Madini Muhimu (Critical Mineral Strategy).

**(i)** ***Mining Vision* 2030: Madini ni Maisha na Utajiri**

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea na utekelezaji wa ***Mining Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri*** inayoweka matamanio ya kuwa na usimamizi thabiti wa rasilimali madini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa; kuboresha maisha ya watanzania; na kutoa fursa kwa mtanzania yeyote wakiwemo wakina mama, vijana na watu wenye mahitaji maalum kujiongezea kipato na hatimaye kutajirika kupitia shughuli za madini.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha hili, mambo yafuatayo yamezingatiwa ikiwa ni maeneo makuu yanayounda misingi ya maono hayo: Upatikanaji wa taarifa za jiosayansi hususani taarifa za kina za jiofizikia *(High Resolution Geophysical Survey)* kutoka asilimia 16 ya sasa hadi kufikia angalau asilimia 50 ifikapo mwaka 2030; kuboresha mfumo wa kisheria na kitaasisi ili kuwa na usimamizi makini na ulio wazi wa Sekta ya Madini; na

kuiwezesha Sekta ya Madini kufungamana na sekta nyingine za kiuchumi hususan Sekta za Viwanda, Kilimo, Ujenzi, Fedha na nyingine zinazotoa huduma kwenye Sekta ya Madini.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine yanayozingatiwa katika *Mining Vision 2030* ni pamoja na kuboresha shughuli za wachimbaji wadogo hususan katika urasimishaji wa shughuli zao, upatikanaji wa teknolojia za kisasa na rahisi, masoko ya madini, upatikanaji wa mitaji; na usimamizi thabiti wa shughuli za utunzaji mazingira kwa kushirikiana na Taasisi nyingine ili shughuli za madini zisiwe na athari hasi kwenye mazingira.

***Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, dhana ya Madini ni Maisha na Utajiri, inamaanisha hauwezi kutenganisha maisha ya Mtanzania na Sekta ya Madini kwa kuwa kufanikiwa kwa tafiti za kina na kupatikana kwa taarifa sahihi kutachochea sekta nyingine kukua ikiwemo Sekta za Maji, Kilimo, Utalii, Ujenzi na Mawasiliano.***

**(ii) Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* – MBT**

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itaendelea kutekeleza Programu ya MBT kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2030. Programu hii ni ya kimageuzi katika Sekta ya Madini ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kushughulikia changamoto na kuboresha fursa kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum ili kuongeza ushiriki wa makundi hayo katika mnyororo wa thamani wa madini.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu ya MBT inatarajiwa kuwa na matokeo yafuatayo: kuongeza kipato na kuboresha maisha ya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum; kuwaongezea fursa za ajira; na kuongezeka kwa kiwango cha uwekezaji kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum katika Sekta ya Madini. Aidha, Programu hii itaimarisha uzingatiaji wa masuala

ya usalama migodini ikiwa ni pamoja na afya katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za madini.

**(iii) Kusomesha Wataalam kwenye Maeneo Muhimu katika Sekta ya Madini**

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kukidhi mahitaji ya wataalam na uwepo wa teknolojia mahsusi katika mnyororo wa thamani wa madini nchini, Wizara itawajengea uwezo wataalam katika Sekta ya Madini kwa kuwasomesha ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo za ukadiriaji wa mashapo (resource modelling), modeli za kifedha (financial modelling), ukaguzi na usimamizi wa rasilimali madini, uthaminishaji wa madini, ukataji wa madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara na uongezaji thamani madini. Mafunzo haya yatajikita zaidi kwenye teknolojia ambazo zinapatikana nje ya nchi mathalani teknolojia za *gemstone heat treatment, enhancement* na *jewellery manufacturing* ambapo shughuli hizo zitafanyika hapa nchini.

**(iv) Kuboresha Usimamizi wa Shughuli za Madini Kidijitali**

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inakusudia kujenga Mfumo wa kidijitali kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa shughuli za madini kwa kuweka uwazi shughuli mbalimbali za madini hususan biashara ya madini, ukusanyaji wa maduhuli, usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini. Mfumo huu utaweza kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za Serikali zinazohusiana na shughuli za madini ili mifumo hiyo iweze kusomana na hivyo kurahisisha utendaji kazi wa wizara na taasisi nyingine za Serikali. Vilevile, mfumo utarahisisha uratibu, ufuatiliaji wa karibu mubashara na uendeshaji shughuli za madini kisasa.

### (v) Mpango Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati (Critical and Strategic Minerals Strategy)

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Madini itakamilisha na kuanza kutekeleza mikakati mbalimbali iliyoanishwa kwenye Mkakati wa Madini Muhimu na Madini Mkakati (Tanzania Critical and Strategic Minerals Strategy). Lengo kuu la mkakati huu ni kuwezesha Serikali kusimamia madini hayo na kupata manufaa zaidi kwa kuboresha maisha ya watanzania na kuleta maendeleo endelevu kwa nchi yetu.

## III. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

### (i) Tume ya Madini

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026 Tume ya Madini inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

#### a) Kuimarisha Utendaji Kazi wa Masoko na Vituo vya Ununuzi wa Madini

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha biashara ya madini inaimarika, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na biashara ya madini katika masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini. Uimarishwaji wa masoko hayo utalenga kununua vifaa vya uthaminishaji wa madini zikiwemo mashine za XRF, mizani, mashine za uthaminishaji wa madini ya vito sambamba na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa masoko na wathaminishaji wa madini.

**b) Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Madini katika Uzalishaji na Biashara ya Madini**

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na uzalishaji wa madini nchini, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha mikakati ya udhibiti wa Sekta hii katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwa masuala yatakayozingatiwa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi za Maafisa Madini Wakazi na Maafisa Migodi Wakazi (MROs) kwa kuziongezea vitendea kazi, kukiongezea Kikosi Kazi cha Kuzuia Utoroshaji wa Madini vitendea kazi yakiwemo magari na vifaa vya kupimia madini; kuimarisha madawati ya ukaguzi wa madini katika maeneo muhimu kama mipakani, viwanja vya ndege na bandarini; kuimarisha utoaji wa vibali vya biashara ya madini ili vitolewe katika mfumo wa kidijitali (e-Permits); na kuendeleza minada ya ndani ya madini ya vito.

**c) Usimamizi na Ufuatiliaji wa Leseni za Madini**

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha uwekezaji unakuwa na tija kwa Taifa, Tume ya Madini itafanya ufuatiliaji na tathmini ya leseni zilizotolewa ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Aidha, katika kuvutia uwekezaji na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha mfumo wa uandaaji na utoaji wa leseni za madini nchini.

**d) Kufanya Ukaguzi wa Masuala ya Usalama, Afya na Mazingira**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kunakuwa na shughuli za uchimbaji madini salama, endelevu na zenye tija Tume ya Madini itaendelea kufanya kaguzi katika masuala ya usalama, afya na mazingira katika migodi midogo, migodi ya kati, migodi mikubwa sambamba na ukaguzi wa mabwawa ya kuhifadhia Topetaka (TSF), *Waste Rock Dam* (WRD) pamoja na

maghala ya kuhifadhia baruti. Pia, Tume ya Madini itafuatilia uwasilishaji wa mipango ya ufungaji migodi, kuidhinisha na kuweka Hati Fungani.

**e) Kuboresha Mazingira ya Utendaji Kazi na Kuwajengea Uwezo Watumishi**

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa watumishi kwa kuwaongezea ujuzi, weledi na ubobezi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa huduma zinazokidhi viwango kwa wateja na wadau wa Sekta ya Madini nchini. Aidha, katika kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora ya utendaji kazi Tume ya Madini itaendelea na ujenzi wa Ofisi za Maafisa Madini Wakazi wa mikoa ya kimadini ya Songwe, Rukwa, Mahenge sambamba na ununuzi wa Samani na vitendea kazi yakiwemo magari na pikipiki.

**f) Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini**

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia masuala ya Ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kutekeleza na kuhakikisha kampuni zinazowekeza zinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini, zinatoa kipaumbele cha ajira na mafunzo kwa watanzania, pamoja na kutumia huduma mbalimbali zinazotolewa na watanzania au kampuni za kitanzania.

**(ii) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, GST inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

**a) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini**

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa, GST itafanya utafiti wa kina wa jiofizikia

kwa njia ya kurusha ndege (High Resolution Airborne Geophysical Survey) ili kuongeza eneo lenye taarifa za kina za jiofizikia kutoka asilimia 16 za sasa hadi kufikia asilimia 34 ifikapo mwaka 2026. Aidha, GST itafanya tafiti maalum kwa ajili ya kutambua maeneo yenye madini muhimu na madini mkakati (critical and strategic minerals) pamoja na kufanya ugani wa jiosayansi na utafiti wa madini katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mfumo wa kanzidata wa taarifa za jiosaynsi; utafiti wa jiolojia na jiokemia pamoja na utafiti wa kimkakati katika QDS mbili (2) na kuchora ramani zake katika skeli ya 1:100,000; tafiti maalum za jiosayansi; utafiti wa kina kwenye madini ya kimkakati, viwandani na ya metali; kufanya utafiti kwa lengo la kuongeza uelewa kwa wadau kuhusu masuala ya jiosayansi na kuchapisha kwenye jarida linalotambulika; na kutoa ushauri elekezi kwa wadau kwenye nyanja za jiolojia, jiokemia, jiofizikia na uchenjuaji wa madini.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itachora ramani 24, kudurufu ramani 30 na kuchakata picha za satelaiti; kuingiza taarifa/machapisho 500 katika mfumo wa digitali; kukusanya, kuhakiki na kutathmini uhalisia wa taarifa na takwimu za jiosayansi kutoka katika leseni 40 za utafutaji na uchimbaji madini nchini; kuhuisha Kanzidata ya Rasilimali Madini ya Taifa pamoja na Kitabu cha Madini yapatikanayo Tanzania (Minerogenic Map); na kukusanya miamba choronge mita 1,000 na kuchakata taarifa zake.

**b) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo**

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo, GST inalenga kufanya utafiti wa jiosayansi na kutoa mafunzo kwa lengo la kutambua ulalo, mwelekeo na tabia za mbale na namna ya kuichenjua katika mikoa minne (4) yenye shughuli hai za uchimbaji mdogo

wa madini nchini; na kufanya utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo wa madini katika eneo moja (1) lililotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**c) Kuboresha Huduma za Maabara**

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za maabara, GST itaendelea kufanya uchunguzi kwa kuzingatia vigezo vya ithibati (accreditation). Aidha, GST itajenga maabara mpya ya kisasa (State of the Art Geoscientific Laboratory) katika eneo la Kizota Dodoma. Maabara hiyo itafanya uchunguzi wa madini ikiwemo yale yanayohitajika kwenye nishati safi kama vile nickel, cobalt na lithium. Aidha, GST itaendelea na ujenzi wa maabara nyingine katika maeneo ya Chunya-Mbeya na Geita kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi wanaojihusisha na shughuli za madini.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea kutengeneza *crucibles* 200,000 na *cupels* 50,000 kwa ajili ya kuyeyusha sampuli za dhahabu; uchunguzi wa sampuli 25,000 za udongo, miamba au madini; na uandaaji wa sampuli rejea (certified reference sample materials) za dhahabu, shaba, fedha, zinki, chuma na *cobalt*.

**d) Ufuatiliaji wa Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kuelimisha Umma Namna Bora ya Kupunguza Athari za Majanga**

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu hilo, GST itakusanya takwimu kutoka vituo vitano (5) vya kudumu vya kunakili mienendo ya mitetemo vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya; kuchakata taarifa kutoka katika vituo hivyo na kuhuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kufanya matengenezo ya vifaa vya kunakili mitetemo; kuendelea kuunganisha vituo viwili (2) vya kupima mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha katika mfumo mubashara (real time) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea pamoja na kusimika mtambo mmoja mpya kwa ajili ya

ukanda wa Bonde la ufa mkondo wa magharibi Mkoa wa Kigoma.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** GST itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia. Elimu itatolewa kwa njia ya machapisho, semina na vyombo vya habari**.**

**e) Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika Kutekeleza Majukumu Yake**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake, GST itaboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi, usambazaji wa taarifa na takwimu za jiosayansi, taarifa za uwepo wa madini pamoja na kuwajengea uwezo watumishi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali ikiwemo masuala ya maabara (watumishi 10) kwa mujibu wa programu ya mafunzo ya mwaka 2025/2026.

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi, GST imepanga kununua vitendea kazi ikiwemo *Helicopter* ya utafiti, vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa sampuli za madini mbalimbali yakiwemo ya kimkakati, kukarabati majengo, kujenga maabara ya kisasa, kuboresha maslahi ya watumishi, kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato na usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

**(iii) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, STAMICO inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

**i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato**

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mapato ya Shirika yanakua na kuimarika, Shirika limepanga kuongeza

usimamizi kwenye uwekezaji uliopo katika miradi yake kama ifuatavyo:

**a) Uzalishaji wa Makaa ya Mawe na Nishati Mbadala (Rafiki Briquettes)**

**220.** ***Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea na uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira ambapo katika mwaka 2025/2026 jumla ya tani 732,770 zimepangwa kuchimbwa. Ili kuimarisha na kuongeza uzalishaji huo, Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa mbalimbali vikiwemo *dump trucks (3)*, *bulldozer D8 (1)*, *longwall coal shearer (2), Hydraulic Prop (1),* kifaa maalum cha mawasiliano mgodini (1) na *excavator (1)* yenye uwezo wa tani 50.

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa kuzalisha nishati mbadala, Shirika litaendelea na uzalishaji wa nishati safi ya kupikia. Aidha, Shirika litakamilisha usimikaji wa mitambo miwili (2) katika Mkoa wa Dodoma, na Tabora. Vilevile, Shirika litanunua mtambo mwingine mmoja (1) utakaosimikwa katika Mkoa wa Geita ili kuongeza uzalishaji zaidi. Kukamilika kwa mitambo hiyo kutaliwezesha Shirika kuzalisha nishati safi (Rafiki briquettes) kwa kiwango cha tani 32,761 kwa mwaka.

**b) Shughuli za Uchorongaji**

**222.** ***Mheshimiwa Spika*,** Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza na kutafuta kandarasi katika migodi mikubwa na ya kati. Aidha, Shirika limepanga kununua mitambo na vifaa kwa ajili ya uchorongaji ambavyo ni: *deep hole drilling rig (1), underground rig (1), light vehicles (5), compressor (1)* na *booster (1)* ili kukidhi ongezeko la uhitaji wa huduma za uchorongaji.

### c) Uzalishaji wa Kokoto – Chigongwe

**223.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika limepanga kuzalisha mita za ujazo 89,604 za kokoto. Aidha, ili kuendelea kuwa na soko la kutosha la kokoto, Shirika litaendelea kufanya mazungumzo na kampuni mbalimbali kubwa za ujenzi katika miradi ya Serikali ikiwemo ujenzi wa majengo, barabara, reli, viwanja vya mpira na viwanja vya ndege.

### ii. Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano

**224.** ***Mheshimiwa Spika*,** STAMICO itaendelea kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kufanya yafuatayo: kuendelea kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vituo vya mfano vya Itumbi, Lwamgasa na Katente; kuendeleza uzalishaji katika mgodi wa mfano Lwamgasa; kufanya upanuzi wa kituo cha mfano cha Katente kwa kusimika mtambo wa *CIP* na *elution;* kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha usafishaji chumvi kilichopo Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi; na ujenzi wa CIP mpya katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

### iii. Kuendeleza Leseni za Shirika

**225.** ***Mheshimiwa Spika*,** Shirika limepanga kufanya utafiti kwenye leseni zake tatu (3) za madini ya dhahabu zilizopo katika mikoa ya Geita na Mara. Aidha, kutokana na uhitaji mkubwa wa madini mkakati, Shirika limepanga kufanya utafiti wa madini ya kinywe katika leseni zake zilizopo katika mikoa ya kimadini ya Manyara na Lindi. Vilevile, Shirika linatarajia kuwa na migodi yake ya uchimbaji wa madini itakayoimiliki kwa asilimia 100 katika kipindi kijacho.

### iv. Miradi ya Ubia na Kampuni Tanzu

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaimarisha ufuatiliaji wa miradi ya ubia ambayo ni Mgodi wa *Buckreef,* Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu-Mwanza na Kampuni tanzu ya *STAMIGOLD* ili kuongeza ufanisi na kuwezesha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye miradi hiyo. Aidha, Shirika litaendelea kuiwezesha *STAMIGOLD* kwa kufanya utafiti zaidi ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, mgodi umepanga kufanya utafiti ambao utajumuisha uchorongaji wa mita 6,000.

### (iv) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo cha TGC kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

### a) Uimarishaji wa Miundombinu

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha TGC kimepanga kuimarisha miundombinu ya kutolea mafunzo kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nane (8); ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchakataji na upimaji wa madini kwa lengo la kuhakikisha kuwa wadau wanapatiwa huduma bora; ufunguzi wa kituo cha mauzo kwa ajili ya kutangaza fursa zilizopo katika Sekta ya Madini na kuuza bidhaa za madini katika eneo la AICC; na kuimarisha Maabara ya Madini ya Vito kwa kufanya ununuzi wa mashine za kisasa.

### b) Utoaji wa Mafunzo na Huduma Nyingine

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha TGC kitafanya udahili wa wanafunzi 50 (Astashahada) na 65 (Ufundi Sanifu na Stashahada) katika fani ya Teknolojia ya Vito na Usonara. Aidha, Kituo cha TGC kitafanya udahili wa wanafunzi 40 wa kozi za muda mfupi (miezi 3 na 6). Kozi hizo zitahusisha fani za ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito (lapidary), utengenezaji wa bidhaa za usonara,

(jewellery design and manufacturing), utambuzi wa madini ya vito (gemology) na uchongaji wa vinyago vya madini ya vito na miamba.

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitatoa huduma za utambuzi wa kimaabara kwa madini ya vito kwa sampuli 520; kufanya ukataji wa vipande 243 vya madini ya Vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara 240 kutoka kwa wadau; kutoa ushauri kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Aidha, ili kuhamasisha umuhimu wa huduma za maabara Kituo kitatoa huduma za ugani ili kuhakikisha wadau wanapata taarifa sahihi za madini ya vito.

**c) Uzalishaji wa Bidhaa**

**231.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo kinatarajia kuzalisha bidhaa za madini ya vito zikiwemo vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyingine za urembo na mapambo. Aidha, bidhaa za usonara 3,120 zinatarajiwa kutengenezwa kwa kutumia metali za fedha, dhahabu na shaba. Vilevile, vipande vya vito 2,880 vitakatwa sambamba na kuzalisha vinyago 7,500 vya miamba na madini ya vito.

**(v) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)**

**232.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026 TEITI inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo: kuandaa na kuweka wazi ripoti ya 16 ya TEITI inayoonesha ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024; kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; kukamilisha rejesta ya wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; na kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya takwimu za ripoti

ya TEITI ili kutambua mchango wa Sekta ya Uziduaji katika uchumi wa nchi.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** TEITI itaendelea na ukamilishaji wa mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na kampuni za uziduaji pamoja na Taasisi za Serikali katika kuripoti malipo yanayofanywa na kampuni hizo kwa Serikali; na kufanya tafiti mbalimbali za namna wananchi wanavyonufaika na wanavyoweza kunufaika zaidi na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

**D. SHUKRANI**

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi, juhudi na ubunifu mkubwa wa utendaji kazi anaoendelea nao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinachochea kukua kwa maendeleo ya nchi yetu.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo anayotupatia katika Sekta ya Madini ambayo yanaifanya Sekta hii kuendelea kukua na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo ambayo amekuwa akiitoa kwa Sekta ya Madini ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa shughuli mbalimbali za sekta kwa manufaa ya Taifa.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni utekelezaji wa programu mbalimbali za Kitaifa, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha

Mapinduzi ya Mwaka 2020, pamoja na msisitizo alioutoa kwenye maeneo mahsusi ikiwemo masuala ya kuzingatiwa katika ukamilishaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050. Hakika Hotuba hiyo imetoa mwelekeo utakaokuwa na tija katika kupanga, kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, ambaye amekuwa na msaada mkubwa kwenye Sekta ya Madini kwa kutoa ushauri, maelekezo na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha sekta hii inakuwa na mchango endelevu kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru ***Mheshimiwa*** Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini kwa jinsi anavyoendelea kunipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha sekta hii inatimiza malengo yake.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru Eng. Yahya Ismail Samamba, Katibu Mkuu na Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Aidha, niwashukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, Bi. Janeth Lekashingo, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Bi. Yokbeth Festo Myumbilwa, Mwenyekiti wa Bodi ya GST, IGP Mstaafu Balozi Simon Nyakoro Sirro, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO, CPA. Ludovick Silemwa Utouh, Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*, Makamishna wa Tume ya Madini na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini na weledi uendeshaji wa Taasisi za Wizara ya Madini.

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa na

kujituma bila kuchoka katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji, wafanyabiashara wa madini na watoa huduma kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Hii imerahisisha usimamizi wa Sekta ya Madini. Aidha, nizishukuru taasisi za fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo wachimbaji wadogo. Vilevile, nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kutuhakikishia usalama na kushirikiana nasi katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo la Dodoma Mjini ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na Taifa. Nawaahidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu kwa kunivumilia, kuniunga mkono, na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu uzima na afya katika utekelezaji wa majukumu ya ubunge na uwaziri katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa.

## E. HITIMISHO

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,405,537,268,755.00, naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha

makadirio ya shilingi 224,984,150,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) shilingi 124,604,788,000.00 sawa na asilimia 55.38 ya bajeti yote ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(ii) shilingi 100,379,362,000.00 sawa na asilimia 44.62 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 24,268,585,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE) na shilingi 76,110,777,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha *https://www.madini.go.tz*.

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na Mwenyekiti anakuja kunipokea.

*Hapa (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ili kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati niwasilishe hii Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini, Fungu – 100 kwa mwaka wa fedha 2024/2025; pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ikiwa ni kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Taarifa hii ya Kamati yote iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi Uliofanywa na Kamati Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini, Fungu – 100 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Maoni ya Kamati Kuhusu Bajeti ya mwaka 2025/2026 ni utekelezaji wa majukumu ya msingi ya kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2), ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa, muundo wa taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza, ambayo inahusu utangulizi na inaeleza msingi na muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya Pili, inahusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Sehemu ya Tatu, inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iv) Sehemu ya Nne, inahusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

(v) Sehemu ya Tano, ambayo ni Hitimisho ikijumuisha Shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Madini (Fungu – 100) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulijikita katika maeneo makuu matano ambayo ni:-

(i) Ukaguzi Kuhusu Miradi Iliyotengewa Fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Uchambuzi Kuhusu Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Uchambuzi Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Uchambuzi Kuhusu Upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025; na

(v) Uchambuzi Kuhusu Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi kuhusu Miradi Iliyotengewa fedha, mwezi Machi, 2025 Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Wizara ya Madini katika Mkoa wa Songwe, Mbeya na Dodoma. Miradi iliyokaguliwa ni hii ifuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Mkaa Mbadala wa Kupikia *(Rafiki Briquettes)* Kiwira, Wilaya ya Ileje, Mkoa wa Mbeya. Utekelezaji wa mradi huu ni mojawapo ya kazi zinazotekelezwa na Shirika la *STAMICO* kwa lengo la kujiendesha kibiashara kwa kutumia rasilimali madini. Gharama za ujenzi wa mradi huo ni shilingi bilioni 1.92 ambazo zinajumuisha shilingi bilioni 1.25 za ununuzi wa mitambo na shilingi milioni 727.3 za ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa, mkaa unaotengenezwa ni rafiki kwa mazingira na tayari umeshafanyiwa

ukaguzi na kutolewa Cheti cha Ubora kutoka Shirika la Viwango *(TBS)* mwaka 2021. Utekelezaji wa huo mradi unaongeza uhakika katika upatikanaji wa nishati safi ya kupikia na kuunga mkono juhudi za kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya Watanzania zaidi ya 80% kutumia kutumia nishati safi ya kupikia kufikia mwaka 2034.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umeendelea kuonesha kuwa, bado wananchi wengi hawana ufahamu kuhusu manufaa yatokanayo na matumizi ya mkaa huo kwa kuwa, hali ya upatikanaji wa mkaa huo katika maeneo mengi nchini iko chini, hususani maeneo ya vijijini. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Wizara kupitia *STAMICO* iongeze juhudi za kutangaza na kusambaza mkaa huo, ili wananchi wengi wahamasike kuutumia na kuachana na matumizi ya mkaa wa miti na kuni. Maelezo zaidi kuhusu mradi huo yanapatikana katika Ukurasa wa Nne na wa Sita wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyeiti, Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mfano *(Demonstration Centre)* kwa Wachimbaji Wadogo cha Itumbi, Wilaya ya Chunya, Mbeya. Uanzishwaji wa kituo hiki ni mojawapo ya kazi za Shirika la *STAMICO* zinazolenga kuendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini. Kituo hicho kinatumiwa na *STAMICO* kutekeleza lengo hilo kwa kutoa elimu kuhusu utafutaji wa madini, teknolojia salama, rahisi na endelevu katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za ujenzi wa Kituo cha Itumbi, Mbeya, ni shilingi bilioni 1.08 ambazo tangu kuanzishwa kwa kituo hiki, mwaka 2020, kimetumika kutoa huduma za uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo ishirini na nne na kuchenjua gramu za dhahabu 20,125.80 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.27. Kwa kuzingatia hali ya mazingira, ambayo Kamati iliiona wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Kamati inashauri Wizara iongeze juhudi katika kuboresha mazingira ya kituo hicho, hususani eneo linalohusu Bwawa la Topesumu. Maelezo zaidi kuhusu mradi huo yanapatikana katika Ukurasa wa saba hadi wa nane wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Madini, Mtumba, Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la

ghorofa tano na eneo la chini *(ground floor)* na unatekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma kwa jumla ya gharama za shilingi bilioni 24.56. Kamati ilitembelea mradi huu tarehe 20 Machi, 2025, utekelezaji wake ulikuwa umefikia 92%, ambapo ujenzi wa jengo *(super structure)* ulikuwa umekamilika kwa 100%. Aidha, hadi tarehe 20 Machi, 2025, kiasi cha shilingi bilioni 19.1 sawa na 77.74% ya gharama ya ujenzi kilikuwa kimelipwa na Serikali kwa mkandarasi anayetekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Oktoba, 2021 na ulipaswa kukamilika mwezi Aprili, 2023. Hata hivyo, mradi umechelewa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kigeni na mabadiliko ya mfumo wa usalama wa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ujenzi wa jengo ulikuwa haujakamilika wakati Kamati ilipofanya ziara ya ukaguzi, hali ya utekelezaji wa mradi huu ilionekana kuridhisha kwa kuwa, kazi zilizokuwa zimebakia zilikuwa ni za umaliziaji. Maelezo zaidi kuhusu mradi huo yanapatikana katika Ukurasa wa Tisa hadi wa 10 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini ilipanga kutekeleza vipaumbele sita ambavyo ni: -

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

(ii) Kuendeleza madini muhimu na madini mkakati;

(iii) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani;

(iv) Kuendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege;

(v) Kuhamasisha uwekezaji, uanzishwaji wa minada, maonesho ya madini ya vito na uongezaji thamani madini; na

(vi) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele hivi na kubaini kuwa, kwa sehemu kubwa utekelezaji wake ni wa kuridhisha. Sekta ya Madini inaendelea kufanya vizuri na kuwa mojawapo ya kutegemewa katika kuongeza ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa. Taarifa iliyotolewa na Serikali mwaka 2025 inaonesha kuwa, mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 9.0 mwaka 2023 hadi kufikia 10.1% mwaka 2024. Hatua hii ni mafanikio makubwa, ambayo yanatokana na maono ya viongozi wakuu wa Kitaifa na kisha kutafsiriwa na kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuendeleza Sekta hii ya Madini kwa kutoa vitendea kazi kwa Maafisa wa Madini wa Kanda na ununuzi wa mitambo ya uchorongaji *(drilling rigs)* kwa 15, jambo lililochochea kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa. Maelezo zaidi kuhusu mradi huu yanapatikana katika Ukurasa wa 11 hadi 14 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia februari, 2025. katika mwaka wa fedha 2024/2025; Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi trilioni 1.165 kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni moja zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi bilioni 165.85 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 jumla ya maduhuli yaliyokuwa yamekusanywa ni shilingi bilioni 737.94 sawa na 63.34% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kiasi hicho kilichokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali shilingi bilioni 690.79, sawa na 69.08% ya lengo la shilingi trilioni moja, zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina; kiwango ambacho ni zaidi ya wastani wa lengo lililofikiwa ambalo lilikuwa ni 66.6% katika kipindi rejewa. Aidha, kwa upande wa makusanyo yaliyopangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi, shilingi bilioni 164.85, hadi kufikia Februari, 2025 ni kiasi cha shilingi bilioni 45.18 ndiyo kilichokuwa kimekusanywa, sawa na 28.6% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inaipongeza Wizara kwa kuwa na kiwango kizuri cha makusanyo ya maduhuli yaliyopaswa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina; jambo lililochangia Sekta ya Madini kuongeza kiasi cha asilimia katika mchango wake kwa pato la Taifa kutoka asilimia tisa kwa mwaka 2023 hadi kufikia 10.1% kwa mwaka 2024. Aidha, kwa upande wa maduhuli yaliyopangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi, kiwango cha makusanyo kipo chini, hali iliyoathiri utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hali hiyo, Kamati imetoa ushauri kwamba, Wizara iongeze juhudi na kuhakikisha lengo la makusanyo linafikiwa kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ufafanuzi zaidi kuhusu makusanyo hayo unapatikana katika Kielelezo Namba Moja na Mbili katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa hadi kufikia mwezi Februari, 2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Madini (Fungu – 100) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 231.98. Hata hivyo, kulitokea nyongeza ya bajeti kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo utekelezaji wa Hati za Makubaliano yaliyotokana na mashauri mbalimbali ya kimadini. Baada ya nyongeza hiyo fedha za maendeleo zilizoongezeka ni kiasi cha shilingi bilioni 231.93 na hivyo kufanya pesa ya Wizara kufikia shilingi bilioni 463. 91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 297.54 ambazo ni sawa na asilimia 64 ya bajeti iliyowasilishwa. Kati ya fedha hizo,

shilingi bilioni 55.5 sawa na 11.87% ni, kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 42.2 sawa na 66.53%, kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 13.29 sawa na 53.44%, kwa ajili ya mshahara. Kwa upande wa Fedha za Maendeleo, kiasi kilichopokelewa ni shilingi 245.03 sawa na 64.96% ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, licha ya kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo kupokelewa, kiasi kikubwa kililenga kulipa fedha, kwa ajili ya kutekeleza hati ya maridhiano *(deed of settlements)* zilizotokana na mashauri mbalimbali ya kimadini. Miradi mingine iliyotengewa fedha, upatikanaji wake haukuwa mzuri. Ufafanuzi zaidi kuhusu kiasi cha fedha kilichopelekwa unaonekana katika Kielelezo Namba Tatu cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa ya Kamati Kuhusu Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitoa jumla ya maoni, ushauri na mapendekezo kumi na sita, ili Wizara iyatekeleze kwa lengo la kuendelea kuboresha utendaji kazi wake. Uchambuzi uliofanywa na kamati umebaini kuwa, Wizara imezingatia na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa kiasi kikubwa. Aidha, baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa utekelezaji wake ni endelevu na Kamati imesisitiza Wizara kuendelea kuyafanyia kazi. Maelezo zaidi katika utekelezaji huo yanapatikana katika Ukurasa wa 20 na 22 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu – 100) kwa mwaka wa fedha 2025/2026; kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilifanya Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu – 100) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Wizara; Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umezingatia miongozo mbalimbali, kama vile; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Tatu wa

Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020/2025 na Sera ya Madini ya Mwaka 2009. Ili kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kikamilifu, Kamati imefanya uchambuzi wa vipaumbele na kubaini kuwa, Wizara imeongeza vipaumbele viwili kutoka vipaumbele sita vya mwaka wa fedha 2024/2025 na kuwa vipaumbele nane katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ufafanuzi zaidi kuhusu vipaumbele vya Wizara ya Madini vya mwaka wa fedha 2025/2026 unapatikana katika Ukurasa wa 23 na 24 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, Wizara ya Madini imekadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi trilioni moja na milioni mia mbili na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo shilingi trilioni moja na milioni mbili sawa na 82.95% zitakusanywa kupitia idara, vitengo vya Wizara na Tume ya Madini na kuwasilishwa Hazina. Aidha, shilingi bilioni 205.54 sawa na 17.05% zitakuasanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio hayo yameongezeka kutoka shilingi trilioni 1.165 mwaka 2024/2025 hadi kufikia shilingi trilioni 1.205 mwaka 2025/2026. Kiasi cha ongezeko hilo ni shilingi bilioni 40.689 sawa na 3.49%. Ufafanuzi zaidi kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli unapatikana katika vielelezo Na. 4 na Na. 5 vilivyoko kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Madini (Fungu 100) inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 238.25. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 140.66 sawa na 59.04% ni kwa ajili ya maendeleo na shilingi bilioni 97.59 sawa na 40.96% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi bilioni 31.14 sawa na 13.07% kwa ajili ya

mishahara na shilingi bilioni 66.45 sawa na 27.89 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, kwa ujumla bajeti ya Wizara imeongezeka kwa 2.7% kutoka shilingi bilioni 231.97 iliyoidhinishwa na Bunge lako mwezi Aprili, 2024 kwa ajili ya makadirio ya fedha ya 2024/2025 hadi kufikia shilingi bilioni 238.27 kwa ajili ya mwaka wa fedha wa 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi umebaini kwamba ongezeko la bajeti liko kwenye eneo la mishahara pekee na maeneo mengine yamebaki kama yalivyokuwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025. Ufafanuzi kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 umeoneshwa katika vielelezo Na.6 na Na. 7 vya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo: Katika maoni ya jumla, kwanza ni ukusanyaji wa maduhuli ya matumizi ya taasisi kutokufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli kwa taasisi ya matumizi ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini, umekuwa haufikii lengo na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na taasisi hizo. Serikali ihakikishe inaweka mikakati na hivyo kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli unaopaswa kutumiwa na taasisi unafikia lengo na hivyo kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuchelewa kwa mradi wa jengo la Wizara; ujenzi wa jengo la Wizara ya Madini katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma ni muhimu ili kuwezesha watumishi wa Wizara kupata ofisi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa kuwa mradi huu umechelewa kukamilika kutokana na mabadiliko ya mifumo ya malipo na usalama wa moto katika jengo hilo, Serikali ihakikishe kwamba inasimamia kwa karibu utekelezaji wa sehemu ya mradi iliyobaki ili ikamilike kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba na fedha zilizopangwa kutolewa zitolewe ili kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa watumishi, bado taasisi za Wizara zilizo chini ya Wizara ya Madini zina uhaba wa watumishi muhimu na hivyo Kamati inashauri watumishi waweze kuajiriwa na wengine kuhamishwa kutoka katika Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni mahususi, Shirika la Madini *STAMICO*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti jielekeze kwenye kuhitimisha tafadhali.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niende kwenye hitimisho. Kwa namna ya pekee nashukuru na kukipongeza kiti cha Spika, hasa Spika mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati kwa kazi kubwa ya miongozo na usimamizi wa shughuli za Bunge mnazoendelea kuzitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa David Mathayo David na Wajumbe wote kwa utekelezaji na usimamizi mzuri wa kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Madini, kijana mwanamapinduzi na mchapakazi, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote walio katika Wizara yao. Kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, na ninaomba kuwasilisha.

**2 MEI, 2025**

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILSHWA MEZANI

---

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023]*

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na afya njema na kutuwezesha Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri kwa Wizara ya Madini na Serikali kwa ujumla. Kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na maoni ya kamati kuhusu bajeti ya mwaka 2025/2026 unatokana na majukumu ya msingi iliyopewa Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 117(2) ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[2].

---

[1] Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja

[2] 7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za kisekta yatakuwa yafuatayo:- (a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Sehemu ya Kwanza ambayo inahusu utangulizi na inaeleza msingi na muundo wa taarifa;

Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

Sehemu ya Nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

Sehemu ya Tano ambayo ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulijikita katika maeneo makuu matano (5) kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi kuhusu miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wafedha 2024/2025;

(b) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(d) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025; na

(e) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

### 2.1 Ukaguzi Kuhusu Miradi Iliyotengewa Fedha Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[3], Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Madini. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 13, 14 na 20 Machi, 2025 katika mkoa wa Songwe, Mbeya na Dodoma mtawalia ambapo Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

#### 2.1.1 Mradi wa Kuzalisha Mkaa Mbadala wa Kupikia (Rafiki Briquettes) Kiwira, (Mradi Na. 1119) Wilaya ya Ileje, mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ni mojawapo ya kazi zinazotekelezwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa lengo la kujiendesha kibiashara kwa kutumia rasilimali madini. Aidha, uzalishaji wa mkaa huu unalenga kuongeza wigo wa matumizi ya makaa ya mawe yanayopatikana katika mgodi wa makaa ya mawe uliopo Kiwira na kuchangia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa unaotokana na kukatwa kwa miti. Vilevile, utekelezaji wa mradi huo unaongeza uhakika katika upatikanaji wa nishati safi kwa urahisi na kwa bei rahisi. Kwa kufanya hivyo, mradi huu utachangia katika kuliwezesha taifa kufikia malengo ya watanzania zaidi ya **asilimia 80** kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034 kwa mujibu wa mkakati wa nishati safi nchini.

**Mheshimwia Spika,** uzalishaji wa mkaa mbadala (*rafiki briquettes)* ulianza kwa majaribio (pilot project) katika eneo la *TIRDO* lililopo jijini Dar es Salaam kupitia kiwanda kidogo chenye uwezo wa

[3] 117.-(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

kuzalisha tani 2 za mkaa huo kwa saa. Mafanikio yaliyopatikana yaliwezesha kuanza majaribio ya mtambo mkubwa wenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa, na bidhaa za mitambo yote zilipata cheti cha ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) mwaka 2021. Kwa sasa Shirika linamiliki mitambo miwili mikubwa yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa katika eneo la Kisarawe Pwani, na Kiwira, Songwe. Kamati ilielezwa kuwa, kwa sasa Serikali iko katika hatua za kusimika mitambo ya aina hiyo katika mkoa wa Dodoma na Tabora.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa, kumekuwa na mwitikio wa watumiaji wa mkaa huu, ambapo hadi sasa taasisi kumi (10) zikiwemo shule za Sekondari za binafsi na Serikali na jeshi la Magereza zinatumia mkaa huu. Aidha, STAMICO ina mawakala katika mikoa 27 ya Tanzania kwa ajili ya kusambaza mkaa huo kwa wananchi wa mikoa hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za ujenzi wa mradi wa mkaa mbadala (*rafiki briquettes)* Kiwira ni **shilingi 1,972,873,023** ambazo zinajumuisha **shilingi 1,245,613,035** za ununuzi wa mtambo na **shilingi 727,259,988** za ujenzi wa miundombinu. Aidha, pamoja na uzalishaji unaoendelea, STAMICO inafanya utafiti kwa lengo la kuendelea kuboresha ubora wa mkaa na usalama kwa watumiaji. Kamati ilipohoji kuhusu mapato ambayo STAMICO itayapata kutokana na uzalishaji wa mkaa, ilielezwa kwamba mradi unatarajia kuliingizia shirika kiasi cha **shilingi 4,992,000,000** kwa mwaka kutokana na kuuzwa kwa mkaa huo, hii ikiwa ni kwa mujibu wa mpango wa biashara wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umeendelea kuonesha kuwa bado wananchi wengi hawana ufahamu kuhusu manufaa ya kutumia mkaa huo, na vilevile bado wengine wanakumbukumbu za mkaa huo kutokuwaka kwa urahisi ikilinganishwa na mkaa wa miti na kuni, tofauti hali halisi ilivyo kwa sasa ambapo maboresho yamefanyika na mkaa huo unawaka kwa urahisi. Vilevile Kamati imeendelea kubaini kuwa, hali ya upatikanaji wa mkaa huo katika maeneo mengi nchini iko chini hususani maeneo ya vijijini, na hivyo wananchi kutokupata muamko wa kuanza kutumia mkaa huo. Vilevile uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ujenzi wa mradi huo umechukua muda

mrefu kukamilika. Hata hivyo, Serikali ilieleza kwamba mradi huu ulichelewa kukamilika na kuanza uzalishaji kadiri ilivyokusudiwa kutokana na changamoto ya mvua kubwa katika eneo la mradi, ambayo ilicheleweshа usimikaji wa mtambo. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, juhudi zaidi zinapaswa kufanyika ili kuboresha zaidi mkaa huu na kuondoa malalamiko kutoka kwa watumiaji yanayohusu uwakaji na upatikanaji wake.**

#### 2.1.2 Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mfano (Demonstration Centre) kwa Wachimbaji Wadogo cha Itumbi, (Mradi Na. 1119) katika wilaya ya Chunya, Mbeya

**Mheshimiwa Spika,** kituo hiki ni mojawapo ya kazi za Shirika la STAMICO zinazolenga kuendeleza wachimbaji wadogo katika sekta ya madini nchini. Aidha, kituo kinatumiwa na STAMICO kutekeleza lengo hilo kwa kutoa elimu kuhusu utafutaji madini, teknolojia salama, rahisi na endelevu katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Vilevile kituo kinatumika kutoa huduma ya uchenjuaji, huduma za maabara, usambazaji kemikali na baruti.

Kituo hiki cha itumbi kilizinduliwa mwezi Oktoba, 2020, ni miongoni mwa vituo vinavyosimamiwa na kutumiwa na STAMICO katika kutoa ushauri na mafunzo ya vitendo kwa wachimbaji wadogo. Vituo vingine ni Katente, kilichopo wilaya ya Bukombe na Lwamgasa kilichopo wilaya ya Geita ambavyo vilizinduliwa mwezi Aprili, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za ujenzi wa kituo cha ItumbiMbeya ni **shilingi 1,084,273,748.** Tangu kuanzishwa kwa kituo hiki, kimetumika kutoa huduma za uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo ishirini na nne (24), ambapo kiasi cha mbali za dhahabu **tani 1.5** kilipokelewa kwa ajili ya uchakataji kwa njia ya mitambo mikubwa (*Carbon In Pulp-CIP)* na kuzalisha **gramu 9,871.70** za dhahabu zenye thamani ya **shilingi bilioni 1.67.** Aidha, kupitia mtambo wa uchenjuaji umewezesha kituo kuchoma **awamu 40** za kaboni yenye dhahabu (*loaded carbón)* na kuzalisha **gramu 10,254.10** za dhahabu zenye thamani ya **shilingi bilioni 1.67.** Njia zote hizo zimewezesha dhahabu iliyochenjuliwa kuwa **gramu 20,125.80** yenye thamani ya shilingi bilioni 3.27

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Januari, 2025 kituo kimetoa mafunzo ya vitendo kwa wachimbaji wadogo 350, sambamba na watumishi wa kituo kuwatembelea wachimbaji wadogo 24 katika maeneo yao ya uchimbaji na kuwapatia ushauri na elimu kuhusu namna bora ya kuendesha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mafanikio ya ujenzi wa kituo hiki ni kujengwa kwa mitambo ya kuchenjua dhahabu kwa njia ya mitambo mkubwa (**CIP**) inayomilikiwa na kuendeshwa na wachimbaji wadogo wawili ambao ni *Finta Processing Plant* na *Lisa Resources Company Limited* kwa kuiga teknolojia na miundombinu ya mitambo kutoka katika kituo cha Itumbi. **Kwa kuzingatia hali ya mazingira ambayo Kamati iliiona wakati wa ukaguzi wa mradi huu, Wizara iongeze juhudi katika kuhakikisha mazingira ya uendeshaji wa mtambo wa kuchenjua dhahabu kwa njia ya mitambo mikubwa (CIP) hususani usimamizi wa bwawa la tope sumu (TSF) yanaboreshwa kwa haraka na kuwa mfano wa kuigwa kwa wachimbaji wadogo na kulinda afya za wananchi wanaozunguka mradi huo.**

### 2.1.3 Ujenzi wa jengo la Wizara ya Madini (Mradi Na. 6389), Mtumba, Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa Tano (5) na eneo la chini (underground floor) kwa ajili ya ofisi za Wizara ya Madini na unatekelezwa katika mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Gharama za mradi ni **shilingi bilioni 24.56** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 1.71** ni kwa ajili ya mshauri elekezi wa mradi TBA na **shilingi bilioni 22.85** ni kwa ajili ya Mkandarasi wa ujenzi NHC. Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 20 Machi, 2025, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 92**, ambapo ujenzi wa jengo (super structure) ulikuwa umekamilika kwa asilimia miamoja (100%). Aidha, hadi tarehe 20 Machi, 2025, kiasi cha **shilingi bilioni 19.1** sawa na **asilimia 77.74** ya gharama ya mradi kilikuwa kimelipwa na Serikali kwa wakandarasi ambapo, mshauri elekezi alikuwa amelipwa **shilingi bilioni 1.34** na mkandarasi wa ujenzi **shilingi bilioni 17.76**.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Oktoba, 2021 na ulipaswa kukamilika mwezi Aprili, 2023. Hata hivyo, mradi umechelewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kigeni (dola za marekani) uliocheleweshа kupatikana kwa malighafi za ujenzi kutoka nje ya nchi na mabadiliko ya mfumo ya usalama wa moto, hali iliyoikumba miradi ya Wizara zote zinazojenga majengo katika mji wa Serikali Mtumba. Aidha, mabadiliko hayo ya mfumo huo yameongeza gharama ya mradi kwa kiasi cha **shilingi bilioni 1.61,** ambapo hadi wakaati wa ukaguzi, Wizara ilikuwa imewasilisha maombi ya malipo hayo Wizara ya fedha (hazina).

Licha ya utekelezaji wa ujenzi huo kuchelewa, Kamati ilihakikishiwa kuwa jengo hilo litakamilika na kuanza kutumika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2025 kwa kuwa vifaa vyote vilivyohitajika vilikuwepo na kazi zilizokuwa zikiendelea ni za umaliziaji.

**Mheshimiwa Spika,** ingawa ujenzi wa jengo ulikuwa haujakamilika wakati Kamati ilipofanya ziara ya ukaguzi, hali ya utekelezaji wa mradi huu ilionekana kuridhisha kwa kuwa kazi zilizokuwa zimebakia zilikuwa ni za umaliziaji, na hivyo kuashiria kuwa jengo linaweza kuwa tayari kwa ajili ya matumizi katika muda mfupi ujao. **Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizobaki ili kuwezesha kukamilishwa kwa kiasi kidogo cha ujenzi kilichobakia mapema na kuwezesha jengo hilo kuanza kutumika katika muda uliopangwa.**

### 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini imepewa dhamana ya kuendeleza Sekta ya Madini nchini kwa kuandaa mifumo madhubuti ya kusimamia ufuatiliaji, uchimbaji, uongezaji thamani na biashara ya madini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini ilipanga kutekeleza vipaumbele sita (6) ambavyo ni: -

Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

Kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani;

Kuendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege (high resolution airborne geophysical survey);

Kuhamasisha uwekezaji, uanzishwaji wa minada, maonesho ya madini ya vito na uongezaji thamani madini; na

Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele hivi na kubaini kuwa unaridhisha. Kutokana na juhudi za Serikali kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa; ukuaji wa sekta ya madini na mchango wake kwenye pato la Taifa umeendelea kuongezeka. Kwa mfano, ukuaji wa sekta ya madini ulifikia wastani wa **asilimia 11.3** katika mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 10.9** mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya madini imeendelea kufanya vizuri na kuwa mojawapo ya tegemewa katika kuongeza ukuaji wa uchumi nchini. Taarifa iliyotolewa na Serikali mwaka 2025 imeonesha kuwa mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa (GDP) uliongezeka kutoka **asilimia 9.0** mwaka 2023 hadi kufikia **asilimia 10.1** mwaka 2024, kiwango ambacho kimefikiwa kwa haraka zaidi ikilinganishwa na malengo ya Wizara ambayo ilipanga kufikia kiasi hicho mwaka 2025, ambapo matokeo ya ongezeko hilo yangeonekana na kutolewa taarifa mwaka 2026.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hii ni mafanikio makubwa ambayo yametokana na maono ya viongozi wakuu wa Kitaifa kisha kutafsiriwa na kutekelezwa kwa ufanisi na Wizara ya Madini na taasisi zake. **Kwa namna ya kipekee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake katika sekta ya Madini na kuiwezesha Wizara kwa kuiongezea vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari ya maafisa madini wakazi wa mikoa (RMOs),**

**ununuzi wa mitambo ya uchorongaji (drilling rigs) na kuajiri watumishi wa Wizara na taasisi zilizochini ya Wizara ya Madini, jambo lililochochea kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa.**

Vilevile, udhibiti katika ulinzi wa rasilimali madini ambao umetekelezwa na Wizara kwa lengo la kukabiliana na utoroshwaji wa madini uliwezesha kukamatwa kwa madini mbalimbali katika mikoa ya Dar es Salaam, Songwe, Mbeya, Kahama, Geita, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro na Lindi yenye jumla ya thamani ya **shilingi Billioni 16.1** katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2024 hadi Februari, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba thamani ya madini yaliyokamatwa imeongezeka kwa takribani **shilingi Bilioni 13.7** sawa na **asilimia 565.79**, kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Tathmini ya Kamati imeonesha kuwa, hali hiyo huenda imechangiwa na Serikali kuongeza udhibiti na ulinzi wa madini uliotokana na uwezeshaji wa vitendea kazi katika ofisi za maafisa madini wakazi wa mikoa hiyo, ama imetokana na ongezeko la watu wanaojihusisha na utoroshaji wa madini, na hivyo kuongeza kiwango cha utoroshaji ambacho kimedhibitiwa.

**Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo hususani hatua ya kudhibiti na kuongeza makusanyo yanayotokana na vitendo vya utoroshaji wa madini kwa kutaifisha madini yaliyokuwa katika hatua mbalimbali za kutoroshwa. Aidha, ni ushauri wa Kamati kwamba, Wizara iendeleze jitihada hizi kwa kuhakikisha vitendo vya utoroshaji wa madini ambayo ni rasilimali inayopaswa kuwanufaisha watanzania wote vinakomeshwa kikamilifu.**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kipaumbele cha kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo, Serikali imeendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu ushiriki wao katika shughuli za madini ikiwa ni mojawapo ya mikakati ya kuendeleza shughuli za wachimbaji wadogo. Katika kutekeleza kipaumbele hicho, mwaka 2024/2025 Serikali imeiwezesha STAMICO kununua jumla ya mitambo kumi na mitano (15) ya uchorongaji (drilling rigs) kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo. Mitambo hiyo

imesambazwa katika maeneo mbalimbali nchini yenye wachimbaji wadogo.

**Kamati inapenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha fedha za ununuzi wa mitambo katika kuhakikisha wananchi wanafidika na rasilimali madini zilizopo kwenye maeneo yao, na kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na nchi kwa ujumla. Aidha, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iendelee kusaidia wachimbaji wadogo nchini kwa kuwafikishia shughuli za ugani, teknolojia na vifaa vya uchimbaji kwa kuwa maeneo yaliyofikiwa na mitambo hii bado ni machache ikilinganishwa na maeneo ya wachimbaji wadogo nchini. Kwa kufanya hivyo, kutawawezesha wachimbaji wadogo kuongeza mchango wao kwenye sekta ya madini kutoka asilimia 40 ya sasa na kuwa asilimia kubwa zaidi.**

### 2.3 Uchambuzi Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia Mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini (Fungu 100) ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 1,164,850,027,000.00** kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kati ya kiasi hicho cha fedha, **Shilingi Trilioni Moja (Tsh 1,000,000,000,000)** kilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na **Shilingi Bilioni Miamoja Sitini na Nne Pointi Tisa (Tsh 164,850,027,000)** zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 fedha zilizokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali na kuwasilishwa Hazina zilikuwa ni **Shilingi 690,763,401639.07,** sawa na **asilimia 69.08**, ambayo ni zaidi ya wastani wa lengo la kufikia **asilimia 66.6** katika kipindi rejewa, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2025**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA 2024/2025** | **KIASI CHA KILICHOKUSANYWA** | **ASILIMIA** |
| Marejesho ya fedha za Serikali | 2,000,000.00 | 0.00 | **0.00** |
| Ada ya Mwaka ya Leseni | 52,026,219,385.00 | 39,780,877,424.14 | **76.46** |
| Ada ya Ukaguzi | 132,188,827,214.00 | 99,767,699,462.42 | **75.47** |
| Ada za kijiolojia | 49,026,747,535.00 | 9,485,878,306.22 | **19.35** |
| Mrabaha | 764,019,608,953.00 | 538,222,685,800.55 | **70.45** |
| Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada | 2,086,596,913.00 | 3,221,129,824.13 | **154.37** |
| Malipo ya huduma za Maabara | 650,000,000.00 | 285,130,821.62 | **43.87** |
| **JUMLA** | **1,000,000,000,000.00** | **690,763,401,639.08** | **69.08** |

**Chanzo:** *Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na usanifu wa KamatI*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua ya makusanyo kuzidi wastani wa **asilimia 66.6** hadi mwezi Februari 2025. Hali hii imechangiwa na baadhi ya makusanyo ambayo katika kipindi hicho yalivuka lengo kwa kiwango kikubwa. Mfano ni adhabu na faini za malimbikizo mbalimbali. **Aidha, eneo la ada za kijiolojia halikufanya vizuri kwani lilikusanya asilimia 19.35 tu ya lengo, hivyo juhudi zaidi zinahitajika ili kurekebisha hali hiyo**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa makusanyo ya **Shilingi 164,850,027,000.00** ambayo yalipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi, hadi mwezi Februari, 2025 ni kiasi cha **Shilingi 47,180,794,677.87** ndiyo kilikuwa kimekusanywa. Kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na **asilimia 28.62** ya lengo kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na.2.**

**Kielelezo Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2025**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI YA TAASISI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 161,509,027,000.00 | 45,861,739,919.79 | **28.40** |
| **GST** | 3,131,000,000.00 | 1,126,747,917.48 | **35.99** |
| **TGC** | 210,000,000.00 | 192,306,840.60 | **91.57** |
| **Jumla** | 164,850,027,000.00 | 47,180,794,677.87 | **28.62** |

**Chanzo:** *Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na usanifu wa Kamatl*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo ya Taasisi kuwa chini ya lengo la angalau wastani wa **asilimia 66** ilielezwa kuwa hali hiyo inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo:-

STAMICO Kuchelewa kusimikwa kwa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briquettes*) iliyonunuliwa kutoka nchini China;

STAMICO kupoteza tenda ya kibiashara kutokana na kufungwa kwa kiwanda cha Tembo ambacho kilikuwa kinatumia makaa ya mawe yaliyokuwa yanauzwa na STAMICO, na hivyo kuathiri mapato; na

Msimu wa malipo ya ada za mafunzo na michango mingine katika taasisi ya TGC kufanyika katika kipindi cha kuanzia Machi, 2025 na hivyo takwimu zake kuchelewa.

**Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kwamba, Wizara iongeze juhudi na kuhakikisha lengo la makusanyo linafikiwa kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, 2025 ili kutoathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa na taasisi. Aidha, Wizara kupitia taasisi zake iendelee kubuni mbinu zaidi za kukusanya maduhuli yake kwani kiwango kilichokusanywa kilikuwa chini sana (28.6%), ikilinganishwa na muda uliobakia.**

### 2.4 Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2025

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Madini (Fungu 100) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 231,983,614,000.00**. Hata hivyo, baada ya bajeti ya nyongeza iliyofanyika ili kukidhi miadi ya mashauri mbalimbali, fedha za maendeleo zilizongezeka kwa kiasi cha **shilingi 231,928,712,006** na hivyo kufanya bajeti ya Wizara kuwa **shilingi 463,912,326,006.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 372,589,912,006** zilitengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo na **shilingi 91,322,414,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo **shilingi 66,449,539,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo **(OC)** na **shilingi 24,872,875,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 297,536,888,981.74** ambazo ni sawa na **asilimia 64** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 55,502,833,741.12** sawa na **asilimia 11.87** ya bajeti yote iliyoidhinishwa[4] ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, matumizi mengineyo (OC) ni **Shilingi 42,211,890,570** sawa na **asilimia 66.53** ya fedha ya matumizi mengineyo iliyoidhinishwa, na **Shilingi 13,290,943,171.12** sawa na **asilimia 53.44 ni kwa ajili ya** mishahara (PE). Kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi kilichopokelewa **ni Shilingi 242,034,055,240.62** sawa na **asilimia 64.96** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2025**

| Eneo la Bajeti | Kiasi kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | **24,872,875,000** | **13,290,943,171.12** | 53.44 |
| Matumizi Mengineyo | **66,449,539,000** | **42,211,890,570** | 63.52 |

[4] Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025: Fedha zilizopokelewa kufikia Februari, 2025 uk. 8&9

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maendeleo | **372,589,912,006** | **242,034,055,240.62** | 64.96 |
| **Jumla** | **463,912,326,006** | **297,536,888,981.74** | **64.12** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kwa ujumla fedha zilizopatikana zilikuwa chini ya lengo la wastani wa kufikia **asilimia 66**, kiwango ambacho kinaweza kuboreshwa kwa kufuatilia fedha za hazina. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa, kulikuwa na ongezeko la bajeti kwa upande wa fedha za maendeleo, na hivyo upatikanaji wa fedha unaoonekana unachangiwa na ongezeko hilo. Hata hivyo, licha ya kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo kupokelewa, kiasi kikubwa kililenga kulipa fedha kwa ajili ya kutekeleza hati za maridhiano (deed of settlements) zilizotokana na mashauri yaliyofunguliwa na wawekezaji mbalimbali katika sekta ya madini. Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, miradi mingine iliyotengewa fedha, upatikanaji wake haukuwa mzuri, ikiwemo mradi wa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege.

**Kamati inatoa ushauri kwamba Wizara ihakikishe sehemu ya fedha iliyobaki inapatikana na kutekeleza kwa ufanisi malengo yaliyokusudiwa katika kufikia vipaumbele vya wizara.**

### 2.5 Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitoa jumla ya maoni, ushauri na mapendekezo kumi na sita (16) ili Wizara iyatekeleze kwa lengo la kuendelea kuboresha utendaji kazi wake. Kamati imepitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yake na kubaini kuwa, Wizara imezingatia na kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, baadhi ya maoni utekelezaji wake ni endelevu na mengine bado hayajatekelezwa kikamilifu, hivyo Kamati inasisitiza Wizara kuendelea kuyafanyia kazi.

Mfano wa maoni ambayo utekelezaji wake ni endelevu ni suala la uimarishwaji wa kanzi data ya miamba ambapo Wizara kupitia GST katika mwaka huu wa fedha imeanza kujenga mfumo wa kisasa wa kutunza, kuchakata na kusambaza taarifa za jiosayansi, ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2026. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali isimamie na kuhakikisha mfumo huu unakamilika kwani utaisaidia nchi kutambua mapema na kuepuka majanga mbalimbali ya asili yanayoweza kutokea ikiwa ni pamoja na maporomoko ya udongo.**

Kuhusu dhamira ya Serikali kuhakikisha inakuwa na taarifa sahihi za kijiofizikia ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha utafiti kutoka asilimia 16 ya sasa. Kamati ilielezwa kwamba, Serikali inakusudia kufanya utafiti huo kwa asilimia 18 zaidi, na hivyo kufikisha asilimia 34 ya eneo la nchi ambalo limefanyiwa utafiti wa kina wa jiofizikia. Aidha, lengo la Serikali ni kufikisha asilimia 50 ifikapo mwaka 2030. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, mchakato wa kuongeza kiwango cha utafiti huo ufanyike mapema ili kuiwezesha nchi kuwa na taarifa sahihi ambazo zitawezesha wananchi na wawekezaji kunufaika na matokeo ya utafiti huo kwa kuepusha upotevu wa mitaji.**

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa maoni ambayo hayajatekelezwa ni linaloitaka Serikali isimamie kikamilifu mchakato wa kuzalisha umeme wa Makaa ya mawe, Kiwira. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, wazo la awali la kutafuta muwekezaji wa kuzalisha **MW 200** kutokana na makaa ya mawe, halijafanikiwa. Hata hivyo, amepatikana muwekezaji (Adan Group Company) ambaye ameonesha nia ya kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe Kiwira ili kuzalisha **MW 2000**. Kamati ilielezwa kwamba, STAMICO anaendelea na mazungumzo na mwekezaji huyo, hata hivyo haijajulikana yatakamilika lini. **Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali itathmini ili kubaini iwapo mwekezaji huyo ana nia thabiti ya kuwekeza katika mradi huo. Iwapo itabaini kwamba, hana nia thabiti, basi mchakato wa kutafuta wawekezaji wengine ufanyike ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu unafanyika na hivyo kuiwezesha nchi kutumia rasilimali ya makaa ya mawe katika kuongeza uzalishaji wa umeme.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita (2024/2025)[5].

Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

**Malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026;**

Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wafedha 2025/2026;

Makadirio ya matumizi mwaka wa fedha 2025/2026; na (d) Ulinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya bajeti ya Taifa.

### 3.1 Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umebaini kuwa, Wizara imezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025[6] na Sera ya Madini ya Mwaka 2009. Ili kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kikamilifu, Kamati imefanya uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara na kubaini kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 vipaumbele viwili (2) vimeongezeka na vipaumbele Nane (8), ikilinganishwa na

[5] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi siku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.
[6] Ilani ya Chama cha Mpainduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 (Uk. 108 -110).

vipaumbele sita (6) vilivyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi umebaini kuwa, licha ya ongezeko la idadi, bado maudhui yanafanana na vipaumbele vya mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilielezwa kuwa, mabadiliko hayo ya nyongeza ya vipaumbele yamelenga kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba vipaumbele vilivyo ongezeka vina maudhui sawa na yale yaliyokuwepo katika mwaka wa fedha unaoisha ikiwemo kuendelea kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege *(high- resolution airborne geophysical survey),* na kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na madini mkakati". Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii muhimu ya kunyumbulisha vipaumbele na kubakia katika maudhui ya utekelezaji wa malengo ya Wizara. **Ni maoni ya Kamati kwamba, Wizara itahakikisha vipaumbele hivi vinatekelezwa kikamilifu na kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika uendelezaji wa sekta ya madini nchini, na hivyo kuifanya ichangie kamilifu katika ukuaji wa uchumi na pato la taifa.**

### 3.2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,205,539,268,735.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,000,002,000,000.00** sawa na **asilimia 82.95** zitakusanywa kupitia idara, vitengo vya Wizara na tume ya madini na kuwasilishwa Hazina. Aidha, **Shilingi 205,537,268,735.00** sawa na **asilimia 17.05** zitakusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 4.**

Kielelezo Na. 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

| **Maduhuli yatakayokusanywa na kuwasilishwa Hazina** | | |
|---|---|---|
| **CHANZO** | **2025/2026** | **ASILIMIA** |
| **Wizara** | 2,000,000.00 | **0** |
| **Tume ya Madini** | 1,000,000,000,000.00 | **82.95** |
| **Jumla Ndogo** | **1,000,002,000,000.00** | **82.95** |
| **Maduhuli yatakayokusanywa na kutumiwa na Taasisi** | | |
| **CHANZO** | **2025/2026** | **ASILIMIA** |
| **TGC** | 398,500,000.00 | **0.03** |
| **STAMICO** | 201,538,768,735.00 | **16.72** |
| **GST** | 3,600,000,000.00 | **0.3** |
| **Jumla Ndogo** | **205,537,268,735.00** | **17.05** |
| **JUMLA KUU** | **1,205,539,268,735.00** | **100** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio hayo yameongezeka kutoka **Shilingi 1,164,850,027,000** mwaka 2024/2025 hadi kufikia **Shilingi 1,205,539,268,735.00** mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo la **shilingi 40,689,241,735** ni sawa na **asilimia 3.49**. Ufafanuzi zaidi ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo na. 5.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kufahamu sababu ya ongezeko la makadirio ya makusanyo yanayopaswa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara hii hasa ikizingatiwa kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, wastani wa lengo la makusanyo kwa Makadirio ya Mwaka 2024/2025 lilikuwa kwa taasisi hizo lilikuwa ni **asilimia 28.82** tu. Wizara ilieleza miongoni mwa sababu zilizofanya ongezeko la makadirio ya makusanyo ni pamoja na:-

(a) Kuongeza huduma za GST na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na ada ya ushauri elekezi, tozo za huduma za maabara na tozo za ramani na machapisho ya jiosayansi.


(b) **Ongezeko la mapato kwa upande wa STAMICO** unaotokana na ongezeko la kufanya huduma ya uchorongaji na ushauri wa kijiolojia, uchimbaji na uchenjuaji, mradi wa wachimbaji wadogo, vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo (Lwamgasa, katente na Itumbi), mradi wa rafiki *briquette,* ada ya usimamizi STAMIGOLD na ignature bonus (fedha inayotokana na kusaini mikataba ya uwekezaji) na mradi wa kusafisha dhahabu (gold refinery); na

(c) Ongezeko la mapato kwa upande wa TGC utatokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma pamoja na ada za wanafunzi ngazi ya cheti katika mafunzo ya ukataji na usanifu wa vito.

### 3.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 238,251,361,287.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 140,661,200,000.00** sawa na **asilimia 59.04** ni kwa ajili ya maendeleo na **Shilingi 97,590,161,287.00** sawa na **asilimia 40.96** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 31,140,622,287.00 (asilimia 13.07)** kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 66,449,539,000.00 (asilimia 27.89)** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa** Fedha 2025/2026




**Chanzo:** *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara kati ya mwaka wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 na imebaini kwamba, kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa **asilimia 2.7** kutoka **Shilingi 231,983,614,000.00** zilizopitishwa na Bunge mwezi Aprili kwa ajili ya mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia **Shilingi 238,251,361,287.00** mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, ongezeko liko kwenye eneo la mishahara tu, na maeneo mengine yamebaki kama yalivyo katika mwaka huu wa bajeti. Kielelezo Na. 7 kinafafanua zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mishahara imeongezeka kwa **asilimia 25.5** kutoka **shilingi 24,872,875,00.00** katika mwaka wa fedha 2024/2025 hadi **shilingi 31,140,622,287.00** katika mwaka wa fedha 2025/2026. **Ni matumaini ya Kamati kwamba, ongezeko hilo la mishahara litalenga kutatua changamoto ya watumishi ambayo inaikumba Wizara na taasisi zake, sambamba na kuzingatia kuboresha stahili na maslahi ya watumishi.**

**Aidha, ni ushauri wa Kamati kwamba, katika maeneo ya maendeleo na matumizi mengine (OC) ambako bajeti**

**haikubadilika, utekelezaji wa majukumu utaendelea kwa ufanisi na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya kiutendaji yaliyowekwa na Wizara na Taasisi zake, na hivyo kuiwezesha sekta ya madini kuendelea kuchangia katika Pato la Taifa zaidi ya lengo la asilimia 10 lililokuwa limepangwa kufikiwa mwaka 2025, na ambalo tayari limefikiwa katika mwaka 2024.**

Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026

| CHANZO | 2024/2025 | 2025/2026 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Dev | 140,661,200,000 | 140,661,200,000 | 0 | 0 |
| OC | 66,449,539,000 | 66,449,539,000 | 0 | 0 |
| PE | 24,872,875,000 | 31,140,622,287 | 6,267,747,287 | 25.2 |
| Jumla Ndogo | **91,322,414,000** | **97,590,161,287** | 6,267,747,287 | 36.86 |
| **JUMLA KUU** | **231,983,614,000** | **238,251,361,287** | **6,267,747,287** | **2.7** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

### 3.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya madini ni miongoni mwa sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa kama ambavyo imeonekana kufikia 2024 mchango ni **asilimia 10.5**. Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha asilimia ya Bajeti ya Wizara hii (Fungu 100) dhidi ya Bajeti ya Taifa kati ya mwaka 2024/2025 na 2025/2026. Uchambuzi umebaini kwamba, Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 15.59** ikilinganishwa na mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo ni tofauti na ilivyo kwa upande wa bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) ambayo uwiano wake dhidi ya Bajeti ya Taifa umepungua kutoka **asilimia 0.47** mwaka 2024/2025 hadi **asilimia 0.42** mwaka 2025/2026 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8.

Aidha, Kamati imebaini kuwa OC imeongezeka kutoka **asilimia 0.19** hadi kufikia **asilimia 1.03**, Mishahara imeongezeka kutoka asilimia **0.21** hadi **asilimia 0.24**. Ni ushauri wa **Kamati kwamba, kutokana na umuhimu na mchango wa sekta ya madini kwenye**

**Pato la Taifa, Serikali iendelee kuiongezea Bajeti Wizara hii ili iendelee kuchangia kwenye uchumi na Pato la Taifa kwa ujumla.**

**Kielelezo Na. 8 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| AINA | BAJETI TAIFA | BAJETI MADINI | ASILIMIA |
| OC | 33,556,600,000,000 | 66,449,539,000.00 | 0.19 |
| MISHAHARA | 11,997,800,000,000 | 24,872,875,000 | 0.21 |
| MAENDELEO NDANI | 12,148,300,000,000 | 140,661,200,000 | 1.16 |
| MAENDELEO NJE | 3,640,800,000,000 | 0 | - |
| DENI LA SERIKALI | 15,746,700,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **49,345,700,000,000.00** | **231,983,614,000.00** | **0.47** |
| | | | |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2025/2026** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI MADINI** | |
| OC | 6,444,293,900,000 | 66,449,539,000 | 1.03 |
| MISHAHARA | 13,174,240,500,000 | 31,140,622,287 | 0.24 |
| MAENDELEO NDANI | 13,320,501,900,000 | 140,661,200,000 | **1.1** |
| MAENDELEO NJE | 6,150,902,600,000 | 0 | - |
| DENI LA SERIKALI | 17,950,311,400,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **57,040,250,300,000.00** | **238,251,361,287.00** | 0.42 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mapendekezo ya Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026, Randama ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, ufafanuzi wa yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha pamoja na uchambuzi wa Bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo: -

## 4.1 MAONI YA JUMLA

**(a) Ukusanyaji wa maduhuli ya Matumizi ya taasisi kutokufikia lengo**

Ukusanyaji wa maduhuli kwa ajili ya matumizi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini umekuwa haufikii lengo, na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na taasisi hizo. Serikali ihakikishe inaweka mikakati na hivyo kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli unaopaswa kutumiwa na taasisi unafikia lengo na hivyo kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa ufasaha.

**(b) Kuchelewa kwa mradi wa Jengo la Wizara**

Ujenzi wa jengo la wizara ya Madini katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ni muhimu ili kuwezesha watumishi wa Wizara kupata ofisi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa kuwa, mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na mabadiliko ya mifumo ya malipo na mifumo ya usalama wa moto, Serikali ihakikishe: -

Inasimamia kwa karibu utekelezaji wa sehemu ya mradi iliyobaki ili ukamilike kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba; na

Fedha zilizoombwa kutoka hazina kwa ajili ya mradi huo zinapatikana kikamilifu na kwa wakati ili kutokwamisha sehemu ya utekelezaji iliyosalia.

**(c) Uhaba wa Watumishi**

Bado taasisi za STAMICO, TGC, na GST zinakabiliwa na uhaba wa Watumishi hasa wa kada muhimu (core carders) kama vile ukaguzi na udhibiti wa madini, hali ambayo inaathiri utendaji wa taasisi hizo. Wizara iendelee kutumia vibali vya ajira mpya na ajira ya uhamisho kutoka taasisi nyingine za Umma, kupunguza uhaba uliopo hasa kwa kujaza mahitaji kwenye kada muhimu ili kutoendelea kuathiri utendaji wa taasisi hizo.

## 4.2 MAONI MAHSUSI

### 4.2.1 SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)

Mkaa mbadala wa "*coal briquette*" ni nishati safi inayoweza kupatikana kwa gharama nafuu kutokana na hazina ya makaa ya mawe ambayo nchi inayo. Kwa kuwa nchi ina malengo ya kuwezesha asilimia 80 ya Watanzania kupata nishati safi ya kupikia ifikapo 2034 kwa mujibu wa mkakati wa nishati safi nchini, Wizara ihakikishe STAMICO inaongeza uzalishaji wa mkaa mbadala wa kupikia na kuhamasisha matumizi yake ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa unaotokana na miti. STAMICO iongeze wigo wa kuutangaza mkaa huo na kuhamasisha matumizi yake ili watanzania wengi waweze kuufahamu na kuhamasika kuutumia. Hadi sasa taasisi 10 ikiwemo shule ya Sekondari ya Baobab na jeshi la Magereza zinatumia mkaa huo.

Serikali ihakikishe usambazaji wa mkaa mbadala wa makaa ya mawe unafanyika nchi nzima ili kurahisisha upatikanaji wake, na kwa gharama nafuu.Tafiti zaidi zifanyike kwa lengo la kuboresha ubora wa mkaa huo na kupunguza gharama, kabla ya kuendelea kusimika mitambo zaidi ya uzalishaji katika maeneo mengine ya nchi. Serikali ihakikishe Taasisi za Umma ambazo zinapika chakula kwa ajili ya watu wengi, zinahamasishwa kutumia mkaa huu ili kuunga mkono juhudi za uzalishaji wake sambamba na kupunguza athari za mazingira. Serikali ihakikishe inaboresha mazingira ya kituo cha Itumbi ili kulinda usalama na afya za Wachimbaji wadogo wanaofika kituoni hapo kwa ajili ya kupata huduma, na wakazi wanaoishi maeneo jirani na kituo.

### 4.2.2 TUME YA MADINI

Kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka: -

Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Madini umechukua muda mrefu bila kukamilika, jambo ambalo linasababisha gharama kuendelea kuongezeka na kuwaathiri watumishi wa tume kwa kukosa mazingira bora ya kufanyia kazi.

Serikali ihakikishe mradi huo sasa unakamilika ili watumishi wa taasisi wapate mazingira bora ya kutekeleza majukumu yao, hasa ikizingatiwa kwamba taasisi hii ina mchango mkubwa katika kuifanya sekta ya madini iendelee kukuza mchango wake kwenye uchumi na pato la taifa.

Hatua ya Serikali kuendelea kufuta maombi ya leseni na baadhi ya leseni ambazo hazijaendelezwa kwa muda mrefu kinyume na matakwa ya sheria na kanuni za madini inaonesha nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha watu wenye leseni wanaendesha shughuli za uchimbaji. Kamati ilielezwa kwamba, kati ya maombi na **leseni 2,648** ambazo Serikali ilitangaza kufuta, maombi na **leseni zipatazo 58** ndizo mchakato wa kufutwa umekamilika baada ya waombaji na wamiliki wake kushindwa kurekebisha makosa yao. Kasi ya utekelezaji wa zoezi hilo ni ndogo, hivyo Serikali iongeze kasi ya kushughulikia makosa yaliyobainika kwenye maombi ya leseni na leseni zinazopaswa kufutwa, ili maeneo hayo yawe wazi na kutoa nafasi kwa wawekezaji wengine wenye nia ya dhati kuomba leseni za maeneo hayo na kuyaendeleza.

Kutokana na kufutwa kwa maombi na baadhi ya leseni ambapo kwa sasa jumla yake ni 58, Serikali itoe leseni za baadhi ya maeneo ambayo yamebaki wazi kwa STAMICO na wachimbaji wadogo ili waweze kuyaendeleza kwa lengo la kujenga uwezo na kulifanya shirika liakisi dhima ya uanzishwaji wake kama shirika la madini la Taifa na kuendeleza wachimbaji wadogo nchini;

Serikali ihakikishe wawekezaji kwenye sekta ya madini wanajenga mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka maeneo yao ya uwekezaji ili kupunguza au kuondoa kabisa migogoro ambayo imekuwa ikizuka baina ya pande mbili hizo. Aidha, wawekezaji wawe mstari wa mbele katika kutekeleza kikamilifu wajibu wao kwa jamii (CSR) jambo ambalo litaimarisha mahusiano kwani wananchi watabaini manufaa ya shughuli za uwekezaji katika maeneo yao.

### 4.2.3 TAASISI YA JIOLOJIA NCHINI (GST)

Ujenzi na upanuzi wa Ofisi za Kanda za GST ikiwemo ofisi inayojengwa katika kituo cha mfano kilichopo Chunya pamoja

na ujenzi wa maabara upewe kipaumbele ili kusogeza huduma karibu zaidi na jamii na kuwafikia wadau wengi zaidi;

Serikali katika bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2024/2025 iliongezeka kwa kiasi kikubwa kwa upande wa fedha za maendeleo ili kuwezesha GST kuongeza utafiti wa kina wa kijiofizikia kutoka asilimia kumi na sita (16) iliyopo sasa na kuongezeka angalau kufikia asilimia 50 ifikapo 2030 kwa kununua ndege ya kufanya utafiti huo. Hata hivyo, hakukuwa na kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya ununuzi wa ndege na vifaa vyake, na hivyo hakuna ongezeko la utafiti wa kijiofizikia uliofanyika. Ili kuendelea kunufaika na rasilimali madini zilizopo nchini, Wizara ihakikishe inafuatilia kutolewa kwa fedha ya kazi hii kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2024/2025; naGST iendelee kujitangaza ili huduma zake zifahamike zaidi kwa wateja na wadau, hasa baada ya kuboresha huduma zake kwa kununua mitambo na vifaa vya kisasa.

### 4.2.4 KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kwa mara nyingine Shilingi 7,000,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majengo ya TGC ikiwemo kununua eneo na ujenzi wa miundombinu ya kisasa. Maandalizi ya mradi huu ni ya muda mrefu, hata hivyo utekelezaji wake haujaanza kutokana na mabadiliko kadhaa ikiwa ni pamoja na usanifu na mchakato wa uongezaji eneo kwa lengo la kukifanya kituo kuwa cha kisasa zaidi. Serikali ihakikishe utekelezaji wa mradi huu unaanza na kukamilika kwa muda uliopangwa ili kuepusha ongezeko la gharama na ucheleweshaji wa mradi. Aidha, utekelezaji wa mradi utakiwezesha kituo kufikia azma ya kutoa huduma za kisasa kwa wadau wake; na

Kwa kuwa eneo la awali lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo na miundombinu mingine limeonekana kuwa dogo ikilinganishwa na mahitaji ya TGC. Aidha, kwa kuwa, shughuli na huduma zitakazotolewa na kituo hicho zitavutia watu mashuhuli na wafanyabiashara wa madini ya vito kutoka sehemu mbalimbali duniani kutembelea kituo hicho, wazo la kuongeza eneo kwa ajili ya miundombinu ya maegesho na huduma nyingine, litekelezwe

kikamilifu ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza kwa wadau na wageni tarajiwa wa huduma za kituo hicho.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu tukufu katika utekelezaji wa majukumu yake. Namshukuru Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu, (Mb) pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna wanavyokusaidia katika uendeshaji wa vikao vya Bunge. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano mkubwa walionipatia ambao umewezesha kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi majukumu ya majukumu ya Kamati. Kwa namna ya pekee naomba majina yao yatambuliwe na kuingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*hansard*) kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb - **M/ Mwenyekiti**
3. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Tabasamu Hamisi Mwagao, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Sophia Hezron Mwakagenda, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. John Marko Sallu, Mb - Mjumbe

14. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Waziri wa Madini Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb), Naibu Waziri Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mhandisi Yahya Samamba akisaidiwa na Ndg. Msafiri Mbibo, kwa ushirikiano wao ambao umeisaidia Kamati kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kikatiba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya Kikatiba.

## 5.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono na naomba kuwasilisha.

Dkt. David Mathayo David, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA NISHATI NA MADINI**
02 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuwasilisha kwa ufasaha na kwa umahiri mkubwa taarifa ya Kamati yako kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tayari tumepata mawasilisho, kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hiyo na Kamati ya Bunge pia imemaliza kutekeleza jukumu lake la kuwasilisha taarifa. Tunaingia kwenye uchangiaji; tutaanza na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae. Mheshimiwa Iddi, karibu.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii leo kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Madini. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema, na mimi leo nimeweza kushiriki kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kujielekeza kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwenye sekta hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi makubwa, kama alivyohitimisha Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kwamba Wizara hii imepata mtu makini na mpambanaji ambaye kimsingi ana nia na malengo ya kuibadilisha sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri, kaka yangu Anthony Peter Mavunde, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwenye sekta hii ya madini. Kabla sijaenda mbali, nampongeza Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Kiruswa; ameendelea kumshauri vizuri na kuwa mtu mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Tumefanya ziara kama ilivyozungumzwa

kwenye hotuba ya Makamu Mwenyekiti. Tumetembelea miradi ya Wizara ambayo ilitengewa fedha na inaendelea kwenye mikoa na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana na niwapongeze sana ma-*RMO*. Tunapozungumzia habari ya mapinduzi makubwa kwenye sekta hii ya madini, wapambanaji na wachezaji ni ma-*RMOs* ambao wako kwenye mikoa yote huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wanafanya kazi kubwa sana. Kipekee sana nimpongeze *RMO* wangu, kijana mpambanaji, amekuja na kasi nzuri, kaka yangu Leons anafanya kazi nzuri sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, aendelee kumtia moyo *RMO* huyu, anafanya kazi nzuri sana kwenye Wilaya yetu ya Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru watu wawili, kwa maana ya Mtendaji Mkuu wa Tume, kaka yangu *Eng.* Ramadhan na kaka yangu Samamba, Katibu Mkuu wa Wizara hii. Katibu Mkuu huyu anafanya kazi nzuri sana. Ni mtu ambaye anaifahamu sekta hii vizuri, kwa umakini mkubwa anamshauri Mheshimiwa Waziri mambo makubwa na mazito ambayo leo tunayaona hapa yanaenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye kuchangia mambo kadha wa kadha. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Waziri kwa kutenga baadhi ya maeneo kwenye maeneo yetu ya wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Msalala nawapongeza sana, tulikuwa na changamoto ya maeneo kwenye maeneo mbalimbali, yeye pamoja na Mheshimiwa Rais; alisikia kilio cha wachimbaji wadogo wadogo na kuona namna gani sasa anaweza kutenga maeneo haya kwa ajili ya wachimbaji hao wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza maeneo ya Segese pale, tumeona kabisa leseni ilitolewa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri sana, na nimpongeze kwa hilo. Pia kama anavyofahamu, baada ya sisi

wachimbaji wadogo wadogo kupatiwa leseni hizo, ili wananchi wetu na wachimbaji waende kuchimba wanahitaji kupata taarifa za kwenye maeneo hayo. Niendelee kusisitiza na kuomba sana, tusaidiwe kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuiomba Serikali, katika bajeti hii ambayo nachangia leo, naomba moja kwa moja niseme kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kwa sababu ni bajeti ambayo itatekeleza na kutatua changamoto za wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye bajeti hii fedha zipelekwe kwa watu wa *GST*. Watu wa *GST* ni muhimu sana ambao kwa kupitia wao kama watatupa taarifa muhimu, itasaidia sana kwa wachimbaji wetu kwenda kupata taarifa muhimu ambazo sasa zitawawezesha wao kwenda kuchimba dhahabu kwa kupitia taarifa ambazo watakuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba, Wilaya ya kahama ndiyo wilaya ya kimkakati kwenye maeneo yale ya wachimbaji. Nimeona tumetoka rigi na tumefikisha bajeti na rigi zinaendelea kuongezeka, lakini kwenye Wilaya ya Kahama Mheshimiwa Waziri bado hatujapata rigi ya uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tayari wametupatia maeneo, naomba sasa waende wakatupatie na taarifa, na pia watenge rigi moja ije ikae pale Kahama ili iweze kusaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa gharama nafuu ili waweze ku-*drill* na kupata taarifa zitakazowawezesha wao kupata ripoti na baada ya hapo waweze kwenda kupata mikopo benki na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo sasa hivi ni kwamba, ni kweli Serikali imetupatia leseni kwa wachimbaji wadogo wadogo, lakini taarifa za kutosha zinakuwa hazipo. Kwa hiyo sasa wanahitaji wapate taarifa za kutosha ili wakusanye zile nyaraka ambazo zitawasaidia kwenda benki kukopa fedha na kuweza kuwekeza kwenye sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amezungumzia habari ya leseni za *refinery;* tumezunguka na tumeona, nimpongeze sana. Ameendelea kuhamasisha na wameendelea kutoa leseni za *refinery*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *refinery* zimefika nane lakini *refinery* hizi, kama hatutaishinikiza Serikali na kama Wizara haitachukua hatua za dharura kuhakikisha ya kwamba inakwenda kusimamia Kifungu hiki cha 123 ambacho tumekisema hapa, kuhakikisha ya kwamba dhahabu zote zinazochakatwa hapa Tanzania ziweze kupita kwenye *refinery* zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *refinery* moja *GGR* kuna *refinery* pale Mwanza, kuna *refinery* Dar es Salaam na maeneo mengine. Tulizungumzie habari ya *refinery* hii ya mama yangu Masasi ambaye yuko pale Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama amewekeza fedha nyingi sana kujenga ile *refinery,* na matarajio yake yalikuwa ni makubwa sana, kuhakikisha kwamba Serikali itahimiza 20% ya kampuni ambazo zinazalisha dhahabu ziweze kuchakata pale, lakini mpaka leo hii tunavyozungumza, bado kampuni hizi kubwa ikiwemo *Barrick, GGM* na nyingine bado hawapeleki hiyo 20% kwenda kuchakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, kama mama huyu Mtanzania ambaye amewekeza fedha zake nyingi kwenye kiwanda kile cha kuchakata, na bado tunaendelea kuhamasisha waendelee kujenga *refinery, raw material* ya kuendesha viwanda hivi, inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hatua za haraka na za kimkakati zichukuliwe ili kuhakikisha ya kwamba kampuni hizi kubwa, hiyo 20% wanatakiwa kuiacha hapa. Wasilete kisingizio cha aina yoyote, apelekewe mama huyu mwenye kiwanda kikubwa ambaye amewekeza fedha nyingi ili kiwanda kile kipate *raw material* na kiweze kujiendesha, kusiwe na sababu nyingine yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tumeshauri sana, nami nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye hatua ya mwisho kama hatakuja na majibu ya kutosha, ya kwamba ni lini sasa hizi kampuni kubwa zitapeleka hiyo 20% kwenye viwanda vyetu hivi vya *refinery* ambavyo vinaweza kwenda kuchakata kwenye maeneo yetu hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie habari ya *CSR*. Nawapongeza sana kampuni ya *Barrick* kwa kuendelea kutenga fedha za *CSR*. Kweli mimi ni mmoja wa mashahidi na mashuhuda kwamba fedha hizi za *CSR* zimeendelea kutuletea maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Msalala kupitia fedha za *CSR* tumeweka miradi mingi. Tumejenga chuo cha *nursing,* chuo cha *VETA,* barabara na sasa ninavyozungumza, tayari mkandarasi Mchina yupo *site* anajenga barabara ya kiwango cha lami inayotoka Kahama kwenda mpaka Bulyanhulu. Kwa hiyo, ni kazi kubwa sana inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri jambo hapa. *Coordination* na mawasiliano ya utekelezaji wa mpango wa *CSR* bado hauko vizuri. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, yeye Wizara yake pamoja na TAMISEMI wakae pamoja na kutafuta njia rahisi ya kwenda kutekeleza miradi hii ya *CSR* ili wananchi waweze kunufaika na fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza hapa, Wazungu walitenga fedha za *CSR* za mwaka 2024, wamekuja kupata *approval* ya kutumia zile fedha mwezi wa 12 mwaka 2024. Bajeti yao wanatenga mwezi wa 10. Leo tunazungumzia habari ya mwezi wa Tano, fedha imeshatengwa, ipo, lakini bado hawajapata *approval* ya TAMISEMI mpaka leo ili kuanza kutumia fedha zile za *CSR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, aweke msukumo mkubwa, yeye pamoja na watu wa TAMISEMI, wakae na kutafuta njia rahisi ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zikitengwa na Wazungu hawa ziende zikatumike ili wananchi waweze kupata maendeleo. Ni aibu, watu wanatenga fedha na fedha zipo lakini

sasa utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. Wanatuona ni watu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nafahamu yeye ni msikivu na ni mtu ambaye ni mchapakazi. Atahakikisha kwamba anakaa, hiyo timu itengenezwe. Mheshimiwa Zainab Katimba yuko hapo ananisikia, akae kuona ni namna gani fedha hizi ambazo zilikuwa zianze kutumika mwezi wa Kwanza, lakini mpaka leo mwezi wa Tano tunakwenda mwezi wa Sita bado *approval* ya TAMISEMI haijatoka ili fedha zile zianze kutumika. Kwa hiyo, tutengeneze mfumo mzuri ambao utatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie habari *STAMIGOLD*. *STAMIGOLD* ina *liabilities* nyingi sana. Yaani ina madeni mengi sana, watu wamefilisika kwa sababu ya madeni ya kuidai *STAMIGOLD*. Kwa sasa *STAMIGOLD* inazo rasilimali ambazo ikijipanga vizuri inaweza kulipa madeni haya ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na kushauri kwamba, sasa umefika wakati kwa *STAMIGOLD* kutangaza tenda na kuleta wawekezaji ili waje wawekeze ndani ya *STAMIGOLD* waweze kulipa madeni haya na wananchi hawa waweze kupatiwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wapo, kama *STAMIGOLD* watakaa kupanga na kutangaza, wawekezaji wapo, wanaweza wakaja kuliendesha shirika hili likaweza kuleta faida na kulipa madeni kwenye maeneo hayo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nafahamu kuwa Bulyanhulu kwa sasa wana mchakato wa kuongeza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, tafadhali hitimisha hotuba yako.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nihitimishe kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri na kuwaomba

Mgodi wa Bulyanhulu. Tulipofanya ziara *North Mara* tuliwashauri watu wa Mgodi wa Bulyanhulu kwamba kutokana na...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako ulishakwisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Mimi ni Mjumbe wa Kamati. Cha kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana aliyoifanya kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza sana kwa kumchagua Mheshimiwa Mavunde pamoja na Mheshimiwa Kiruswa. Ni halali kabisa kwa sababu hata mimi mwenyewe ninaamini sasa kwamba Wizara hii kama tutaboronga tena, sidhani kama kuna Waziri mwingine mwenye taaluma na madini atakuja kutusaidia kama Waziri Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabla ya kuwa Mbunge na kuingia kwenye Uwaziri, yeye alikuwa ni mwanasheria wetu wa *FEMATA* na kwa hiyo, anazijua shida zote za wachimbaji. Sasa amekabidhiwa rungu, tuna imani kubwa kwamba atatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Katibu Mkuu, *Eng.* Samamba, tunamfahamu amekulia kwenye madini. Kwa hiyo, ni ninyi wenyewe tu sasa kwa kweli sasa mboronge, lakini tuna imani

hakuna uchochoro wowote ambayo hamuufahamu. Tusaidieni tuepushe migogoro kwa wachimbaji, lakini tuikuze hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua *Engineer* Lwamo kuwa Mtendaji wa Tume. Wote hawa ni vijana ambao wamekulia kwenye madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, nina mambo ambayo natamani kushauri. Mimi natoka Geita, na leo nitazungumza kwa upole. Nisipopata majibu leo nitashika shilingi kwa mara ya kwanza, na siiachii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoka Geita; tuna Sheria yetu ya *CSR*. Tunapokubaliana na mwekezaji wa mgodi, inaletwa Wizara ya Fedha, yale makubaliano yetu yanaenda Wizara ya Fedha, TAMISEMI na kwa Mheshimiwa Waziri wa Madini, halafu amemkasimishwa Mkuu wa Mkoa. Baada ya kujiridhisha, tunasaini mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa akili yangu mimi, tukisaini mkataba huo, tayari ni utaratibu, ni sheria ambayo iko Wizara ya Fedha, iko Wizara ya Madini, na TAMISEMI. Sasa Mheshimiwa Waziri, kwenye halmashauri yangu na Halmashauri ya Geita Mjini tunadai zaidi ya shilingi bilioni 20. Ukipiga hesabu yetu sisi, tunadai shilingi bilioni 27. Waliyoikubali wao ni shilingi bilioni 23. Mheshimiwa Waziri, shilingi bilioni 23 kwenye halmashauri zetu kama zingekuja, hiki ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu *imagine* katika miaka hiyo, ni miradi mingapi imesimama na hela yetu, wao wenyewe wameizuia? Mheshimiwa Waziri, matokeo yake wameanza kuleta barua ya kuondoa baadhi ya miradi kwa matakwa yao wenyewe. Mheshimiwa Waziri, tumekuja kwako, wewe ndio *regulator* wetu. Sasa usipotusaidia wewe, labda sasa uturuhusu tukatumie njia za *shortcut* ambazo mimi ninazijua. Tukizitumia siku mbili tu, tutakaa na kuelewana, kwa kweli shilingi bilioni 23 natamani kuiona inaingia kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, najiuliza au Mheshimiwa Waziri hatamani niendelee kurudi kwenye hii nafasi, hiki kiti nimwachie mtu mwingine? Kama anatamani niendelee, shilingi bilioni 23 bila kauli yake, haki ya Mungu hatutaelewana, lazima nikueleze ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pesa nyingi, na hii pesa imeshaingizwa kwenye mipango ya Serikali ya Mama Samia. Tunaiomba hiyo pesa itoke kabla ya mimi sijamaliza siku zangu, tarehe 28 mwezi wa Sita tuwe tumeshaanza kupambana kwenye miradi. Mheshimiwa Waziri, mimi ni Mjumbe wa Kamati. Tumeenda kwenye ziara Nyamongo Wajumbe wote, tulifurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *model* ya *CSR*, waanzilishi wa *CSR* ya migodi mikubwa ni sisi Geita, lakini sasa sisi ndio tunaongoza kwa kufeli. Tulipoenda Mgodi wa Barrick tulikuta wao wana ushirikiano mzuri, kwamba wakishamaliza kusaini ile *MOU* watekelezaji wanakuwa halmashauri. Kazi ya mgodi wao ni kuchimba na kulipa. Tukapongeza, baadaye mkaja mkatoa kanuni za kuwapa mamlaka yao wenyewe ku-*procure*, wao wenyewe wasimamie, sisi halmashauri tunakuwa watazamaji. Hata kujua huu mradi unaendaje, haturuhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tumesimama muda mrefu sana na kisingizio imekuwa ile kanuni. Ukisimama hapa, nataka uniambie. Kanuni ile ya kuturuhusu sisi halmashauri, unaiachia lini? Ikiwa Mama Samia anatuletea trilioni za hela, halmashauri yangu ina karibu shilingi bilioni 67 na hatuna matatizo, tunakaguliwa tunakutwa tuko vizuri. Inakuwaje shilingi bilioni 23 tunashindwa kuwaamini wataalamu wetu? Wafanye *procurement* tusimamie, wataalamu wetu mainjinia wa Serikali. Wao wafanye kazi ya kulipa, na ndicho kilichowaleta. Hawakuja kufanya kazi ya kujenga madarasa, wao kazi yao ni dhahabu. Sitakubali nisipopatiwa majibu mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu pale Geita wana mipasuko, mpaka leo hatupati majibu. Mheshimiwa Waziri, kuna Kijiji kinaitwa Nyakabale, kina watu zaidi ya 30,000. Mgoni umechukua barabara yao.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma tafadhali, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mchangiaji, Mheshimiwa Musukuma. Mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC,* wanakataa kutoa pesa kwa sababu haitumiki ipasavyo. Kwa hiyo, halmashauri hazina utaratibu mzuri wa kutumia hizo pesa za *CSR*. Ndiyo maana wao wameamua sasa kuwa wenyewe ndio *Purchasing Officers*, wenyewe ndio wanaotengeneza huo mradi. Kwa hiyo, halmashauri zijirudi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, unapokea Taarifa?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa ya mama kwa sababu mama ameshaniambia anaenda kustaafu, sitaki kumjibu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Halmashuri ya Geita tumeletewa zaidi ya shilingi bilioni 67 na hatuna hoja ya ukaguzi kwenye Kamati yao ya *LAAC*, lakini tunazo hoja ndogo ndogo. Tumezitumia vizuri, *why* shilingi bilioni 23 unatuambia halmashahuri hazina uwezo wa kutumia? Kwa vile ni mstaafu, naomba nimhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi wananchi 30,000 wa Nyakabale mgodi umechukua barabara yao, halafu unatoa gari moja ya kubeba watu 50; kule ni porini, mahitaji yako mjini. Wanatoa gari moja tu kwa siku, watu 53 wapelekwe mjini saa 12 na kurudishwa saa 12. Hii siyo haki. Mheshimiwa Mavunde hii siyo haki. Kama wanataka kupora hiyo barabara waweke utaratibu, watoe magari saa *24/7* watu wafanye kazi zao za maendeleo. Mahitaji yako mjini. Tunaishi kama tuko *South Africa* Mheshimiwa Waziri! Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili ulizingatie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la ndege. Mimi nilikuwa wa kwanza mwaka jana 2024 kukupigia makofi Mheshimiwa Waziri. Helikopta ya kupimia madini imefika wapi? Kama imeishiwa mafuta, nikuchangie. Mbona sikuelewi! Sasa hivi umekuja tena na Sera ya Ndege Nyuki. Mheshimiwa Waziri, wachimbaji wadogo hawaaminiki popote kwa sababu hawana taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuja na mpango wa kununua helikopta, kila mtu anayetoka kwenye sekta ya madini alimuunga mkono na tulipiga makofi. Akisimama hapa atuambie ile ndege, kama iko njiani au inamaliziwa au bado inapakwa rangi, ili tuweze kujua. Mheshimiwa Waziri usije tena na mambo ya ndege nyuki hapa, hatutakuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *technical,* wageni. Natamani kukushauri Mheshimiwa Waziri, ile *operation* iliyofanyika Kariakoo kuwaondoa wawekezaji *fake* wanaouza mpaka *t-shirt*, Mheshimiwa, nimeona umetoa na kanuni, lakini hizi kanuni hata kwenye Kamati mimi sikushiriki, sikuziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Mheshimiwa Waziri ameshatoa kanuni, ninazisoma hapa. Siyo sawa Mheshimiwa, hebu jaribu kutembea kule migodini, yaani wageni nao tena wanaingia duarani na moko, eeh! Tunahitaji wageni wa *design* hiyo! Sasa sisi tutafanya kazi gani Mheshimiwa Waziri? Hiyo ndiyo sehemu peke yake iliyobaki ya watu wa Darasa la Saba na watu wengine, unapofeli, unaenda kuhangaika kwenye madini ambayo tumewekewa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuja mtu tena huku naye anaingia na moko, tunapishana naye kwenye maduara. Mheshimiwa Waziri, hii siyo sawa. Kama *operation* hii imefanyika Kariakoo, tunaomba na kwenye sekta ya madini waje na wao. Tunataka wawekezaji, ndiyo, lakini waje na kitu. Hata sisi tunaenda kuwekeza huko nje, kuna masharti. Huwezi kuwa na mwekezaji anakuja na dola laki moja, unaita mwekezaji. Mheshimiwa Waziri, hii siyo sawa; tunakuomba sana ufanye doria kwenye... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, (kwa sababu mtoa taarifa alichukua muda wangu), tunayo sekta ya wachimbaji wadogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uhitimishe tafadhali.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha. Naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri katika haya ya *CSR* na ubadilishaji wa kanuni, asipokuja na majibu mazuri nimeshaandika kabisa, nitashika shilingi. Kwa hiyo, ajiandae majibu vizuri kwa niaba ya wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Madini, hii hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Conchesta, ambayo ilihusisha Taarifa ambayo alipewa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma inayohusiana na *disbursement* za *CSR* na utaratibu wa *procurement*, nadhani pia uifanyie kazi kidogo ili utakapokuja uweze kutoa majibu ya uhakika kuhusu ukwamaji wa eneo hili; kwa sababu siyo maeneo yale yenye madini tu, hata yale maeneo ambayo *CSR* za uchimbaji maeneo mengine, yameenda kwenye halmashauri ambazo hazina madini. Nadhani kumekuwa na hiyo changamoto, labda ni vizuri ukajiridhisha Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Namkaribisha Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara kwa imani kubwa sana waliyonipa mwaka

2020 na hata sasa hivi wameendelea kunitumia ujumbe mbalimbali, kwamba Mbunge wetu tuko pamoja. Kazi tuliyokufanyia mwaka 2020 tunaenda kuifanya tena mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameendelea kuniambia kuna sehemu tunaitwaitwa tunaenda, wewe usiwe na wasiwasi, tunachokwenda kukifanya kule tunakijua. Wewe tuwakilishe Bungeni, hii shughuli tuachie sisi tuko pamoja. Ninawashukuru sana wananchi wa Ngara kwa imani kubwa sana wanayoendelea kunipatia, nami kwa kweli nafurahi kuwatumikia. Ahadi yangu kwao ni kuendelea kuwawakilisha vizuri kwa viwango vile walivyovitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni Rais ambaye kwa kweli amelitendea Taifa haki hasa kwenye sekta ya madini. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amejipambanua kwa kutoa leseni nyingi kwa wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amejipambanua kwa kutengeneza mazingira wezeshi ili wachimbaji wadogo wapate maeneo ya kuchimba. Nina hakika kila Mtanzania ambaye yuko kwenye sekta ya madini anasema Rais Dkt. Samia mitano tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamwombea heri, tunamwombea afya njema. Nina hakika uwekezaji alioufanya kwenye kuboresha maisha ya Watanzania, anakwenda kuuona kwenye sanduku la kura mwaka huu kwenye Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, ndugu yangu *Eng.* Lwamo, na ndugu yangu *Eng.* Samamba. Wakati Mheshimiwa Mavunde unateuliwa kuwa Waziri wa Madini, watu wengi walihisi wewe ni mtoto wa mjini, na watu wanajua madini yanachimbwa porini. Kumbe ndugu yangu wewe ni mtoto wa mjini, lakini ni mwanaapolo. Ulipopewa Wizara hii ya Madini Mheshimiwa Mavunde hakika umeitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kukua kwa makusanyo ya maduhuli Wizara ya Madini. Sasa wanakusanya mpaka kwa zaidi ya 10% waliyokuwa wamepewa kama *target*. Wameongeza vituo vya kununulia madini kutoka 102 mpaka 109. Mheshimiwa Mavunde, kazi yako Watanzania wanaiona, wachimbaji wanaiona, kila mmoja anaiona. Wewe na timu yako hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya kwenye Wizara yetu ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye eneo hili la *Tembo Nickel* kule Ngara. Tunamshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia, tarehe 25 Oktoba, 2021 alitoa leseni kubwa ya uchimbaji wa madini ya *Nickel* kule Ngara, na tunawashukuru *Tembo Nickel* wamejitahidi kufanya kazi kubwa. Wameshatoa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni 26 na fidia hii imeenda kwa wananchi 1,276 na hii ni 96% ya wananchi wote ambao wanatakiwa kupewa *compensation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Waziri na Wizara nzima, kuna vitu vya kufanyia kazi *Tembo Nickel*. Moja, wananchi 1,276 ambao tayari wameshalipwa fidia zaidi ya shilingi bilioni 26 walizuiliwa kufanya maendeleo ya chochote kwenye maeneo ambayo wanaishi mpaka sasa. Wamezuiliwa mpaka kupanda mihogo. Walishapewa fedha, wameitumia imeisha, wali-*retain* 40% ya fedha waliyolipwa. Sasa hivi wanaishi kwa taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakoelekea, ile fedha ambayo wananchi wa Ngara kutoka Kata za Bugarama, Bukiriro, Muganza, Kibogora, na maeneo mengine ya Tarafa ya Rulenge, wananchi wanaoishi maeneo haya ambao wameshatathminiwa na wamepewa fedha, wameanza kuishi maisha ya taabu. Kuna fedha waliahidiwa kwamba watapewa kama fedha za kujikimu na chakula za *Tembo Nickel*. Mpaka hivi ninavyosimama mbele yako, wananchi hawa hawajalipwa hata senti moja ya fedha za kujikimu. Huku wamezuiliwa wasilime hata muhogo; fedha waliyolipwa wameitumia imeisha, bado wako pale pale. Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie kusimamia vizuri *Tembo Nickel* ili ipeleke fedha za kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa wananchi hawa, waliahidiwa kujengewa nyumba ili wahamishwe. Muda mrefu umepita tukielezwa *Tembo Nickel* wanajenga nyumba tano za mfano peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwenye *architecture,* unapoletewa jengo limefanyiwa *engineering design* litaonekana hivi, kuna haja gani ya kujenga kwanza majengo matano ya mfano, wananchi wasubiri kuteseka huko eti mnasubiri mjenge majengo matano yaende yakaguliwe, umwulize mwananchi, unaridhika au huridhiki? Akisema haridhiki unaanza upya tena kujenga jengo la mfano kwa miezi mingine 12!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, itumike *engineering* kufanya *decision*. Mfanye *decision* nyumba zote zijengwe kwa pamoja, wananchi wangu wahamishwe wapelekwe kule. Vinginevyo kinachoendelea, kinakwenda kuongeza gharama za huu mradi wa *Tembo Nickel* na fidia inakwenda kulipwa mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba Mheshimiwa Mavunde unisaidie. Kwenye 40% ya fedha iliyoshikiliwa na *Tembo Nickel*, kwa sababu wananchi sasa wako kwenye taabu, angalau wapewe 20% au 10% ya fedha hizo, ili ziweze kuwasaidia kujikimu katika kipindi hiki ambacho wananchi wako kwenye taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni kwenye fidia. Wananchi ambao ardhi zao zimethibitika kuwa na madini, Sheria ya Madini, *Section* 97 ya *Mining Act* inasema kwamba, "Mmiliki wa leseni ya madini akishafika pale atatatakiwa kumfanyia *compensation* mwananchi anayemiliki *Surface Right* kwa kutumia Sheria ya Ardhi". Hapa kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria za Ardhi, lakini kuna Sheria za Madini. Kuna mmiliki wa ardhi kwa maana ya *Surface Right*, kuna mmiliki wa Haki Madini mwenye leseni ya kuchimba madini. Eneo hili linawapasua kichwa Ma-*RMO*, Maafisa Ukaguzi wa Madini nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *model* nzuri tumeanza kuziona huko Musoma. Mwananchi mmoja alipotaka kupewa fedha alikataa akaomba angalau 0.002 ya *percentage* inayotokana kwenye uzalishaji. Amelipwa hela nyingi sana, tofauti na wale ambao wanalipwa *Surface Right* kwa kufuata sheria za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali, wananchi wa Ngara walinituma nije humu Bungeni kuishauri Serikali. Naomba niishauri Serikali iunde tume itakayounganisha watu wa madini na watu wa Wizara ya Ardhi. Waende wachunguze migogoro iliyopo kati ya *Surface Rights* na *Mineral Rights*, waje na mapendekezo ili nchi hii iweze kutoa msaada kwenye eneo hilo ambalo linatesa Watanzania, na kwa kweli watu wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye *rush*. Hapo nyuma waliweka utaratibu kwamba eneo fulani likigundulika lina madini watu wanavamia wanaanza kuchimba madini, wanatengeneza utaratibu wa kuwaratibu. Maeneo mengine yanayovamiwa unakuta ni leseni halali ya mtu, ameifanyia utafiti, unakuta leseni ina zaidi ya thamani ya shilingi trilioni moja, au shilingi trilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nini? *Rush* kwenye eneo la mtu ambaye ana leseni halali ni sawasawa na kuruhusu watu waende Kariakoo kwenye duka la mtu limejaa bidhaa, waingie ndani na kuanza kuiba bidhaa zilizopo dukani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtu amehangaika, amepata leseni, amefanya utafiti, mojawapo kati ya watumishi sio mwaminifu, anavujisha taarifa, unaamka asubuhi unakuta leseni yako kuna watu 4,000, au 5,000 wamejaa pale wanachimba madini. Kama Serikali zinapigana vita huko, kupambana huko, kama Serikali inazuia watu wanaofanya maandamano, Serikali haiwezi kushindwa kuzuia watu 300, au 400, au 2,000 waliovamia leseni. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba eneo hili liangaliwe, *rush* zizidhibitiwe. Kama ni *rush* iruhusiwe kufanyika eneo ambalo siyo leseni ya mtu, lakini mmempa mtu leseni ana haki pale, naomba Serikali iwalinde. *Principle function ya State* ni kuhakikisha raia wanalindwa na mali zao zinalindwa. Naomba eneo hilo lifanyiwe kazi. Kwa kweli Watanzania wenye leseni wanateseka katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye maslahi ya watumishi wa Tume ya Madini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako ulishaisha tafadhali.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea tumepata wageni kwenye *session* hii ya Bunge, ukiondoa wale ambao tuliowatangaza asubuhi.

Walioongezeka kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge, Waziri wa Madini ambao ni Wakuu wa Idara, Vitengo na Maafisa kutoka Wizara ya Madini, nadhani tukiwatamka msimame kama mpo. Maafisa wa Madini Wakazi wa Mikoa, *RMOs*, karibuni sana. *(Makofi)*

Kampuni za Madini zenye ubia na Serikali, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kutoka Kampuni za Madini katika ujumla wake, Chama cha Wachimba Madini *FEMATA* kama wapo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Chama cha Wanunuzi Madini CHAMATA, karibuni sana; pia tunao Taasisi za Fedha *NMB, CRDB, NBC* na Azania Bank, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa Dini kutoka Dodoma, kama wapo, karibuni sana viongozi wetu. Vile vile, tunao Machifu kutoka Dodoma. Karibuni sana Machifu. *(Makofi)*

Tunao Baraza la Madiwani kutoka Dodoma, karibuni sana; pia tunao Wenyeviti na Makatibu wa UWT, UVCCM na jumuiya ya wazazi kutoka Dodoma wale ambao mmekuja, karibu sana. *(Makofi)*

Tunawashukuru sana kwa kuja na kwa kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Anthony Mavunde, ambapo sisi hapa Bungeni tunaamini kwamba ndio injini ya Wizara ya Madini. Tunaamini mtaendelea kumuunga mkono kwa heshima ya Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge ambao ni wachimbaji wa madini kutoka Makongorosi Wilaya ya Chunya, Mkoa wa Mbeya kama wapo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Mbunge ambao ni walimu na wanafunzi wa *Tayrol Day Care Centre* kutoka Jijini Dodoma, kama wapo, sijawaona. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanausharika wanawake 47 na Wachungaji watatu wa Kanisa la KKKT Isanga Jimbo la Mbeya Mashariki, karibuni kama mpo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsante, tunaendelea. Tunaye Mheshimiwa Mary Mwanjelwa mwakilishi wa *Kudu Graphite,* ni mgeni wetu pia yupo kwenye Jukwaa, ahsante sana, nimekuona, huyu ni Mheshimiwa Mbunge na Naibu Waziri mstaafu. Tunashukuru sana kwa kututembelea Bungeni, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu na kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Madini hii iliyopo mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na Wenyeviti wengine kwa namna mnavyotuongoza vizuri katika Bunge hili. Kwa kweli namwomba Mwenyezi Mungu kupitia siku hii ya leo ya Ijumaa na kuwaomba Wajumbe waweze kuwarejesha tena kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini Mheshimiwa Anthony Mavunde, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Steven Kiruswa, Katibu Mkuu Samamba na Naibu Katibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watendaji wote wa Wizara, kwa kweli kazi kubwa mnaifanya baada ya kuondoka aliyekutangulia Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Dkt. Doto kuuwasha moto na wewe unahakikisha kwamba moto huo hauzimiki na kweli moto huo unaendelea kuwaka vizuri. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha nyingi kwenye Wizara hii ya Madini na kwa kuweza pia kubadilisha taratibu, sheria na tozo mbalimbali kwenye Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kutoa fedha nyingi kwa kuagiza mitambo kwa

ajili ya kuchoronga ili kujua wapi pana madini ili kuwasaidia wachimbaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niseme maneno machache yafuatayo: Mheshimiwa Rais, ameweza kutoa leseni za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo zaidi ya leseni 6,227, hongera sana Mama. Nami kama mchimbaji nimepata leseni hizo nikiwa mmojawapo kwenye hizo leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo Serikali iliweza kutangaza na kuwakaribisha wawekezaji waweze kuwekeza kwenye utengenezaji ama uchakataji, ama kupandisha thamani ya dhahabu ili wanapotaka kuisafirisha dhahabu ile iwe imeshapandishwa thamani. Serikali ikatoa maelekezo kwa wawekezaji waje wawekeze na kweli wawekezaji wetu wamepatikana na wakawekeza, na kuna *refinery* zaidi ya nane ambazo zimejengwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *refinery* hizi mpaka leo hii hazipati msaada wa kutosha kutoka kwa Serikali. Mfano kuna mama yetu ambaye ametajwa hapa, mama huyu anaitwa Mama Masasi mwenye *refinery* yake eneo linaloitwa Geita *Gold and Refinery.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yule ameweza kuwekeza kwenye fedha ambazo ameweza kukopa kwenye mikopo kupitia benki. Mama huyo amewekeza pamoja na wengine wote, lakini mpaka leo hii tayari Serikali haijawapa *support* ya kutosha ili waweze kupata manufaa na kurejesha majukwaa hayo kutoka benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali yangu, kwa sababu tulitangaza tunahitaji wawekezaji kwenye upande huo, sasa hivi kama kuna uwezekano tubadilishe taratibu. Leo hii kuna tani za dhahabu, kilo ya dhahabu zinapelekwa nje zikiwa ghafi wakati sisi tuna viwanda ambavyo tuliwaomba waweke viwanda hivyo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, abadilishe au kama kuna uwezekano, alete sheria tuweze

kuzirekebisha tuwasaidie hawa wawekezaji kwa sababu wamewekeza fedha nyingi. Leo hii dhahabu nyingi zinakwenda nje zikiwa ghafi. Kwa kweli naomba hili suala lije hapa mezani, liletwe Bungeni tubadilishe hizo sheria ziweze kusaidia viwanda hivi. Hawa hawataweza kurejesha bila Serikali kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa wachimbaji wadogo. Tunaishukuru Serikali, imeleta mitambo 10 kwa ajili ya kuchoronga. Naomba mitambo hii isambazwe kwenye kanda kwa sababu tuna kanda mbalimbali ambazo zinachimba, pelekeni hiyo mitambo ili iweze kuwasaidia hao wachimbaji na siyo hivyo tu, gharama ya uchorongaji ni kubwa, punguzeni gharama za uchorongaji ili wachimbaji wetu hawa wadogo waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, namwomba Mheshimiwa Waziri, hotuba yake imegusa maeneo yote, yaani nilipokuwa nataka kuchangia amepagusa, lakini naomba nikazie kuhusu hawa wachimbaji wadogo, wahakikishe taasisi za fedha zinapunguza masharti na riba ili wawekezaji wadogo waweze kukopeshwa, waweze kuendesha hizo kazi zao na kuweza kupata manufaa, lakini kupandisha pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri, anaingia kwenye Wizara hii, mwenzake aliyetangulia aliweza kukusanya mapato ya Taifa kwa 9.3%, yeye leo hii amefikia 10.1%. Mimi kama mchimbaji nasema bado haitoshi, tuwezesheni au wezesheni wachimbaji wadogo. Wizara hii ina uwezo wa kuchangia pato la Taifa hata zaidi ya 20%. Wekezeni fedha nyingi kwenye upande wa kuwasaidia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wachimbaji wadogo, anaenda kuchimba mzamo mmoja kwa siku tatu au siku nne anatumia zaidi ya shilingi 35,000, lakini mtakapowekeza ninyi na kupunguza gharama za uchorongaji na kuhakikisha kwamba hapa mchimbaji wetu anachimba, atakuwa amepata dhahabu; lakini mtakapoweka uchorongaji wenu mkaweka gharama ya shilingi 50,000/= itakuwa mmewasaidia hawa ambao wanatumia nguvu kubwa na fedha zao kwa kutumia ramli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wachimbaji walio wengi mmetoa lesenii zaidi ya 6,227, lakini kwenye leseni hizo utakuta mnanufaika na kupandisha hili pato la Taifa kwa 10.1% labda ni leseni 200 au 300, leseni nyingine zote wachimbaji wadogo hawanufaiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema analeta ndege nyuki, sijui ile ndege ya kumulika na kujua kwamba hapa kuna miamba! Naomba hilo ulifanywe haraka sana ili kuwasaidia hao wachimbaji wetu wadogo waweze kupandisha pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, kwa kweli leo nilikuwa sina mchango mkubwa sana baada ya kuisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amenigusa maeneo yote. Hapa nilikuwa nakazia tu, kwa hiyo, naomba alete hiyo sheria mezani tuhakikishe kwamba tunaibadilisha, na watu waache kupeleka dhahabu ghafi nje, kwanza zisafishwe hapa nchini ndiyo ziende nje, tuwasaidie hawa ambao wameweza kukopa fedha zao nyingi kwa ajili ya kujenga hizi *refinery*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Watu wanamshukuru Mheshimiwa Rais, jana amefanya jambo kubwa sana la kuongeza mishahara watumishi wa umma. Ukisoma kwenye mitandao, kila mahali wanasema pochi la Mama wa Taifa limetema, na wakisema pochi limetema maana yake mambo ni mazuri mwaka huu. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka niishukuru sana Wizara, kuanzia kwa Mheshimiwa Dkt. Biteko alipokuwa katika Wizara hiyo na Mheshimiwa Mavunde, ameanzia pale

alipoishia Mheshimiwa Dkt. Biteko na Mheshimiwa Musukuma amezungumza, mambo ni mazuri kule Tarime. Ndiyo waone ile hasira ya kuvua koti hapa, ndiyo maana mambo ni mazuri Tarime Vijijini kwenye Barrick. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nalalamika hapa Bungeni, siku ile ilikuwa eneo la Mrwambe na Nyamuchere wanatakiwa walipwe kifuta jasho na majibu ya Serikali hayakuwa mazuri. Tulipotofautiana pale tukagombana gombana tukakaa kwenye vijiji, tukakaa kwenye vikao, wale wananchi kile kifuta jasho wamelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hapa tunavyozungumza, Mheshimiwa Mavunde ameshanipa ratiba kwamba kesho tarehe 3 Mei, 2025 atakuwa Ingwe Sekondari, wameunda vikundi 47, vijana zaidi ya 1,700, anaenda kukabidhi leseni ya wachimbaji wadogo ili wafanye kazi ya uchimbaji, wasigombane na mgodi wa Barrick, hayo ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwombea Mheshimiwa Mavunde, Waheshimiwa Wabunge hawa wapitishe haraka haraka hii bajeti twende kule *Barrick North Mara* akabidhi leseni kwa vijana wa Nyamungo na Tarime Vijijini, kazi iendelee na tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano kwa kweli yameimarika sana kati ya halmashauri, na wananchi ambao wanazunguka mgodi kwa maana ya viongozi wale, lakini pia Wizara na mimi kama Mheshimiwa Mbunge wa eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kumekuwa na vikao vya mara kwa mara mpaka Rais wa Barrick mwenyewe anaingia mtaani anakutana na viongozi wa vijiji, maana yake wale wanaofanya kazi katika mgodi; vile vikundi vya akina mama, wajasiriamali, makampuni binafsi wameshatoa fedha, wame-*pump out* fedha kwenye eneo lile zaidi ya shilingi bilioni 65 ambazo watu binafsi wanazungusha katika shughuli mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani hata mchele ulikuwa unatoka *South Africa*. Sasa hivi mchele wanauza akina mama wadogo wadogo pale Nyamungo na biashara yao inaendelea kukua, hayo mahusiano hapo mwanzo hayakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mgodi umeendelea kulipa. Ninavyozungumza, kwenye Halmashauri Tarime Vijijini wameshalipa kodi ya ushuru wa huduma zaidi ya shilingi bilioni 21.6, lakini wameshalipa vijiji. Nimeingia madarakani tangu mwaka 1995 walikuwa wanagombana na mgodi, vile vijiji vitano vilipwe asilimia moja na walikuwa hawajawahi kulipwa, wameanza kulipwa mwaka 2023, ninapozungumza hapa leo wana shilingi bilioni 6.8 kwenye *account* za vijiji vitano vinavyozunguka ule mgodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa na kesho nimemwambia pia Mheshimiwa Waziri atakabidhi asilimia hapa moja nyingine katika vijiji vile. Maana yake hili, fedha zikisimamiwa vizuri viongozi wa vijiji, madiwani, vijiji 11 kata tano wakapanga vipaumbele, sitarajii katika maeneo yale atakuja Mwenyekiti wa Kijiji kuanza kuomba tena mshauri zahanati, wakati ana shilingi bilioni 1.7 katika *account* ya Kijiji. Haya mafanikio makubwa ndiyo tuliyofanya yawepo ili watu waweze kupata huduma kubwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi huu, umetoa huduma mbalimbali katika jamii. Kama kuna shida kwenye zahanati, kwa mfano pale Nyangoto walikusanya makampuni, wanafanya kazi pale mgodini wakapeleka fedha ile shilingi milioni 62, wamepeleka vifaa vya akina mama na mtoto wana-*support,* tunajenga nyumba ya mama na mtoto pale zaidi ya shilingi bilioni 350.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo yote ni mambo tulitamani yawepo kwa muda mrefu na ninashukuru ndani ya uongozi wangu na wenzangu, haya mambo yameweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo sasa zimesambaa katika jimbo zima. Nina jimbo ambalo lina kata 26,

walikuwa wananufaika kata tano, vijiji 11 ninavyozungumza hapa kata zote 26 kuna miradi ya maendeleo kutoka fedha ya *CSR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vijiji vinavyozunguka vyenyewe wana zaidi ya shilingi milioni 291 kila Kijiji. Kwa hiyo, kipi waseme nini wanahitaji katika eneo lao kwa vipaumbele kupitia mikutano ya vijiji ili waweze kufanya kazi vizuri sana? Leo unapozungumza hapa, kule Tarime Vijijini pale Nyamongo tunajenga soko la dhahabu zaidi ya shilingi milioni 800 kwa kuanzia, lakini ukienda Nyamwaga Makao Makuu ya Halmashauri, tunajenga stendi na soko kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kata ambazo tunajenga jengo la mama na mtoto kama pale Kioruba kwa shilingi milioni 180, tunajenga zahanati pale Mangucha - Nyamungu shilingi milioni 120, tunajenga pale Nyabirongo – Susuni zahanati shilingi milioni 120, tunajenga pale Gwitiro shilingi milioni 120, Getakasembe milioni shilingi 120 zahanati, tunalima barabara kule Susuni kwa masista shilingi milioni 150, tunajenga daraja pale Nyantare – Gorong'a tunajenga zahanati kabisa. Miradi ipo pale *online* inafanya kazi. Zile shilingi bilioni 9.64 zinafanya kazi. Haya mambo yakifanyika vizuri malalamiko yatapungua sana katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zipo, Mheshimiwa Waziri asikilize, moja amesema Mheshimiwa Musukuma hii miradi yote shilingi bilioni tisa ambayo inaendelea na Geita shilingi bilioni 23 kuna *double standard.* Ndugu yangu wa Nyang'wale hapa na watu wa Kahama wao miradi hii inatekelezwa kupitia halmashauri, mgodi unalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime na kule Geita kwa akina Mheshimiwa Musukuma mgodi ndiyo unaotekeleza miradi. Serikali imetoa mwongozo kwamba darasa moja lijengwe kwa shilingi milioni 25 pale Tarime, darasa moja ni shilingi milioni 37 kinyume na Mwongozo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile miradi mingi itapunguzwa kwa sababu nyumba haizidi shilingi milioni 100, watajenga 150 kupitia mkandarasi. Tunaomba mwongozo ule utekelezwe, mgodi

hauna kazi ya kujenga madarasa, kuchimba visima, kujenga choo, kazi yao ni uchimbaji na *operations.* Ile kazi ya kusimamia miradi iachiwe halmashauri, mgodi ufanye kazi ya malipo ili uweze ku-*deal* na *operations*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea changamoto katika halmashauri zetu, halafu mgodi ukaacha kutekeleza miradi utaenda kwenye *operations.* Naomba, Mheshimiwa Waziri hili lifanyiwe kazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili, Tarime Vijijini ambayo tayari utaenda, utaulizwa na kesho, ni fidia. Kuna changamoto ya malipo ya ardhi katika maeneo yetu. Sasa maeneo yale mgodi unatakeleza malipo kwa namna ambavyo Mdhamini Mkuu wa Serikali amepeleka malipo yake. Unalipa fedha kidogo sana pale. Ukienda Murwambe kuna malalamiko, Nyamichele kuna malalamiko, Komarera kuna malalamiko, Kewanja kuna malalamiko, Nyakunguru kuna malalamiko, kuna malalamiko pale mpaka Nyamichune mpaka Matombo fedha inayolipwa ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi unasema, mkituambia tulipe kilomita moja shilingi milioni saba, 10 tutalipa, hii mmewaambia walipe shilingi milioni tano. Leta sheria hapa ibadilike ili watu walipwe ardhi yao kulingana na ambacho kipo chini ya ardhi ile ili kupunguza mgogoro na malalamiko ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja Mheshimiwa Waziri, uifanyie kazi sana, ile fidia mnayolipa haiwasaidii wananchi. Kwa nini mwananchi asipewe *share* na mgodi? Kama mtu anakuja anachimba eneo hilo, unanihamisha badala ya kunilipa fidia, tuingie kwenye *shareholder.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tarime, Nyamwaga kuna Mzee Msabi analipwa mabilioni ya fedha, amekuwa tajiri mkubwa, yeye hakupokea fedha ya kujengea nyumba, aliingia *shareholder,* mgodi ukichimba nyingi anapata mgao mkubwa, mgodi ukipata kidogo...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya, kwa hiyo, tuombe...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kutokana na muda, hitimisha hotuba yako, muda wako ulishaisha. Nakuomba radhi Mheshimiwa Hussein.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwangu mimi kama Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, mgodi umefanya kazi nzuri sana, Wizara imefanya kazi nzuri sana. Nitoe wito kwa wananchi wa Tarime Vijijini waliopata fedha hizi na hata vijiji vile 11 hawana sababu ya kulalamika. Wakipata mgao wa fedha kuna ile asilimia ya Serikali waende kwenye mikutaniko ya wananchi wapange miradi kulingana na vipaumbele na mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana wakapiga hatua kubwa zaidi na maisha ya wananchi pale yakabadilika na wakaimarisha mahusiano mazuri sana. Mheshimiwa Waziri karibu sana kesho Nyamongo tufanye kazi ya kutoa leseni kwa vijana wale, wafanye kazi ya uchimbaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita, nakushukuru. Mheshimiwa Hussein nakuomba radhi, niliona ulihitaji kutoa taarifa, lakini kwa bahati mbaya muda wetu umekwisha, nakuomba radhi sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na hotuba hii itahitimishwa na mtoa hoja leo alasiri. Natambua kwamba leo ni siku ya ijumaa na nimepewa maelekezo mahususi kabisa na Katibu wa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi kuzingatia utaratibu wetu wa kupitisha bajeti saa 11.00 jioni Waheshimiwa Wabunge wote tuwepo ndani ya ukumbi.

Wachangiaji wetu wa mchana ambao tutaendelea nao ni Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

Utaratibu wa uchangiaji ni kama ambavyo nimetamka, wale ambao wametajwa mwanzoni wahakikishe wanakuwepo kwa wakati huo.

Baada ya matangazo hayo, nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 alasiri.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBA MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa hapa kwenye orodha naona kuna Mheshimiwa Magessa, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Mariki, na Mheshimiwa Maganga.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote wa Bunge hili kwa kunipatia fursa hii, na vilevile kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya ya uratibu na uongozi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ambayo ametupatia tena leo kuweza kupata nafasi ya kuongea kuhusu hotuba hii ya Waziri wa Madini au Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa usimamizi na uongozi thabiti wa Wizara hii na kufanikiwa kufanya ichangie vizuri kwenye pato la Taifa. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uongozi mzuri pamoja na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wanafanya kazi na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia huko tunakotoka ambako kuna machimbo, sasa biashara hii ya machimbo imechangamka sana. Ni dhahiri kwamba Waziri ana kazi kubwa anayoifanya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha sasa uwazi na uwajibikaji katika sekta hii unaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mitambo ya uchorongaji ambayo sasa inapatikana kwenye maeneo yetu. Hii imesaidia sana uchorongaji uwe rahisi, lakini ni ombi langu kwamba mitambo hiyo iongezwe kwa sababu ilipopatikana na wachimbaji nao wamekuwa wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina kata 14 zinachimba dhahabu, kwa hii mitambo 10 inawezekana isitoshe kabisa. Pia, ndugu zangu; Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Kalemani, na Mheshimiwa Maganga, wanao. Kwa hiyo, ninaamini tukiongeza mitambo hii tutakuwa tunawarahisishia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia habari ya hiyo ndege nyuki. Hapa kuna majibu ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa, lakini hasa wachimbaji wadogo. Tunataka utafiti ufanyike wa kutosha ndani ya nchi hii. Mwaka 2024 kumbukumbu zetu zilikuwa zinaonesha wazi kwamba tume-*survey* 16% na *plan* yetu ni kwenda kwenye 50%, lakini utekelezaji wa utafiti huu ambao umeshafanyiwa majaribio, kwenye hotuba wamesema wazi wamejaribu Geita na Dodoma kuthibitisha kwamba tukienda kwenye zoezi hili tutakuwa tumefanya kazi kwa faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana zoezi hili liharakishwe ili kuona wananchi wetu wanafanya kazi vizuri. Hiyo *Geophysics (airborne survey)* naomba sana ifanyike ili tupunguze ubashiri wa wachimbaji wetu kwa sababu katika ubashiri, wapo wanaopoteza mitaji na watu wengi wanakuwa maskini badala ya kupata kipato cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ambacho nilitaka kushauri ni namna ambavyo tunashughulika na haya madini muhimu na madini mkakati. Hii hotuba yetu inasema wazi kwamba sasa mnatengeneza mkakati ambao baada ya kukamilika, tutakwenda kuhakikisha kwamba madini haya sasa yanafanyiwa kazi. Naomba sana, kwa sababu tunaona kabisa katika teknolojia za kisasa, madini muhimu na madini mkakati ndiyo yatakayoingia kufanya kazi vizuri na yatatutoa mahali fulani kwenda mahali fulani kwenye uchumi. Kwa hiyo, naomba mkakati huo unaotengenezwa, kama ni wataalamu wanatengeneza, basi wawahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa nasikia wanasema inawezekana shughuli hizi kukawa na mkataba una miaka 50 au 45. Kwa namna hiyo, kwa teknolojia ya zamani inawezekana, lakini kwa sasa teknolojia inabadilika kila baada ya miaka mitano, ukisubiri miaka 30 au 40 utakuta teknolojia tena haikuungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kuhusu *CSR*. Kila aliyesimama hapa ambaye anatoka kwenye *CSR,* wamesimama hapa Mheshimiwa Mwita, na Mheshimiwa Musukuma; *CSR* ina *volume* kubwa ya fedha, lakini utekelezaji wake unatupa

changamoto kwa sababu kila wakati kuna fedha *pending* imebaki labda shilingi bilioni 21, au shilingi bilioni 22. Kwa nini hizi fedha zinabaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu, nilimsikia mchangiaji mmoja alitoa taarifa hapa asubuhi, akasema, halmashauri hawana uwezo wa kutumia shilingi bilioni nne wakati wanapelekewa shilingi bilioni 50 na Serikali, wanatumia. Kuna mahali Serikali inatakiwa ione namna gani wanaweza kumiliki fedha zile ili wafanye kazi vizuri zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia kengele imelia hapo, najua hujawasha taa. Niseme tu wazi tumetembea kwenye makaa ya mawe, lakini Serikali inashughulika na watu binafsi kutengeneza mkaa mbadala wa mawe *(briquettes)*. Hoja yangu tu ni kwamba ukiangalia takwimu, karibu misitu hekta 400,000 kwa mwaka inakatwa ili tupate mkaa wa kupikia nyumbani. Sasa tukipata *briquettes* maana yake tutapunguza kiwango cha misitu inayoharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nitoe kama wazo au ushauri. Kule Zanzibar nina mashaka sana misitu siyo mikubwa, hivyo nao wapelekewe hizi *briquettes* ili tupunguze ukataji wa ile mikoko na mikarafuu ili waweze kupata nafasi ya kutumia huo mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nataka niishie hapa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kanyasu, wajiandae Mheshimiwa Mariki na Mheshimiwa Maganga.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima, Naibu Waziri na Watendaji Wizarani kwa kazi nzuri ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa kazi kubwa ambayo tuliifanya pamoja kule Geita kushughulikia mgogoro wa wananchi ambao wamekuwa kwenye mateso kwa takribani miaka 27 ya kusubiri Serikali iweze kuwasimamia ili waweze kupata haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme ukweli Mheshimiwa Waziri ni mtu *accessible*, yuko *punctual* na anasikiliza. Sasa hivi wananchi wa Geita wanatazama Bunge, wanataka kufahamu juhudi zote tulizozifanya kwa takribani miaka miwili, wewe ukiwa kwenye hiyo Wizara, hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Musukuma amesema hapa asubuhi, wananchi wa Nyakabale na ninatamani sana unisikilize vizuri, na ningetamani labda pengine angekuwa ni mtu unayemfahamu ambaye anaishi Nyakabale, anataka kutoka hapa kwenda pale Jakaya Kikwete kwenye mkutano, lakini ili afike hapo aende Kizota, aende kule *SGR* halafu ndiyo arudi kutokana na zuio lililowekwa na mgodi halafu jambo hilo tu kuliamua limechukua miaka 25 Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanapopata matatizo usiku, wanasafiri kwa bodaboda na mama mjamzito. Hawa watu wanapopata matatizo usiku, hawaruhusiwi kupita mgodini katika eneo ambalo mgodi uliwakuta. Sheria zote tumezipitia, zimetaka hao watu waondolewe, lakini Serikali inapata kigugumizi kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikusudii kushika shilingi yako leo, lakini nakusudia kutaka kufahamu, hivi ni kweli kwamba jambo hili limeshindikana na kwamba wananchi hawa sasa kwa miaka yote hii haiwezekani kuwapa haki yao? Kwa sababu haiwezekani tukawa tunashuhudia jambo hili linaendelea kuwepo halafu tunazungumza hapa linabaki kama lilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha, aniambie hatma ya wananchi wa Nyakabale na Nyamalembo ambao mazungumzo yao yamechukua zaidi ya miaka miwili, ambapo mgodi unatakiwa ujue kwamba hawa ni wananchi ambao umewakuta pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni hili ambalo amelizungumza vizuri Mheshimiwa Magessa. Tunapozungumzia Geita, tunazungumzia madini; na sisi uchumi wetu ni madini. Wapo wakulima, wapo wavuvi, lakini tunajulikana kwa sababu ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mitambo ya kuchoronga ambayo imekuja, na tunashukuru sana Serikali kwa msaada ambao inawapa wachimbaji, lakini kama ambavyo nimezungumza pale awali, kwamba, kwa kuwa biashara yetu ni madini, iko haja ya Serikali kuendelea kuwekeza kwenye teknolojia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ambao niliutoa hapo awali kwenye mchango wangu mwingine ni kwamba, hizi kampuni nyingi kubwa ambazo zinazunguka na wachimbaji wadogo wadogo pengine ingekuwa ni sehemu ya masharti kwamba watoe msaada wa kiteknolojia kwa wachimbaji wadogo wadogo hasa misaada ya kiutafiti badala ya kusubiri mitambo 10 iende kwenye mikoa 26. Hii Mikoa 26 ina wilaya zaidi ya mia moja na kitu na wachimbaji wako zaidi ya 100,000 kuja kuwasaidia. Kwa hiyo, hawa wangeweza kutoa msaada wa kiufundi na wakaongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la *CSR* ni wajibu wa kampuni. Kilichotokea mwaka huu ni kampuni kuidharau Serikali. Baada ya mwezi Desemba kufika wakafuta ile *CSR* wanasema kwamba wamecheleweshewa majibu na Serikali. Hata hivyo, shida iko wapi? Shida iko kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemweleza Mheshimiwa Waziri, unatenga shilingi bilioni tisa, ule mgodi hauna wataalamu wa kusimamia miradi. Unataka wao wafanye manunuzi, wao wakafanye usimamizi; matokeo yake, miradi yote iliyoanza miaka mitatu nyuma imeshindikana kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, wanang'ang'ania kutangaza na kutafuta wazabuni. Matokeo yake hatuwezi kwenda mbele kwa sababu hiyo kazi itakuwa kubwa kwao. Kwa hiyo, sisi tunataka mabadiliko ya Kanuni za *CSR* yafanyike

mapema ili hizi pesa ambazo wanatuambia tumezirudisha *South Africa,* huo ni wajibu na tumetunga sheria hapa. Kama tunaweza tukakaa hapa kujadili sheria ambayo mtu anaweza akajifungia ndani akaamua pesa zirudi *South Africa,* hakuna sababu ya kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, naomba nimalizie. *Geita Gold Refinery* tulijenga kwa maelekezo ya Serikali na Serikali iliahidi itatenga 20% ya dhahabu kwa ajili ya ku-*process* ndani. Tumetunga sheria hapa, ikaonekana ina upungufu, tuka-*review* ile sheria kwa mara ya pili tukasema ni wajibu wa *Mine Right Holder* kutenga dhahabu 20% kwa ajili ya viwanda vya ndani na sheria imesema vizuri kwamba wasipotenga, unawanyima kibali cha kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinafanya kigugumizi? Viwanda hivi havikuanzishwa kwa sababu wanataka kukopa wawekeze. Huyu mama namwonea huruma sana. Amekopa fedha nyingi kwa maelekezo ya Serikali kwamba watampa dhahabu. Leo benki wanataka kuuza kiwanda kwa sababu hawezi ku-*process* dhabahu, kwa sababu Serikali imeshindwa kum-*supply* dhahabu. Tumetunga sheria ambayo mgodi wowote lazima uache 20%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuifute hiyo sheria, kwa sababu hatuna uwezo wa kuitekeleza. Tunajadili jambo ambalo tumelitungia sheria, tunajadili kama vile ni jambo ambalo ni *discretion* ya mtu mwenye leseni kutoa hiyo dhahabu wakati tumesema tunataka kufanya *value addition* kwenye dhahabu ili kutengeneza ajira nchini. Sasa utatengenezaje ajira kama unaonea huruma hata sheria uliyoitunga, unashindwa kuisimamia?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hili jambo wala sio yeye, ni sheria tumetunga. Migodi isimamiwe iache dhahabu ili hizi *refineries* zifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tena Mheshimiwa Kanyasu unavyosema ni sahihi kabisa. Kulikuwa na mpango hapa wa dhahabu iondoke nchini.

Nafikiri Mheshimiwa Waziri, vilevile umesikia taarifa. Migodi ilitaka iondoe dhahabu ikasafishie kwao. Mkifanya hivyo mtafanya makosa makubwa sana. Msikubali kabisa, dhahabu itapotea na nchi itakosa mapato yake. Kwa hiyo, msikubali kabisa. Tanzania kuna *refinery*, dhahabu isafishwe Tanzania, thamani ya dhahabu ipatikane hapa hapa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mariki, wajiandae Mheshimiwa Maganga na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uzima na afya njema. Pia, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Antony Mavunde, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Kamishna pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Madini kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika Sekta hii. Sote tumeshuhudia Sekta ya Madini ikikua siku mpaka siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunapozungumza, Sekta ya Madini imeweza kuchangia zaidi ya 10.1% katika pato la Taifa. Yote haya yanatokea ni kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka jicho la kipekee katika Sekta hii ya Madini. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya mpaka Sekta ya Madini kwa sasa inaenda kuwa mkombozi kwa kuchangia ajira kwa akina mama pamoja na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ningependa kuchangia mambo machache jioni hii ya leo. Kwanza ni suala la uendelezaji kwa wachimbaji wadogo, na hapa tena ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo 15 kwa ajili ya uchorongaji. Tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu mitambo hii imeenda kuleta mapinduzi katika Sekta ya Madini na imeenda kugawanywa maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ihakikishe kwamba pamoja na mitambo hii, wanawake waweze kutengewa baadhi ya mitambo na waweze kukodishiwa kwa bei nafuu kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi na ana dhamira nzuri kuhakikisha kwamba akina mama nao wanainuliwa katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za nyuma akina mama walikuwa nyuma sana katika uchimbaji wa madini, lakini kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli mama yetu amedhamiria kuhakikisha kwamba wakina mama na wenyewe wanafaidika na hii Sekta ya Madini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tulishuhudia Rais wetu kipenzi alitoa leseni kwa wachimbaji wadogo wakiwemo wanawake. Tunampongeza sana Rais wetu kwa kuona umuhimu wa wachimbaji wadogo na kwa kuwagusa akina mama na kuwapatia leseni za uchimbaji ili na wenyewe waweze kufaidika na madini yaliyopo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la ufutaji wa leseni, na hapa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwani kulikuwa na leseni zaidi ya 2,648 ambazo zilikuwa zimeshikiliwa na watu mbalimbali, lakini walikuwa hawazifanyii kazi. Waziri wa Madini kwa kuwa ni kiongozi makini akaona kwamba suala hili siyo zuri kwa sababu watu wanashikilia maeneo, lakini hawayafanyii kazi, akaamua kufuta leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea, zoezi hili bado linaendelea na mpaka sasa kuna leseni zaidi ya 58. Mheshimiwa Waziri, nakuomba katika hizi leseni 58 pia watengee wanawake kwa kuwa ni waaminifu, wakiwezeshwa watachimba madini na wataongeza pato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwamini Mheshimiwa Waziri, ni mtendaji kazi mzuri. Namwomba sana aende na akina mama katika uchimbaji wa madini. Juzi tulishuhudia katika kurasa 345 za Mheshimiwa Rais, tumeona akina mama wanafanya vizuri na walijieleza na tukaona wana uwezo. Hivyo, akina mama wakiwezeshwa katika Sekta hii ya Madini wanaweza kufanya mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni utekelezaji wa ahadi za viongozi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wote tunakumbuka, Bunge kupitia Kamati ya Nishati na Madini, nami ni mjumbe wa Kamati hii, tulisema kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yapo katika hifadhi zetu, tukaiomba Serikali na mama yetu kipenzi akaridhia baadhi ya maeneo ambayo yapo katika hifadhi, likiwepo eneo la Kigosi kwamba liweze kutolewa na kupewa wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza ahadi hii na eneo la Kigosi tayari limetolewa na wachimbaji wadogo wadogo wameweza kugawiwa maeneo kwa ajili ya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kumejitokeza changamoto. Katika eneo la Kigosi na maeneo mengine ambayo yalikuwa ya hifadhi, kumekuwepo na baadhi ya sheria ambazo ni ngumu. Naiomba sana Serikali yangu sikivu kuangalia sheria hizi. Mfano, labda mtu anaambiwa akikata mti katika eneo la uchimbaji anatakiwa alipe pesa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri dhamira ya Serikali na dhamira ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kuwasaidia wachimbaji wadogo. Tukiwawekea masharti magumu sana mwishoni watashindwa kufanyia kazi leseni hizi na

matokeo yake leseni wataenda kuwauzia wachimbaji wakubwa, na dhamira ya kuwapa wachimbaji wadogo itashindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana tufuatilie jambo hili tuweze kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo ndio wanachimba katika maeneo haya. Serikali ni moja, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Madini tukae tuweze kuangalia vibali hivi kupitia *TFS* tuweze kupunguza masharti ili wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusiana na mkaa mbadala. Naipongeza *STAMICO* kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Kwa kweli suala la mkaa mbadala linakwenda kuleta mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali wakishirikiana na *STAMICO* tuzidi kutoa elimu kwa akina mama kwa sababu tunatambua watu wanaoathirika sana na kutumia nishati chafu ni akina mama. Tumesema kwamba ifikapo 2034 tunataka kwamba 80% ya Watanzania tuweze kutumia nishati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara tushirikiane kwa pamoja na Serikali kuhakikisha elimu inatolewa na ikiwezekana mkaa mbadala uweze kupewa ruzuku kama tulivyofanya kwenye mitungi ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Serikali yangu ni sikivu na jambo hili linawezekana. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, mkaa mbadala tuweze kuleta ruzuku ili wananchi waweze kupata kwa bei nafuu zaidi na tunaamini mkaa huu mbadala utaleta ajira kwa vijana, lakini utahudumia akina mama na utawaokoa akina mama ambao walikuwa wanaangamia maisha yao kutokana na kutumia nishati chafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tena kuipongeza Wizar ana pia niipongeze sana Kamati yangu ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa na nzuri tuliyoifanya na mpaka Wizara imeweza kuongeza ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba kutokea mwaka 2022 mpaka 2023 tulikuwa na ukusanyaji wa maduhuli zaidi ya shilingi bilioni 678, lakini mwaka wa fedha 2023/2024 ukusanyaji wa maduhuli uliweza kufikia shilingi bilioni 754, lakini kufikia mwaka 2024/2025 tunatarajia kukusanya zaidi shilingi trilioni moja. Nawapongeza Wizara, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na mmeshafikia zaidi ya 66% ya lengo. Hivyo hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maganga, ajiandae Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa, namshukuru Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kupata nafasi hii tena jioni ya leo kuweza kuchangia hii hotuba ya Waziri wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuturuhusu Pori la Kigosi wachimbaji wadogo waanze kuchimba kwenye hilo pori. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, wamefanya kazi kubwa, wametoa leseni kwa uaminifu, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kingine kinachonifurahisha hapa, Waziri wa Madini ni yule ushauri wa Kamati, tumekuwa tumkushauri ndani ya Kamati anatusikia kwa sababu ushauri wetu ni ushauri wa wananchi. Sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi tu, hata kama kauli zetu zitakuwa ngumu sana, ina maana tunatumwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zote hizo, lakini nielekee kwenye changamoto, kwa sababu kila palipo na jema changamoto hazikosekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *issue* ya pori la Kigosi kwa Sheria za *TFS* pamoja na Sheria za Madini zimeleta mkanganyiko, maana vikundi vingi vilikata leseni, lakini leseni hizi mpaka sasa hivi

hazichimbwi kulingana na sheria zilizopo kwamba kitalu kimoja unatakiwa unapopigiwa hesabu zaidi ya shilingi milioni sita kulipa ili kung'oa ile miti na kuweza kuchimba, sasa hili limeleta uchonganishi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo hilo la Mbogwe ambalo Kigosi kwa ukubwa wake ndiyo iko pale. Kwa hiyo, kumekuwa na manung'uniko makubwa sana, na hili naiomba Wizara ya Maliasili pamoja na Wizara ya Madini, Wabunge watunga sheria na wabadilisha sheria, ikiwezekana haraka haraka tubadilishe hizi sheria watu wakachimbe, kwa sababu watu wameshauza ng'ombe zao, wameshanunua leseni na leseni hizo hazisaidii tena, zipo ndani tu, kwa sababu wameshindwa baada ya kwenda *site* kuonyeshwa maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye upande wa wachimbaji wadogo wadogo, katika Jimbo langu kuna migodi zaidi ya 15. Zipo kero ambazo wamenituma wachimbaji niseme hapa zikiwemo tozo nyingi kidogo kidogo zinawasumbua, wanaomba kulegezewa hizo tozo ili kusudi waendelee kuchimba vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo wamenituma hapa, hizi mashine ambazo zililetwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2024 zimegawiwa kwenye maeneo mengine, Mbogwe hatujapata mashine hata moja. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri huwa wanakuja kuangalia eneo la Mbogwe liko vizuri kwenye uchimbaji. Kwa hiyo, kwenye bajeti hii aliyoiomba ambayo amekusudia kwenda kukusanya zaidi ya trilioni 1.4…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anaongea vizuri sana. Hizo mashine yeye anasema

Mbogwe hajapata, hata sisi Nyang'hwale bado mashine hatujapata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naipokea taarifa ya Baba yangu, lakini nilindie muda ili kusudi niweke nondo za wananchi wa Mbogwe pamoja na huko Nyang'hwale kwa sababu ni mkoa mmoja wa kimadini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuhalisia, hizi mashine zinapokuja kwa sababu zimelenga kuwasaidia wachimbaji wadogo, ni vyema mikoa ya kimadini hii angalau hata kama ni chache ziende mbili mbili kila mkoa wa kimadini ama moja moja ili kujenga usawa kuliko kuwapa *STAMICO* peke yake, kwa sababu tunao watu walio na uchungu na Taifa hili, ila wamekosa vitendea kazi tu vya kuweza kuchimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwaangalia watu hawa kiukweli wanachimba kwa kukadiria, hawajawahi kupimiwa na *GST* wala kufanyiwa tafiti yoyote na Serikali, lakini wanaingiza mapato makubwa Serikalini. Kwa hiyo, kuna kila namna ya kuweza kuwashika mkono wachimbaji wadogo hasa kwenye huu mkoa wa kimadini wa Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nimeliona Mheshimiwa Waziri ameliweka kwenye mpango wake, ni kujenga Ofisi ya Mkoa wa Kimadini. Naiomba sana haraka iwezekanavyo hiyo, kwa sababu watumishi wote wamepanga kwenye *slop*e sasa hivi. Wanafanya kazi kwa kujibana utafikiri siyo wakusanya matrilioni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii na yenyewe iende haraka sana, pale Mheshimiwa Waziri atakapoanza tu bajeti yake hii utekelezaji uhakikishe hilo jengo linajengwa haraka iwezekanavyo hapo Masumbwe na liwe jengo la ghorofa lenye kupendeza sana, kwa sababu hawa watu wanakusanya makusanyo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watumishi hawa hawana magari ya kufanyia kazi. Nasi huko Mbogwe kila siku migodi inaibuka, unaweza ukasikia Nungwiza pameibuka, Kanegere, na maeneo mengi kwa sababu watu wa Mbogwe ni wajanja, wanazijua dhahabu na wamejaliwa na Mwenyezi Mungu kujua sehemu zenye dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna kila sababu hawa watumishi wa sekta ya madini wawezeshwe ili waweze kuwa wanawahi pale inapojitokeza *rush* kabla leseni haijatoka ili kusudi yasiwe yanapotea mapato kwenye Wizara ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine napenda tu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa usikivu wake. Kadri tunavyozidi kuwa naye kiukweli nilikuwa na mashaka makubwa sana kama atatuelewa vizuri, kwa sababu Wagogo na Wasukuma ni vitu viwili tofauti sana, lakini kiuhalisia tunaona miujiza. Kila tunachomwambia anatuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la maduara. Wanatoa leseni, lakini leseni hizi wanakuta watu walishaanzisha maduara zaidi ya miaka mitano au minane, wanawapa watu leseni kwenda kumiliki maeneo yale. Wakifika wale watu, sana sana walio wengi huwa sio wastaarabu sana, wanafikia kwenye Jeshi la Polisi na kuwafukuza hawa wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** …na kuwafanya kama hawako kwenye nchi yao. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Madini, yeye ni kijana mwenzetu, ana kila sababu ya kuwalinda Watanzania wenzake wale wanaojishughulisha na uchimbaji, kwa sababu na wao hawakutaka waishi hayo maisha ila wanapokosa ajira, inalazimika waende wakapambane kwenye machimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi, wanapotoboa ama wanapopata zile mali halafu anakuja mtu tu na leseni

kujitambulisha kwenye Mamlaka na Dola za Kiserikali, wachimbaji wadogo wanafukuzwa bila fidia. Kwa hiyo, hii naomba aiweke sawa ili wachimbaji wenye maduara waweze kulipwa haraka iwezekanavyo pale wanapoenda kwenye maeneo ya kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine ambalo nimetumwa na watu wengi sana, wenye maeneo ya mashamba. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Madini ameamua kutusaidia Watanzania, kuna kila sababu hao wanaomiliki mashamba wapewe kipaumbele, ikiwezekana wawe wanaingizwa kwenye leseni, kwa sababu fidia ni ndogo sana ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mtu amekuwa na shamba kwa muda zaidi ya miaka 100, inatokea dhahabu, anaenda kupigiwa hesabu za kiserikali, anatoka na shilingi milioni tatu mpaka nane halafu limgodi linaendelea kutema watu wanatajirika kwenye eneo hilo. Unakuta kuna makaburi wa mababu zao hapo kwenye maeneo, wanaambiwa waondoke, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla lazima liangaliwe upya. Mtu amekaa na ardhi yake ama amekaa na mbuga yake muda mrefu, halafu inakuja *GST* kusema hapa kuna mali, mtu anahamishwa kama mkimbizi. Kuna watu wengi ambao wameniletea haya malalamiko ikiwemo mgodi wa Mabomba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, malizia.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgodi wa Nyakafuru, mgodi wa Bukandwe, Mgodi wa Kanegere, Mgodi wa Nungwiza na Mgodi wa Mpakani. Hawa watu wametoka kwenye maeneo yao, lakini haya maeneo yanatoa dhahabu na wanalia sana. Wanaomba Serikali iliangalie kwa macho mawili ili warudi kwenye maeneo yao, walipwe malipo mazuri, ama waingizwe kwenye leseni, nao wawe wanafaidika kwenye mashamba yao, kwa sababu waliishi babu

zao na walizika pale pale, na hawana namna nyingine, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Karibu Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Kapufi mjiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii. Kwanza nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Madini, bajeti hii tuiunge mkono moja kwa moja. Zaidi ya wachimbaji milioni mbili wanatuangalia sasa hivi kwa kazi nzuri iliyofanyika tokea miaka minne ya Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Madini alikuwa Mwanasheria wetu sisi wa Chama cha Wachimbaji *(FEMATA),* kwa hiyo, anayajua matatizo ya wachimbaji moja kwa moja. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Spika, sisi wachimbaji kuwa ndio Wajumbe wa Kamati hii. Hili ni jambo kubwa sana, aliona mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunaozungumza hapa ni wachimbaji, na wenzetu wachimbaji zaidi ya milioni mbili leo hawajaingia *underground,* wako wanaamgalia TV kuona je, akina Tabasam watasema nini kuhusiana na hili suala la madini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo magumu mengi kwenye nchi hii wachimbaji, ndiyo yanaanza kurekebishwa. Katika vitu Mheshimiwa Rais alivyofanya vikubwa ni kuwaweka hawa watu katika eneo hilo. Kumpa nafasi hii Mheshimiwa Mavunde kama mchimbaji mwenzetu, anayajua maisha ya wachimbaji, lakini Naibu Waziri pamoja na kwamba Wamasai ni wafugaji, kule wachimbaji pia na sisi tunao wafugaji, naye kule anao wachimbaji Arusha, anayaishi maisha haya ya wachimbaji. Pia Katibu Mkuu wa Wizara hii yeye ameanzia chini kabisa, alikuwa ni Afisa tu wa Madini, baadaye akaja akawa Afisa wa Mkoa, baadaye akaenda kule kuwa Afisa katika Wizara upande wa kukagua hii migodi. Bahati nzuri amepelekwa kwenye nafasi hii kama Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, anajua machungu

yaliyoko kule, hana anachoweza kudanganya, wanajua matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mwenyezi Mungu kamjalia kawa Katibu Mkuu, mkifeli kwenye hii nafasi, labda kuna muujiza utakuja, tusikilizeni sisi wachimbaji, Mheshimiwa Waziri na timu yako pelekeni kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alikuja hapa tarehe 22 mwezi wa nne, mimi nina kumbukumbu, hapa ametoka kuapa tu, baada ya siku tatu akaingiza timu hapa Bungeni na akaja akazungumzia suala la madini kwa ukubwa wake. Akasema, maeneo yote yaliyo katika *game reserve* ambako hakuna nyani, hakuna chochote, haya yaliwekwa na wakoloni kwa ajili ya kuja kuyalinda kwamba baadaye sisi huko mbele ya safari tuje tuyachunge tuwazuie Watanzania wasiingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni miaka sabini tunakwenda toka ameondoka hapa mkoloni, bado Watanzania hatuwezi hata kufikiria kwamba sasa hizi sheria walizoziweka Wajerumani huko kuzuia haya maeneo, yana nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa hivi tumeshapata akili na elimu ya uchimbaji na Wasukuma tunayajua. Ukiona tu kuna miti inaitwa Mirojaminze, ukiiona tu mingi katika eneo hilo unajua tayari mzigo uko chini hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi hatuhitaji hata hii nyuki unayotuambia, yaani mkishafungua tu kwenye maeneo haya ya *game reserve,* kwa mfano kuna maeneo yako Ruangwa kule, wenzetu wale watani zetu Wamakonde kule, walikuwa hawajui dhahabu. Wameenda Wasukuma kule, wamegundua, wakakuta Mirojaminze mingi tu, wamefika pale wakaanza kuona kwamba hapa tayari kuna maeneo ya machimbo. Nachingwea yako maeneo yamewekwa *game reserve* kuna mali za kutosha, lakini haya maeneo ya Sikonge, Tabora dhahabu uko mzigo wa kutosha, hapa Itigi, Manyoni hapa kuna mzigo wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mavunde ukishindwa kulitengeneza Jiji la Dodoma, fungueni Manyoni hapa, kaa na wenzio wa maliasili, kwani hii mifumo haisomani? Maliasili bahati nzuri kule kwa Mheshimiwa Waziri Pindi Chana naye ni mzalendo, ni *green guard* mwenzetu, tulikuwa naye huko kwenye *game*, kwa hiyo, anajua kabisa kwamba Tanzania tunataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Tanzania ni ya kukosa Dola! Wachimbaji wadogo hawana mahali pa kupeleka dhahabu yao isipokuwa kwenye masoko ya ndani. Wanamaliza kuchimba, tuna masoko zaidi ya mia moja na kumi na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimepata machungu, nimeenda kule namsikia Mheshimiwa Hussein Bashe anasema ana wakulima milioni nane wanajulikana kwa simu. Sisi wachimbaji tunajulikana; anawajua Mheshimiwa Mavunde zaidi ya milioni nane, yaani katika sekta ambayo wachimbaji wanaweza wakaingiza uchumi na wakaigeuza nchi hii ni kwenye dhahabu. Sisi wachimbaji, tunaigeuza nchi kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fungueni hizi *game reserve* ambazo hazina hata nyani, zishusheni hadhi zije kwenye *forest reserve* watu waanze kuchimba. Hii Dodoma hapa hakuna viwanda, hakuna nini. Kuufanya huu uwe Mji Mkuu, fungueni Manyoni hapa na Itigi muone. Hhii Chemba yote imejaa dhahabu, kote mmeweka *forest reserve*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Bahi yote imejaa dhahabu. *Forest reserve, game reserve,* haya maneno yanakuwaje? Mpwapwa yote hii imejaa *game reserve*. Mkifungua Mheshimiwa Rais, maneno aliyoyatamka tarehe 22 hapa, kama ungefungua hapo ukasikia aliyoyasema Rais tarehe 22 Aprili, 2021 alisema fungueni haya maeneo tutengeneze uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka amezungumza Rais mwaka 2021, 2022 mwezi wa nne mwaka, 2023 mwaka, 2024 mwaka, 2025 mwezi wa nne, miaka minne, kazi haijafanyika. Tunaliomba Bunge lako liunde Tume tupite sisi wachimbaji tuwaonyeshe hapa, hapa kuna mali, kuna mzigo uko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu aunde hii Tume tuungane na timu ya Waziri Mkuu, timu ya Wizara ya Madini na timu ya Wizara ya Maliasili tukawaoneshe dhahabu iko wapi? Halafu mwone kama hatuwezi kupima hapa sisi tani kumi kwa mwezi. Kila mwezi tutapima tani kumi katika nchii hii na suala la dola kwenye Benki Kuu tutakuwa *giant* duniani. Mtatoa ajira zaidi ya milioni 10 inayotafutwa iliyopo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Tukaribisheni wachimbaji wadogo, mwone, tuubadilishe huu uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuna *subsides* zinatolewa, wenzetu wanapewa ruzuku, wachimbaji wadogo hatupewi ruzuku. Wenzetu sasa hivi wameshawekewa mpaka pesa za kufungua Benki ya Ushirika ya Wakulima. Sisi Mheshimiwa Mavunde umetoka kwetu, tunao mpango wa kuwa na benki ya wachimbaji, huizungumzi hapa. Tunakushangaa sana Mheshimiwa mavunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Waziri alikuwa kwenye *game,* muda huu ameshatusahau tena! Wachimbaji tunamsubiri, wachimbaji tuna imani naye sana na timu yake, tunawaambia watu wa Dodoma tuachieni Mheshimiwa Mavunde, Mungu akijalia ninyi mnaopitapita Dodoma, bado Mavunde tunamhitaji wachimbaji aje atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaambia Ndugu zangu watu wa Ilala, Wazaramo, tunamhitaji sana Mheshimiwa Zungu humu ndani ya *game*. Mheshimiwa Zungu anahitajika sana, ninyi watu wa Mchikichini tunaokaa wote Mchikichini kule, hakikisheni Mheshimiwa Zungu anakuja; wadau wa Buguruni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda kidogo tu nimalizie mchango wangu, nakuomba sana dakika moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna leseni imetolewa Sengerema ya uchimbaji wa madini, wenzetu wa *Sotta Minning* wametuambia tokea tarehe 28 mwezi wa nne, 2025 mgodi unaanza kujengwa, lakini kuna leseni ambayo walikuwa wametupangia wapunguze leseni kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mavunde aje na majibu mazuri kwa sababu tayari watu kule mimi wanataka kunijeruhi. Wanataka kupitishia hapo nafasi, Jimbo limebana kabisa Sengerema.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tabasam, mengine changia kwa maandishi.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Kapufi, na Mheshimiwa Lulida ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kupata nafasi niweze kuchangia hotuba hii nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri Mavunde, Naibu Waziri Kiruswa pamoja timu yote ya Wizara wameendelea kufanya kazi kubwa na nzuri kuhakikisha kwamba madini yanaendelea kuwa mkombozi kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mmeona, kabla ya muda ambao ulikuwa umepangwa, sasa tumeweza kufikia 10.1% katika pato la Taifa, tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo ameendelea kuhakikisha kwamba, hii sekta inaendelea kuwa nafuu kwa wachimbaji wetu wadogo na kuhakikisha kwamba, inaendelea kuwasaidia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumeona namna ambavyo changamoto mbalimbali ambazo zipo kwenye Wizara yake ameendelea kuzitatua. Migogoro mbalimbali ameendelea kuitatua na sisi watu wa Chunya wiki moja tu iliyopita alikuwa amekuja kule katika mgogoro wa Mto Zira, amefanya kazi kubwa na nzuri. Leo wananchi wa Chunya na Ifumbo wanafurahi na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo wanaendelea kuitumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi tutoe rai kwa wananchi wa Dodoma kwamba, watu wa Dodoma wamepata lulu, wamekupata wewe ndugu yetu Mheshimiwa Mavunde, wasikuache, wasikupoteze. Wao wakikupoteza, Taifa litakuwa limepata hasara kubwa sana na sisi tunakutegemea, hasa kwenye upande wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nianzie pale ambapo ndugu yangu Mheshimiwa Tabasamu alizungumza sana. Maeneo mengi ambayo yana *reserve* kubwa ya dhahabu yako kwenye maeneo ya misitu. Haya maeneo ya misitu, mengi ukiyaangalia sasa hivi ni leseni za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo kule Chunya mengi yamezungukwa na hifadhi za misitu. Mfano, Hifadhi ya Mto Mbiwe, pale kuna leseni. Karibu hifadhi yote ni leseni za watu, na watu sasa hivi wanaanza kuchimba mle ndani, lakini vibali vinavyotolewa na *TFS* vimekuwa vikwazo vikubwa sana kwa wachimbaji wetu wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaona umefika muda haya baadhi ya, mengine yashushwe hadhi yawe maeneo ya uchimbaji. Wananchi wetu wa Chunya na maeneo mengine ya Tanzania, hasa kule Mbiwe na maeneo mengine kule Itumbi, waweze kwenda kuchimba kwa unafuu mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wetu wengi wanazo leseni ndogo ndogo. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amefanya kazi ya kutunga kanuni mpya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, zile leseni za wachimbaji wadogo, hasa *PML*, ziweze kumilikiwa na

wachimbaji wazawa ila inapotokea kwamba kunahitaji utaalam, ndiyo tuweze kupata *expert* kutoka nje, waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni zuri, lakini angalizo lake ni nini? Leo hii kuna wachimbaji kutoka nje wanaojiita ma-*expert,* wataingia kwa mgongo kwamba, wao wanakuja kuleta utaalam, lakini watakuja kufanya kazi ambazo siyo za kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwenye maeneo yetu ya uchimbaji kuna raia wa kigeni wengi sana ambao wanafanya shughuli nyingi ambazo zinapaswa kufanywa na wazawa. Watu wanafanya shughuli za usekesaji wa kawaida, shughuli za uchimbaji wa kawaida, wanaendesha mpaka maguta. Sasa haya tusiyaruhusu kwa kigezo kwamba, wanaingia kama ma-*expert*. Tuache huu utaalam, ule mkubwa waingie kama wawekezaji au wachimbaji wakubwa, lakini wasiingie kwa kigezo kwamba ni wataalam, ili waingie kwenye leseni ambapo ingepaswa kubakiwa na wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wetu wengi wanafanya uchimbaji huu bila kufanya utafiti. Leo karibu Tanzania nzima wachimbaji wadogo wanapata hasara kubwa kwa sababu, maeneo mengi hayajafanyiwa utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ya mwaka ambayo ndiyo tunaenda ukingoni mwezi Juni, ilielekeza kwamba, tutaenda kununua vifaa vya utafiti ikiwemo ndege, lakini sasa hivi tumebakiza takribani kama miezi miwili tu. Naomba sasa ile ndege ambayo tuliahidi kwenda kununua, tunaomba inunuliwe, ili utafiti ufanyike wa kina, ili wachimbaji wetu hawa waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza mmerusha ndege nyuki, imeweza kufanya kazi, lakini imani yangu ni kwamba, maeneo mengi yakiweza kufanyiwa utafiti kwa wachimbaji wadogo, tukifikia angalau 40% ya wachimbaji wetu hawa, tutaweza kuongeza pato. Hili ambalo tumepata sasa hivi, tutaongeza kufikia hata 15% au zaidi ya hapo kwa sababu, tutakuwa tuna uhakika na maeneo ambayo wachimbaji wetu wanaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilinunua vifaa vya uchorongaji nashukuru. Sisi Chunya tumepata rigi moja na inaendelea kufanya kazi, lakini rigi hii na kwa ukubwa wa Tanzania, bado ni chache. Tuombe Serikali, nikuombe Mheshimiwa Waziri, kupitia *STAMICO,* muweze kuona namna gani ya kuweza kuongeza hizi rigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto moja ambayo tunakutananayo; rigi zipo, lakini maeneo yetu hayajafanyiwa utafiti, hivyo wachimbaji wetu kuna wakati wanachukua rigi wanaenda kuifanyia kazi, akienda kuchimba kule anakosa kile ambacho alitegemea kukifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niombe hizi taasisi mbili, *STAMICO* ambao ni wamiliki wa hizi rigi pamoja na *GST,* waweze kufanya kazi pamoja, ili unapoenda kuichukua ile rigi uwe na mtaalam wa kukufanyia utafiti hapo hapo ili ukilipia mtaalam, unalipia na rigi, viweze kwenda pamoja, ili wachimbaji wetu hawa wasiweze kupata hasara, kama ambayo wanapata sasa hivi. Mtu anachukua rigi anaenda kuifanyia kazi na baadaye rigi hii inakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niweze kumalizia. Kuna mambo mawili; jambo la kwanza ni changamoto ya tozo na kodi ambazo zipo kwenye uchimbaji wetu. Leo hii kila taasisi ambayo inahitaji kupata tozo inaangalia kwa wachimbaji, hasa wachimbaji wadogo. Imefikia hatua mchimbaji huyu hapati faida kwenye uchimbaji wake. Kila ambacho anakipata kwa gharama kubwa chote kinaishia kwenda kulipa kodi, kinaishia kwenda kulipa tozo na hizi tozo zinaenda kukatwa bila utaratibu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kila mmoja anapojisikia, kwa wakati wake, mtu wa OSHA anakuja kudai tozo pale, mtu wa halmashauri anakwenda pale na wanafungua mapropela na vitu vingine pale; mtu wa zimamoto, mtu wa Mkemia wa Serikali na wengine kama hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuwe kuna utaratibu maalum au kiundwe chombo, kupitia *TRA,* kimoja kikusanye hizi tozo zote, baadaye kiwe kinawagawia wachimbaji hawa, kwa

maana ya kugawia hizi Taasisi za Serikali ili zisiwe zinaleta usumbufu kwa wachimbaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni maeneo ya wachimbaji. Bado tuna changamoto ya maeneo mengi kumilikiwa na leseni kubwa. Tunaipongeza Serikali iliweza kuzichukua zile leseni za utafiti ambazo hazikufanyiwa kazi na kuwagawia wachimbaji wadogo, lakini tunaomba, bado tuna maeneo mengi makubwa ambayo yapo ya kiutafiti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, malizia.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali, yale ambayo hayajafanyiwa kazi wayachukue waweze kuyafanyia utafiti, wawape wachimbaji wadogo, wataweza kuwasaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kapufi, na Mheshimiwa Lulida na Mheshimiwa Prof. Manya mjiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake Wizarani, nikimtaja pia Ndugu yangu Samamba, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara. Kwa ujumla Wizara hii imesheheni watu wenye weledi na kwa misingi hiyo natamani kuona sekta ikikua kwa sababu, watu walioko katika eneo hili wana weledi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amejielekeza kwa maana ya *main vision* ya 2030 inayozungumzia kwamba, madini ni maisha na utajiri. Kwa misingi hiyo, inanirejesha, kwenye mgongano wa kisheria kati ya Sheria ya Ardhi, Sheria ya *TFS* na Sheria ya Wizara ya Madini. Ukisema unamtaka mtu akawe tajiri, kwa maana ya *vision* 2030, mtu huyu ambaye kwa bahati nzuri alikuwa na shamba lake kubwa, chini kuna akiba ya madini, unamtoa kwa Sheria ya Madini unamleta kwenye Sheria ya Ardhi,

kwa tafsiri ya *vision 2030* ya madini ambayo ni maisha na utajiri, unakuwa umegongana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatamani kuona nchi ikizalisha matajiri wa kutosha. Kwa hiyo, bado naomba turudi huko kwenye kuangalia mgongano wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua madini yanachangia sekta nyingine, iwe ni kilimo, mifugo, maji, uvuvi, ufugaji na kwa taarifa tu wachimbaji wengi wakitengeneza mitaji ndiyo hao unakuta wamesaidia hata sekta kama ya uwekezaji wa watu wa boda boda na watu wengine wa namna hiyo. Maana akihakikisha amepata hela yake kidogo, anakuja kuwekeza huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukiwafanya hawa watu kukua, nami niendelee kusema wakati fulani niliwahi kuchangia hapa nikasema, Mji kama Johannesburg umejengwa kwa dhahabu ya palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii niendelee kuomba sana, Baba wa Taifa kipindi chake alituacha tusiguse madini haya mpaka pale Watanzania watakapokuwa tayari. Kwa sasa hivi naamini tumezalisha wataalam wengi ambao wana nafasi ya kufanya uchumi wa nchi hii ukawa kwenye mikono yetu. Kwa sura hiyo wataalam wasituangushe.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tumezungumzia kwa ujumla, sekta imechangia asilimia hiyo kumi ya pato la Taifa kwa mwaka 2021/2022 na baadaye 2025 mpaka 2026 imefikia 10.1 ni jambo jema, ninapongeza sana hilo, lakini ningetamani kuona wakati tukiipongeza Wizara hii msisahau na maslahi ya watu wanaotusaidia kufika hapo. Angalieni *scale* zao za mishahara na vitu vingine vya namna hiyo, ili kuwatia shime waendelee kutusaidia katika kukuza sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru suala la maduhuli, lakini naomba sana katika maeneo mengine ambayo tunaambiwa kwamba tumesomesha wataalam, kuna mpango wa kusomesha wataalam wa ukadiriaji mashapo. *Point* yangu ni nini hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakwenda kusomesha wataalam, tusisahau kitu kimoja kinaitwa inteligensia ya uchumi. Inashangaza, baadhi ya nchi hazina madini, lakini leo hii utakuta ndio wauzaji wakubwa labda, kama ni dhahabu, hata *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetamani ofisi ya Mheshimiwa Waziri na hasa kwa kupitia suala hilo la kuendelea kuwa na watu wenye weledi, tufike sehemu tufunguke, tujue ni kwa nini sisi kama nchi, tunaweza tukawa na madini yote haya, lakini leo kuna baadhi ya watu hawazalishi dhahabu, lakini ndio wanunuzi wakubwa na wazalishaji wa dhahabu, kwa maana ya kuiuza sehemu nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, *point* yangu mimi hapa? Nataka kusema nini? Tusiache kufungua milango pamoja na masoko ya ndani. Tatizo linakuja, mtu anaweza akawa anatamani kuja kufanya biashara na sisi, kama nchi, tunapokuwa na masharti makubwa, masharti ya ajabu, inaweza ikafanya watu hawa wasije kwetu. Kwa hiyo, tusijifungie, tufungue milango pamoja na uzalishaji huu wa ndani, lakini tuhakikishe kwamba, tumefungua milango.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, nashukuru, nimeona tunaambiwa habari ya Wataalam wa Wizara kujikita katika kujua Sheria mbalimbali za Mikataba na mambo mbalimbali yanayogusa suala hilo. Naomba wataalam hawa watakaokuwa wamejitahidi katika kujua Sheria za Mikataba tusiishie tu kwenye Serikali na wawekezaji. Sheria hiyo ya Mikataba, Wizara ijaribu kuielekeza kwa wachimbaji wadogo wadogo na watu wengine wa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu gani tunasema hivi? Watu wetu pamoja na kutamani kuchimba, lakini hawana elimu ya mikataba. Inapofika sehemu tunakutana na wenzetu wenye uelewa mpana wa biashara ya Kimataifa, wachimbaji wetu inapokuja kwenye suala la mikataba wanapata shida. Nalisema hilo makusudi kwa sababu, leo mtu hata kama ana eneo lake, utaalam ukifanyika maeneo ambayo yako *surveyed,* ukumbuke Mheshimiwa Waziri, tusiishie tu kusema kwamba, hawa watu wachimbe, na wasomeke kama wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja ambacho ni muhimu sana. Zile taarifa za kiutafiti, ile peke yake ni *document*. Taarifa ya kiutafiti ambayo maeneo yamefanyiwa utafiti, mchimbaji anaweza asichimbe yeye, lakini kwa kumiliki ile taarifa ana uwezo wa kwenda kwenye vyombo vyovyote na akafanya biashara. Ndivyo ambavyo wenzetu wengine wamekuwa wakifanya, wanakuwa na tafiti wakizimiliki taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni sisi wengine tutaishia kuonekana kama waganga wa kienyeji au tunapiga ramli. Kupitia Wizara yako na hili nimeliona, kwa maana taarifa yako imesheheni mambo mengi mazuri yanayoelezea habari zote za masuala ya utafiti, achilia hilo suala la ndege na vitu vingine vya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu nchi yetu, pamoja na hili linalosemekana, kasi ya ukuaji wa shughuli kutoka 10.8 kwa 2020/2022 hadi 11.3 kwa mwaka 2020/2023 tuna uwezo wa kutoka hapo. Nchi hii yote kwa ujumla wake, ukijaribu kuiangalia ni kama imesheheni madini ya namna mbalimbali. Hili ambalo nimelisema hapo mwanzo la kwamba, Baba wa Taifa alisema watu wetu wakiwa tayari, basi tutoe nafasi ya madini yetu kuweza kutumika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naliona hilo...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kapufi, kwa mchango mzuri.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida, hayupo, Mheshimiwa Profesa Manya, ajiandae Mheshimiwa Mpakate, ajiandae Naibu Waziri.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri

wa Madini, ambaye katika mwaka huu wa fedha anatamani apewe shilingi bilioni 224.9, ili aweze kutekeleza majukumu yake. Nitangulie kusema kwamba, naunga hoja mkono Waziri apewe bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ni sekta binafsi zaidi na fedha hizi ni kwa ajili ya taasisi ili kufanya uwezeshaji, lakini wengi wa wahusika ni sekta binafsi, wachimbaji wadogo kwa wakubwa. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kwa nini tusimpe Waziri, ambaye yeye anataka uwezeshaji ili kwamba, aweze kufanya kazi ya usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wa Wizara. Waziri Mavunde, ambaye watu wengi wanajua kwamba ni mtu ambaye anapatikana akihitajika, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Katibu na Watendaji wa Taasisi zote za Wizara, *TET, GST,* Tume ya Madini, *STAMICO* na *TGC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawapongeza wachimbaji wadogo na wakubwa maana wao ndio wadau wakubwa wa sekta hii na jitihada zao ndizo ambazo zimeifanya sekta kufikisha hatua hii ya mchango wa sekta ya madini kuwa asilimia kumi katika pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taswira ya miaka kama 30 iliyopita kwamba, mchango huu wa sekta kuwa, 10% ni zao la Sera yetu ya Madini ya tangu mwaka 1997, ambapo mwaka huo mchango wa sekta ulikuwa ni 1.7% tu. Kwa hiyo, ni sera ililenga kwamba, ndani ya miaka 30 sekta iweze kuwa imefikisha mchango huu mkubwa. Hii inatupa faraja kwamba, sera zinapokuwa zimetungwa kwa malengo ya muda mrefu, kumbe zinaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwapongeze walioko ofisini na hata wale ambao wameweka mchango wao katika miaka yote hii 30 hadi tunapokuwa tunafikia hatua hii kubwa ya mchango wa 10% katika sekta ya madini. Katika safari yetu ya miaka hii 30 ya mageuzi ya madini ni kweli kwamba, sekta imepata mafanikio makubwa sana, mojawapo ikiwa ni kukuza

uchimbaji mdogo, pia, kuweka uwazi katika biashara ya madini kupitia masoko ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la msingi sana katika hii miaka, ambalo tumeliona, ni kufufua Shirika letu la *STAMICO* ambalo limeendelea kufanya vizuri sana kukuza mtaji wake na hatimaye kujiendesha kwa faida bila kuchukua *OC* kutoka Serikalini. Haya ni mapinduzi makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kanuni zile za kuweka *CSR* ambazo Wabunge wenzangu wamezitaja, zimeleta mapinduzi. Kuwepo kwa *CSR* kumeleta mapinduzi kwa kampuni kubwa kutoa mchango wake wa *CSR* katika maeneo ambayo yanazungukwa na migodi, imekuza maeneo haya, uchumi wake umekua. Ukiangalia maeneo yote ambayo migodi ipo, ni kweli kwamba ni maeneo mazuri yameendelea kwa sababu ya kuwepo kwa *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari yetu hii haikosi changamoto na ningependa kuangalia changamoto kama mbili tatu hivi, kwamba, katika muda wote ambao tumekuwa na mageuzi ya sekta yetu ya madini, kuna wakati ambapo tumekuwa na mikataba ambayo siyo rafiki, na wakati mwingine Serikali imelazimika kulipa fedha, kuwalipa wawekezaji kwa sababu ya ubovu wa mikataba. Tunapokwenda mbele, maana naelewa kwamba tuko katika *transition,* tupo katika *point* ambayo tunataka kuanza tena kuwa na migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na migodi mpaka mwaka 2005 na baada ya hapo hatukuwa na migodi mikubwa tena hapa Katikati, lakini sasa hivi tangu mwaka 2023 tumekuwa na Mgodi wa *Shanta* na hapa mbele tutakuwa na migodi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda mbele ningetamani kwamba Wizara ya Madini pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wafanye kazi yao vizuri ili kuliepusha Taifa katika hasara inayotokana na mikataba mibaya. Yaani tusiende huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uzoefu wa miaka 30 katika sekta, kuna watalamu wabobevu katika sekta, wengine ambao

wamekuwa ni ma-*CEO* katika nchi za wenzetu wakisimamia uchimbaji na *exploration* na mambo yote ya biashara ya madini. Sasa tukishakuwa na uzoefu huu mkubwa, hatuna sababu tena ya sisi kuingia katika mikataba mibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, kutokuwepo kwa migodi mikubwa kati ya 2005 – 2009 mpaka 2023 siup tokeo ambalo ni la bahati mbaya. Wakati mwingine nahisi kwamba Serikali imekuwa haiweki kipaumbele kwenye *explorations,* na yawezekana inapotokea watu wana leseni ile ya *explorations* pia kunakuwa na tozo tozo ambazo zinawafanya wasiendelee sana na *explorations.* Kwa jinsi hiyo, tunaendelea kuchakata mashapo ambayo yanakuwa yameshaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba majadiliano yanachukua muda mrefu. Ningependekeza kwamba ingewezekana mambo makubwa yanayohitajika kwa mwekezaji yaingizwe kwenye sheria na kwenye kanuni, anapofika anaangalia, kwamba sheria inanitaka nini? Kanuni inanitaka nini? Kwenye majadiliano kuwe na kipengele kidogo tu, muda mfupi sana, la sivyo tunaweza tukajikuta kwamba, kupitia haya majadiliano ambayo yanaweka *human interface* tukarudi katika mikataba mibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningetamani tuuondoe sana muda mrefu wa majadiliano mambo makubwa makubwa ya sekta yaingizwe katika sheria na kanuni halafu mwekezaji akija aangalie halafu aweze kuendelea haraka. La sivyo, tunachukua muda mrefu kwa sababu Serikali imeshasaini *framework agreements* sita *so far,* tangu 2017, lakini hatuna mgodi bado. Shida ni nini? Majadiliano yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majadiliano yakiendelea Mheshimiwa Waziri anahitaji kuweka *legacy* ya yeye kuwa Waziri ambaye pia anatupatia migodi mingine mipya kama ilivyokuwa katika Sera ya mwaka 1997, ambapo tulipata migodi mikubwa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa migodi hii mikubwa, wahandisi migodi pamoja na wajiolojia wanaotoka

vyuo vikuu, wamejikuta hawana kazi, kwa sababu hatuna migodi mikubwa mipya ambayo inawaajiri. Kwa hiyo, wanasoma kule vyuo vikuu lakini hawawezi kuajirika kwa wachimbaji wadogo kwa sababu mtaji siyo mkubwa, tungetamani sana Mheshimiwa Waziri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA** …chochote kinachokwamisha ufunguzi wa migodi mipya Tanzania kishughulikiwe haraka ili tuweze kupata migodi mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia, malizia.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kwamba, ufanisi wa shirika letu la *STAMICO* ni zao la menejimenti nzuri. Tunapo-*spot talent* kwamba huyu kiongozi anatufaa kama ilivyo kwa Dkt. Mwase wa *STAMICO,* tumpe *support,* tusimvute miguu nyuma, tumfanye aendelee. *STAMICO* ikiwa kubwa *Barrick,* yaani najaribu kuweka mfano kwamba, *suppose STAMICO* ikawa kubwa kama *Barrick,* fedha zote zinabaki ndani. Kwa hiyo, tuifanye *STAMICO* iwe kubwa ili ichote uzoefu ambao uko mwingi sana Tanzania. Tanzania walio *age* yangu ya ma-*geologists* na wahandisi migodi ni watu ambao ukichota uzoefu wao *STAMICO* inaweza ikawa kubwa na ikatutoa tulipo tukawa na *Barrick* ambayo ni *STAMICO* ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umewasha maiki na sitaki kukukosea adabu. Naunga mkono hoja, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate, jiandae Naibu Waziri.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Madini jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimshukuru sana Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutembelea Tunduru kutuzindulia na kufungua soko letu la madini lililojengwa kwa njia ya *PPP*. Vilevile namshukuru Waziri wa Madini kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kuhakikisha kuwa soko lile linafunguliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nawashukuru Mkurugenzi pamoja na Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa kukubali na kupitisha wazo la kujenga soko la madini kwa njia ya *PPP,* kwa sababu halmashauri ilikuwa na kiwanja tu. Wadau wetu, kwa maana ma-*dealers* ndio ambao wamejenga kwa kutumia fedha zao, na kwa kutumia mkandarasi ambaye walimchagua wao wenyewe ili kuhakikisha kwamba soko lile linajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko limejengwa kwa kiwango kikubwa sana, na nitakosa fadhila bila kumtambua kijana aliyejenga jengo lile ambaye ni kijana wa Tunduru. Amefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wazabuni wetu ili soko lile lifanye kazi ipasavyo. Huyu kijana anaitwa Abdulkadir. Alifanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wadau wetu kwa asilimia kubwa, na soko lile kwa kweli Mheshimiwa Waziri atakuwa anajua, ni zuri na la mfano kwa Kanda yetu ya Kusini, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizo, lile soko wanunuzi wako wengi, afadhali, kwamba 99% ya eneo lile limechukuliwa na hawa wanunuzi. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa alikuwepo pale, kuna changamoto ambayo tunatakiwa tuifanyie kazi ili kuhakikisha lile soko linafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, wanunuzi sasa wamegeuza lile soko ni sehemu tu kama ofisi, lakini bado madini wananunulia kwenye maeneo yao ambayo wanalala, kwa maana ya nyumba za kuishi. Kwa nini wanafanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wengi wadogo wadogo wanapata mikopo kutoka kwa hawa ma-*dealer*. Wakishapata mkopo wanakwenda kuchimba, wakipata madini wanampigia simu wanasema njoo saa mbili nyumbani, leta madini yako, na kwa hiyo hawezi kuleta kwenye soko lile. Jambo hili kwa kweli linadhoofisha uchumi wetu, na umaana wa kuwa na lile soko unapotea kwa sababu madini mengi yanakwenda kwenye nyumba zao kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati ya Ulinzi na Usalma ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, wanajitahidi kupambana nao lakini wanazidiwa nguvu. Kikubwa ni kwa sababu ya wachimbaji wetu wadogo hawana uwezo, na wakipata madini wanalazimika kupeleka kule kwa sababu ndio waliowapatia mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia sahihi ni kuwapa mikopo hawa wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kwenda kuuza mahali popote anapoweza kupata maslahi mazuri. Soko bado ni zuri na lina wafanyakazi wote katika vitengo vyote; kuanzia ulinzi, *evaluation* mpaka *TRA* wako pale, lakini bado matumizi yake yamekuwa madogo sana kwa sababu wachimbaji hawa hawana uwezo wa kuchimba kwa kutumia rasilimali zao wenyewe, watategemea rasilimali kutoka kwa *dealers.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa sana niliongelee ni suala la mitambo. Nimefurahi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kwamba amenunua mitambo 10 kwa ajili ya kufanya *explorations* ya madini katika maeneo tofauti tofauti, hasa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusini huku atuletee angalau mtambo mmoja utusaidie kwa ajili ya Lindi, Mtwara na Mkoa wa Ruvuma, kwa sababu madini ya *gemstone* yamekuwa mengi sana. Kuna *nickel*, *copper* na *graphite* zinazopatikana kusini. Sasa, tusipokuwa na mitambo, hawa wachimbaji wetu wadogo wanafanya kazi kwa kupiga ramli kama hapa pana madini; lakini kukiwa na mtambo huo, utatusaidia angalau kuangalia maeneo ambayo yale madini yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na madini watuletee; nimeona kwenye maandishi yake amezunguzia suala la maabara. Basi na huku kusini kanda yetu ya Lindi, Mtwara na Ruvuma tupate maabara moja ili wachimbaji wetu wadogo wawe na uhakika na wanachokichimba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** …kinaweza, kuwasaidia kwamba wanachimba jambo la fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kuna tatizo la mfumo katika kuomba leseni. Mfumo uliopo walioubadilisha unaleta kero sana kwa wachimbaji wadogo kupata *PML*. Kwa hiyo, tujitahidi huu mfumo urekebishwe ili vijana wetu ambao ni wachimbaji wadogo wanapoomba hizi *PML* wapate kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu inamchukua siku tatu hadi wiki kuomba hii leseni mpaka afanikiwe. Hii ni kero kubwa sana kwa vijana wetu ambao wanajihusisha na masuala ya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba uende ukurasa wa 27, namshukuru sana, amezungumza jambo zuri sana, *item number* 27, amesema; "Mheshimiwa Spika, hadi sasa Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni nane za viwanda vya kusafisha madini nchini. Kati ya hizo leseni saba ni za viwanda vya kusafisha dhahabu na leseni moja ni viwanda vya kusafisha madini ya shaba, nickel, cobalt. Aidha, leseni hizo zimetolewa kwa Makampuni ya Geita Gold…" na hao wengine mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwenye *comments* zake, nitoe rai kwa kampuni zote za uchimbaji na wafanyabiashara wa madini ya dhahabu kusafisha madini kupitia viwanda vilivyopo nchini kwa mujibu wa Sheria ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hana sababu ya kuomba, sheria anayo Sura ya 123 inamsaidia yeye kutekeleza. Wale wasiotekeleza, basi sheria ichukue mkondo wake. Hii ni aibu, sisi tumejenga viwanda vyetu, lakini watu hawataki kufuata. Maana yake ni kwamba wana tabia ile ile ya kutorosha madini kwenda nje kabla hayajasafishwa kwa kutumia viwanda vyetu vya ndani; na hii inasababisha mapato yetu kupitia njia tofauti za ushuru yanapotea kwa sababu hawapiti eneo ambalo linatakiwa lijulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa

Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mbunge na Waziri wa Madini kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Madini, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya sekta ya madini, Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kuimarisha zaidi sekta hii muhimu ili kukabiliana na athari za kiuchumi kutokana *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kutokana na athari ya kiuchumi ulioikumba dunia nzima, hii inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, madini ya chuma na madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza, na kutokana pia na kuyumba kwa thamani ya shilingi na hata dola ya Marekani, Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu ya Tanzania kama ilivyo kwa Benki Kuu nyingine duniani, imeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na misukosuko ya vita za kibiashara kati ya Marekani na China, bado kuna fursa za bei ya dhahabu kuendelea kuimarika, na pia nashauri Benki Kuu ya Tanzania kuuza dhahabu kwa faida mara tu bei zinapopanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita vya Urusi na Ukraine vimesababisha upungufu mkubwa wa uzalishaji wa mbolea na hii ni fursa kwa Serikali kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini kama vile *phosphates, calcium carbonate, limestone* na *natural gas.* Katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, bei ya madini ya chuma na hata makaa ya mawe haiyumbi, na Serikali inaweza kupata mapato mengi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuchukua hatua za makusudi na kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa chuma *(Liganga Iron Ore)* ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe *(The Mchuchuma Coal Mining and Power Projects)*. Mradi wa Liganga na Mchuchuma ulitarajia uwekezaji wa *US$ 3 billion* na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na hii inaweza kuwa fursa nzuri katika hiki kipindi cha balaa la athari za *Covid-19* na vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa Kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi nyingine ili yachakatwe hapa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya *Niobium* ambayo inapatikana milima ya Pandahill Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji kujiwekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara kukabiliana na athari za *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(modern manufacturing plant and smelter)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itachangia huduma za kijamii *(corporate social investment in community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kuwepo na ushirikiano wa karibu kwa taasisi zinazohusiana na miradi ya kimkakati katika kuinua uchumi wetu. Pamoja na fursa kubwa za

mgodi na Kiwanda cha *Ferroniobium*, inaelekea *TANESCO* na Wizara ya Nishati hawana taarifa ya huo mradi; na kwa mshangao wa wadau wote, *TANESCO* wanajenga njia ya umeme mkubwa wa *TAZA* ndani ya eneo la mgodi na kiwanda cha *Ferroniobium*. Mazingira ya kukosa mawasiliano ya taasisi za kimkakati zinasababisha kero kwa wawekezaji *(FDIs)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Madini Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mbunge na Naibu wake Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge; na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu *Eng.* Yahya Ismail Samamba na Bwana Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na wadau wa sekta ya madini kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu madini ya kimkakati Tanzania, lulu inayotazamwa na dunia na nini kifanyike kulinufaisha Taifa. Tanzania ni nchi yenye neema kubwa ya utajiri wa asili katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utajiri huo wa asili unaweza kuondoa kabisa umaskini na kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo kutoka nje. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Tanzania ipo eneo zuri kiuchumi. Tuna Bahari ya Hindi, tumepakana na nchi nane, tuna ardhi yenye rutuba, vivutio vya utalii, maji safi, gesi asilia, gesi ya helium, mafuta na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini ina mchango mkubwa sana kwenye Taifa letu kiuchumi. Takwimu za Serikali zinaonesha kwamba mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa la mwaka 2024 ni 10.1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, mchango huo ni mdogo sana kwenye pato letu la Taifa. Nchi yetu ilistahili kupata mchango mkubwa zaidi kutoka kwenye pato la Taifa kutoka sekta ya madini. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikajiandaa kimkakati ili kunufaika na raslimali ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini yanayopatikana Tanzania ni dhahabu, chuma, *silver, copper, nickel* na *platinum*. Madini mengine ni *coal, soda ash, gypsum, salt, phosphate* na *gravel.* Tanzania pia ina vito maarufu kama *Tanzanite,* almasi, *rubies, sapphires, tourmaline, tsavorite* na *spinel.* Aina nyingine za vito ni pamoja na *garnet, aquamarine* na *amethyst*.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinatuonesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye rasilimali madini kwa wingi yakiwemo madini mkakati. Pamoja na uwepo wa madini makubwa tuliyoyazoea (dhahabu, almasi, chuma, makaa ya mawe na kadhalika), Tanzania imejaliwa kuwa na akiba kubwa ya madini mkakati ya kiwemo nikeli, *graphite* (kinywe), *rare earth elements* (vipengele adimu vya dunia), *cobalt, lithium, manganese, vanadium, niobium, titanium, tin* na *copper* (shaba), *zinc* na *aluminium*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa madini mkakati haya, nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa teknolojia katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani wa madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini hayo yanahitajika kwa wingi duniani kwa sasa. Kinachohitajika kwetu ni ushirikiano kati ya Serikali na wawekezaji mahiri kwenye masuala ya utafiti wa kina, uchimbaji wa kisasa na uchakataji wa bidhaa za ndani na kuyaongeza thamani madini haya ndani ya nchi, suala ambalo litaongeza tija na kutoa fursa za ajira kwa wazawa na kukuza biashara ya bidhaa za madini yaliyoongezwa thamani kwa walaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya kimkakati ni lulu inayotafutwa na kutazamwa na dunia. Madini mkakati hayo yanayotumika katika teknolojia za kisasa ikiwemo kutumika kuzalisha aina tofauti za vyanzo vya nishati, kutengenezea betri za magari ya umeme, betri za simu, vifaa vya simu, mota, *oil, grease, brake pad* za magari, penseli, vizuia joto na teknolojia tofauti za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhitaji wa madini haya ya kimkakati duniani, wakubwa wameshapiga hodi hapa nchini kwetu wakiomba leseni na kufanya ubia na nchi yetu. Kuthibitisha hilo, kasi ya utafutaji wa madini ya kimakakati imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, taarifa ya Tume ya Madini inaonesha kuna ongezeko la maombi ya leseni za madini ya kimkakati za utafiti ambapo kwa mwaka 2018 leseni za utafiti zilizoombwa zilikuwa 120, lakini mwaka 2023 leseni zilikuwa 333 na leseni maalumu za uchimbaji zimetolewa nne ndani ya miaka miwili kutoka mwaka 2021 - 2023. Hata hivyo, kuna malalamiko ya kuwa wenye hizi leseni wanahodhi maeneo, jambo linalohitaji kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utafiti uliofanyika, kuna uwekezaji umefanyika kwenye uchimbaji wa madini ya kimkakati hapa nchini. Taarifa zilizoko ni kwamba nchi yetu tayari imeingia kwenye makubaliano ya kuchimba kama ifuatavyo: -

(i) Januari 2021, Tanzania iliingia mkataba na Kampuni ya Uingereza, LZ Nickel, iwekeze kwenye Mradi wa Uchimbaji wa Nikeli kwa miaka 33.

(ii) Aprili 2023, Tanzania iliingia mkataba wa madini wenye thamani ya dola milioni 667 na kampuni tatu za Australia yatakayochimbwa Lindi, Morogoro na Songwe.

(iii) Mei 2024, Tanzania ilisaini makubaliano na nchi ya Korea Kusini kuhusu kuwekeza katika madini ya kimkakati *(nikel, lithium* na kinywe).

(iv) Juni 12, 2024 Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko alifanya mazungumzo na Naibu Katibu wa Idara ya Nishati ya Marekani *(Deputy Secretary of Energy), Mr.* David Turk kuhusu nishati safi na madini ya kimkakati hasa *graphite* (kinywe) na *nikel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kujiuliza kama Taifa ni kwamba, je, tumejiandaa kama Taifa kimkakati kunufaika na rasilimali zetu za madini ya kimkakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, kujiandaa kimkakati ni kuwa na mipango ya kufaidika na rasilimali hizi na kuchukua tahadhari za kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika kiuchumi. Mipango hiyo ni lazima ianze kwa kuandaa mifumo ya kisheria *(legal framework)* ya namna ya kushughulikia na kunufaika na madini haya ya kimkakati. Sheria iliyopo ni ya jumla inayotumika kwenye madini mengine ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba kabla hatujachelewa, ni vyema:-

(i) Serikali isiingie zaidi mikataba ya uchimbaji madini bali ipeleke Muswada Bungeni wa mfumo wa kisheria *(legal framework)* wa madini ya kimkakati, kuanzia sera maalum ya madini ya kimkakati na mfumo wa kikodi kuiwezesha Tanzania kumiliki zaidi miradi yote kwa ubia, uwe siyo chini ya 51% kwa Tanzania na siyo gawio kidogo.

(ii) Bunge litumie mamlaka yake kutazama makubaliano ya Serikali yanayohusu madini ya kimkakati na kuyachambua kuona ni kwa namna gani Taifa litanufaika, kwa kutumia Sheria ya Mikataba ya Utajiri wa Maliasili na Rasilimali (Upitiaji na Uboreshaji wa Masharti yenye Shaka) ya mwaka 2017? Bunge litunge sheria maalumu itakayohusu madini haya.

(iii) Tume ya Mipango iratibu mjadala wa kitaifa kuhusu rasilimali za madini ya kimkakati. Kwenye hili, ni vyema kuwashirikisha wadau wote wakiwemo wananchi wa maeneo yanakopatikana haya madini, asasi za kiraia, watu wa mazingira na wataalamu wa sekta ya madini. Maazimio ya mjadala huu yatengenezewe mkakati wa muda mrefu *(long term strategic mineral plan)* katika kuisaidia nchi kutatua matatizo ya kiuchumi na jamii kama vile tatizo la ajira na huduma za jamii (afya, barabara, elimu na nishati).

(iv) Kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani katika mnyororo mzima wa thamani wa madini ya kimkakati kwa kubadilishana uzoefu na taasisi nyingine za utafiti, uchimbaji na uchakataji wa haya madini ili kuwajengwa uwezo wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Serikali isipofanya maamuzi ya haraka, ipo hatari kwamba Taifa letu halitanufaika ipasavyo na haya madini ya kimkakati. Ni vyema kuhakikisha kwamba wawekezaji hawaji kutunyonya bali ni kushirikiana ili Taifa linufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni muda muafaka wa kuhakikisha madini ya kimkakati yanawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla. Ni vyema kabisa kuandaa mkakati maalumu wa kunufaika na madini haya sasa ikizingatiwa kuwa madini hayo kwa sasa yana mahitaji makubwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha madini yetu yanadhibitiwa yasipate kutoroshwa na mapato kwenye madini yameongezeka na kuwanyanyua wachimbaji wadogo kwa kuwasaidia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hii inayoongozwa na Waziri Mheshimiwa Antony P. Mavunde na Naibu Waziri Mheshimiwa Stephen Kiruswa na watendaji wote wa Wizara hii ya Madini kwa kazi nzuri wanazozifanya na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Zanzibar katika Mkoa wa Kaskazini Unguja wanawake bado wanateseka na kutumia matumizi ya kuni na mkaa. Nilikuwa naomba sana Serikali, mkaa

mbadala uanze kutumika kule ili wanawake hawa wapate kutumia kwa matumizi ya kupikia, pamoja na gesi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nina ushauri kwa Serikali kwamba, kuanzishwe kwa soko la madini kule Zanzibar kwa sababu kuna ongezeko la watalii ambao wanaoingia siku hadi siku hasa kule Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuna mahoteli makubwa na madogo ya kulala wageni, tutapata ongezeko la mapato makubwa kwenye madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kituo cha jiologia kilichopo kule Arusha ambacho ni kituo cha kuongeza thamani madini ya vito. Kule Zanzibar tuna wageni wengi sana wa kitalii. Tukiweka kituo cha kuuza vito, wageni wataweza kununua pamoja na wananchi, na pia itainua pato letu la kuuza vito, litaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vituo vya kufundishia viongezeke kule Zanzibar Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwani vijiji vingi vimezungukwa na bahari, wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na maeneo mengine watapata mafunzo, basi wataweza kujiajiri na kupata kipato kupitia madini vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 10.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja ya sekta yetu ya madini. Kabla sijasema machache ambayo nitayasema ili nimpishe Waziri wangu aje kumalizia na kutoa maelezo ya kina kwa baadhi ya maeneo ambayo nitayapitia, nitangulie kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa kibali cha kuwa hapa leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Rais wangu Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumwamini Waziri wangu pamoja na mimi na

akatupa fursa ya kumsaidia katika kuisimamia sekta hii nyeti katika ujenzi wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sekta ya madini ni sekta nyeti sana na ambayo kwa muda mrefu Watanzania hawajailewa vizuri. Katika mtazamo wa mambo makubwa ambayo yameendelea kufanyika na ushahidi umetolewa katika hoja zilizotoka hapa mezani, na hotuba ya Waziri wangu pamoja na Taarifa ya Kamati, inadhihirisha umuhimu wa sekta hii kwa uchumi wa Taifa letu na kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kusemea ni taarifa ya Kamati. Taarifa ya Kamati yetu imesheheni ripoti nzuri ambayo imetupongeza mimi kwa niaba ya wenzangu wote tukiongozwa na Waziri wetu. Tunapokea hizo pongezi. Nimeona kwamba ripoti yenu imeridhia mambo ambayo tumeyafanya, na yale machache ambayo mmeelekeza kama maoni ya jumla sisi tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipengele cha pili, tumepokea maoni mbalimbali, ushauri na hata maswali yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani. Mimi kwa sababu ya dakika chache nilizonazo nitatoa tu maoni ya jumla na majibu ya baadhi ya hoja halafu mengine nitamwachia Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza ambalo limezungumziwa sana na wasemaji mbalimbali hapa ndani ni maslahi ya wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wamesemewa sana. Sisi kama Wizara ya Madini, sekta ndogo ya uchimbaji tunaifahamu, ni moyo wa mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Anajua umuhimu wake na anajua imebeba kwa kiasi gani ajira zinazoweza kupatikana kupitia sekta hii ambayo mpaka sasa hivi ni zaidi ya watu 19,000 wanapata ajira ya moja kwa moja kutokana na kujishughulisha na biashara ya madini kama wachimbaji au *brokers* au wanatoa huduma katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi kuliko yote ni kwamba sekta hii inaendelea kusimamiwa kwa jicho la karibu sana na

Serikali ya Mama Samia. Ndiyo maana Rais wetu ametuelekeza kwamba sekta hii iendelee kuratibiwa na irasimishwe ili asiwepo mchimbaji Tanzania anayejulikana kama mchimbaji asiye rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishawaona wachimbaji wadogo wakijigawa katika makundi na wakijasajili. Tuna vyama vyao; wako *FEMATA;* kuna vikundi vya akina mama; vipo *TAHOMA na TWIMI;* kuna wale *brokers* wa madini na kuna *dealers* wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi pia hata katika huu mfumo wa kisheria tuliouweka, tuna utaratibu ambao tumeuanzisha ili hata wale wasio na leseni ambao wanachimba kwenye maduara ya leseni za watu, nao wasajiliwe na watambulike rasmi na sekta hii, na Serikali ya Mama Samia kwamba ni wachimbaji wanaopata uhai wao, wanaopata kipato chao kupitia sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ndogo ya uchimbaji wa madini imeendelea kuchangia pato la Taifa. Zaidi ya 40% sasa inatoka katika hii sekta. Kwenye makusanyo yote yanayokusanywa na Wizara ya Madini, mmeona kwamba tulipewa lengo la kufikia 10% ya mchango wenye pato la Taifa kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha, na tayari tumevuka lengo la kufikia 10.1%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza sana juhudi za Rais wetu ambaye ameendelea kuilea hii sekta ya uchimbaji wa madini hasa sekta ya wachimbaji wadogo, ambayo kipekee kabisa ni sekta ya pekee yenye wajasiriamali ambao wanaweza wakaibuka siku moja wakawa mabilionea. Hakuna watu wengine wadogo wanaoweza kuibuka siku moja katika sekta nyingine yoyote isipokuwa katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ya *Tanzanite,* tuna mabilionea. Sasa hivi tuna mabilionea wawili; watu wa kawaida wameibuka wakawa mabilionea kwa sababu ya kufanya biashara ya kuuza madini ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hiyo hiyo kwenye madini ya *ruby,* tuna bilionea wa *ruby;* ukienda kwenye dhahabu Kanda ya Ziwa tuna mabilionea wa dhahabu; ukienda Nyanda za Juu Kusini, tuna mabilionea ambao wametengenezwa kupitia sekta hii muhimu na nyeti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wameendelea kutoa hoja mahsusi kuhusu changamoto ya *CSR,* najua Waziri wangu atakuja kulielezea kwa kina. Ninachelea kusema kwamba tumetunga kanuni za *CSR,* lakini kwa sababu watu wengi hawajapata uelewa wa kina, imeendelea kuonekana kwamba kuna kikwazo kikubwa kati ya namna ya kutekeleza miradi inayotokana na *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CSR* ina kanuni zake, na siyo kwamba mwekezaji ndiye anayetoa fedha na kwamba ndiye anayekwenda kufanya mfumo mzima wa manunuzi. *CSR* Kanuni zake zimeelezea namna ya kuunda Kamati ya pamoja yenye wajumbe kutoka ndani ya halmashauri, kutoka kwa mwekezaji mwenyewe na ndani ya jamii husika ili kuweza kusimamia miradi hiyo iende bila kucheleweshwa. Hata hivyo, kwa sababu maoni haya yametolewa, tutaendelea kuyafanyia kazi kwa kina kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojitokeza hapa na ambalo ningependa kuchombeza kidogo ili wajumbe waelewe, kuna Waheshimiwa waliochangia hoja kwamba tunauza madini ghafi, hasa dhahabu, nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhahabu yote inayozalishwa Tanzania huchakatwa katika viwanda mbalimbali vya usafishaji hapa nchini. Tuna *refiners* nane, lakini tatizo lililopo mpaka sasa hivi ni kwamba zote bado hazijapata ile ithibati ya mwisho inayotambulika na ile taasisi ya Kimataifa ya *land,* inaitwa *LBMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile *London Billion Market Association (LBMA)* ina vigezo vyake ambapo usipovifikia wachimbaji hawa wakubwa wanaweza wakaweka masharti ya kutaka kuuza madini na kutuachia ile 20% ambayo mpaka sasa hivi kwa mujibu wa sheria iliyopo tumeendelea kwenda kuisimamia ile 20% ya madini ya wachimbaji ibaki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wadogo tunaendelea kutengeneza mifumo ya kuwasaidia kupitia mikopo ya benki, ambayo wameendelea kuwakopesha na mfuko maalumu ambao Benki Kuu ya Taifa wameendelea kuichakata…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** …ili wapate mikopo waache kuchukua mikopo ya wawekezaji kutoka nje ambao wanawalazimisha kupeleka ile dhahabu nje badala ya kuiacha hapa nchini ili zile *refiners* zilizowekwa nchini ziweze kutumia rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo ya Mama Masasi tu ambayo imeongelewa hapa nchini ndiyo tunayo, tunazo nyingi, tunayo ya kwetu na *STAMICO* iko Mwanza, tuna iliyoko Dar es Salaam na tuna iliyoko hapa Dodoma. Zipo nane na zote zinaweza zikasafisha hii dhahabu mpaka ikafikia 99.99%, lakini hazijapata ithibati ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulisemea kwa haraka haraka ni eneo la sisi kama Wizara kuendelea kupanua wigo wa kuhakikisha kwamba madini yetu yanaendelea kuwanufaisha Watanzania kwa kuangalia maeneo ambayo tulipungikiwa. Kuna wakati kulikuwa na minada ya madini na maonesho ya madini ya vito. Tulivisimamisha kwa muda, lakini sasa tumevirejesha tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tangu tulivyoanza tena kurejesha minada, tarehe 14/12/2024 madini ya vito na hasa *Tanzanite* ziliwekwa tena kwenye mnada na baadaye tarehe 08/04/2025 tukatangaza *tender* ya madini ya kuuza kwenye mnada mwingine na kwa ujumla tulipata mauzo ya jumla shilingi 2,509,245,216/= ambapo katika mapato hayo Serikali ilipata mrabaha zaidi ya shilingi milioni 163.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba minada ina tija na sasa tunakwenda hatua nyingine ya juu zaidi ya kuanzisha maonesho ya madini ya Kimataifa kwa madini ya vito na tunategemea katika huu mwaka wa fedha mtakapotupitishia

bajeti hii tutakwenda kuwa na hiyo minada katika mikoa mbalimbali mikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutakuwa na siku ya kuendesha minada Arusha na siku nyingine tutafanyia Mererani. Mzunguko mwingine tunafanyia katika Miji mingine kama Mahenge, Ruvuma, na Tanga, hii miradi inakuwa ina-*rotate*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, mengine atamalizia Waziri mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, nimalizie tu kwa kusema kwamba naunga mkono hoja na maoni yote na ushauri uliotolewa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunachukua kwa ajili ya kufanyia kazi. Tunaomba Waheshimiwa mpitishe bajeti yetu ili tuweze kwenda kazini kutekeleza kazi ambayo mama ametupatia dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wangu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo tumesaidiana kuifikisha Wizara hii mahali ilipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, naleta kwenu matangazo ya wageni waliopo Bungeni jioni hii ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 54 wa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, ni wapigakura wake kutoka Chato Mkoani Geita wakiongozwa na Mheshimiwa Prospus Makoye, Diwani wa Kata ya Butengo na Mheshimiwa James Kahola Diwani wa Kata ya Bwanga, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 18 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi na Vijana 64 kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, dakika 25.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa nafasi uliyonipatia kwa ajili ya kuhitimisha hoja ambayo nimeiwasilisha asubuhi hii siku ya leo. Naomba nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, na Naibu Waziri Mkuu kwa miongozo yao ambayo wamekuwa wakiitoa ambayo imesaidia sana katika kuimarisha na kuiboresha sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, kwa namna ambavyo wamekuwa na ushirikiano mkubwa na msaada mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba, sekta hii inafanya vizuri na inatoa mchango mkubwa kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba uniruhusu niwashukuru sana Naibu Waziri wa Madini, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara wote kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wameendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini, ambapo tunafanya kazi kwa umoja, upendo na mshikamano mkubwa sana. Hivyo, nichukue fursa hii kuwashukuru sana wote ambao mmefanya kazi hii kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na Wabunge 16. Wabunge 13 kwa kuchangia hapa Bungeni na watatu kwa njia ya maandishi. Kwa sababu ya ufinyu wa muda, na hoja ni nyingi, naomba sasa uniruhusu niende kwenye hoja moja baada ya nyingine ambazo zimewasilishwa na

Waheshimiwa Wabunge. Baadhi ya hoja tutazijibu kwa maandishi, ili tuweze kuwa tumetoa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wameleta hoja zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nilianza leo asubuhi kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye sekta ya madini. Ndani ya miaka minne tumeshuhudia mageuzi makubwa kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara ya Madini kwa muda mrefu sana haikuwahi kuwa imeongezeka kutoka ule utamaduni wake wa kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 89 mpaka 90. Katika kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, bajeti ya Wizara ya Madini imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuonesha utashi mkubwa ambao Mheshimiwa Rais anao katika kuiendeleza hii sekta ya madini, tumeshuhudia ndani ya miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchi yetu ya Tanzania kupitia Benki Kuu ilikuwa haina akiba ya dhahabu. Kwa Bara la Afrika nchi inayoongoza kwa kuwa na akiba ya dhahabu nyingi ni Algeria ambao wana tani 174 na nchi ya 10 kwa akiba ya dhahabu ni Msumbiji, wana dhahabu ya tani 3.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya marekebisho ya sheria hapa ambayo iliwezesha Benki Kuu ya Tanzania kuanza kununua dhahabu na tumeanza kununua dhahabu tarehe 01 Oktoba, 2024. Mpaka ninavyozungumza sasa Benki Kuu imeshanunua dhahabu ya tani 3.7 ndani ya muda mfupi sana. Hivyo, hivi sasa Tanzania imeshaingia kwenye 10 bora ya nchi ambazo zina akiba ya dhahabu. Hii ni ndani ya miezi sita. Haya ni mageuzi makubwa sana ambayo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la maduhuli, mwaka 2015/2016 nchi yetu ya Tanzania ilikusanya maduhuli kwenye sekta ya madini ya shilingi bilioni 162 kwa mwaka mzima. Baada ya mabadiliko ya Sheria ya Mwaka 2017 ambayo ilipelekea

uanzishwaji wa masoko na vituo vya ununuzi, hivi sasa tunayo masoko 43 na vituo vya ununuzi 109.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa makusanyo yetu ya maduhuli yameongezeka. Mwaka 2022/2023 sekta ya madini iliingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 678 kwa mwaka mzima. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 sekta ya madini imeingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 753. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 tumewekewa malengo ya kuingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi trilioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na ndugu zangu Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuvunja rekodi mwaka huu katika kusimamia kuingiza maduhuli kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Leo ni tarahe 2 Mei, 2025 tuna *targets* ya kuingiza shilingi trilioni moja. Mpaka siku hii ya leo tumeingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 882 na tuna mwezi wa Tano haujaisha, tuna mwezi wa Sita, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuvunja rekodi katika maduhuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja ya *drilling rigs* hapa. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na hoja ya kusema kwamba wanaomba zitawanywe maeneo mengi na ziweze kuwasaidia watu wengi zaidi. Ni kweli Mheshimiwa Rais alilielekeza Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kununua *drilling rigs* kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Tulianza na tano, tukazigawa kikanda, tumeona mahitaji ni makubwa, Mheshimiwa Rais akaelekeza zinunuliwe *drilling rigs* nyingine 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza na wewe hivi sasa, *drilling rigs* 10 zimeshaingia, zipo Ofisi ya *STAMICO* Dodoma tunasubiri kuzizindua huu mwezi wa Tano kwa ajili ya kugawa kwa wachimbaji wetu, zipo tayari. *Drilling rigs* mbili zitaelekezwa kwa ajili ya vijana na akina mama kwenye Programu ya *MBT (Mining for a Brighter Tomorrow)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa. Mwaka wa fedha

2021/2022 sekta ya madini ilikuwa inachangia kwenye pato la Taifa kwa 7.2%. Mwaka wa fedha 2023 sekta hii imekuwa na mchango katika pato la Taifa kwa 9.0%. Malengo ya kupitia sera ilikuwa ni ikifika mwaka 2025 sekta hii ichangie 10% kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninasimama hapa mbele ya Bunge lako kwa furaha kubwa ya kutamka kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amevunja rekodi nyingine. Sekta ya madini hivi sasa inachangia katika pato la Taifa kwa 10.1% kabla mwaka 2025 kufika ambapo ulikuwa umesemwa kwa mujibu wa sera yetu na mipango tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Mheshimiwa Prof. Manya amechangia vizuri sana, amesema hatukuwahi kuwa na mradi mkubwa hapa katikati baada ya kutunga sera yetu, hatukuwa na mradi mwingine wowote mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake, katika mgodi ambao ulisubiriwa kwa miaka mingi sana wa eneo la Nyanzaga Sengerema, taarifa imetoka rasmi ya maamuzi ya mwisho ya kiuwekezaji ya Kampuni ya *Perseus* ambao ni wabia wa Serikali kwenye Kampuni ya *SOTTA*. Kampuni hii sasa imetoa tamko la mwisho inakwenda kufanya uwekezaji wa shilingi trilioni 1.4 kujenga mgodi mkubwa katika eneo la Sengerema, Mkoani Mwanza. Hii ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Tabasam, huu mgodi ni wa kwake, utawanufaisha watu wake. Mimi na yeye tulikwenda kuwatembelea wananchi wa Sengerema, ninaamini watajiandaa vizuri, manufaa makubwa yanakuja. Mheshimiwa Mbunge wa Sengerema kwa hoja yake ya pili alioyoisema ya kuhusu leseni za wachimbaji wadogo, mimi na yeye tulikwenda mpaka Nyanzaga pale Sengerema na nilitoa maelekezo kwa mwekezaji ya kwamba, lazima atenge leseni kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie mbele ya Bunge hili, tumeshakubaliana na mwekezaji, anamalizia kufanya

tafiti za mwisho, atatenga leseni ndogo kwa ajili ya wananchi wa Sengerema. Mzee wangu, Mbunge wa Sengerema kaa kwa kutulia leseni zinakuja kwa ajili ya wananchi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja ya kuhusu utafiti wa kina. Waheshimiwa Wabunge wamesema ni kweli nchi yetu ya Tanzania ina ukubwa wa kilometa za mraba 945,000 sawasawa na ekari milioni 233. Nchi yetu tumeigawa katika *QDS (Quarter Degree Sheets)* 322 ambapo kila *QDS* moja ina urefu wa kilometa 50 na upana wa kilometa 50 na inakupatia eneo la kilometa za mraba ambayo ni 2,817 sawasawa na ekari 722,000. Tumefanya utafiti wa kina katika eneo la 16% tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba niliposoma bajeti yangu mwaka uliopita niliwaambia kuhusu helikopta. Ndugu zangu helikopta ile ambayo niliisema hapa, ipo katika mpango na itanunuliwa, na ninavyozungumza hivi sasa, tulifanya mazungumzo na wenzetu Wakala wa Ndege pamoja na *GST,* ndiyo wanasimamia zoezi hili, wamekamilisha taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 ya mwezi Mei ndiyo siku ya mwisho ya kufunga mstari ya wale wadau waliojitokeza. Tarehe 16 *suppliers* wote wa helikopta watakuwa nchini Tanzania kwa ajili ya kikao na *presentation*. Baada ya hapo, tunaanza zoezi la manunuzi ya helikopta kwa ajili ya kuipima nchi yetu kwa kufunga vifaa maalumu ili isaidie kuongeza eneo la utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la utafiti pia niligusia kuna mradi mkubwa wa kurusha ndege ambao ni sisi na Serikali ya Hispania. Tukifanikiwa kurusha ndege katika mradi huo ambao unaendelea hivi sasa katika hatua za mwisho, Wizara ya Fedha tuta-*recover* eneo la kilometa za mraba 165,834 sawasawa na 18% ya nchi yote ya Tanzania. Kwa hiyo, itaongeza idadi kutoka 16 kufikia 34 ifikapo mwaka 2026/2027. Nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imejiweka vizuri katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu eneo lingine ambalo ninataka niligusie hapa, tunakwenda kufanya mabadiliko makubwa sana katika Mgodi wetu wa pale Mererani katika kudhibiti utoroshaji wa madini na upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wale wathaminishaji wote wanaokwenda chini ya mgodi kufanya *valuation* kuanzia mwaka wa fedha ujao, tarehe mosi mwezi wa Saba tutawapatia kofia ngumu zenye *camera* na zenye *mic*. Akishuka chini mgodini mimi nikiwa Wizarani ofisini nitakuwa namwona akiwa chini, anachokisema na ambacho tunakiona pale. Lengo ni kudhibiti mapato na kufanya utoroshaji wa Tanzanite upungue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, ndugu zangu tumezungumza kuhusu kuijengea uwezo *STAMIGOLD*. Ni kweli *STAMIGOLD* ina madeni mengi. Ina zaidi ya shilingi bilioni 58 inadaiwa. Kama Serikali, ni lazima tuje na mikakati ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tarehe 02 Mei, 2025 *STAMIGOLD* wametoa tangazo la kuwakaribisha wadau kwenda kuendeleza mgodi, ili tuweze kupata fedha za kuendesha mgodi na vilevile tuweze kurejesha madeni na mgodi uweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mgodi ule una wakia 90,000. Kwa bei ya leo ya dhahabu ya wakia moja ni dola 3,200. Tukifanya kazi pale, ukiondoa gharama zote, tuna uwezo wa kupata shilingi bilioni 614. Ndiyo kazi ambayo tumewekeza *STAMIGOLD* hivi sasa. Tunategemea kupata waendelezaji wa ule mgodi ili mwisho wa siku tuweze kutatua changamoto za *STAMIGOLD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nizungumze kuhusu hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wameisema sana. Hoja ya kuhusu *CSR* imezungumzwa kwa urefu sana. Mimi nilikaa na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini wakaielekeza Serikali kwenda kuipitia upya kanuni ya uwajibikaji kwa jamii (*CSR)* ambayo ilionekana ina matatizo. Matatizo sugu ya kanuni zile yalikuwa ni haya yafuatayo: -

(i) Suala la ucheleweshaji ukamilikaji wa miradi;
(ii) Ubora wa miradi; na
(iii) Gharama kubwa inayotumika katika miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliitikia wito wa Kamati yangu ya Bunge, nikaitisha kikao *St. Gaspar Hotel.* Wabunge wote mlialikwa wale mnaotoka katika maeneo ya uchimbaji na wadau wote wakaja pale tukajadiliana. Mkatoa maoni yenu kurekebisha zile kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie kwamba kanuni zile ndani ya Wizara tumeshamaliza kazi yake. Hivi sasa zitakwenda kwa *AG,* zitapitishwa na zitakwenda ku-*address* matatizo yote yale magumu ambayo mlikuwa mnayaona hasa katika ubora na ucheleweshaji wa miradi. Nataka niwatoe hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Musukuma alikuwa ana hoja *specific*. Pale Geita ilitokea sintofahamu ya fedha za *CSR* ya miaka iliyopita kuwekwa pembeni kana kwamba haziwezi kutumika tena na kuwakosesha fursa wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba niliwaita *GGM*, Mkuu wa Mkoa, na Wabunge wote akiwemo Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Magessa pamoja na Mheshimiwa Musukuma. Tumekubaliana na ni maelekezo ya Wizara kwamba hakuna senti hata moja itakayorudi isiache kutekeleza mradi ambao ulipangiwa mpango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Msukuma kwamba zile fedha ambazo zilitengwa zitafanyika kama ambavyo ilielekezwa katika miradi iliyokusudiwa. Hatuwezi kwenda tofauti na kile ambacho kilisemwa. Hivi sasa nasubiri taarifa ya mwisho kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, na maelekezo yangu ni kwamba, fedha zote zitumike kwa ajili ya miradi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfuatiliaji mzuri sana, lakini nataka nimhakikishie kwamba, jambo hili tutalifanya na ile miradi ya

wananchi wake itakwenda kujengwa. Hakuna atakayekwepa na kukimbia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Kanyasu na ameisema hapa, wananchi wa Geita wapo wananiangalia hivi sasa wanasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni ya GGM imetolewa mwaka 1999. Miaka 26 iliyopita imekuwa na mgogoro mkubwa na wananchi wanaozunguka maeneo yale. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana aliyekuwa Waziri wa Madini na hivi sasa ni Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko alifanya kazi kubwa ya utatuzi wa mgogoro huu akaufikisha sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeingia Wizarani tarehe 30 Mwezi Agosti, 2023 nikakuta kuna hoja 11 hazijafanyiwa kazi. Mheshimiwa Mbunge Kanyasu ni shahidi yangu, katika hoja 11, nane zote tumezimaliza, zimebaki hoja tatu. Tumebaki na hoja ya fidia Nyakabale, Nyamilembo, Mizingamo na Magema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kanyasu ni shahidi, kwani mimi na yeye tulizunguka kwa pamoja, wote tulikwenda mpaka Nyakabale kuangalia hali ya wananchi ilivyo. Alichokisema Mheshimiwa Kanyasu ni cha kweli, nami niliwaambia watu wa mgodi kwamba, katika mazingira yaliyopo pale lazima wale wananchi tuwahamishe ili waweze kupisha yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kanyasu anakumbuka, baada ya maelekezo yangu hayo palitokea sintofahamu, baadhi viongozi walionekana kwamba wao shida yao, siyo kuhama. Shida yao ni wapate huduma zote za elimu, afya na barabara ya kuwafikisha Geita. Vilevile shida yao ni wapate huduma zote za elimu, afya, maji na wapate barabara ya kuwafikisha Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye tukagundua kwamba huo haukuwa msimamo wa wananchi wa Nyakabale. Kwa hiyo, tukakubaliana kwamba tutengeneze timu mpya ya kwenda

kusikiliza wananchi na hoja zao ili tuweze kuwasaidia. Timu ile tuliiunda, timu imeenda na imekamilisha taarifa yake na wiki ijayo itawasilisha mbele ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie wananchi wa Nyakabale, Nyamilembo, Magema, Mizing'amo ambao wote mnaniangalia hapa, Mbunge wenu amefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba jambo hili linafikia mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika ule muda aliousema, tutajitahidi kuhakikisha kwamba kero hii inafikia mwisho, na hatua ambayo tumeifikia ni hatua ya uwasilishaji taarifa, baada ya hapo tutatoa taarifa nini kimefanyika na wananchi wale wajue muafaka wa maeneo yao na nini Serikali itafanya katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo *status* ambayo tumeifanya katika eneo lile ambalo Mheshimiwa Mbunge Kanyasu amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limesemwa sana hapa ni eneo la uongezaji thamani madini, hasa katika *refinery*. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, mlikuwa mnahoji Serikali kwa nini haijasaidia? Serikali imefanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapitishe kwenye mchakato, Sheria yetu ya Madini kifungu cha 59(1) kinasema vizuri kabisa, Waziri kwa kushirikiana na wamiliki wa leseni watatenga kiasi cha asilimia kisichopungua 20% ya madini kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa na kusafishwa ndani ya nchi. Ndiyo kifungu kilikuwa kinasema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mimi kuingia Wizarani nikaunda kamati maalum, maarufu kama Kamati ya *Section 59* ikawaita wadau wote, tukakaa nao mezani, kwamba kwa nini hamtengi 20% ya madini yachakatwe, yasafishwe na kuyeyushwa hapa nchini? Wakaja na hoja wakawaambia, Mheshimiwa Waziri sisi ni *compliant* wa Kifungu cha 59. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madini haya *especially* dhahabu yanachakatwa, tunaya-*smelt*, kwa hiyo, tupo ndani ya kifungu. Tukaona sheria yetu ilikuwa na upungufu. Kupitia *finance bill* tukafanya marekebisho tena ya Kifungu cha 59. Tukaongeza maneno pale mbele kusafishwa, kuyeyushwa, kuchakatwa na kuachwa kwa ajili ya biashara ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, hiyo ndiyo hatua ambayo Serikali imeichukua, tukisema Serikali haijafanya kazi yake, hapa hatuitendei haki. Huo ndiyo mchakato ambao tumeuchukua kuhakikisha kwamba madini haya yanabaki nchini, yanasafishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kiwanda kiweze kupata *LBMA certification* kwenye kusafirisha dhahabu, lazima kiwe kina uwezo wa *feedstock* ya madini ya dhahabu tani 10 kwa mwaka na *silver* tani 15. Hapa kinachogomba ni upatikanaji wa *feedstock*, ndiyo maana tukatunga hii sheria na siyo kwamba hatuisimamii. Ndugu zangu sheria hii tunaisimamia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua gani? Serikali hatua ambazo imechukua hivi sasa ili kurahisisha upatikanaji wa madini kwenda katika viwanda vya kusafisha, cha kwanza, tumeondoa, tumepunguza mrabaha kutoka asilimia sita kwenda asilimia nne kwa madini yote yanayopelekwa katika viwanda vya kusafishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, tumeondoa ada ya ukaguzi; cha tatu, tumeondoa kodi ya *VAT* madini yote yanayokwenda katika viwanda vya kusafisha ni *zero rated,* lakini madini hayaendi, kwa nini? Swali la msingi, kwa nini madini hayaendi? Ni kwa sababu watu wetu Watanzania wengi wadau hawana uwezo mkubwa wa kimitaji wa kuweza kuchimba na kuamua sehemu ya kupeleka. Fedha nyingi zinatoka nje ya nchi ambapo wao ndiy wanaotoa fedha za mitaji, awe anachimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnafahamu msemo, "anayemlipa mpiga zumari, ndio anayechagua wimbo." Kwa hiyo, kwa mitaji ambayo inawekezwa kwao, wao ndio wanapeleka madini hayo huko, lakini kama Serikali, tukasema hili hapana, tumetunga hii

sheria, Kifungu cha 59, ndugu zangu *BoT,* amenunua dhahabu ambayo imetengwa kupitia *Section* 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadogo wote wameanza kupeleka na wakubwa ambao mnasema tunawaogopa, ndugu zangu nataka niwahakikishie ndani ya Bunge hili, hivi sasa hakuna mzalishaji mkubwa yeyote anayesafirisha madini nje ya nchi pasipo kuacha 20%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayatamka haya mbele ya Bunge hili kama sehemu ya uthibitisho ya usimamizi wa kifungu hiki, isipokuwa tumebakiza hivi sasa kikao cha mwisho cha tarehe 5 Mei, 2025 kati ya watu wa Benki Kuu, kati ya wadau *refineries* zote akiwemo Mama Masasi na wengine pamoja na makampuni makubwa kutafuta namna nzuri ya kuyafanya madini haya yachakatwe na kufanyiwa kazi hapa nchini pasipo ku-*compromise* taratibu za kisheria. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wanaogopwa, hamna ambacho kimesimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja pia ya kuhusu uwezeshaji wa Tanzania. Mimi nimezunguka katika mikutano mingi. Sekta ya Madini haiwezi kukua, haiwezi kuendelea kwa kasi kubwa kama Watanzania hawatakuwa *at the centre of this sector,* na kama hawatakuwa katika sehemu ya kwanza ya kushiriki katika hii *sector,* lazima tuwajengee uwezo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeunda kamati ya watu sita ya kwenda kufanya utafiti ya kuona namna bora ya kuwawezesha wachimbaji wadogo, tutawa-*cluster* wachimbaji wadogo na watoa huduma, kuanzia yule mdogo, wa kati na mwenye nafuu na Serikali, lazima tuwashike mkono. Nimeshazungumza na Waziri wa Fedha, nimeongea na Gavana, lazima tuwashike mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Wizara ya Fedha kuna mfuko wa dhamana wa *credit guarantee scheme* tutahakikisha kwamba tunawaongezea mitaji Watanzania. Watanzania wamiliki migodi mikubwa wawe sehemu ya utekelezaji wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya uongezaji thamani madini, tumepiga hatua sana hivi sasa, tumepiga hatua kubwa sana. Mathalani kwa Mkoa wa Dodoma peke yake, tuna viwanda saba vya kuongeza thamani madini ya Metali *(Base Metals)* tuna viwanda saba vikubwa ambavyo vitanunua shaba, vitanunua *nickel*, vitanunua *lithium* watai-*process* hapa hapa, itafanyikia hapa hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa lengo letu, ni sisi kuwa kitovu cha uzalishaji wa bidhaa za kupitia madini ya *Metali*. Hivi sasa ukienda pale Nala Dodoma, kuna kiwanda cha kutengeneza *copper cathode*. Nimekwenda Chunya nimefungua kiwanda cha kutengeneza *copper cathode*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kwenda mpaka kutengeneza *copper wire,* jambo hili linawezekana kwa mipango tuliyonayo na mikakati iliyopo. Nataka niwahakikishie Watanzania, tunakwenda kuongeza viwanda vya uongezaji thamani madini yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *STAMICO,* Prof. Manya kasema kama alikuwepo katika majibu yangu. Nimeshawaelekeza *STAMICO*, imetosha sasa kuuza mkaa, imetosha ku-*drill*, nataka *STAMICO* akisimama Dkt. Mwasse yule awe na hadhi kama Mark Bristow, Rais wa *Barrick* hivyo hivyo kwa ukubwa wa *STAMICO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tumewatengea fedha, wana leseni tatu. Tumewaambia wakazifanyie utafiti, waziendeleze, maana nataka kuona mgodi mkubwa wanamiliki *STAMICO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maduara, Mheshimiwa Maganga alisema vizuri, sheria inasema vizuri kabisa, kila anayepewa leseni achimbe. Leseni siyo upangishaji, leseni ni ya kuchimba. Kumekuwepo na utaratibu hivi sasa Watanzania wengi wanachukua leseni halafu wanakubali kuwaingiza wachimbaji wadogo wanatengeneza maduara katika leseni zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme mbele ya Bunge lako Tukufu, ni marufuku mtu yeyote mwenye leseni ndogo ya uchimbaji kumwingiza mchimbaji mdogo wa maduara pasipokuwa na makubaliano yaliyosajiliwa Tume ya Madini. Leseni haikutaki wewe kumwingiza mchimbaji mdogo. Ukimwingiza chukua *risk* ya kusajili mkataba makubaliano yenu, lakini pia chukua *risk* ya kwamba, utakapopata uwekezaji mkubwa yule mtu asiondolewe mpaka afidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuacha nguvu ya Watanzania inapotea kwa sababu tu ya watu wanaamua kuchukua leseni kwa ajili ya upangishaji. Hayo ndiyo ambayo tumeona katika eneo hili tuliseme. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele. La mwisho ni *issue* ya leseni, tutaendelea kutoa leseni kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuwawezesha. Leseni kubwa tunatoa, tunashukuru sana hivi sasa tuna kampuni ya *Duma Tanz Graphite* wataanza uzalishaji pale Mahenge, Mantra wanakwenda vizuri kule kwa Mheshimiwa Kawawa. Pia tutaendelea kutoa leseni kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesho sasa tatu asubuhi nitakuwa Nyamongo Tarime ninagawa leseni kwa vijana 2,000 wanaouzunguka mgodi wa *North Mara* ambao walikuwa wanavamia mgodi na kupora mali. Tumekaanao, tumewapa elimu, kesho nawapa leseni, na *North Mara Barrick* watawapa na msaada wa kiufundi watawasaidia namna ya kuweza kuchoronga na kuchimba na itakuwa ni sehemu ya manufaa makubwa sana kwa wananchi wa eneo la Tarime Nyamongo pale kwa ajili ya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda wangu umefikia mwisho, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba hoja ni nyingi sana, ningeweza kuzijibu zote, lakini muda hautoshi. Kwa hiyo, nyingine nitazijibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli moja tu nataka niwaambie, tusijichukulie kwa udogo, sekta hii ya madini hivi sasa inafanya vizuri sana katika kuchochea uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa kiongozi wa kweli kwa kuifanya sekta hii iweze kuleta mabadiliko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba mtuunge mkono kwenye bajeti yetu hii na niliombe Bunge lako tukufu likubali kutupitishia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2025/2026 ya takribani shilingi 224,984,150,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*…………………………..Sh.8,041,532,427

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………Sh.1,771,315,861
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*………....Sh.2,210,549,391
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..……….……....Sh.778,492,594
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*……………….…....Sh.2,269,770,585
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*……………………………………Sh.1,262,115,086
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*….…..Sh.934,136,390
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit* ……………….……..…...Sh.802,689,796
Kifungu 2001 – *Minerals Division*…………………....Sh.81,385,581,870
Kifungu 1008 – *Monitoring and Evaluation Unit*……….Sh.923,178,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 100 – Wizara ya Madini**

Kifungu 2001 – *Minerals Division*……….……...….Sh.124,604,788,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 Kanuni ndogo ya 3(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu

za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu ya wataalamu kwa kazi nzuri mliyofanya. Bajeti yako imepita vizuri sana na nikupongeze vilevile kwa namna ulivyokuwa unajibu hoja kwa weledi mkubwa sana, hongera sana. Na hiyo tai kidogo ilitaka kuelekea elekea, lakini baadaye ukaamua, sijui ulibadilisha vipi, lakini niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri. Nawatakia *weekend* njema. *(Makofi/Kicheko)*

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.58 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 5 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*